# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA NANE

**Kikao cha Thelathini na Tano – Tarehe 31 Julai, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008.

**MHE. BENSON M. MPESYA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA):**

Taarifa ya Kamati ya Ulinzi na Usalama Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha uliopita pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2007/2008.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI:**

Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha uliopita pamoja na Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2007/2008.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 320

### Umeme Vijiji vya Makonga na Juhudi – Newala

**MHE. KAPT. GEORGE H. MKUCHIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika kipindi cha Uongozi cha Awamu ya Pili kati ya mwaka 1993 hadi 1995, Shirika la Ugavi wa Umeme *(TANESCO)* lilianzisha Mradi wa kuweka umeme kwenye vijiji vya Makonga na Juhudi Wilayani Newala, lakini mradi huo umesimama kwa zaidi ya miaka sita (6) sasa; na kwa kuwa wananchi wa Vijiji hivyo walishapata matumaini ya kupata umeme maana nguzo zilishawekwa:-

(a) Je, ni sababu zipi zilisababisha mradi huo usiendelee hadi kukamilika?

(b) Je, Serikali inawaahidi nini wananchi wa Vijiji hivyo kuhusu kukamilishwa kwa mradi huo ili wapate umeme kama ilivyokusudiwa na Serikali wakati mradi unabuniwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Kapt. George H. Mkuchika, Mbunge wa Newala, lenye sehemu (a) na (b), naomba kutoa maelezo ya utangulizi yafutayo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 1993 kulikuwa na mradi wa kupeleka umeme Kitangali kwenye mashine za kusukuma maji zilizo kwenye vyanzo vya maji vya Mitema. Lengo la mradi huu lilikuwa ni kupunguza gharama za matumizi ya mitambo ya dizeli iliyokuwa inatumika kwenye vyanzo hivyo. Njia kuu ya umeme inayokwenda kwenye vyanzo hivyo vya maji imepita katika vijiji vya Makonga na Juhudi. Gharama za mradi huo ilikuwa ni shilingi milioni 403. Baada ya mradi huo kukamilika mwaka 1993, mitambo ya dizeli iliyokuwa ikitumika katika vyanzo hivyo ilihamishiwa kwenye kituo cha uzalishaji umeme Mkoani Mtwara.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kapt. George H. Mkuchika, Mbunge wa Newala lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa fedha zilizokuwa zimepangwa wakati wa utekelezaji wa mradi wa kupeleka umeme Kitangali, vijiji vya Makonga na Juhudi havikuweza kupatiwa umeme licha ya nguzo kupita katika vijiji hivyo.

(b) Mheshimiwa Spika, unganishaji wa umeme kwa vijiji vya Makonga na Juhudi kwenye njia kuu inayopeleka umeme kwenye vyanzo vya maji vya Mitema, ulikuwa utekelezwe chini ya mpango wa upelekaji umeme vijijini. Serikali inakamilisha majadiliano na *Artumas* kuhusu mikataba ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme katika Mikoa ya Lindi na Mtwara. Mikataba hiyo itaiwezesha *Artumas* kuendesha shughuli hizo badala ya *TANESCO*. *(Makofi)*

**MHE. KAPT. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri yanayowapa matumaini wananchi wa vijiji vya Makonga na Juhudi kule Newala na wenyewe wamesikia. Nina swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Je, Mheshimiwa waziri anaweza kututhibitishia kwamba mwaka huu wa fedha suala hili litashughulikiwa na kumalizwa?

(ii) Kwa kuwa tunao umeme wa gesi asilia kutoka Msimbati, ambao ni mwingi na tunajiandaa mwingine kuwasaidia wenzetu mikoa mingine kwenye *National grid*. Je, Wizara inachukua hatua gani kuhakikisha kwamba vijiji vingine vya Mkoa wa Mtwara vinapata umeme badala ya umeme kuwepo kwenye maeneo ya miji peke yake?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; Mheshimiwa Spika ni matarajio yetu kwamba utekelezaji wa usambazaji wa umeme kupitia kampuni ya *Artumas* utaanza kufanyika ndani ya mwaka huu wa fedha 2007/2008 kwa sababu moja kuu ambayo mazungumzo yapo katika hatua nzuri sana kati ya *TANESCO* ambayo ndiyo mwakilishi wa Serikali pamoja na *Artumas* kampuni mwekezaji katika mikoa hiyo ya kusini na taifa zima. Kwa hivyo tuna hakika umeme huu utaanza kusambazwa katika maeneo ya Mbunge hivi karibuni ndani ya mwaka huu wa fedha.

Kuhusu swali la pili; tunamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwa niaba ya serikali kwamba baada ya mpango wa *TANESCO* na *Artumas* kuanza, hasa kupitia *Artumas* kuanza kusambaza umeme tuna hakika umeme huu hautaishia sehemu za mijini tu. Lakini si hivyo tu, bali pia tuna usambazaji wa umeme vijijini kupitia wakala wa nishati vijijini. Tuna hakika kwamba mambo yote mawili yakianza kutekelezwa basi maeneo mengi ya Kusini si tu kwamba maeneo ya mijini bali ya vijijini yatapata huduma ya umeme.

Na. 321

**Hitaji la Umeme – Kwimba**

**MHE. BUJIKU P. SAKILA** aliuliza:-

Kwa kuwa Jineri za Mwalujo *(LINTEX),* Sangu *(AFRISIA)* na vijiji vya Hungumalwa, Ilula, Mwamashimba, Kikubiji na Shilima, vimo katika mpango wa kupatiwa umeme:-

(a) Je, umeme huo utasambazwa lini kwa Jineri hizo na vijiji hivyo?

(b) Je, umeme huo utasmbazwa chini ya mpango gani na mpango huo unatarajiwa kutekelezwa lini na kwa gharama gani ?

(c) Je, kwa nini umeme wa grid usipozwe kwanza katika kijiji cha Hungumalwa na kutokea hicho uweze kusambazwa kwenda maeneo niliyotaja na maeneo mengine mbali mbali katika Wilaya ya Kwimba, Misungwi, Shinyanga Vijijini na Maswa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mbunge wa Kwimba, lenye sehemu (a), (b) na (c), naomba kutoa maelezo ya utangulizi yafutayo:-

Wilaya ya Kwimba ni mojawapo ya Wilaya za Mkoa wa Mwanza ambazo zina umeme katika Makao yake Makuu. Miji ya Misungwi na Ngudu hupata umeme kupitia laini ya umeme wa kilovoti 33 inayotokea kituo cha kupozea umeme *(Sub Station)* cha Nyakato.

Mheshimiwa Spika, utafiti uliofanywa na *TANESCO* mwaka 2005 ulipendekeza uendelezaji wa umeme katika maeneo tajwa ufanyike kwa njia ya umeme wa kilovoti 33. Mipango imeandaliwa kuweka kituo cha kupoza umeme cha *220/33KV* katika kijiji cha Mabuki kwa ajili ya kuongeza ubora wa umeme katika miji ya Misungwi, Ngudu na kwenye pampu za maji za Ihelele. Serikali ya Ufalme wa Hispania imeonyesha nia ya kufadhili mradi huu ikiwa ni pamoja na kusambaza umeme katika vijiji vya jirani na vinu vya kuchambulia pamba vya *Lintex* na Afrisia. Gharama ya mradi huo inakadiriwa kufikia shilingi bilioni 12.0.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo ya utangulizi sasa naomba nijibu swali la Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mbunge wa Kwimba, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, umeme utasambazwa kwenye jineri na vijiji alivyotaja Mheshimiwa Mbunge mara fedha za utekelezaji wa mradi huo zitakapopatikana. Taratibu zinaendelea za kupata fedha kutoka Serikali ya Hispania.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu la sehemu (a), fedha zinategemewa kupatikana kutoka Serikali ya Ufalme wa Hispania na gharama za kusambaza umeme chini ya mradi huu zinakadiriwa kufikia shilingi bilioni 12.0.

(c) Mheshimiwa Spika, utafiti uliofanyika unapendekeza kujenga kituo cha kupooza umeme *(Sub Station)* cha *220/33 KV* katika kijiji cha Mabuki na utasambazwa kwenye maeneo ya jirani kutokea hapo.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana. Lakini, nina swali moja la nyongeza: Kwa kuwa, mradi huu umekuwa wa siku nyingi sana na kwa mawasiliano ya nyuma gharama imekuwa ikibadilika, kwanza ilikuwa bilioni 1.3, milioni 800 na leo tunaambiwa gharama nyingine. Lakini, vile vile hata wafadhili hawaaminiki. Kwa nini sasa mradi huu usipelekwe kwenye mradi wa umeme vijijini ambao unaanza hivi karibuni ili wananchi wa Wilaya ya Kwimba niliowataja waweze kupata umeme mapema?Kwa kuwa hitaji la msingi la wananchi wa maeneo niliyoyataja pamoja na wenye Jineri nilizozitaja, kwa kweli siyo mahali wapi umeme utatoka, lakini shida yao kubwa sana ni umeme utapatikana lini. Je, pamoja na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa leo sasa anawaambiwa wananchi wa maeneo hayo waendelee kuwa na matumaini tena kwa kipindi cha muda gani? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; tunaelewa jinsi Mheshimiwa Mbunge suala hili linavyomgusa kwa sababu mradi huu amekuwa akiuongelea kwa muda mrefu. Kuhusu pendekezo kwamba kwa nini mradi huu tusiuhamishie kwenye mradi wa usambazaji vijijini, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na kumkumbusha kuwa gharama za mradi huu ni kubwa kama ambavyo imeelezwa kwenye jibu la msingi kwamba ni bilioni 12 na sote tunafahamu uwezo wetu wa kifedha, maendeleo ya nchi yetu pia yanategemea kuongezewa nguvu na *Partners* wetu katika maendeleo yetu. Kwa hiyo, ni jambo la msingi kuona kuwa pale ambapo tunaweza kupata msaada wa wahisani, tushirikiane nao vizuri natujenge imani kwao. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge tunamhakikishia kwa kuangalia gharama zilivyo bilioni 12 na juzi tumesema tulikuwa na bilioni 10 kwa ajili ya Mfuko wa Umeme Vijijini, kwa namna yote ile haiwezi kufanyika kwa mradi mmoja. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge awe na imani. Lakini pia kama tulivyosema kwenye jibu la msingi, mazungumzo yanaendelea vizuri, matarajio ni makubwa, Serikali ya Ufalme wa Hispania tunaamini kwamba itatusaidia hizo pesa ili tuwezeshe huo miradi.

Mheshimiwa Spika, la pili; naomba niwahakikishie wananchi, umeme utafika. Kama tulivyosema kwamba hii miradi itakapotekelezwa kupitia Wakala wa Usambazaji wa umeme vijijini, tuna hakika kwamba ikiishaanza hii, na ipo mipango mingi inayoendelea, tuna hakika kwamba baadhi ya maeneo ya Mheshimiwa Mbunge pia yatanufaika na huduma ya usambazaji umeme vijijini kupitia Wakala wetu wa Tanzania.

Na. 322

**Kilimo cha Alizeti - Iramba Magharibi**.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH** aliuliza:-

Kwa kuwa, miongoni mwa zao la biashara lililoshamiri hivi sasa katika jimbo la Iramba Magharibi ni alizeti na kwa kuwa zao hilo limechukua nafasi kubwa ya zao la pamba:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani madhubuti ya kuliendeleza zao hilo kama zao la biashara ndani ya Jimbo la Iramba Magharibi?

(b) Je serikali imeweka utaratibu gani wa kulitambua zao hilo na kulipa kipaumbele katika bei kwa nia ya kumwinua mkulima; kwa kuwa, mafuta ya alizeti yametokea kupendwa sana na watumiaji wake ni wengi nchini?

(c) Je, ni tani ngapi zimezalishwa na wakulima wa jimbo la Iramba Magharibi kwa kipindi cha mwaka 2006/2007; na wastani wa bei kwa kilo ulikuwa kwa kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI WA CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika**,** kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Killimbah, Mbunge wa Iramba, naomba kwanza nimpongeze yeye na Mkoa mzima wa Sindgida kwa sababu Mkoa wa Singida ndiyo unaoongoza kwa uzalishaji wa zao la alizeti ukifuatiwa na Mkoa wa Dodoma na Rukwa.

Mheshimwa Spika, baada ya pongezi hizo, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Juma H. Kilimbah mbunge wa Iramba Magharibi kama ifuatavyo:-

(a)Kuanzia mwaka 2006/2007, serikali imekuwa ikiratibu utekelezaji wa programu ya kuendeleza sekta ya kilimo, kupitia mipango ua Wilaya ya kuendeleza kilimo ambapo miradi iliyoibuliwa na wananchi wa maeneo husika hupewa kipaumbele. Kwa kuzingatia utaratibu huo, katika mwaka 2006/2007 serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 154.225 kwa ajili ya kugharamia miradi ya kilimo iliyoibuliwa na wananchi wa wilaya ya Iramba likiwemo Jimbo la Iramba magharibi. Kati ya miradi hiyo iko, inayohusu uzalishaji usindikaji na upatikananji wa masoko ya zao la alizeti.

(b) Kwa kutambua umuhimu wa zao la alizeti, serikali imeendelea kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuendeleza utafiti wa alizeti katika vituo vya utafiti wa kilimo. Tayari aina moja ya alizeti ijulikanayo kama *Record* imetolewa na kituo cha utafiti wa kilimo cha Ilonga na inatumiwa na wananchi katika maeneo mengi yanayozalisha alizeti nchini.

(ii)Kuhimiza sekta binafsi ishiriki katika uzalishaji wa mbegu bora za alizeti na kuziuza kwa wakulima. Hadi sasa jumla ya aina saba za mbegu za alizeti bora zinapatikana nchini. Aina hizo ni *CRN*-1435, *PAN*-7369, *PAN*-7352, *AGSUN*-8251, *AGSUN*-5551, *AGSUN*-8751 na *AGSUN*-4672. Mbegu hizi zinafaa kuzalishwa katika maeneo mbalimbali nchini.

Aidha, ili kuhakikisha kuwa mbegu za mafuta na mafuta yanayozalishwa nchini yanaendelea kupata soko la uhakika na hayaathiriwi na ushindani kutoka mafuta yanayoingizwa kutoka nje. Serikali kuanzia mwaka wa 2003/2004, iliweka kodi ya asilimia 10 ya mafuta ghafi yanayoingia nchini. Kodi hiyo imetoa mchango mkubwa katika kuchangia kuongeza uzalishaji wa zao la alizeti kutoka tani 80,870 mwaka 2000/2001, hadi tani 134,360 mwaka 2004/2005.

(iii)Kwa kuwa uzalishaji wa alizeti kwa ajili ya msimu wa 2006/2007 nchini bado unaendelea, na takwimu tulizonazo ni za malengo ya uzalishaji katika misimu iliyopita. Uzalishaji wa alizeti katika msimu wa 2005/2006 katika Wilaya ya Iramba ulikuwa tani 18,237 kati ya hizi, inakadiriwa kuwa takriban tani 7,200 zilizalishwa na wananchi wa Jimbo la Iramba Magharibi.

Aidha, wastani wa bei ya alizeti katika msimu wa 2005/2006 ulikuwa kati ya shilingi 7,000/= kwa gunia la kilo 70 sawa na shilingi 100/= kwa kilo moja ya alizeti, na kiwango cha juu kilikuwa shilingi 15,000/= kwa gunia la kilo 70 sawa na shilingi 250/= kwa kilo.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na hasa kwa kutambua kwamba Mkoa wa Singida ndio Mkoa unaoongoza kwa uzalishaji wa alizeti.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu hayo mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali dogo la nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri wakati akijibu swali kipengele (b) ameeleza kwamba baada ya kuufanya utafiti kupitia Chuo cha Ilonga, ameeleza kwamba zipo mbegu saba ambazo zinatumika kwa ajili ya kuzalisha hili zao la Alizeti: Sasa nina swali lifuatalo; J, Mheshimiwa Waziri anawezza akaniambia ni mbegu ipi kati ya zile saba ambayo inafaa kwa udongo na mazingira ya Jimbo la Iramba Magharibi?

**NAIBU WAZIRI WA CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA):** Mheshimiwa Spika, mbegu hizi zimefanyiwa utafiti na utafiti tunapoufanya tunakwenda kwa kuangalia *ecological areas* tulizonazo hapa Tanzania. Mikoa ya Singida, Dodoma na hata Tabora inafanana kwa kiwango kikubwa sana. Kwa hiyo, megu hizi mimi nina hakika kwamba ukizizalisha katika maeneo haya, bado zitakuzalishia kwa tija kubwa sana kwa sababu mazingira ya Mikoa hii ambayo tunaita Mikoa Kame, yanafanana.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, bado ninamkaribisha Mheshimiwa na Mkoa mzima wa Singida kuwasiliana na sisi Wizara ya Kilimo kama kuna haja ya kusema tu-*recommend* kabisa kwamba tumia mbegu hii, tutafanya hivyo kwa sababu utaalamu huu upo katika Wizara ya Kilimo.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa wataalam wamethibitisha kuwa mafuta yanayotokana na alizeti hayawezi kuleta chorestrol katika mwili wa binadamu; na kwa kuwa nchi hii inatakiwa tujitegemee kwa mafuta ya kupikia.

Je, Wizara itakubaliana nami kwamba ingekuwa vizuri kutoa mwongozo kwa wenye viwanda waingie mikataba ya kulima alizeti na Mikoa inayozalisha alizeti? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA):** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Mzindakaya kwa swali lake hili zuri. Napenda kumhakiishia kwamba zao hili la alizeti, siyo tu kwamba halina *chorestrol*, lakini kama ilivyo kwa mbegu za mafuta, ni zao muhimu pia kwa ajili ya *Bio-Diesel*.

Sasa utaratibu huu wa kuwahamasisha wananchi kuingia mikataba ni utaratibu ambao hivi sasa Serikali inautilia maanani na unaendelea. Hivi sasa tunavyozungumza, Chuo Kikuu cha Kagoshima kule Japan wamekwishafika huku na wamefanya utafiti zaidi kuhusu uzalishaji wa zao hili na lengo lao ni uwekezaji katika zao hili la alizeti. Wamefanya utafiti huu kushirikiana na Kituo chetu cha Utafiti cha Siriani.

Kwa hiyo, mipango ipo mbioni, nawaomba tu wananchi ambao wako tayari kujiingiza katika uwekezaji wa kilimo, wawe huru, waje kwetu na waende *TIC* kwa sababu ndio mambo ambayo tunataka yachukuliwe kwa kipaumbele. *(Makofi)*

Na. 323

**Suala la Mpaka wa Tanzania na Malawi**

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA** aliuliza**:-**

Kwa kuwa suala la mpaka kati ya Tanzania na Malawi katika Ziwa Nyasa bado lina utata mkubwa unaowaletea usumbufu mkubwa Watanzania wengi waishio kando ya Ziwa hilo wanalolitegemea kwa Uchumi na Maendeleo yao, na kwa kuwa Rais wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin W. Mkapa na Rais wa Malawi aliyemaliza muda wake, Mheshimiwa Bakili Muluzi walianza kulishughulikia tatizo hilo:-

Je, Juhudi zilizoanzishwa na Ma-Rais hao wastaafu ziliishia wapi, na ni nini mkakati wa Serikali ya Awamu ya Nne katika kulishughulikia tatizo hili?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu**:-**

Mheshimkiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tatizo linaloukabili mpaka kati ya Tanzania na Malawi na linalohitaji ufumbuzi wa haraka ni mafuriko kwenye eneo la Mto Songwe hasa wakati wa vipindi vya mvua. Mto huu una tabia ya kuhamahama wakati wa vipindi vya mvua na kuhatarisha mali na maisha ya wananchi wanaoishi kandokando ya Mto huo. Hivyo, Serikali ya Awamu ya Nne itaendeleza juhudi za kutekeleza miradi na mazungumzo yaliyoanzishwa na Serikali ya awamu ya Tatu. Kwa sasa, Serikali za Tanzania na Malawi zinatekeleza kwa pamoja, Programu ya Maendeleo ya Bonde la Mto Songwe *(Songwe River Basin Development Program)* ambayo inalenga kudhibiti na kuimarisha mapato ya Mto Songwe na pia kuboresha maisha ya wakazi wa bonde la mto huo kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza juhudi zilizoanzishwa na Awamu ya Tatu, Tanzania na Malawi zilishirikiana kuitisha kikao na Wadau wa Maendeleo *(Development Partners)* kilichofanyika mjini Blantyre tarehe 10 Mei, 2006. Wadau waliohudhuria ni pamoja na *EU, USAID, FAO, UNDP* n.k. Mkutano huu ulionyesha kuwa *FAO* tayari wanafanya tathmini juu ya hali ya uchumi wa jamii inayoishi katika Bonde hili. Kazi hii ilifanyika katika hatua ya upembuzi Yakinifu. Hivyo Tanzania na Malawi, kwa pamoja zilipeleka ombi rasmi *FAO* kuomba kutumia fedha ya utafiti huu kugharimia hatua ya Ubunifu wa kina wa Mradi wa Maendeleo ya ya Bonde la Mto Songwe. Wadau wengine kwenye mkutano huo wametaka taarifa za ziada juu ya Mradi huu ndipo watatoa msimamo wao. Taarifa husika zimekwishapelekwa kwa wadau hao.

Mheshimiwa Spika, Tanzania na Malawi zilikutana tena mwezi wa Februari 2007 kutathmini upatikanaji wa fedha za kutekeleza programu hii. Kwa bahati mbaya hadi tarehe hiyo hakuna mfadhili aliyepatikana. Hivyo Mkutano huo uliamua kuwa Serikali ya Tanzania na Malawi kwa pamoja zitenge fedha katika Bajeti za nchi zao kugharimia awamu ya usanifu wa kina wa programu hii. Kwa upande wa Tanzania tayari Waraka wa Baraza la Mawaziri umeandaliwa ili uwasilishwe kwa uamuzi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo kwa matatizo ya mpaka kwenye Mto Songwe, kimsingi hakuna utata mwingine juu ya mpaka huu. Wananchi wanaoishi kandokando ya Ziwa Nyasa wameendelea kutumia maji na rasilimali zingine za Ziwa hilo kwa amani.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana na fasaha. Lakini, pamoja na majibu hayo, nina swali moja dogo la nyongeza. Pamoja na matatizo ya kuhama hama kwa Mto Songwe, pia kuna tatizo la uchoraji wa ramani ambapo nchi ya Malawi inachora mpaka wa Tanzania kwamba uko kando kando ya Bandari ya Kyela,

lakini Kimataifa na Tanzania tunachora ramani ambayo inaonyesha kwamba mpka uko kati kati ya Zia Nyasa.

Je, Serikali inafanya juhudi gani ya kuwaelimisha Wamalawi kwamba mpaka uko kati kati ya Ziwa Nyasa na siyo pembeni mwa Kyela?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, suala hilo la kuhama kwa mpaka na kutoelewa mpaka kamili wa eneo hilo tumelihjadili katika vikao vyote viwili vya mwaka 2006 na 2007. Sasa hivi tunatumia mipaka ambayo inatambulika Kimataifa, ambapo kama nchi mbili zinatenganishwa na Ziwa, mpaka unakuwa kati kati ya lile Ziwa. Kilichobaki ni kuwaelimisha watu wa Malawi ambao kwa kiwango kikubwa sdana mwaka 2007 walielewa suala hilo. Naomba nimtoe wasi wasi Mheshimiwa Mbunge kwamba halina wasi wasi.

**MHE. DR. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii kuuliza swali la nyongeza. Baada ya majibu mazuri ya Mhehimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza; hivi sasa katika nchi yetu zipo ramani nyingi sana zinauzwa hata barabarani na mashuleni ambazo zinaonyesha kwamba mpaka wa Tanzania na Malawi ni kando kando ya ardhi badala ya kati kati ya Ziwa.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kupiga marufuku ramani hizi na ikiwezekana zote zikakusanywa, zikachomwa na katika shule zetu tuwe na zile ambazo zinaonyesha mpaka uko kati kati kama ilivyo Sheria ya Kimataifa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa yote aliyosema tulizipata ramani hizo wakati wa Bajeti yetu mwaka 2006 tukiwa Dodoma na watendaji wote. Tumezikusanya zile ramani na tayari tumekwishatoa taarifa na kupiga marufuku kwa wale wanaohusika kwamba wasifanye tena kitendo hicho. Napenda kuwasilisha. (*Makofi*)

**MHE. DR. HARRISON B. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Spika, nimefarijika sana kusikia kwamba ile *Songwe River Development Program* imeshaanza kutekelezwa kwa mikutano mbalimbali na *DevelopmentParterres* ambayo imefanyika Blantayre mwaka 2006 na mwingine mwaka huu mwanzoni. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kuwa umuhimu sasa katika hiyo mikutano mbalimbali unayoifanya kumhusisha angalau Mbunge wa Kyela katika mikutano ili *ownership* ya *program* ionekane toka mwanzoni? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kuna umuhimu wa kuwahusisha Wabunge katika mikutano yetu na tutazingatia wakati unaofuata kama tutakwenda Malawi tutajaribu kwenda na Mheshimiwa Mbunge, ili aweze kutusaidia katika hoja ambazo zinajitokeza wakati mto unapohamahama. (*Makofi*)

Na. 324

**Mtwara Development Corridor**

**MHE. SULEIMAN OMAR KUMCHAYA** aliuliza:-

Kwa kuwa ni muda mrefu sasa Serikali imekuwa ikizungumzia Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara na wananchi wa Mtwara kwa ujumla wamekuwa wakisubiri kwa hamu kuanza kwa mradi huo:-

(a) Je, mpaka hivi sasa ni miradi mingapi iliyokamilika katika mpango mzima wa *Mtwara Development Corridor?*

(b) Je, miradi ya Ukanda wa Mtwara inao wafadhili kutoka nje na kama wapo ni kutoka nchi gani?

(c) Je, Serikali yetu ina utaratibu wa kutenga fedha kila mwaka wa ajili ya miradi ya ukanda huo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Suleiman Omar Kumchaya, Mbunge wa Lulindi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Tokea kuanzishwa kwa mpango wa kuendeleza ukanda wa Maendeleo wa Mtwara *(Mtwara Development Corridor)* iliyobuniwa mwishoni mwa miaka ya 1990, miradi kadhaa imeshabuniwa. Baada ya miradi mihimili *(anchor projects)* ni kama ifuatavyo:-

(i) Ujenzi wa daraja la umoja kati ya Tanzania na Msumbiji sehemu ya Mtambaswala.

(ii) Ujenzi wa barabara ya Dar es Salaam hadi Mingoyo.

(iii) Mradi wa umeme kutumia gesi asilia ya *Mnazi Bay (Mnazi Bay Gas to power project).*

(iv) Mradi wa gesi asilia wa Songosongo.

(v) Upembuzi yakinifu *(feasibility study)* wa barabara ya Mtwara – Masasi – Songea – *Mbamba Bay.*

(vi) Upembuzi yakinifu wa ujenzi wa njia ya umeme kati ya Mchuchuma na Mufindi *(feasibility study of Mchuchuma – Mufindi Power Transmission line).*

Katika miradi niliyoitaja hapo juu, miradi iliyokamilika inahusisha upembuzi yakinifu wa barabara ya Mtwara – Masasi – Songea – *Mbamba Bay* uliokamilika mwaka 2004, ujenzi wa sehemu ya barabara ya Somanga – Matandu (33 km) uliokamilika mwaka 2005, upembuzi yakinifu wa ujenzi wa njia ya umeme kati ya Mchuchuma na Mufindi uliokamilika mwaka 2004 na mradi wa gesi asilia wa Songosongo.

(a) Mheshimiwa Spika, miradi ya ukanda wa Maendeleo wa Mtwara inao wafadhili kutoka nje ambao ni kama ifuatavyo:-

(i) Serikali ya Afrika ya Kusini ambayo imeshatoa dola za Kimarekani 1,200,000 kwa ajili ya uandaaji wa programu mbalimbali na uendeshaji wa ukanda huu.

*(ii)* *Arab Bank for Economic Development in Africa* ambayo imetoa kiasi cha Dola za Kimarekani 420,000 kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa njia ya umeme kati ya Mchuchuma na Mufindi.

(iii) Mfuko wa *Kuwait Fund* ambao ulitoa kiasi cha Dola za Kimarekani 1,000,000 kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa barabara kutoka Mtara hadi *Mbamba Bay.*

(iv) Serikali ya Japan imegharimia usanifu wa kina wa sehemu ya barabara ya Masasi – Mangaka. Sasa wamekubali kugharamia ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara hiyo kwa gharama ya fedha za Kijapan *(Yen 692* milioni).

Aidha, Serikali ya Tanzania inaendelea na mazungumzo na wafadhili mbalimbali kuhusu usanifu na ujenzi wa barabara sehemu ya Mangaka – Tunduru na ujenzi wa sehemu ya Tunduru – Songea – *Mbamba Bay.*

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali yetu imejiwekea utaratibu wa kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali katika ukanda huu kama kama ifuatayo:-

(i) Ujenzi wa daraja la Umoja: Mradi huu unagharimiwa na Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na nchi ya Msumbiji. Kuanzia mwaka wa fedha 2005/2006 hadi 2007/2008 jumla ya shilingi 14 bilioni zimeshatengwa na Serikali ya Tanzania.

(ii) Barabara ya Masasi – Tunduru - Songea mpaka Mbamba Bay fedha zilizotengwa na Serikali kwa ajili ya shughuli mbalimbali kama vile usanifu na michango ya Serikali kwenye mikataba ya wafadhili ni shilingi 3.67 bilioni kuanzia mwaka 2004/2005 hadi 2007/2008.

(iii) Barabara ya Dar es Salaam – Lindi – Mingoyo: Serikali ya Tanzania imekuwa ikitumia fedha zake za ndani kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Somanga – Matandu na Nangurukuru – Mbwemkulu – Mingoyo na kuchangia miradi inayofadhiliwa na *Kuwait Fund* ya Mkuranga – Kibiti – Ndundu – Somanga.

Fedha zilizotengwa na Serikali kwa ajili ya miradi yote hii kuanzia mwaka wa fedha 2002/2003 hadi 2007/2008 ni jumla ya shilingi 166.072 bilioni.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008 Serikali kupitia Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko pia imetenga kiasi cha shilingi 523,000,000 kwa ajili ya maandalizi ya utekelezaji wa miradi ya makaa ya mawe ya Mchuchuma na Chuma cha Liganga.

**MHE. SULEIMAN OMAR KUMCHAYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya kutia matumaini ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza swali kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa huko nyuma kulikuwa na reli kutoka Mtwara mpaka Nachingwea, ile reli ikang'olewa na sasa hivi kuna mradi wa *Mtwara Corridor*. Je, Serikali haioni kwamba sasa ni wakati muafaka wa kufikiria kurudisha reli ile kutoka Mtwara mpaka *Mbamba Bay* mpaka Mchuchuma ili kurahisisha uchukuaji wa mkaa wa mawe na chuma cha Mchuchuma? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kulikuwa na reli hiyo kati ya Mtwara na Nachingwea ambayo iling'olewa. Katika mpango huu wa *Mtwara Corridor* inafikiriwa kujengwa reli nyingine ambayo itapita maeneo hayo mpaka kwenye mkaa wa mawe wa mchuchuma.

Bado Serikali inatafakari ni namna gani ujenzi huo unaweza kufanyika kwa maana ya kupata ufadhili kutoka wapi na mambo yatakapokamilika ipo katika mpango lakini kwa sasa ni hiyo miradi ambayo tayari imeshaanza niliyoitaja ambayo ndiyo itakuwa ya kwanza. (*Makofi*)

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara ya Miundombinu ambayo ndiyo Mwenyekiti wa Utekelezaji wa Mpango huu wa *Mtwara Corridor* inavyoelekea imezidiwa na kazi hasa za ujenzi wa barabara. Je, kwa nini Serikali isifikirie kuhamisha Unyekiti huo kwa Wizara mmoja mtambuka kama ya Waziri Mkuu au Mipango au Ofisi ya Makamu wa Rais, ili kwamba mipango mingine inayohusiana na utalii, umwagiliaji n.k. iweze kutekelezwa kwa urahisi na bila kukwama kama ilivyo sasa sasa hivi kwa miradi hiyo mipya? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, kwa sasa uamuzi wa Baraza la Mawaziri ni kwamba Wizara ya Miundombinu ndiyo *Champion Ministry* ambayo inasimamia shughuli zote hizi za Mtwara *Development Corridor.* Mpaka sasa kwa kweli Wizara hii haijashindwa

kuendelea ku-*champion* shughuli hizi. Kama kutakuwa na mabadiliko yoyote basi tutajulishwa. (*Makofi*)

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika maelezo yake Naibu Waziri ya miradi ndani ya Mtwara *Corridor* ametaja na gesi asilia ya songosongo ambayo matumizi yake yako kwenye *grid* ya Taifa ya Dar es Salaam na siyo sehemu ya ukanda wa Mtwara. Je, anatuambia nini juu ya kufikisha gesi hiyo asilia walau katika Wilaya ya Kilwa ili Ukanda wa Mtwara uweze kufaidika na gesi hiyo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kwa kuanzia gesi ya songosongo inakwenda mpaka Dar es Salaam. Lakini vile vile kwa ukanda wa Mtwara tunaelewa kwamba kuna *Mnazi Bay* ambayo tayari italeta umeme maeneo hayo lakini bado Serikali imekuwa ikiangalia kwamba mradi huu wa songosongo ni namna gani unaweza kufaidi maeneo ambapo inapitia kutoka huko Kusini ikiwemo pamoja na Kilwa. Kwa sababu miradi yote hii inaendelea kushughulikiwa mimi naamini kabisa kwamba Serikali itazingatia umuhimu wa kupatikana kwa gesi hiyo, maeneo ya Kilwa na maeneo yote ya kule Kusini.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa sijamwona Mheshimiwa Mpanda na si mara nyingi sana anauliza. Kwa hiyo, naomba nimpe nafasi. *(Makofi)*

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa huu mradi wa *Mtwara Corridor* umeingia mpaka Songosongo mpaka huku Rufiji naomba niulize swali moja. Je, Barabara kutoka Ndundu mpaka Somanga mradi wake uko kwenye hali gani? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mradi wa Barabara wa Ndundu mpaka Somanga km 60 mwezi huu ujao ambao unaanza kesho tutawekeana mikataba na yule mkandarasi aliyekuwa ameshinda na baada ya miezi michache kabla ya mwisho wa mwaka huu tunategemea kuona barabara ile ikianza kujengwa na itakamilika kabla ya mwisho wa mwaka 2010. (*Makofi*)

Na. 325

**Ubinafsishaji wa Shirika la Ndege Tanzania (ATCL)**

**MHE. LUCAS L. SELELII** aliuliza:-

Kwa kuwa Shirika la Ndege Tanzania *ATCL*) lilibinafsishwa kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi wake na kwa kuwa hali ya Shirika hilo limedorora kinyume na matarajio ya Serikali:-

Je, Serikali ina mpango gani wa makusudi wa kuliokoa shirika hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii, Mbunge wa Nzega, kama ifuatavyo:-

Baada ya ubia kati ya Shirika la Ndege la Tanzania na Shirika la Ndege la Afrika ya Kusini kuvunjika rasmi tarehe 29 Agosti 2006, pamoja na mambo mengine Serikali imechukua hatua zifuatazo ili kufufua kampuni ya ndege ya Tanzania:-

(a) Katika mwaka wa fedha 2006/2007 Serikali ilitenga fedha kiasi cha shilingi bilioni 13 kwa ajili ya kuwezesha kampuni kuandaa na kukamilisha mifumo muhimu ya kampuni ambayo itaiwezesha *ATCL* kusimama yenyewe bila kuendelea kuitegemea Shirika la Ndege la Afrika Kusini. Mifumo hiyo ni pamoja na matumizi ya *code* ya *ATCL* ambayo ni 197 badala ya kutumia *code* 083 ya Afrika Kusini, kubadilisha mfumo wa mapato ya kampuni *(Revenue Accounting),* huduma za mafuta kujiandaa kwa tiketi za elekroniki, mfumo wa mahesabu ya kampuni, maandalizi ya nembo mpya ya kampuni pamoja na kulipa madeni mbalimbali ya kampuni.

(b)Mheshimiwa Spika, mwezi Februari 2007, Serikali iliteua bodi mpya pamoja na Mkurugenzi Mtendaji mpya wa kampuni. Kazi kubwa ya Bodi pamoja na uongozi ni kuweka mikakati ya kuifufua *Air Tanzania* kwa kuandaa mpango wa kibiashara ambao utawezesha kampuni kuboresha huduma na kuongeza mtandao wake ndani na nje ya nchi. Bodi na Menejimenti pia itachukua hatua ambazo zitawezesha *Air Tanzania* kuacha kupata hasara na kuanza kupata faida kwa kuangalia mtandao wa njia zake za sasa na aina ya ndege za kutumia ambazo zinakuwa na tija.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hivi sasa tuna juhudi za kufufua uchumi na hasa katika kuinua sekta ya utalii na kwa kuwa Shirika la Ndege *(Air Tanzania)* linahitaji kupanua mbawa zake mpaka ambako watalii walio wengi wanatoka ili waje moja kwa moja kule wanakotoka Marekani, China na Ulaya waje moja kwa moja kwenye vivutio vyetu vya utalii.

(a) Je, katika hizi juhudi za Serikali ni lini italipatia shirika hili la ndege, ndege kubwa za kuwawezesha watalii wanaopenda kuja Tanzania wakaja kuona vivutio vyetu? (*Makofi*)

(b) Kwa kuwa wakati wa mchakato wa kulibinafsisha Shirika la Ndege na *SAA* walichukua kiwanda cha kutengeneza ndege, hanga ya kutengeneza ndege iliyoko *Kilimanjaro Airport (KIA).* Wakapeleka vitu vyote kwao kule South Afrika na kiwanda hicho sasa hivi hakina hata kitu kimoja ambacho kimesalia. Je, katika madeni wao hatuwezi tukawadai wakarudisha hivyo vitu walivyovichukua na inawezekana walichukua kwa kuviiba? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Lucas Selelii, kwamba katika

kufufua shirika la ndege la *Air Tanzania. Air Tanzania* imepanga kununua ndege zake zenyewe na zitaongeza *route* za ndani na za nje lengo ni kuhakikisha kwamba tunaboresha uchukuzi na usafiri kwa njia ya anga na kupata abiria wa kutosha kuweza kuchangia uchumi wa nchi. Kwa hiyo, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hilo la ndege linazingatia. Suala la Hanga hivi ninavyozungumza watendaji na mkurugenzi mkuu wa shirika la *Air Tanzania* yuko Kilimanjaro kufanya uhakiki wa mambo yanavyokwenda. Kama hayo anazungumza ni ya kweli basi hatua zifaazo zitachukuliwa. (*Makofi*)

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake sahihi katika swali la msingi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hivi sasa Shirika la Ndege la Tanzania limekabidhiwa mambo yote ya kuendesha shughuli za ndege hapa Tanzania na kwa kuwa hivi sasa asilimia 100 ya *share* inakwenda Serikalini. Lakini mwelekeo ni kuziuza *share* hizo kwa wananchi hadi kufikia asilimia 70 kwa wananchi na asilimia 30 kubakia Serikalini. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba sasa umeshafika wakati ili kuipa nguvu *Air Tanzania,* kile kitengo cha uegeshaji wa magari katika Kilimanjaro na Dar es Salaam kikaenda moja kwa moja katika shirika hili?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, kama alikusudia ni kile kitengo ambacho kinashughulikia uingiaji na utokaji wa magari katika viwanda vya ndege hivi kile kitengo kiko *out sorted* kama nimempata. Lakini kama ni kitengo kingine cha magari ambacho mimi sikielewi labda nimpate Mheshimiwa Hafidh anieleze vizuri zaidi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Sasa ni zamu ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba, namshukuru Waziri jana amefafanua vizuri sana. Tutaanza kulitumia jina la Katiba na Sheria mpaka *GN* itakapobadilishwa.

Na. 326

**Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

**MHE. OMAR SHABANI KWAANGW'** aliuliza:

Kwa kuwa, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, imekuwa ikitembelea Magereza na vituo vya Polisi nchini ili kuona kama Haki za Binadamu na Misingi ya Utawala Bora inaheshimiwa na kulindwa:-

(a) Je, ni malalamiko yapi ya msingi yaliyojitokeza kutoka kwa wafungwa na mahabusu kutoka sehemu mbalimbali za nchi?

(b) Je, Serikali inasema nini kuhusu hali ya Wilaya ya Babati na Mkoa wa Manyara kwa ujumla?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omar S. Kwaangw' Mbunge wa Babati Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imeweza kutembelea Magereza 120, Kambi za Magereza 18 na Vituo vya Polisi 192 kwa upande wa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, katika kutembelea wafungwa na mahabusu malalamiko ya msingi yaliyopokelewa ni kama ifuatavyo:-

(i) Ucheleweshwaji wa nakala za mienendo ya kesi na hukumu kutoka Mahakamani;

(ii) Kesi za mauaji kutosikilizwa mapema;

(iii) Kuchelewa kusikilizwa kwa rufaa;

(iv) Kubambikizwa kesi;

(v) Kucheleweshwa kwa upelelezi wa kesi hususani za mauaji;

(vi) Hati ya kufuta mashataka kutowasilishwa mapema Mahakamani;

(vii) Msongamano wa Wafungwa na Mahabusu;

(viii) Ucheleweshwaji wa majibu ya vielelezo kutoka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali; na

(ix) Uchakavu wa majengo ya Magereza.

(b) Mheshimiwa Spika, mwaka 2003 na mwaka 2006 Tume iliweza kutembelea Mkoa wa Manyara na kukagua Gereza la Wilaya ya Babati na Mbulu.

Mheshimiwa Spika, yaliyojitokeza katika ukaguzi wa Magereza Mkoani Manyara kwa kiasi kikubwa yanafanana na yale yaliyo katika Magereza mengine nchini kama nilivyoeleza hapo juu. Nyongeza ni kuwa Gereza la Babati, walilalamika kuhusu uchakavu wa majengo maana yaliyojengwa tangu enzi za mkoloni. Aidha, Askari Magereza wa Babati walilalamikia ucheleweshaji wa posho na stahili zao. Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kupitia Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara yangu kuwa kushirikiana na Wizara aya Usalama wa Raia na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi tunayafahamu matatizo hayo na tumekuwa tukichukua hatua mbalimbali katika kutatua matatizo ya mahabusu na wafungwa walio katika Magereza ya Mkoa wa Manyara na nchi nzima kwa ujumla. *(Makofi)*

**MHE. OMAR SHABANI KWAANGW':** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nitumie nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kukiri kwamba kuna uchakavu wa majengo kwenye Gereza la Babati kwa kukiri vile vile kwamba askari wa magereza ya Babati wana matatizo na vile vile kusikiliza na malalamiko ya wafungwa pamoja na mahabusu. Kwa kuwa kuna tatizo kubwa sana la wananchi kutokujua haki zao na pili kwa kutokuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu haki zao. Je, Serikali ina mikakati gani ya kutosha kuhakikisha kwamba wananchi wanafahamishwa vya kutosha kuhusu kazi za Tume ya Haki za Binadamu na utawala bora? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ina mikakati ya kutoa elimu kwa umma ili umma upate kuelewa kazi za Tume na katika utaratibu huo inatumia vipindi vya *radio* na tume ya vipindi vya *television*. Kila wanapofanya ukaguzi katika Mikoa wanachukua nafasi pia kuelimisha wananchi kuhusu kazi za tume.

Vile vile yapo mashirika yasiyo ya Kiserikali ambayo yamekuwa yakitoa elimu kwa umma hasa kuhusu haki za binadamu, mashirika hayo ni kama *Legal Human Right Centre*, na mengineyo ambayo yamekuwa yakisaidia kuwapa elimu wananchi kuhusu haki zao na kazi za Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. *(Makofi)*

Na. 327

**Miradi Iliosimamiwa na Umoja wa Ulaya**

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA** aliuliza:-

Kwa kuwa, kabla ya kurekebisha makubaliano ya *COTONOU*, Umoja wa Ulaya (*EU*) ulikuwa unasimamia mikataba ya miradi mmoja mmoja;-

(a) Je, ni miradi mingapi na ipi iliyosimamiwa na *EU* ?

(b) Je, ni miradi mingapi iliyokamilika na mingapi ambayo haikukamilika na nini sababu za kutokamilika?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamza Abdallah Mwenegoha, Mbunge wa Morogoro Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo :-

(a) Mheshimiwa Spika, jumla ya miradi 6 ilipangwa kutelekezwa chini ya mipango ya maendeleo ya nane na tisa *(EDF 8 NA EDF 9)*. Kwa mujibu wa makubaliano kati ya Jumuiya ya Ulaya (*EU*) na nchi za Afrika, *Caribbean* na *pacific* (*ACP*), Miradi yote ya *EDF* inasimamiwa kwa pamoja na *EU* na Serikali ya Tanzania, kila moja ikiwa na majukumu yake katika kufanikisha utekelezaji wa mradi husika.

(b) Mheshimiwa Spika, jumla ya miradi 52 imekamilika na 5 ipo katika hatua za mwisho za kukamilika ambapo miradi mingine 11 ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Orodha kamili ya mriadi yote ya *EDF* 8 na *EDF* 9 kwa majina, mahali ilipo na hatua iliyofikiwa ya utekelezaji ni ndefu, nitampatia Mheshimiwa Hamza Abdalaah Mwenegoha wakati wote atakapohitaji.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali na *EU* inashirikiana kusimamia miradi hii na naamini miradi hii inaibuliwa na Serikali, sasa katika miradi hiyo ama *EDF* 10 ikitokea Mheshimiwa Waziri yuko tayari sasa kuweka mradi wa umeme vijijini katika Morogoro Vijijini ili vijiji ya Matombo, Mbuha, Kisaki viweze kupata mradi huo ili Morogoro Vijijini ipate umeme? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Spika, *country strategy* imeshapelekwa *European Union* na sasa hivi wakati wowote inaweza ikaidhinishwa na ikaanza kutumika. Imepangwa kutumika kati ya mwaka 2008 mpaka 2013.

Miradi inayokusudiwa kutekelezwa katika *EDF* 10 imeshaainishwa na Serikali. Kama mradi wa *Rural Energy* kwa Matombo umo, nitamhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mradi huo utatekelezwa ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na tunakaribia kufikia muda mwisho wa kipindi cha maswali. Matangazo tunaanza na wageni. Wageni wetu Bungeni leo ni kwanza Ndugu Amos Kishimba, mgeni wa Mheshimiwa Anthony Diallo, huyu ni Katibu wa CCM Wilaya ya Ilemela, Mwanza. Yule pale karibu sana Katibu. (*Makofi*)

Wengine ni kama ifuatavyo: wanafunzi nadhani na walimu wa shule ya sekondari Kikuyu Dodoma. Ahsanteni sana karibuni sana Bungeni. Tunafurahi sana mnapokuja kuona jinsi Bunge linavyofanya kazi. Ahsante sana walimu kwa kazi hiyo.

Pia tunao wanafunzi wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Ardhi Dar es Salaam, sijui wako upande gani naomba wasimame naona hawapo. Wanafunzi wa shule ya Msingi Kizota Dodoma naomba wasimame na walimu wale pale nadhifu kabisa na sare nzuri. Ahsante sana karibuni sana walimu na wanafunzi wa shule ya msingi Kizota, ninyi mna kila haki mko karibu hapa ni vizuri kuja kuona Bunge linavyofanyakazi kuliko kusoma tu katika karatasi. Ahsanteni.

Vikao, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi anawaomba Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi, wakutane leo saa 4.30 asubuhi katika ukumbi namba 231.

Halafu Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, anaomba Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati ya Mambo ya Nje wakutane saa 5 asubuhi chumba Na. 133. Kamati ya Mambo ya Nje saa tano Ukumbi Na. 133.

Mheshimiwa Haroub Masoud, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, anatoa wito kwa Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii kukutana saa 7 mchana, Ukumbi Na. 231 gorofa ya pili. Kwa hiyo, Kamati ya Maendeleo ya Jamii saa 7 mchana Ukumbi Na. 231. Ahsante. *(Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2007/2008
### Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa mapema leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bunge, likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote najiunga na wenzangu kuzipa pole familia za wenzetu Marehemu Mheshimiwa Juma Jamaldini Akukweti na Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia, waliotutangulia mbele ya haki mwaka uliopita. Naungana na familia kumwomba Mola awape raha ya milele na wapumzike kwa amani. Amen.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Waheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango Uchumi na Uwezeshaji kwa hotuba zao nzuri ambazo kwa pamoja zilitoa mwelekeo wa Bajeti ya Serikali na hali ya uchumi na maendeleo kwa ujumla. Kwa hiyo hotuba yangu ni ya ufafanuzi wa Makadirio na Matumizi yanayohusu Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza kwa madaraka mapya waliyopewa Waheshimiwa Dr. Asha Rose Mtengeti Migiro, Mheshimiwa Bernard Kamillius Membe, Mheshimiwa Dr. Batilda Salha Buriani, Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo, Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura na Mheshimiwa Florence Essa Kyendesya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wote wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bunge chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa William Kusila, Mbunge mashuhuri wa Bahi, na Naibu wake Mheshimiwa Kapteni John Mkuchika, Mbunge wa Newala, kwa kuyachambua na kuyapitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi pamoja na ushauri wao katika masuala mbalimbali ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Wajumbe wa Kamati hiyo wanao uzoefu mkubwa wa mambo ya Ulinzi na Usalama na Serikali kwa ujumla. Wamekuwa ni msaada mkubwa kwangu niliye mpya katika sekta hii na kwa hiyo nawashukuru san asana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali ya usalama nchini, jukumu la msingi la Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ni kuchangia katika kudumisha usalama na amani nchini kupitia vyombo vyake vya Idara za: Magereza, Uhamiaji, Wakimbizi na Zimamoto na

Uokoaji. Kwa ujumla Mheshimiwa Spika, hadi sasa nchi yetu imeendelea kuwa na amani na usalama isipokuwa kwa matukio madogo madogo kama lile la mgomo wa baadhi ya mahabusu ambalo limeisha waliokataa kushuka kwenye magari ili kuhudhuria kesi zao Mahakamani. Kwa kufuata sheria zilizopo, suala hili la migomo ya mahabusu sasa limekwisha. Mahabusu kugoma kwenda mahakamani ni kosa la jinai na wamefahamishwa wazi kuwa mahabusu atakayegoma tena atahukumiwa kwanza papo kwa papo kwa kosa hilo na kubadilika kuwa mfungwa wakati kesi yake ya awali bado inaendelea.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa tathmini ya utekelezaji ya mwaka jana na matarajio ya mwaka 2007/2008, sasa naomba kutoa tathmini ya utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2006/2007, na kuelezea matarajio yetu kwa mwaka wa fedha ujao 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, mapato ya mwaka 2006/2007 katika mwaka wa fedha 2006/2007 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ilipangiwa kukusanya maduhuli ya Serikali ya jumla ya Shilingi Bilioni 11.5. Mpaka kufikia Aprili, 2007 ilikusanya Shilingi Bilioni 9.1 ambazo ni asilimia 79 ya lengo. Tunategemea kukamilisha lengo au kulivuka mahesabu yetu yatakapofungwa rasmi tarehe 30 Juni 2007.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya mwaka 2006/2007 matumizi ya mwaka mwaka wa fedha 2006/2007 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 53.9 Bilioni kwa ajili ya matumizi mengineyo *(Other Charges - OC).* Mpaka Aprili 2007 zilikuwa zimetumika Shilingi Bilioni 38.9, sawa na asilimia 72. Bajeti ya Mishahara ilikuwa Shilingi Bilioni 29.4; na hadi Aprili 2007 zilitumika Shilingi Bilioni 26.1, sawa na asilimia 89.

Mhesimiwa Spika, Bajeti ya Maendeleo ilikuwa Shilingi Bilioni 12.9 na mpaka Aprili 2007 zilitumika Shilingi Bilioni 4.6, sawa na asilimia 36. Ukiritimba wa Zabuni ni miongoni mwa vikwazo vinavyopunguza kasi ya matumizi kwenye fedha za Maendeleo. Aidha, sehemu ya fedha za maendeleo iliyopangwa kwa ajili ya udhibiti wa UKIMWI zilichelewa kutolewa.

Mheshimiwa Spika, Muundo wa Wizara una Idara Sita (6) zikiwemo mbili (2) za huduma za kiujumla na nne (4) za kiutendaji wa majukumu maalumu. Idara za huduma za kiujumla ni: Idara ya Utawala na Rasilimali Watu na Idara ya Sera na Mipango. Idara hizi mbili hutoa huduma zao kwa Idara nyingine zote na Wizara kwa ujumla. Idara za kiutendaji wa majukumu maalumu ni: Idara ya Magereza; Idara ya Zimamoto na Uokoaji; Idara ya Uhamiaji na Idara ya Wakimbizi. Baada ya maelezo ya kiujumla ya utekelezaji wa Bajeti niliyoyatoa awali, sasa ifuatayo ni taarifa kwa kila Idara ya kiutendaji wa majukumu maalumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Idara ya Magereza, jukumu la Jeshi la Magereza ni kuwahifadhi Magerezani wahalifu wa aina zote pamoja na kurekebisha tabia zao wakati

wanatumikia adhabu za vifungo. Kazi hizi zimeendelea kuendeshwa na kutekelezwa vizuri kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, urekebishaji wa tabia za wafungwa ili wamalizapo vifungo vyao wawe raia wema katika jamii hufanywa kupitia programu za mafunzo kwa njia ya vitendo katika miradi ya kilimo na viwanda vidogo vidogo; na mafunzo ya nadharia katika Vyuo vya Magereza vya Ruanda-Mbeya, na Vijana Wami, pamoja na utoaji ushauri nasaha kwa kutumia Walimu wa Dini na Maafisa Ustawi wa Jamii. Hata hivyo Mheshimiwa Spika, jukumu hilo limeendelea kutekelezwa katika mazingira magumu kutokana na ufinyu wa bajeti ya kuendesha chombo hiki muhimu cha huduma ya marekebisho ya tabia *(correctional service).*

Msongamano wa wafungwa na mahabusu magerezani, tatizo la msongamano wa Wafungwa na Mahabusu bado lipo ingawa upo unafuu kidogo. Jumla ya Mahabusu na Wafungwa *(inmates*) Magerezani wamepungua kutoka 44,565 walivyokuwa tarehe 1 Juni 2006 hadi 39,432 tarehe 1 Juni 2007. Kati ya hao 39,432; Wafungwa ni 20, 410 na Mahabusu ni 18,759. Tatizo la idadi kubwa mno ya mahabusu magerezani bado ni sugu. Uwiano wa mahabusu kwa wafungwa umeongezeka kutoka mahabusu 42.6 kwa kila wafungwa 100 mwaka 1990 hadi mahabusu 89.3 kwa kila wafungwa 100 mwaka 2007 na hiyo inaonyeshwa na inaonekana wazi kuwa sehemu kubwa ya msongamano inatokana na wingi wa mahabusu usio wa kawaida

Mheshimiwa Spika, msongamano unaotokana na Sheria, sehemu ya msongamano Magerezani inatokana na baadhi ya Sheria kama vile: Sheria zinazotoa adhabu ya kima cha chini *(minimum sentences)* ya kifungo kirefu kama vile miaka 30 kwa makosa ya kujamiiana na makosa ya wizi kwa kutumia silaha. Wafungwa wa aina hii hawajawahi kutoka magerezani tangu Sheria hizo anza kutekelezwa;

Sheria zinazotoa adhabu ya kima cha chini *(minimum sentence)* bila kujali ukubwa wa kosa kwa mfano katika Sheria ya wizi wa mifugo adhabu inayotolewa ya kima cha chini ni miaka mitano (5) bila kujali wingi wa mifugo iliyoibiwa. Kwa hiyo ni kawaida kuwakuta gerezani mwizi wa mbuzi mmoja (1); na wa mbuzi ishirini (20), au wa ng'ombe thelathini (30) wote wamehukumiwa miaka mitano (5).

Mheshimiwa Spika, hatua za kupunguza msongamano magerezani, njia mojawapo tunayotumia katika kupunguza msongamano Magerezani ni kujenga mabweni mapya na kukamilisha ujenzi wa viporo. Katika jitihada hizo, tumeweza kuongeza nafasi za kuhifadhi Wafungwa na Mahabusu kutoka 22,699 hadi kufikia 27,653. Njia ingine ni utekelezaji wa Sheria ya Bodi za *Parole* Na. 25/1994 iliyofanyiwa marekebisho kwa Sheria Na. 5 ya 2002, Wafungwa 2,651 waliachiliwa kwa *Parole* tangu tarehe 19 Agosti, 1999 utekelezaji ulipoanza. Tatizo lililopo ni ufinyu wa wigo unaoruhusu wafungwa kuachiliwa kwa Parole kwa mujibu wa Sheria iliyopo. Hata hivyo Januari, 2007 nilikutana na Bodi ya Taifa ya *Parole* ili kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais la kuimarisha mfumo wa *Parole* nchini ili wafungwa wengi zaidi waweze kufaidika na utaratibu huo. Natarajia mwaka huu kuliomba Bunge lifanye marekebisho ya Sheria husika ili kuongeza wigo wa *Parole.*

Mheshimiwa Spika, msamaha wa Rais, katika hatua nyingine ya kupunguza msongamano wa wafungwa magerezani ni ya Msamaha wa Rais. Kwa njia hii Kamishna Mkuu wa Magereza kupitia Wizara humshauri Mheshimiwa Rais kutoa msamaha kwa Wafungwa wenye tabia njema na waliorekebishika tabia zao. Katika mwaka wa fedha uliopita jumla ya wafungwa 8,686 waliachiliwa kwa msamaha wa Rais wakiwemo:-

Wafungwa 4,664 waliopewa msamaha wa Rais tarehe 09/12/2006 siku ya sherehe ya miaka 45 ya Uhuru wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Wafungwa wengine 4,022 waliopewa msamaha wa Rais tarehe 26 Aprili 2007, siku ya kilele cha sherehe za miaka 43 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kifungo cha nje, hatua nyingine ya kupunguza msongamano ni kutumia Kifungo cha Nje, kwa mujibu wa Sheria ya Magereza Namba 34 ya mwaka 1967 *(Prisons Act,No.34 of 1967).* Wafungwa wanaostahili uwezekano wa kupewa kifungo cha nje ni wale wa kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili (12). Hata hivyo utaratibu huu unashindwa kutekelezwa katika baadhi ya Wilaya kwa kuwa Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji wanadai hawana fedha za kuwahudumia. Kuanzia tarehe 1 Julai, 2006 hadi tarehe 1 Aprili, 2007 wafungwa wapatao 931 walikuwa wameachiwa na kupewa kifungo cha nje kwa mujibu wa kifungu cha 72 cha Sheria ya Magereza ya mwaka 1967

Mheshimiwa Spika, njia nyingine za kupunguza msongamano, njia zingine zifuatazo zinaweza kuchangia kupunguza msongamano Magerezani: Wahalifu wengine kupewa adhabu zisizo kifungo *(non-custodial sentences)* kama vile za faini, viboko, na fidia kwa mhalifu badala ya kuzingatia adhabu za vifungo *(Custodial Sentences)* peke yake. Washitakiwa wenye familia zenye mke na watoto kupewa mdhamana bila masharti magumu kwa sababu siyo rahisi kutoroka na kuzikimbia familia zao.Watuhumiwa wenye nyumba na ajira ya kudumu kupewa mdhamana bila masharti magumu kwa sababu nao siyo rahisi kutoroka kuacha nyumba na ajira ya kudumu.Mahabusu kuachiwa baada ya siku sitini *(sixty days rule)* kama upande wa mashtaka haujawa tayari kuendelea na kesi.Kila inapowezekana mtuhumiwa kukamatwa baada ya upelelezi kukamilika ili kesi isikilizwe upesi.Kuharakisha utaratibu wa kutenganisha upelelezi na uendeshaji wa mashtaka mahakamani ili kuwapunguzia Polisi kazi na hivyo kubakiwa na jukumu la upelelezi peke yake.

Mheshimiwa Spika, kuimarisha programu za urekebishaji wa wafungwa. Programu za urekebishaji wafungwa zimeendelea kutekelezwa kama nilivyoahidi katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka wa fedha 2006/2007. Katika kuboresha kilimo, mifugo na uboreshaji wa mazingira Magerezani, Serikali imeendelea kuchukua hatua za makusudi za kuendeleza mashamba ya Magereza kwa kununua matrekta mapya na kukarabati ya zamani.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Magereza limeweza kuboresha mazingira ambapo mwaka 2006 ilipandwa miti 650,000 na kuanzia Januari hadi Mei, 2007, imepandwa miti 1,200,000 katika maeneo mbalimbali nchini. Kwa upande wa kilimo cha umwagiliaji, kazi ya ukarabati wa bwawa la kumwagilia mpunga Gereza Mang'ola (Wilayani Karatu) kwa ufadhili wa *Tanzania /Japan Food Aid Fund* kupitia Wizara ya Kilimo Chakula

na Ushirika inaendelea vizuri. Aidha Jeshi la Magereza kwa kushirikiana na Wizara hiyo linaendelea na mpango wa uzalishaji wa vipande vya mihogo yenye kinga dhidi ya ugonjwa wa batobato katika Magereza ya Kiabakari, Ushora, Kitengule, Butundwe, Handeni, Namajani, Lilungu, Nachingwea, Liwale, Kibiti, Mvuti, Kigongoni, Kanegele, Idete, Malya, Msalato, Mahabusu Urambo, Ilagala, Kibondo, na Kasungamile. Vipande hivyo ni Mbegu ambazo pia huuzwa kwa bei nafuu kwa wananchi wanaoishi jirani na makambi ya Magereza hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mifugo, uchimbaji wa mabwawa manne ya kunywea maji mifugo umekamilika katika Gereza Ubena. Katika kuboresha lishe kwa mifugo uanzishaji wa mashamba ya nyasi bora za mifugo *(improved pasture farms)* umefanyika katika Magereza Kigongoni (Wilayani Bagamoyo), Mbigiri na Gereza Mtego wa Simba (Wilayani Morogoro). Aidha, ujenzi wa majosho manne (4) unaendelea katika Magereza ya Ushora, Malya, Wazo Hill na Kambi Kimbiji pamoja na ukarabati wa majosho katika Magereza Arusha, Mollo na Kitai. Pia, pembejeo mbalimbali za kilimo na mifugo zimenunuliwa na kusambazwa kwenye vituo husika.

Mheshimiwa Spika, viwanda vidogo vidogo *Small Scale Industries)* katika kuimarisha viwanda vidogo vidogo Magerezani zimenunuliwa mashine mpya kwa ajili Viwanda vya Uhunzi Ukonga (Jijini DSM) na Viatu Karanga (Manispaa ya Moshi). Ufungaji wa mashine hizo unaendelea katika viwanda hivyo. Mafunzo ya ufundi kwa askari na wafungwa yanaendelea katika Chuo cha Ufundi Mbeya; ambapo masomo yanayofundishwa ni uashi, useremala, ufundi bomba, ufundi umeme na kupaka rangi. Mafunzo haya yanakusudia kuboresha utendaji kazi kwa kwenye miradi yetu ya maendeleo na shughuli mbalimbali Magerezani na hivyo kutekeleza kwa nadharia na vitendo Sera ya Urekebishaji wa Wafungwa.

Mheshimiwa Spika, miradi iliyotekelezwa mwaka 2006/2007 miradi ya Jeshi la Magereza iliyotekelezwa mwaka wa fedha 2006/2007 ni ile inayolenga kuimarisha utawala na kuboresha utendaji katika maeneo ambayo yamekuwa ni kero kubwa katika uendeshaji wa magereza nchini kwa muda mrefu. Miradi hiyo ni :-

(a) Uimarishaji wa Magereza Makongwe yenye Ulinzi Mkali *(Central Prisons)* Mheshimiwa Spika, kazi ya kukarabati na kuboresha majengo na miundo mbinu ya Magereza yenye Ulinzi Mkali imeendelea katika Magereza ya Ukonga - Dar es Salaam, Isanga - Dodoma, Lilungu -Mtwara, Uyui - Tabora, Maweni - Tanga, Keko – Dar es Salaam na Lindi.

(b) Mheshimiwa Spika, upanuaji wa mabweni ya wafungwa na mahabusu kama nilivyoahidi katika Hotuba ya Bajeti ya mwaka 2006/2007, kazi ya upanuaji na ukarabati imetekelezwa katika Magereza ya Kahama, Bangwe, Njombe, Mahabusu Morogoro, Mahabusu Iringa na Arusha. Aidha, ukamilishaji na ukarabati wa majengo ya Magereza umeendelea kama ilivyopangwa katika Magereza ya Shinyanga, Kayanga, Singida, Kiberege, Kingolwira, Matongo, Kihonda, Kibondo, Kwitanga, Mang'ola -, Maswa, Masasi na Loliondo. Utekelezaji katika Magereza hayo umefikia katika viwango mbalimbali.

(c) Ukamilishaji, Ukarabati na Ujenzi wa Nyumba za Askari, kazi ya kukamilisha, kukarabati na kujenga nyumba za askari imeendelea kutekelezwa katika Vituo vya Mpwapwa, Muleba, Arusha, Chuo Ukonga, Chuo Kiwira, Gereza Keko, Morogoro, Mahabusu Iringa, Kambi Kimbiji na Ruanda Mbeya.

(d) Uimarishaji wa Mifumo ya Maji Safi na Maji Taka Mheshimiwa Spika, Magereza mengi yaliyo mijini yanakabiliwa na tatizo kubwa la ukosefu wa maji na uchakavu wa miundo mbinu ya maji safi na maji taka ambayo pia inaelemewa na tatizo kubwa la msongamano wa wafungwa. Katika jitihada za kuhakikisha kuwa kero ya maji safi zinapunguzwa magerezani na makambini, Jeshi la magereza limeendelea kuimarisha mifumo ya maji safi kwa kuchimba visima virefu katika magereza ya Kambi Kimbiji, KMKGM, Kambi Singa, Segerea, Wami Vijana, Mbozi, Chuo Ukonga, Manyoni na Kambi Chikuyu – Manyoni. Pia mifumo mipya ya maji taka inajengwa katika magereza ya Sumbawanga, Mbozi, Mvuti, Urambo na Kitai. Aidha, mifumo ya maji taka inakarabatiwa katika Magereza ya Mahabusu Tanga, Bukoba, Lindi, Lushoto, Bangwe na Tarime.(f)Uimarishaji wa Mashamba ya Magereza Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007, Jeshi la Magereza liliendeleza juhudi za kuimarisha mashamba ya kilimo na mifugo kwa kufanya yafuatayo:-Kununua matrekta mapya matano (5) na pembejeo kwa ajili ya kuongeza uzalishaji;Kukarabati matrekta kumi (10) ya zamani na kuyapeleka kwenye Magereza ya Isupilo, Kitai, Mafia (Kambi Kilombelo), Mollo, Wazo, Kimbiji, Kigongoni (matrekta 2), Mang'olala na Karanga;Kuchimba mabwawa manne (4) ya kunywea maji mifugo Gereza Ubena; na. Kuboresha mashamba na afya ya mifugo kwa kupanda aina maalum ya nyasi katika Magereza ya Mtego wa Simba, Mbigiri, na Kigongoni pamoja na kununua zana za kuvunia nyasi hizo.

(f) Ufufuaji wa Viwanda Vidogo Vidogo vya MagerezaMheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007, mashine mbalimbali na vitendea kazi vingine katika viwanda vya viatu Karanga Moshi na karakana Ukonga vimenunuliwa na sasa vinafungwa. Aidha, ukarabati umefanywa katika kiwanda cha Henzerani - Ukonga na mashine ya korona - Kihonda. Pia mashine ya kuvuta maji kwa ajili ya kiwanda cha Chumvi – Machole - Lindi imenunuliwa. Hizo ni hatua na azma ya urekebishaji wa wafungwa ili wanapomaliza adhabu zao wawe raia wema wenye kazi halali za kufanya.

(g) Utunzaji na Hifadhi ya MazingiraMheshimiwa Spika, Jeshi la Magereza limekuwa mstari wa mbele katika utunzaji na hifadhi ya mazingira yetu. Katika maeneo ya Magereza Upandaji miti umekuwa ni sehemu ya kazi yao ambapo maandalizi ya vitalu huenda sambamba na maandalizi ya kilimo kwa kila gereza kila mwaka.

Siku ya upandaji miti Kitaifa iliyoadhimishwa tarehe 1 Januari 2007 jumla ya miti 124,040 ilipandwa katika vituo mbalimbali. Jeshi la Magereza kwa kuzingatia umuhimu huo limeanzisha mashamba ya miti katika magereza ya Mgagao, Uyui, Mollo, Ngudu, Wami kuu, Mtego wa Simba, Idete, Isupilo na Msalato. Aidha, juhudi za kupanda miti zinaendelea katika vituo vingine baada ya hali ya hewa kuwa nzuri.

(h) Kuandaa Mpango wa Nishati Mbadala ya *Biogas* Mheshimiwa Spika, Jeshi la Magereza linakabiliwa na tatizo sugu la kutegemea kuni peke yake kama nishati ya kupikia vyakula vya wafungwa na Mahabusu. Karibu mita za ujazo 120,000 za kuni zinatumika kwa mwaka. Utumiaji wa kuni kwa kiasi hicho unaathiri sana mazingira Aidha, kila siku gharama ya usafirishaji wa kuni inaongezeka kutokana na kwenda mbali zaidi kuzifuata.

Mwezi Februari 2007 niliongoza Ujumbe wa Jeshi la Magereza kwenda Rwanda kujionea na kujifunza matumizi ya *biogas* inayotokana na maliwato ya wafungwa na mahabusu kwa kupikia katika magereza yao karibu yote. Tulikuta utaalamu wanaoutumia umetokana na Watanzania waliotoka *CARMATEC* Arusha wakiongozwa na Injinia Aenea Kimaro ambaye anatambulika Kimataifa kama bingwa wa *biogas.*

Mheshimiwa Spika, ninayo furaha kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa Jeshi la Magereza kwa kumtumia Injinia Aenea Kimaro limekwishaandaa upembuzi yakinifu wa mradi na michoro ya mtambo wa biogas kwa ajili ya Gereza la Ukonga ambao utatekelezwa katika Bajeti ya mwaka huu 2007/2008 kama hatua ya mwanzo ya kuelekea kwenye utumiaji kamili wa biogas katika Magereza yetu yote.

Aidha, mitambo ya biogas inayojengwa kwa uhisani wa *UNHCR* na *DANIDA* katika Magereza Karagwe na Bangwe - Kigoma inatarajiwa kuanza kazi hivi karibuni. Kutokana na mradi huu nchi itaokoa mita za ujazo 120,000 za kuni zinazotumika kupikia wafungwa na mahabusu kwa mwaka. Faida ingine kubwa inayotokana na mfumo wa biogas ni usafi wa mazingira kwa sababu mchakato wa kutengeneza *biogas* hubadilisha uchafu wa maliwatoni kuwa mbolea salama ambayo inafaa sana na inaweza kutumika bila madhara yoyote. Kwa kuwa ukubwa wa mtambo wa *biogas* unategemea kiasi cha mali ghafi inayopatikana, kuanzia ngazi ya kaya hadi taasisi mbalimbali kama vile shule na hospitali zinaweza kunufaika sana kutokana na utaalamu huu.

Mheshimiwa Spika, namshukuru na nampongeza sana Injinia Aenea Kimaro kwa kuamua kurejesha nyumbani utaalamu wake. Kwa taarifa ya Waheshimiwa Wabunge anapatikana katika mtandao kupitia *email: ainea 2000@yahoo.com.* Injinia Kimaro ni mtaalamu bingwa wa *biogas* na uvunaji wa maji ya mvua *(rain water havesting)* anayetambulika Kimataifa. *(Makofi)*

(i)Elimu Kwa UmmaMheshimiwa Spika, Kuhusu elimu kwa Umma, Jeshi la Magereza limeendelea kutangaza kipindi cha: "IJUE MAGEREZA" kinachorushwa na Redio Tanzania kila wiki. Aidha, vipeperushi vya 'Mkataba wa Huduma kwa Mteja' kwa lugha ya Kiswahili vimeendelea kuchapishwa na kusambazwa katika magereza yote pamoja na kuweka mabango kwenye milango ya magereza ili kuendelea kuielimisha jamii kuhusu majukumu muhimu ya Jeshi la Magereza. Mafunzo ya kinga dhidi ya UKIMWI hutolewa katika mabaraza ya Wafungwa na Mahabusu kwa kuzingatia Sera ya UKIMWI ya kitaifa na miongozo mbalimbali ya Kimataifa kuhusiana na UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha Huduma kwa Jamii, utekelezaji wa Sheria ya Huduma kwa Jamii Na. 6/2002 inayolenga kupunguza msongamano magerezani unaendelea katika Mikoa sita ya Majaribio ya Dar es salaam, Dodoma, Mwanza, Mbeya,

Mtwara na Kilimanjaro. Aidha, Wizara yangu imeendelea kupanua utekelezaji wa Sheria hii katika Mikoa mingine mitatu ya Iringa, Arusha na Tanga. Mafunzo elekezi kwa wadau yametolewa kuhusu Sheria hii katika Mikoa hiyo mipya ili kuhakikisha utekelezaji wake unakuwa ni wa mafanikio.

Mheshimiwa Spika, Tangu kuzinduliwa rasmi kwa mpango wa Huduma kwa Jamii Februari 2005, kama nilivyokwishasema hapo awali, jumla ya wafungwa 548 wamehukumiwa kutumikia adhabu zao chini ya Sheria hii. Wafungwa hawa wamekuwa wakifanya kazi bila malipo katika taasisi mbalimbali za Serikali huku wakiishi na familia zao. Kazi ambazo zimekuwa zikifanyika ni pamoja na kukarabati barabara vijijini; usafi wa mazingira kwenye ofisi na hospitali za Serikali; ujenzi wa vyumba vya madarasa na nyumba za walimu; na kutunza bustani za miche ya miti kwenye Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji.

Idara ya Zimamoto na Uokoaji, majukumu ya msingi ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ni kuokoa maisha na mali kwa mfano kwenye majanga ya moto, majanga ya matetemeko, na ajali za barabarani pia kuzima moto kila unapotokea.Kazi nyingine zinazofanywa na Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ni kutoa elimu ya moto kwa umma kinadharia na kivitendo kuhusiana na tahadhari na kinga ya moto, kufundisha namna ya kutumia vifaa vya kuzima moto vinavyowekwa kwenye maeneo ya ofisi au nyumbani, pamoja na kufanya ukaguzi wa tahadhari na kinga ya moto kwenye maeneo mbalimbali *(Fire Prevention and Protection)* ili kuhakikisha kunakuwepo usalama wa watu na mali zao dhidi ya moto.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007 yalitokea matukio 452 ya moto, Maokozi 63 na miito ya moto ya uongo 58. Katika matukio hayo Vikosi vya Zimamoto na Uokoaji vya Serikali, Kampuni binafsi na Kampuni za Umma kwa ujumla vilishiriki katika kuzima moto. Pia kulifanyika miito ya mazoezi miwili (2).

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2006/2007, mafunzo ya zimamoto yaliendeshwa katika Chuo chetu cha Zimamoto na Uokoaji cha Ukonga. Idadi ya waliopata mafunzo kupitia Chuo hicho ni 354. Pia yalitolewa mafunzo sehemu za kazi kwa Wafanyakazi 6,570.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada za kuzima moto na kuokoa maisha na mali, suala la ukaguzi wa tahadhari na kinga ya moto lilipewa uzito unaostahili. Jumla ya maeneo 9,345 yaliyofanyiwa ukaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lengo kubwa la Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ni kuhakikisha maisha na mali vinakuwa salama. Kwa hali hiyo juhudi zinafanywa kuboresha shughuli za Zimamoto na Uokoaji Nchini. Juhudi hizo ni pamoja na kuipatia baadhi ya Mikoa yetu Magari ya Zimamoto. Katika mwaka wa fedha 2006/2007, Halmashauri za Manispaa za Arusha, Shinyanga, Sumbawanga, Musoma; na Halmashauri za Miji ya Babati, Korogwe, Arumeru na Kahama, zilipatiwa fedha za kununulia Magari ya Zimamoto. Utaratibu wa kuunda Vikosi vya Zimamoto na Uokoaji katika Halmashauri ambazo zilikuwa hazina magari umeanza. Vibali vya ajira ya Askari

wa Zimamoto vimetolewa kwa baadhi ya Halmashauri hizo na mchakato wa ajira umeanza.

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya mwaka wa fedha 2006/2007 tuliahidi kuitunga upya Sheria ya Zimamoto na Uokoaji iliyofutwa. Nafurahi kuliambia Bunge lako tukufu kwamba Rais ameridhia na kutia saini Sheria ya Zimamoto na Uokoaji Na. 14 ya 2007 *(The Fire and Rescue Force Act No.14 of 2007).* Kazi inayoendelea sasa ni ya kutunga kanuni za kiutumishi na kanuni za kiutendaji na Amri zake. Suala jingine ambalo liko kwenye mchakato ni kuhusu Muundo mpya wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na ukamilishwaji wa Sera ya Taifa ya Moto. Jeshi la Zimamoto na Uokoaji litafanya kazi kwa utaratibu wa Kamandi Moja *(Central Command)* na litakuwa na viongozi katika ngazi za Mkoa na Wilaya. Baada ya kukamilika yote hayo tutakuwa na chombo chenye kufanya kazi kwa taratibu zinazotakiwa. Nakusudia kutangaza kwenye Gazeti la Serikali kuanza kutumika kwa Sheria hiyo tarehe 1 Septemba, 2007. Idara ya Uhamiaji, katika kipindi cha Julai 2006 hadi Aprili 2007 Idara ya Uhamiaji imeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ambayo ni kudhibiti uingiaji, utokaji na ukaaji wa wageni nchini na pia kuwawezesha raia wa Tanzania kupata hati za kusafiria nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2006 hadi Aprili 2007, jumla ya wageni 531,834 waliingia nchini, ikilinganishwa na wageni 404,899 walioingia kipindi kama hiki mwaka jana; ambalo ni ongezeko la asilimia 31.3. Aidha, wageni 504,742 walitoka nchini ikilinganishwa na wageni 380,758 waliotoka katika kipindi kama hiki mwaka uliopita ambalo ni ongezeko la asilimia 32.6. Kwa ujumla wageni walioingia na kutoka nchini ni wengi zaidi; na hii inatokana na: kuwepo kwa hali ya amani; utulivu na usalama; mazingira bora ya uwekezaji; na kupungua kwa hofu ya ugaidi miongoni mwa wageni. Aidha, kuongezeka kwa matangazo ya vivutio vya utalii huko nje na hapa ndani kumechangia kuleta ongezeko la wageni wanaoingia na kutoka.

Mheshimiwa spika, ili kuwawezesha raia wetu kusafiri nchi za nje kwa shughuli mbalimbali, Idara ya Uhamiaji imetoa Pasipoti 52,345 kuanzia Julai 2006 hadi Aprili 2007. Kati ya hizo 50,309 ni za kawaida, 1,675 ni za Afrika Mashariki, 273 za kibalozi, na 88 za watumishi, ikilinganishwa na jumla ya pasipoti 142,707 zilizotolewa wakati kama huu mwaka wa fedha 2005/2006 zikiwemo 736 za watumishi, 2,075 za kibalozi na 139,089 za kawaida. Kitakwimu inaonesha kuwa kwa kipindi kama hiki mwaka juzi Pasipoti nyingi zaidi zilitolewa kwa sababu kilikuwa kipindi ambacho Pasipoti zilikuwa zinabadilishwa.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Uhamiaji pia huratibu maombi ya wageni wanaoomba uraia wa Tanzania. Katika kipindi cha Julai 2006 hadi Aprili 2007, Wizara yangu ilitoa uraia wa Tanzania kwa waombaji 110 waliotimiza masharti ikilinganishwa na waombaji 104 waliopata uraia mwaka wa fedha 2005/2006. Aidha, katika kipindi hicho, Watanzania 79 waliukana uraia wa Tanzania kwa kupata uraia wa nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha hali ya udhibiti wa wageni inakuwa ni ya kuridhisha, Idara ya Uhamiaji iliendelea kutoa vibali vya kuishi nchini *(residence permits)* kwa wageni waliostahili kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi Ajira na

Maendeleo ya Vijana, na Wizara ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Kituo cha Uwekezaji pamoja na Asasi nyinginezo za Kitaaluma. Katika kipindi cha Julai 2006 hadi Aprili 2007 wageni 4,943 walipewa vibali hivyo ikilinganishwa na wageni 5,475 waliopewa vibali hivyo mwaka wa fedha 2005/2006. Aidha, kuanzia Julai 2006 hadi Aprili 2007, vibali 1,604 viliongezwa muda ikilinganishwa na vibali 1,663 vilivyoongezwa muda katika kipindi kama hiki mwaka uliopita.

Mheshimiwa Spika, wakati ambapo utoaji vibali vya kuishi nchini kwa wageni umepungua, lakini limekuwepo wimbi la wageni wanaoingia na kuishi nchini kinyume cha sheria. Kutokana na doria na misako yenye lengo la kudhibiti ukaazi wa wageni haramu nchini ilifanyika sehemu mbalimbali kama vile hotelini, migodini, Vijijini, Mijini na sehemu nyingine za maficho. Jumla ya wageni 1,876 walikamatwa na kushitakiwa katika kipindi cha Julai 2006 hadi Aprili 2007 ikilinganishwa na 1,016 wa mwaka 2005/2006. Katika mwaka wa fedha 2006/2007 hatua za kisheria zilizochukuliwa dhidi ya wageni hao 1,876 waliokamatwa zilikuwa kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| Waliofukuzwa nchini | - | 980 |
| Walioshtakiwa | - | 473 |
| Waliotozwa faini | - | 26 |
| Waliofungwa | - | 80 |
| Walioachiwa huru | - | 227 |
| Kesi zinazoendelea | - | 140 |
| **Jumla** | | **1,876** |

Mheshimiwa Spika, katika siku za hivi karibuni kumekuwepo na wimbi la wahamiaji haramu wanaoingia Tanzania kutoka katika nchi za Pembe ya Afrika hususan nchi za Ethiopia na Somalia. Katika kipindi cha Aprili hadi Juni, 2007 jumla ya wahamiaji haramu wa namna hiyo wapatao 232 walikamatwa na hadi hivi sasa wanashikiliwa katika magereza yetu mbalimbali hapa nchini wakisubiri kurejeshwa nchini kwao. Serikali yetu imefanya mawasiliano na Serikali ya Ethiopia kupitia Ubalozi wake ulioko Nairobi ili wawatambue wahamiaji hao haramu na kuweza kurejeshwa kwao.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu pia imekuwa ikikabiliwa na tatizo la vijana wetu wa Kitanzania kutorokea nje ya nchi kinyume cha sheria kwa visingizio vya kutafuta maisha bora zaidi. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2006/2007 vijana 193 walirudishwa nchini na kushitakiwa kwa mujibu wa sheria, ikilinganishwa na vijana 398 waliorudishwa nchini mwaka wa fedha 2005/2006 kipindi kama hicho. Mradi wa vitambulisho,katika Bunge la bajeti la mwaka wa fedha 2006/2007 niliiahidi Bunge lako tukufu kwamba baada ya kukamilisha zoezi la upembuzi yakinifu Wizara yangu ingeanza utekelezaji wa Mradi wa Vitambulisho. Napenda kulijulisha Bunge hili kuwa Wizara imeanza utekelezaji wa mradi kwa kununua jengo kwa ajili ya Ofisi anzilishi ya mradi. Hali kadhalika Wizara yangu ikishirikiana na Wizara ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na Asasi nyingine zinaendelea na mchakato wa kuundwa kwa Wakala *(Agency)* itakayosimamia na kuendesha zoezi la utoaji wa Vitambulisho vya Taifa. Wizara inakamilisha Andiko la Maelezo ya Mradi *(Project Design Document)* ambalo ndiyo

litatoa dira ya mwelekeo wa utekelezaji wa mradi hatua kwa hatua. Aidha, zoezi la kuwatambua na kuwaorodhesha wageni wanaoishi vijijini na mijini linaendelea katika Mikoa ya Kagera, Kigoma, Rukwa, Mbeya, Ruvuma, Mtwara, Mwanza, na Mikoa ya kati. Hii ni hatua muhimu ya maandalizi ya utoaji vitambulisho. Lengo la Serikali ni kukamilisha mradi wa Vitambulisho ifikapo Desemba, 2009.

Mheshimiwa Spika, miradi ya ujenzi na ukarabati, ukarabati wa Chuo tarajiwa cha Mafunzo ya Uhamiaji mjini Moshi upo katika hatua za mwisho, ikiwemo ufungaji wa mtandao wa mawasiliano ya Kompyuta. Chuo kinatarajiwa kufunguliwa rasmi mnamo Septemba 2007. Hali kadhalika ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji ya Mkoa wa Dar es Salaam umekwishaanza na Mshauri mtaalam na msimamizi wa mradi huo tayari amekwishapatikana.

Mheshimiwa Spika, uimarishaji wa shughuli za uhamiaji, katika kuboresha utoaji wa huduma za Uhamiaji, Idara ikishirikiana na Chuo Kikuu cha Mzumbe inafanya Utafiti juu ya tatizo la Wimbi la Wahamiaji haramu linaloongezeka siku hadi siku, ili kubainisha chanzo chake. Zoezi hili litaiwezesha Idara ya Uhamiaji kupambana na wimbi la wahamiaji haramu hapa nchini kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na harakati za kupambana na wahamiaji haramu, Idara ya Uhamiaji imefanikiwa kuboresha eneo la ukusanyaji mapato ya Serikali kwa kufunga mitambo ya kutolea Visa Stickers pamoja na jenereta 17 ambazo zimesimikwa kwenye vituo 17 vya kuingilia nchini ili kukidhi mahitaji ya nishati mbadala katika uendeshaji wa mitambo hiyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeshiriki vyema katika kukuza na kuendeleza ushirikiano na nchi za Jumuiya ya *SADC* kupitia mikutano ya ujirani mwema na ile ya *Organ on Politics, Defence and Security,* ambapo kwa mwaka huu Tanzania ndio Mwenyekiti wa Mikutano yote. Kwa hiyo, Idara ya Uhamiaji tayari imeshiriki kwenye mkutano unaozihusisha Idara za Uhamiaji kutoka nchi wanachama uliofanyika jijini Arusha kuanzia Januari 31 hadi Februari 1, 2007.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Wakimbizi, kuhusu Wakimbizi mwaka 2006/2007 tumeanza kuona mwanga mwishoni mwa handaki/taruma. Wakimbizi wengi tulionao wanatoka Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (JJK). Nchi hizo zote mbili sasa zina Serikali za Kidemokrasia zilizochaguliwa baada ya makubaliano na muafaka wa kitaifa. Kwa hiyo Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo *(DRC)* sasa kuna usalama. Kwa hiyo Tume ya Utatu *(Tripartite Commission)* ya Burundi, Tanzania na *UNHCR* imeamua tuingie katika hatua ya kuwahimiza wakimbizi wa Burundi kurejea kwao. Tunafanya vivyo hivyo kwa wakimbizi kutoka JKK *(DRC).* Kutokana na hatua hizo idadi katika makambi ya wakimbizi yanayo hudumiwa na *UNHCR* na Serikali imezidi kupungua kufikia 260,865 kama inavyooneshwa kwenye Kiambatisho F. Hatua kama hiyo tumeianzisha Juni 2007 kwenye Makazi ya Wakimbizi ya (1) Katumba na (2) Mishamo (Wilaya ya Mpanda); na (3) Ulyankulu (Wilaya ya Urambo) yanayohudumiwa na Serikali peke yake yenye wakimbizi 210,865. Kwa hiyo jumla katika Makambi na

Makazi tumebakiwa na wakimbizi 480,730 kulinganisha na wakimbizi 1,300,000 tuliokuwa nao mwaka 1996.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuimarika kwa hali ya amani na usalama katika nchi za Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo, Idadi ya waomba hifadhi wapya wanaopokelewa kutoka nchi hizo imepungua sana hadi kufikia 340 katika kipindi cha kuanzia 1 Julai 2006 hadi 31 Mei 2007. Hali hii ni tofauti na uzoefu wa miaka ya nyuma ambapo maelfu ya waomba hifadhi walikuwa wanapokelewa kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007, utekelezaji wa zoezi la kuwarejesha wakimbizi wa Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo *(DRC)* nchini kwao limeendelea. Tangu 2002 hadi kufikia tarehe 31 Mei 2007 jumla ya wakimbizi 319,983 kutoka Burundi na 34,348 kutoka *DRC* walikuwa wamerejea nchini kwao. Tangu zoezi hili lianze, Wizara imeweza kuyafunga makambi sita ya wakimbizi kutokana na kupungua kwa wakimbizi. Makambi ya Wakimbizi yaliyofungwa ni (1) Mtendeli (2) Muyovosi (3) Mkugwa na (4) Lukole 'B'. Aidha, hivi karibuni nimeidhinisha hatua ya kufungwa kambi la Lugufu II ianze kutekelezwa. Hata hivyo pamoja na kufanikiwa kwa zoezi hili, bado kasi ya urejeshaji wakimbizi inaathiriwa na kukosekana kwa meli kubwa za kubeba abiria kwenye Ziwa Tanganyika kwa sababu uwezo wa MV Mwongozo inayotumika sasa ni kubeba abiria 500 tu na hufanya safari moja tu kwa wiki kwenda *DRC.*

Mheshimiwa Spika, mchakato wa uchaguzi katika nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo ulichangia kupunguza kasi ya wakimbizi kurejea nchini kwao, lakini kwa sasa baada ya uchaguzi ari ya wakimbizi wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo kutaka kurejea kwao ni kubwa kutokana na kufanyika kwa uchaguzi wa kidemokrasia na Rais Joseph Kabila kuchaguliwa na wananchi. Wizara kwa kushirikiana na Wadau wengine tunaangalia uwezekano wa kupata meli za ziada za kusaidia kuwasafirisha wakimbizi hawa. Kwa upande wa Burundi, kasi ya zoezi imekuwa ndogo kutokana na ukame na njaa vilivyoikumba nchi hiyo mwaka jana, ambapo wakimbizi wengi walishindwa kurejea kwa kuogopa janga hilo. Kwa sasa kasi ya urejeaji wakimbizi inatarajiwa kuongezeka hasa baada ya mavuno na baada ya *UNHCR* kutangaza ongezeko la vivutio ikiwa ni pamoja na kuongeza muda wa msaada wa chakula kutoka miezi minne kuwa sita, pamoja na malipo ya fedha taslimu ya *USD 50* mara wafikapo kwao kwa wale tu watakaorejea mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, matatizo yanayodumaza utekelezaji wa urejeaji Wakimbizi yamekuwa yakijadiliwa na Kamisheni mbili za kuratibu zoezi la urejeshaji Wakimbizi wa Burundi na *DRC* ambazo zimekuwa zikikutana kujadili utekelezaji wa zoezi hilo. Aidha, Kamisheni ya Pande Tatu (Burundi, Tanzania na *UNHCR)* ya kuratibu zoezi la urejeaji Wakimbizi wa Burundi mwezi Juni 2007 imetembelea Makazi ya Wakimbizi wa Burundi ili kuwahamasisha kurejea Burundi. Lengo ni kwamba kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha 2007/2008 Wakimbizi wote wawe wamerejea nchini kwao. Natarajia ndani ya mwaka huu wa fedha kuyafunga rasmi makambi na makazi yote ya wakimbizi. Nachukua fursa hii kuwahimiza wakimbizi wote kurejea kwao kwa kutambua ukweli kuwa MTU KWAO na MWENDA KWAO SIYO MTUMWA. Aidha, ninawakumbusha

kuwa katika usemi usemao: "Chelewa Chelewa Utakuta Mtoto si Wako" au maneno 'mtoto si wako' yanaweza kubadilishwa kuwa, "shamba si lako" au "cheo si chako".

Aidha, kama nilivyowaambia kwa maneno ya wafugaji wa Kihehe yasemayo: "*Iyilongwe Yayinywa Ululengu*" yaani: Ng'ombe iliyotangulia kufika mtoni hunywa maji safi na kwa hiyo ni kheri kuwahi kurejea kwao kuliko kuchelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa upande wake inaendelea na taratibu za kuhuisha Sheria ya wakimbizi Na.9 ya mwaka 1998 *(Refugee Act No. 9 of 1998)* ili iweze kulingana na Sera ya Taifa ya Wakimbizi pamoja na mabadiliko mengine. Tumeandaa nyaraka zenye mapendekezo kuhusu suala hilo ili zisambazwe kwa Wadau wapate fursa ya kuzijadili kwa pamoja na kuzitolea maoni. Kwa mwelekeo huo, kazi ya kuhuisha Sheria ya Wakimbizi itakamilika ndani ya mwaka huu wa fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, Msajili wa Vyama vya Kijamii *(Registrar of Societies)*Wizara yangu kupitia Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Kijamii inaendelea na kazi ya kusajili Vyama vya Hiari vya Kijamii pamoja na Mashirika na Taasisi za dini. Kuanzia mwaka wa fedha unaomalizika sasa, Ofisi ya Msajili wa Vyama imeendelea na zoezi la kuhakiki uhalali wa vyama vyote vilivyoandikishwa ili kubaini vyama ambavyo havijiendeshi kwa mujibu wa sheria, kanuni, pamoja na taratibu zilizopo na vile vinavyokwepa kulipa ada. Lengo kubwa ni kuhakikisha kuwa vyama hivi vinajiendesha kulingana na malengo yake na kwa kuzingatia sheria za nchi. Vyama vyote vitakavyobainika kwenda kinyume na taratibu zilizopo vitachukuliwa hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufutiwa usajili wake. Hili litakuwa ni zoezi la kudumu ambalo utekelezaji wake unalenga kuwa na vyama makini vitakavyohudumia jamii katika mazingira mazuri na yenye kuheshimu maadili ya taifa.

Mheshimiwa Spika, Shabaha na malengo kwa mwaka 2007/2008. Jeshi la Magereza limepanga kufanya yafuatayo:-

Kupima na kulipia fidia maeneo yaliyotolewa kwa Jeshi la Magereza katika vituo vya Ubena, Wami Kuu na Wami Vijana, Ngwala, Chuo Kiwira, Matongo na Segerea.(a)Kuajiri askari wapya 812 na kuwapa mafunzo ya awali.

(b) Kutoa mafunzo kwa watumishi wa Magereza 300.

(c) Kuendeleza ukarabati wa majengo na miundo mbinu yaMagereza yenye ulinzi mkali likiwemo Gereza Maweni - Tanga, Uyui - Tabora, Ukonga – Dar es Salaam na Gereza maalum *(special wing)* Isanga – Dodoma, Lilungu - Mtwara na Gereza Keko – Dar es Salaam.

(d) Kuendeleza ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Magereza Mkoa wa Dar es Salaam.

(e) Kuendeleza ukamilishaji wa baadhi ya viporo vya miradi ya mabweni ya wafungwa na Ofisi za Utawala katika magereza ya Magu, Geita, Kayanga, Mahabusu Mugumu, Mahabusu Iringa, Mbinga, Wami Vijana, Segerea, Kambi Kanegele, Isupilo,

Mkuza, Ileje, Kyela na Mahabusu Tabora. Aidha, ujenzi wa magereza utaendelea kufanyika katika magereza ya Mahabusu Singida, Mbozi, Isupilo, Rombo, Igunga, Kigongoni, Kwamungumi, Wazo, Mng'aro, Kahama, Kambi Kizwite – Sumbawanga, Mahabusu Ifakara mjini na Nkasi.

(f) Kuendeleza ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa nyumba za maafisa na askari katika vituo vya Ukonga, Muleba, Magereza (M) Manyara, Magereza (M) DSM, Chuo Ruanda, Mbinga, Igunga, Mahabusu Iringa, Rombo, Utete, Keko na Mbarali.

(g) Kuendelea kuimarisha mifumo ya maji safi na maji taka kwa kuhakikisha kuwa kero za maji taka na maji safi zinapunguzwa Magerezani.

(h) Kupima na kulipia fidia maeneo yaliyotolewa kwa Jeshi la Magereza katika vituo vya Ubena, Wami Kuu na Wami Vijana, Ngwala, Chuo Kiwira, Matongo na Segerea.

(i) Kuendeleza ukarabati wa Chuo cha Maafisa wa Magereza Ukonga na Kiwira-Mbeya.

(j) Kuendeleza uzalishaji katika mashamba ya kilimo na mifugo kwa kuyapatia zana na pembejeo zinazotakiwa ikiwemo ununuzi wa matrekta manne.

(k) Kuendelea kupanda miti kwa lengo la kuhifadhi mazingira.

(l) Kuendelea kununua mashine mbalimbali za kuendeleza viwanda vya useremala kwa ajili ya vituo vya Arusha, Ukonga na Tabora pamoja na ununuzi wa mashine za karakana ya Gereza Ukonga.

(m)Kutekeleza Mradi wa Uendeshaji wa Shughuli za Wafungwa kwa Kutumia Mtandao wa Kompyuta *(OMIS)*.

(n) Kujenga miundombinu ya matumizi ya nishati mbadala ya *biogas* katika Gereza Ukonga na gesi asilia *(natural gas)* katika Gereza Keko.

(o) Kuendeleza kazi ya kuandaa na kutekeleza miradi ya nishati mbadala ya biogas badala ya kuni katika Magereza ya Segerea - Dar es Salaam na Gereza Ruanda - Mbeya na kuendelea baadaye katika Magereza mengine nchini.

(p) Kukamilisha mchakato wa kupata mikopo yenye masharti nafuu kutoka mifuko ya jamii ikiwemo *NSSF* na *PPF* ili kujenga nyumba za Askari Magereza.

(q) Kuendelea kutoa Elimu kwa umma kupitia kipindi cha "Ijue Magereza" kinachorushwa na Redio Tanzania kila wiki. Aidha vipeperushi vya Mkataba wa Huduma kwa Mteja vitaendelea kuchapishwa na kusambazwa kwenye vituo vyote vya magereza.

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha Huduma kwa Jamii, Mwaka wa fedha 2007/2008 Sheria ya Huduma kwa Jamii itatekelezwa katika Mikoa ya Shinyanga, Mara na Kagera ambayo imebakia kutoka mwaka wa fedha 2006/2007 kutokana na ufinyu wa bajeti. Hali kadhalika tunatazamia kuongeza Mikoa ya Morogoro, Pwani na Lindi kwenye Mpango wa Huduma kwa Jamii katika mwaka huu wa fedha. Mikoa mingine iliyobaki itaendelea kuongezwa hatua kwa hatua kadri bajeti itakavyoruhusu ili hatimaye Sheria itekelezwe nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyolieleza Bunge lako tukufu katika bajeti iliyopita, utekelezaji wa Sheria ya Huduma kwa Jamii umeendelea kuwa na matatizo kutokana na watendaji *(Probation Officers*) wake wakuu Mikoani na Wilayani kuwa wachache na ni waajiriwa wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Hivyo kiutendaji Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa ujumla hatuna mamlaka ya moja kwa moja katika kuwasimamia watumishi hao. Wizara yangu inawasiliana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ili kurekebisha hali hii.

Mheshimiwa Spika, Sheria mpya ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji itaanza kutumika rasmi mwaka huu wa fedha. Hatua kadhaa zitachukuliwa kuunda Jeshi la Zimamoto na Uokoaji la kisasa lenye ufanisi bora zaidi katika kukabiliana na majanga mbalimbali. Kwa dhana hiyo na ili kuleta ufanisi unaotakiwa zitaanzishwa Ofisi za Mkoa na Wilaya kama ilivyo kwa majeshi ya Polisi na Magereza. Tutatumia mwaka mzima wa fedha 2007/2008, kujipanga upya na katika mwaka wa fedha 2008/2009 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji litaanza kazi kwa nguvu mpya, kasi mpya na ari mpya kama sheria inavyosema ya kuwa na Kamandi moja ya kijeshi *(Command of force discipline)* . Ni azma ya Wizara kuhakikisha suala la mafunzo kwa Askari wa Zimamoto na Uokoaji linapewa kipaumbele sawia na: upatikanaji wa Chuo cha Kitaifa cha Zimamoto na Uokoaji; na Ofisi za Makao Makuu ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji; na uanzishwaji wa Ofisi za Zimamoto Mkoa na Wilaya.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio yetu kuwa katika mwaka wa fedha 2007/2008 zoezi la ukaguzi wa tahadhari na kinga ya moto kwenye maeneo mbalimbali litatekelezwa kwa kasi ya hali ya juu, na wale watakaokiuka sheria au utaratibu watachukuliwa hatua kali za kisheria. Pia elimu ya moto kwa umma itatolewa ili kuhakikisha tunaishi vizuri na 'rafiki yetu' moto ambaye huweza kugeuka kuwa 'adui' wakati wowote.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sasa tunayo tena Sheria ya Zimamoto na Uokoaji itakuwa ni wajibu wa Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kuhakikisha Sheria inatekelezwa kikamilifu. Utekelezaji huo utakuwa ni pamoja na Askari wa Zimamoto na Uokoaji wote kuwa chini ya usimamizi mmoja *(Central Command),* na mafunzo ya Askari wa Zimamoto na Uokoaji nchini yataendeshwa kupitia Chuo cha Kitaifa cha Zimamoto na Uokoaji kilichopo. Pamoja na mafunzo ya taaluma ya moto pia mafunzo ya kijeshi yatatolewa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2007/2008 Idara ya Uhamiaji imelenga kufanya yafuatayo:-

Kuendeleza kazi ya ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Dar es Salaam na kuanza ujenzi wa Ofisi za Manyara na Kagunga.
Kununua wa magari 11 na pikipiki 17. Kuajiri Maafisa wapya 374 na kuwapeleka watumishi 140 kwenye kozi mbalimbali za kujiendeleza za muda mrefu na mfupi.Kuendeleza misako na doria ili kupambana na tatizo la wahamiaji haramu. Kukarabati jengo lililonunuliwa kwa ajili ya Ofisi anzilishi ya Mradi wa Vitambulisho vya Taifa. Kuendeleza mpango wa kukarabati Ofisi na nyumba za makazi ya watumishi katika vituo vya kuingilia nchini vya Rusumo, Manyovu, na Sirari.

Mheshimiwa Spika, jukumu muhimu la Idara ya Wakimbizi mwaka wa fedha 2007/2008 ni kutekeleza maamuzi ya Tume ya Pembe Tatu *(Tripartite Commission)* yanayohusiana na kuwahimiza Wakimbizi kurejea kwao, na hatimaye kuyafunga Makambi na Makazi ya Wakimbizi. Hii itakuwa hatua muhimu kwa Bara la Afrika kuondokana na aibu ya kuwa na Wakimbizi na Makambi ya Wakimbizi.

Mheshimiwa Spika, Idara pia itaendelea kutekeleza awamu ya pili ya mpango wa kukabiliana na athari za uharibifu wa mazingira unaotokana na ujio wa Wakimbizi katika Mikoa ya Kigoma na Wilaya ya Ngara Mkoani Kagera. Mpango huu unafadhiliwa na Serikali ya Denmark kwa gharama ya Shilingi Bilioni 10.9 sawa na *Danish Kroner 60* milioni. Miradi inayotekelezwa katika awamu hii ni:-

(a) Miradi Shirikishi ya kuhifadhi Maliasili/Mazingira *Integrated Natural Resources Management (INRM);*

(b) Mafunzo ya Ufundi Stadi na uhifadhi wa mazingira makambini;

(c) Miradi ya maji na usafi ndani ya kambi na vijiji jirani;

(d) Kuimarisha uwezo wa kuhifadhi wakimbizi *(Improved Refugee Protection Capacity);* na

(e) Kukamilisha ujenzi wa majengo ya nishati mbadala ya biogas badala ya kuni katika magereza ya Bangwe na Ngara.

Imeamuliwa kuendelea na mradi huu baada ya tathmini ya awamu ya kwanza kuonyesha mafanikio na Serikali ya Denmark kuridhishwa na utekelezaji huo. Serikali ya Denmark imeendelea vile vile kutoa misaada chini ya *Strengthening Protection Capacity Project* ikiwemo ununuzi wa vifaa vya Ofisi, magari na ujenzi au ukarabati wa Ofisi na nyumba za kuishi watumishi katika Mikoa ya Kigoma na Kagera (Wilaya ya Ngara). Aidha, Wizara itaendelea kuiomba Jumuiya ya Kimataifa kusaidia maeneo yaliyoathiriwa na wakimbizi hususan katika nyanja za hifadhi ya mazingira, ukarabati wa miundombinu ya maji; ujenzi na ukarabati wa zahanati, shule na sekta nyingine zinazolenga kupunguza umasikini.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu iliridhia ombi la Serikali ya Marekani la kuwahamishia nchini kwao *(resettlement)* wakimbizi wa Burundi kati ya 13,000 na 15,000. Wakimbizi hawa ni wale waishio katika Mikoa ya Kigoma na Kagera na ambao waliingia nchini katika miaka ya 1970 ambao inaonekana kuwa wameshindwa kurejea kwenye nchi yao ya asili. Baada ya kukamilika matayarisho ikiwa ni pamoja na utambuzi wa wakimbizi na kuwaweka katika eneo moja, na upanuzi wa uwanja wa ndege wa Kibondo, wakimbizi hawa walianza kusafirishwa kwenda Marekani mwezi Mei 2007.

Mheshimiwa Spika, uhamisho huo *(resettlement)* unatekelezwa na Shirika la *International Organization for Migration (IOM)* kwa kushirikiana na *UNHCR*. Serikali inafuatilia kwa makini zoezi hili ili lisiathiri zoezi zima la urejeshaji wakimbizi makwao.

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha Usajili wa Vyama, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Kijamii *(Registrair of Societies)* kwa mwaka wa fedha 2007/2008 imepanga kuboresha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali ili kufikia malengo yanayotarajiwa ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa vyama vyote vinalipa ada kwa wakati na kukusanya madeni yaliyopita. Sambamba na hili ni kuendeleza zoezi la uhakiki wa uhalali wa vyama vyote vilivyoandikishwa pamoja na kuwachukulia hatua za stahili vile vinavyokiuka Sheria Nia ya Msajili wa Vyama ni kuhakikisha kuwa vyama hivi vinafanya kazi kwa kuzingatia malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, shukrani, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu naomba nitoe shukrani za pekee kwa Waziri mwenzangu katika Wizara hii Mheshimiwa Lawrence Kego Masha Mbunge wa Nyamagana, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ambaye ananisaidia vizuri sana kuiongoza Wizara hii na kila mara amekuwa hachoki kunipa ushauri na ushirikiano wenye manufaa makubwa kwa Wizara.

Aidha, naomba kutoa pia shukrani zangu kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Bwana Salmon Odunga pamoja na Wakurugenzi na Wafanyakazi wote ambao ushirikiano wao umewezesha Bajeti hii kuandaliwa. Naomba kutoa pongezi za pekee kwa Kamishna Mkuu wa Magereza Mstaafu *(PCP)* Nicas Pius Banzi kwa kustaafu tarehe 20 Juni 2007 kwa heshima ya utumishi uliotukuka. Ujasiri na umahiri wake umechangia kwa namna ya pekee katika kuendeleza na kuimarisha Jeshi la Magereza tunalojivunia Watanzania na ambalo ni mfano unaotakiwa kuigwa na majirani zetu ikiwemo Rwanda. Kwa dhati kabisa niwashukuru wahisani wote ambao misaada yao imeiongezea nguvu Wizara yangu katika kutekeleza majukumu yake. Wahisani hao ninaowashukuru ni pamoja na nchi za Uholanzi na Denmark; na Mashirika ya Kimataifa ya *UNHCR, UNAFRI, WFP, IOM* na *UNDP*. Natoa shukurani ya pekee kwa Shirika la Umoja wa Mataifa la Wakimbizi *(UNHCR)* kwa namna tunavyoshirikiana kuwahimiza Wakimbizi kurudi kwao na pia kwa motisha wanayowapa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, baada ya maelezo haya, sasa naliomba Bunge lako tukufu lituwezeshe kutekeleza hayo yote niliyoyaeleza kwa kupitisha makadirio ya

matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ya jumla ya Shilingi 94,712,920,000.00 kwa mwaka wa fedha 2007/2008 kama ifuatavyo:-

Fungu la 29 – Magereza jumla shilingi bilioni 72,046,888/=. Fungu la 51 – Utawala jumla shilingi bilioni 4,878,888/=. Fungu la 93 Uhamiaji jumla shilingi bilioni 17,787,144/=. Jumla Kuu kama nilivyosema shilingi bilioni 94,712,920/=. *(Makofi)*

**WAZIRI MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Sasa kama ulivyo utaratibu wetu Mheshimiwa Waziri atafuatiwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama anakuja tena kwa niaba ya Mwenyekiti, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini. *(Makofi)*

**MHE. BENSON M. MPESYA – (K.n.y. MHE. WILLIAM J. KUSILA - MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA ULINZI NA USALAMA):** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni Na. 81(1) ya Kanuni za Bunge - Toleo la Mwaka 2004, ninatumia fursa hii kuwasilisha Taarifa na Maoni ya Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadiro ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2007/2008 na kuliomba Bunge lako Tukufu lipokee na kuijadili.

Mheshimiwa Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati unatokana na Taarifa ya Wizara ya Mambo ya Ndani kuhusu Hali ya Ulinzi na Usalama wa nchi iliyowasilishwa mbele ya Kamati Tarehe 31 Mei, 2007 na Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara iliyowasilishwa Tarehe 05 Juni, 2007 Jijini Dar es salaam. Kwa kuzingatia Kanuni Na. 81(1) na Na. 81(4) ya Kanuni za Bunge Toleo la 2004; Kamati ilipitia na Kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa ahadi za Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007 pamoja na Ushauri wa Bunge uliotolewa kwa Wizara hii. Aidha, Kamati ilipitia Mafungu ya Makadirio kwa Mwaka 2007/2008 ya Fungu 29 (Magereza), Fungu 51(Wizara ya Mambo ya Ndani – Utawala) na Fungu 93 (Uhamiaji). Kabla ya kutoa Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kutumia nafasi hii Kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa juhudi zake za kuboresha utendaji wa Wizara hii hasa pale alipoamua kufanya ziara katika Magereza.

Mheshimiwa Spika, vile vile ningependa kutumia fursa hii kumpongeza Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Joseph J. Mungai, Naibu Waziri,

Mheshimiwa Lawrence K. Masha, Katibu Mkuu, Ndugu Salmon Odunga na Wataalam wote wa Wizara kwa juhudi wanazoendelea kuzifanya katika kuboresha Utendaji wa Wizara hii ikiwa ni pamoja na kutembelea magereza mara kwa mara, kuhamasisha wakimbizi walioko katika makambi kuweza kurejea makwao na kuandaa na kuwasilisha mbele ya Kamati Taarifa inayoelezea bayana utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2006/2007. Aidha, tunampongeza Ndugu Augustino Ndukuu Nanyaro kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Kamishina Mkuu wa Magereza nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kwa namna ambavyo wamekuwa wakitoa ushirikiano mzuri katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Wajumbe wa Kamati wamekuwa bega kwa bega katika kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara zilizo chini ya Kamati kwa kutoa maoni yao na ushauri ambao Wizara imekuwa ikifanyia kazi. Ningelipenda kuwatambua Wajumbe hao wa Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa ridhaa yako kama Ifuatavyo:- Mheshimiwa William J. Kusila, Mwenyekiti , Mheshimiwa Capt. George H. Mkuchika - Makamu Mwenyekiti Wakati wajumbe wengine ni Mheshimiwa Col. Saleh A. Farrah, Mheshimiwa Mohamed A. Abdulaziz, Mheshimiwa Maria I. Hewa, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mheshimiwa Dr. John S. Malecela, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa. Wilson M. Masilingi, Mheshimiwa Col. Feteh S. Mgeni, Mheshimiwa Benson M. Mpesya, ninaye soma taarifa hii, Mheshimiwa Brig. Gen. Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Masoud A. Salim, Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya na Mheshimiwa Dr. Guido G. Sigonda.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Katibu wa Bunge, Ndugu Damian S. L. Foka na Sekretarieti ya Kamati, Ndugu Peter Magati na Ndugu Patson A. Sobha kwa kazi na huduma nzuri walizotoa kwa Kamati na hivyo kuiwezesha kutekeleza majukumu yake na pia kukamilisha taarifa hii. Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni na Ushauri Wakamati na Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2006/2007, Kamati ilipokea na kuchambua kwa kina taarifa kuhusu Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati na Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2006/2007.

Maelezo ya kina yalitolewa kuhusu dira, mwelekeo na majukumu ya Wizara, Utekelezaji wa Maagizo/Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Mwaka 2006/2007 pamoja na mafanikio na matatizo ya utekelezaji katika mwaka wa Fedha wa 2006/2007. Aidha, Kamati ilipata maelezo ya kazi zitakazotekelezwa katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2007/2008 na yalitolewa Maombi ya Fedha za Matumizi kwa kazi zilizopangwa kufanyika katika mwaka wa Fedha 2007/2008. *(Makofi)*

Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba Wizara hii imetekeleza kwa kiasi kikubwa Majukumu yake na pia imefanyia kazi Maoni na Ushauri wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama na utekelezaji wake unaonekana dhahiri. Pamoja na Mambo mengine, Wizara imeonyesha mafanikio katika utekelezaji wa masuala mbali mbali yakiwemo:- (i)Kufanikiwa kuwarejesha makwao kwa hiari yao jumla ya Wakimbizi 54,920 hadi Mei, 2007 na kufanikiwa kufunga makambi ya Mkungwa-Kibondo, Mtendeli-Kibondo, Mwisa-Karagwe na Muyovosi-Kasulu.

(ii) Kuimarisha hali ya usalama katika Makambi.

(iii) Kuimarisha msako wa Wahamiaji haramu na hivyo kufanikiwa kukamata Wahamiaji Haramu 812 kutoka Ethiopia na Somalia.

(iv) Kuongeza udhibiti wa uingiaji na utokaji wa wageni nchini.

(v) Kununua Jengo la Ofisi ya Mradi wa Vitambulisho vya Kitaifa na kuendelea na mchakato wa kuundwa kwa Wakala atakayesimamia mradi huo, na

(vi) Utekelezaji wa kampeni ya upandaji miti,mradi unaotekelezwa katika Magereza yote nchini kwa kupanda jumla ya ekari 6,158 za miti ipatayo 3,879,540.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, katika maeneo mengine ambako Kamati imeona kuna upungufu na juhudi zaidi zinahitajika, imeweza kushauri ipasavyo. Maeneo husika ni pamoja na:-

§ Bado tunaiomba Wizara ijitaidi kupunguza Msongamano wa Mahabusu

§ Kutenganisha mahabusu ya watoto na watu wazima.

§ Kuongeza juhudi katika udhibiti wa Wahamiajiharamu hasa wa Somalia na Pakistan, na

§ Kuboresha utendaji wa Kikosi cha Zimamoto naUokoaji.

Mheshimiwa Spika, Matatizo Yaliyojitokeza Wakati wa Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara, pamoja na mafanikio ambayo Kamati imeyataja kwa muhtasari, pia kulikuwepo na matatizo yaliyojitokeza katika utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2006/2007:-

· Ufinyu wa Bajeti ambao umeathiri utekelezaji wa mipango mbalimbali ya Wizara.

· Upungufu wa idadi ya Askari Magereza, Maafisa Uhamiaji na Maafisa wa Vikosi vya Zimamoto na Uokoaji.

· Upungufu wa Ofisi na Vitendea kazi vya kisasa ikiwa ni pamoja na magari ya kusafirisha mahabusu, magari kwa watumishi wa Wizara na Idara zake, magari ya Zimamoto na vyombo vya mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, Vipaumbele vya Wizara kwa Bajeti ya 2007/2008, Kamati iliridhika na vipaumbele vya Wizara kwa bajeti ya mwaka 2007/2008 ambavyo baadhi yake ni:-

(a) Maendeleo ya watumishi, ambapo Wizara inatarajia kuajiri askari wa Magereza wapya 850 na kuwapatia mafunzo ya awali *(Basic Training)* na Kutoa mafunzo mbali mbali *(Advanced Training)* kwa watumishi wa Magereza, askari, Maafisa na Makamanda wa Zimamoto pamoja na Maafisa Uhamiaji.

(b) Kuanzisha Ofisi za Mikoa na Wilaya (*Comand Posts*) za Zimamoto na Uokoaji.

(c) Kukarabati majengo na miundombinu ya Magereza yenye ulinzi mkali, kukamilisha miradi inayoendelea ya mabweni ya wafungwa na Ofisi za Utawala katika Magereza, kukarabati nyumba za maafisa na askari, kuimarisha Mifumo ya Maji Safi na Maji Taka na kuendelea na ukarabati wa Chuo cha Maafisa wa Magereza Ukonga na Kiwira - Mbeya na Kuendeleza ujenzi wa Jengo la Ofisi Makao Makuu.

(d) Kupima na kulipia maeneo yaliyotwaliwa na Idara ya Magereza katika vituo vya Ubena, Wami Kuu na Wami Vijana, Ngwala, Chuo cha Kiwira, Matongo na Segerea.

(e) Kuendeleza uzalishaji katika mashamba ya kilimo na mifugo kwa kutoa zana na pembejeo zinazohitajika. Pia kuhifadhi mazingira kwa kupanda miti katika Magereza mbali mbali.

(f) Kuendeleza viwanda vya useremala kwa Vituo vya Arusha, Tabora na Ukonga kwa kununua mashine za karakana.

(g) Kuendeleza juhudi za mapambano dhidi ya UKIMWI.

(h) Kuendelea na mradi wa kuboresha uendeshaji wa shughuli za wafungwa kwa kutumia kompyuta *(OMIS) Offenders Management Information System*. Mfumo huu utaliwezesha jeshi la Magereza kuendesha shughuli zake kisayansi kwa kupata taarifa muhimu za wafungwa kwa taasisi zote zinazosimamia sheria nchini.

(i) Ununuzi wa magari, piki piki na Boti za doria katika Bahari na Maziwa kwa ajiri ya Idara ya Uhamiaji na,

(j) Kufanya matengenezo ya mitambo ya kuchapisha Paspoti. Miradi Ambayo Haikutekelezwa 2006/2007 Kutokana na Ufinyu wa Bajeti

- Ukamilishaji wa Makao Makuu ya Magereza, Dar es Salaam

- Ukamilishaji wa ukarabati wa mabweni mawili ya Wafungwa yaliyosalia kwenye Gereza la Uyui, Tabora

- Ukamilishaji wa ukarabati wa mfumo wa majitaka kwenye Gereza la Ukonga, Dar es Salaam.

- Ujenzi wa nyumba za familia 24, nyumba ya Mkuu wa Gereza la Ubena, Kibaha na ujenzi wa nyumba za Wakuu wa Vituo vya Namajani, Utete, Rombo na Kibiti.

- Ujenzi wa banda la kupumzikia Wafungwa Gereza la Wanawake Arusha, Ofisi ya Gereza la Wanawake Magu na Ujenzi wa Bweni la Wafungwa Sumbawanga.

- Kulipia fidia ya ardhi na majengo katika maeneo ya Gereza, la Lushoto.

- Kuimarisha viwanda vya Mbao vya Uyui, Ukonga na Arusha pamoja na ununuzi wa vifaa vya Karakana ya Ukonga.

- Kuimarisha mtandao wa Kompyuta magerezani.

- Ununuzi wa mitamba ya Borani kwa ajili ya Gereza Isupilo, Ubena na Mafia.
    - Ulipaji wa madeni yaliyotokana na uboreshaji wa mazingira ya kazi za Watumishi kutokana na kuundwa kwa Wizara mbili sehemu moja ya Mambo ya Ndani ya Nchi na ya Usalama wa Raia.

    - Kushindwa kumalizia deni la waliofanya upembuzi yakinifu juu ya mradi wa vitambulisho vya Taifa.

    - Kushindwa kufanya malipo kwa mujibu wa Mkataba wa ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Dar es Salaam.

    - Kushindwa kujenga majengo ya Ofisi ya Mkuu wa Manyara na Kituo cha Kagunga.

    - Kushidnwa kukarabati nyumba za makazi ya Askari kaika Mikoa ya Pwani, Kilimanjaro, Mtwara, na vituo vya Manyovu, Mabamba Rusumo na Sirari.

    - Kushindwa kununua mafuta ya jenereta zilizofungwa mipakani kwa ajili ya kuendesha mitambo ya (*Visa Sticker*).

    - Kushindwa kupata malighafi (*Consumables*) kwa ajili yakuchapishia pasipoti.

Mheshimiwa Spika, Malengo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2007/2008, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007, vilevile Kamati ilipokea maelezo kuhusu kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka huo. Katika Makadirio hayo Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inaomba kuidhinishiwa kwa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida Jumla ya Shilingi 67,377,888,000/= kwa Fungu 29 ambalo ni la (Magereza), Shilingi 3,994,937,000/= kwa Fungu 51 (Utawala) Shilingi 13,379,144,000/= kwa Fungu 93 (Uhamiaji).

Kwa upande wa Maendeleo, Wizara inaomba kuidhinishiwa Jumla ya Shilingi 4,669,000,000/= kwa Fungu 29 (Magereza), Shilingi 884,000,000/= kwa Fungu 51 (Utawala) na Shilingi 4,459,000,000/= kwa Fungu 93 (Uhamiaji). Ambapo jumla kuu ya maombi yote ni shilingi 94,763,969,000/=

Mheshimiwa Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati, baada ya kutoa Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2007/2008, sasa naomba kutoa ushauri wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka 2007/2008:

- Kamati inaishauri Serikali kuwa mjadala unaoendelea kuhusu uraia wa nchi zaidi ya moja *(dual nationality)* ukamilishwe haraka.

- Serikali ikamilishe utaratibu wa upatikanaji wa vitambulisho vya kitaifa haraka.

- Kamati inashauri Mradi wa Jengo la Makao Makuu ya Wizara uwezeshwe kwa kuongezewa fedha zaidi ili kuweza kukamilishwa kwa ujenzi huo ambao kwa mwaka wa fedha 2007/2008,umetengewa shilingi milion 884 tu,wakati tayari kuna deni la shilingi bilioni moja na hivyo kufanya ujenzi usimame.

- Kamati inashauri kuwa Serikali iangalie namna ya kujenga mahakama karibu na magereza ili kupunguza kusafirisha wafungwa na mahabusu kwa umbali mrefu.

- Serikali iongeze idadi ya Mabweni ya Wafungwa na Mahabusu ikiwa ni pamoja na magari ya kusafirishia Wafungwa na Mahabusu hao.

- Serikali iimarishe ulinzi wa Mipakani, Viwanja vya Ndege na Bandari. Aidha, Serikali iwe makini zaidi na Wahamiaji kutoka Pakistan na Somalia ambako kuna viashiria vya mahusiano ya Kigaidi.

- Serikali itoe semina na mafunzo zaidi kwa Askari wetu ili waweze kukabiliana na changamoto zinazowakabili. Aidha utaratibu wa kujaza mapengo kutokana na askari wengine kufa,kustaafu au kufukuzwa uwe ni zoezi la kuendelea kwa kadri mapengo yanavyojitokeza.
- Vikosi vya Zimamoto na Uokoaji viimarishwe kwa kupatiwa zana na vitendea kazi vya kisasa, ikiwa ni pamoja na kuboresha *Fire and Rescue Services* kwa kuongeza fedha zaidi na kuhakikisha kwamba miji na manispaa zote zinakuwa na magari ya zimamoto.

- Ili kuweza kuharakisha uendeshaji wa kesi, na kupunguza msongamano wa Mahabusu, Serikali iunde Kamati ya kufuatilia wale wenye kustahili kuendelea kuwepo mahabusu na wanaostahili kutolewa.

- Ili kuimarisha uzalishaji katika Kilimo Serikali iwezeshe Idara ya Magereza kwa kuipatia pembejeo na zana za kutosha ikiwemo kuongeza idadi ya matrekta.

- Kiasi kikubwa cha maduhuli ya Wizara ya Mambo ya Ndani yaelekezwe kutumika ndani ya Wizara yenyewe katika kuendeleza miradi ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, Mwisho, mwisho naomba nikushukuru tena wewe binafsi kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MHE. MHONGA SAID RUHWANYA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI, WIZAYA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 43 (5)(b)(c) na 81(1) toleo la 2004 kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusiana na Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani kwa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwepo hapa leo kujadili mambo muhimu kwa maslahi ya umma wa Watanzania na kwa mema yote ambayo amekuwa akitujaalia. Ni matumaini yangu kwamba majadiliano yetu yataweka mbele maslahi ya Umma. Mungu atusaidie.

Mheshimiwa Spika, napenda kwa nafasi ya kipekee kabisa kukishukuru chama changu cha CHADEMA kwa kuendelea kuniunga mkono katika kazi walizonikabidhi katika kipindi cha 2005-2010. Ninawaahidi kuwa kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu nitaendelea kuwatumikia wananchi kwa uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, pia natoa shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Hemed Mohammed, Naibu Waziri Kivuli wa wizara yangu, kwa mchango wake mkubwa katika kufanikisha uandaaji wa hotuba hii. Nawashukuru sana pia Mhe. Hamad Rashid Mohammed, Kiongozi wa Upinzani Bungeni na Naibu wake Mhe. Dr. Willibrod Slaa , kwa kutoa muongozo sahihi kwa Kambi kwa mujibu wa kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2006/2007 tumempoteza mwenzetu, Hayati Juma Jamaldin Akukweti na hivi karibuni tu Hayati Amina Chifupa. Hivyo kwa majonzi makubwa, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba niungane na wenzangu kutoa salamu za pole kwa ndugu, rafiki, jamaa na familia za marehemu. Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi. Amin.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuungana na wenzangu kutoa pole kwa wale wote waliofikwa na misiba na ajali katika kipindi hiki chote tukiwa hapa Bungeni. Mungu awafariji katika wakati huu mgumu. Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza kwa dhati Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri mpya ya wilaya Tarime kwa kupata ushindi wa kishindo dhidi ya wagombea wa CCM. Matokeo yanayoifanya CHADEMA kutawala/kuongoza Halmashauri ya Wilaya ya Tarime. Naamini kabisa watatumia fursa hii adhimu kuwaletea maendelea wananchi wa Tarime kama tulivyofanikiwa katika Halmashauri tunazoziongoza! Ninawaasa viongozi hao

wapya wa Tarime washirikiane na wananchi ili kutimiza kauli mbiu yetu ya mabadiliko ya kweli na uhuru wa kweli hivyo basi hakuna kulala mpaka maendeleo ya Tarime yapatikane kutokana na rasilimali nyingi zilizopo Tarime. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Idara ya Magereza idara ya magereza ni mojawapo ya idara muhimu katika Serikali yetu ya Tanzania, iliyopewa jukumu muhimu sana kwa maendeleo ya jamii yetu. Dira ya idara hii ni kuwa mfumo wa kurekebisha raia waliopatikana na hatia ya kuvunja sheria za nchi ili watokapo gerezani wawe raia wema katika jamii yetu.

Ni ukweli kuwa kila sehemu ya kazi kuna kanuni na sheria zinazoendesha pahala hapo. Katika idara hii kuna malalamiko kuwa pindi askari anapotenda kosa anakatwa fedha kiasi kadhaa toka katika mshahara wake na mara nyingi bila mhusika kupewa risiti, Kambi ya Upinzani inataka maelezo fedha hizo huwa zinapelekwa wapi?

Na kwanini zikatwe kwenye mshahara wake kabla bila taratibu za kisheria kufuatwa ikiwa ni pamoja na haki ya kumsikiliza mhusika kikamilifu?

Mheshimiwa Spika, Kwanza naomba niongelee magereza ya kilimo kama vile:- Gereza la Kigongoni- Bagamoyo, Gereza la Kiberege –Morogoro, Gereza la Wami Mkuu, Gereza la Kibiti- Pwani n.k. Magereza haya yanazalisha japokuwa takwimu zinaonyesha si kwa kiasi kama kile kilichokuwa kikizalishwa miaka ya nyuma. Pamoja na uzalishaji huo wafungwa katika magereza hayo wanaishi katika hali ngumu sana inayosababishwa kwa upande mmoja na ukatili wa mfumo wenyewe wa Magereza, kwani kuna malalamiko kuwa baadhi ya wakuu wa Magereza husika huwafanya baadhi ya wafungwa kama ni wa kwao binafsi kwa kufanya kazi hadi za kuosha vyombo majumbani mwao, kulima katika mashamba yao na kwa hali kama hii mfungwa anaweza kukaa jela hata baada ya kifungo chake kumalizika. Mbali ya hayo swali la msingi la kujiuliza ni kuwa ni kiasi gani kinazalishwa katika magereza hayo ni nani anakidhibiti, Serikali inapata kiasi gani au kinasaidiaje kupunguza bajeti ya magereza.

Mheshimiwa Spika, Kwa mtazamo wa kambi ya upinzani na kwa kupitia ripoti za utekelezaji za Wizara hii mwaka 2006/2007 inaelekea bado hoja nilizotoa mwaka jana hazijatekelezwa au kupewa maelezo yanayoridhisha.

Mheshimiwa Spika, katika ripoti ya *Legal and Human Rights Centre* (*LHRC*) na *Zanzibar Legal Service Centre (ZLSC)* kwa pamoja ya mwaka 2006, magereza yetu yameendelea kulalamikiwa kwa uvunjaji wa misingi ya haki za binadamu kwa kutozingatia haki za wafungwa na mahabusu. Msongamano mkubwa wa wafungwa katika magereza zetu hasa zile za Dar Es Salaam limekuwa jambo linalosababisha uvunjifu mkubwa wa haki za binadamu, japokuwa vyumba vya magereza yetu kuwa na uwezo wa kuchukua wafungwa 15 hadi 25 lakini hali halisi vinachukua wafungwa mara 2 hadi tatu ya uwezo wake jambo linalosababisha uwezekano wa kupoteza maisha yao au kutokea milipuko ya magonjwa.Kutokana na hali hii na ukweli kuwa wanaoingia gerezani ni wengi kuliko wanaotoka, hivyo basi tunaiomba Serikali ilieleze Bunge hili ni wafungwa wangapi wamefungwa gerezani kati ya mwaka 1995 na 2005 na kutoka

salama bila kuathirika kiafya au kupoteza maisha, na ni wangu wamepata magonjwa ya kuambukiza wakiwa gerezani na ni wangapi wamefariki wakiwa gerezani.

Mheshimiwa Spika, vitisho kwa wafungwa, rushwa, kubambikizwa kesi kwa wasio na hatia, kuchelewesha hukumu, na kuswekwa rumande kwa muda mrefu, ni miongoni mwa shida kubwa zinazowakumba Watanzania wenzetu walioko katika kuta za magereza. Katika malalamiko yaliyotolewa na wafungwa wa gereza la Maswa Mkoani Shinyanga Mei mwaka huu kwa Mhe. Waziri, kama ilivyoripotiwa na vyombo vya habari, ni kuwa licha ya misamaha inayotolewa kila mwaka na Rais, na uwepo wa *PAROLE ACT NO. 25 OF* 1994 na marekebisho yake ya mwaka 2002, na ile ya *COMMUNITY SERVICE ACT NO*. 6 *OF* 2002 hakuna hata mfungwa mmoja aliyeachiwa huru katika Wilaya ya Maswa tokea mwaka 1996. Ingawa kuna maelezo ya Waziri yanaonyesha kuwa wafungwa 2651 wametolewa kwa payroll wafungwa 8651 kwa msamaha wa Rais na wafungwa 931 kwa kifungu cha nje. Lakini bado kwa ujumla wake Kambi ya Upinzani inaona sheria hizi kama ni kiini macho kwa watanzania, hivyo basi inaitaka Serikali ilieleze Bunge hili kati ya wafungwa wapatao 60,000 pamoja na idadi hii aliyoitaja, tangu sheria hii ianzishwe ni wangapi wameishatoka gerezani kwa sheria hizi? Na ni wangapi wanatumikia kifungo cha nje chini ya Sheria hizi? Sheria ambazo kimsingi zililenga kupunguza kwa kiasi kikubwa msongamano magerezani. Kambi ya vyama vya Ushindani inapenda ielezwe kwa kina ni matatizo gani yamejitokeza katika utekelezaji wa sheria hizi.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa tatizo la Watanzania wanaokaa mahabusu kwa muda mrefu kwa kisingizio cha kutokamilika kwa upelelezi, Serikali ni lazima ichukue maamuzi mazito kwa makusudi katika sekta ya mahakama zetu ili kushughulikia matatizo ya kisheria yanayowakumba ndugu zetu waliopo katika magereza yetu. Serikali ihakikishe kuwa kesi zilizokaa kwa muda mrefu zinashughulikiwa haraka ili wahusika watendewe haki. Ahadi ya Serikali ya Awamu ya nne ya maisha bora kwa kila Mtanzania iwaguse hata wafungwa na mahabusu kwani nao ni Watanzania, walau kwa Kuboresha mazingira yao waishiyo, chakula chao na kuzingatiwa haki zao za msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa taarifa zilizopo ni kuwa kila mfungwa anatengewa na Serikali shilingi 2500/= kwa siku kwa ajili ya chakula chake. Lakini kwa kulingana na taarifa zilizopo ni kuwa wafungwa hao wanapata mlo mmoja ugali na maharage tu kwa siku, na katika magereza mengi bila kubadilisha chakula hiki siku nenda siku rudi jambo linalohatarisha afya ya Wafungwa na watuhumiwa.

Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ilieleze Bunge hili hizo pesa zinazowekwa kwenye Bajeti hiyo zina mhudumia mfungwa kwa chakula cha aina gani kwa siku ili utaratibu mahususi wa kuwahudumia wafungwa na watuhumiwa wetu ujulikane kwa wote ikizingatiwa kuwa hata kama ni wafungwa bado wana haki zao za msingi kama binadamu.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana pia nilizungumzia tatizo la watoto wanaojikuta katika matatizo na sheria *(Children in Conflict with Law*). Jambo muhimu ambalo kambi ya upinzani ilihitaji kujua lilikuwa ni 'mkakati wa serikali' katika upanuzi wa magereza

machache ya watoto yaliyopo na utoaji wa fedha za kutosha kwa ajili ya huduma ya malezi kwa watoto na vijana mara wakutwapo na matatizo ya kisheria na kufungwa.

Mheshimiwa Spika, katika kupitia taarifa inayoonesha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka wa fedha 2006/2007 pamoja na ripoti inayoonesha Shabaha na Malengo ya Bajeti ya mwaka 2007/2008 kwa Wizara ya Mambo ya Ndani suala la upanuzi wa magereza ya watoto halionekani kupewa kipaumbele kabisa.

Mheshimiwa Spika, cha kushangaza ni kwamba vipaumbele upande wa shughuli za ujenzi za jeshi la magereza katika mwaka 2006/2007 havitofautiani na vya mwaka 2007/2008. Naweza kusema kuwa kazi iliyofanyika ni kunakili ya mwaka uliopita kwa ajili ya mwaka mpya wa bajeti (*copy and paste*).

Hii ina maanisha nini? Je, ni kwamba hakuna kilichofanyika? Na kama ndivyo, je kiasi kilichotengwa kwa shughuli hizo kimeenda wapi? Kama shughuli hizo zilifanyika, kwa nini basi ziendelee kupewa vipaumbele wakati zipo shughuli nyingine nyingi za kufanywa kama hizi tunazozipendekeza? Kwa mfano; kwa nini fedha nyingine zisipangwe kwa ajili ya utanuzi wa magereza ya watoto au kuboresha chakula, na afya za wafungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kambi ya upinzani inataka maelezo ya kina kuhusiana na suala zima la upanuzi wa magereza ya watoto na jinsi utekelezaji wa vipaumbele vinavyowekwa katika Bajeti unavyokwenda.

Mheshimiwa Spika, katika nyakati hizi za mapambano dhidi ya UKIMWI kambi ya upinzani inataka kuelezwa juhudi ambazo zimefanywa na Serikali katika kupiga vita UKIMWI Magerezani. Naibu Waziri hapo tarehe 11 Julai katika majibu yake alikana uwepo wa maambukizo ya UKIMWI magerezani jambo ambalo si kweli. Ni wazi na kila mmoja wetu anatambua kuwa maambukizo ya janga la UKIMWI yameenea sehemu zote za jamii yetu hata kwa wale walio magerezani. Mheshimiwa Spika, katika malengo ya bajeti ya mwaka jana inaelezwa kuwa Benki ya dunia ilitoa kiasi cha shilingi billion 2 kwa ajili ya mradi wa kuzuia ukimwi *(Tanzania Multi-Sectorial Aids Project*).

Mheshimiwa Spika, ni vizuri serikali ikatueleza ni jinsi gani fedha hizi zilitumika na zilisaidiaje kuboresha mfumo mzima wa utoaji huduma za afya na kupiga vita dhidi ya gonjwa la UKIMWI magerezani. Vile vile, ni mikakati gani mingine ambayo imepangwa ili kuwasaidia wenzetu waliopo magerezani kupambana na janga la UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, sanjari na janga la UKIMWI huduma za afya kiujumla wake katika magereza ni duni sana. Kibaya zaidi ni kwamba yamekuwepo magonjwa ya kuambukizwa kutokana na hali ya usafi duni iliyopo katika magereza yetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa waziri alikanusha, taarifa zilizopo ni kuwa wafungwa wanataabika sana hasa wale wasio na ndugu au wenye ndugu masikini. Hii ni kwa sababu ndugu hao ndio ambao wamekuwa wakibeba mzigo wa kuwahudumia wafungwa ndugu zao, baadhi yao wakilazimika hata kuwanunulia dawa na ushahidi upo ukihitajika, wakati hili ni jukumu la Serikali. Kambi ya upinzani inaiomba Serikali

kuliangalia hili kwa umakini sana kwani hali ya kiafya huko magerezani si ya kuridhisha hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika hotuba yangu ya mwaka jana narudia kusema kwamba inatupasa tutambue kuwa walio ndani ya kuta zile za magereza ni binadamu kama sisi na wanastahili kutendewa haki na usawa kama binadamu wengine. Kupatikana na hatia ya kuvunja sheria za nchi hakumfanyi mtu kuondolewa utu wake.

Mheshimiwa Spika, mwanzoni mwa mwaka 2007, kulikuwa na wimbi kubwa la watuhumiwa walioko Rumande kugoma kuteremka kwenye makaranginga, hali iliyoikumba hasa mikoa ya Dar-Es-Salaam na Arusha. Serikali ilifanya mpango maalum wa kuwatuma viongozi wa ngazi ya juu kuwatembelea na kuwatuliza Watuhumiwa hao. Kambi ya Upinzani inapenda kupata taarifa ya kina ya mambo yafuatayo:-

(i) Je, Serikali inaweza sasa kuliarifu Bunge hili, ni sababu zipi hasa zilizowafikisha watuhumiwa hao kugoma?

(ii) Serikali iliatoa ahadi kupitia mawaziri wake waliotembelea magereza hayo kuwa ndani ya miezi miwili itashughulikia kero mbalimbali zilizoorodheshwa na watuhumiwa hao. Leo ni karibu miezi mine tangu ahadi hiyo, Serikali inaweza kulieleza Bunge hili ni ahadi zipi zimetekelezwa kati ya ahadi zilizotolewa katika ziara zile?

(iii) Serikali imechukua hatua zipi za makusudi kuona kuwa hali kama ile haitajirudia tena, na wakati huo huo haki za msingi za Watuhumiwa zikizingatiwa? Iwapo kuna dosari za kisheria, ni Sheria zipi zinahitaji kufanyiwa marekebisho, na ni lini sasa Serikali itawasilisha Marekebisho hayo ya Sheria Bungeni?

Mheshimiwa Spika, Suala lingine linalohusiana na idara hii ya magereza ni kuhusu shughuli na miradi ya vitega uchumi na uzalishaji mali magerezani kama vile kilimo, useremala, ujenzi, ufugaji nakadhalika, ambazo zimekuwa chanzo kikubwa cha mapato magerezani.

Katika makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ya mwaka wa fedha uliopita, kiasi cha shilingi milioni 500 (500,000,000) zilipitishwa kwa ajili ya kuboresha viwanda vya magereza na shilingi milioni 500 ziliombwa kwa ajili ya kuboresha mashamba ya magereza.

Mheshimiwa Spika, kabla hatujapitisha mamilioni mengine kwa mwaka huu, Watanzania wanapaswa kujua yafuatayo:-

(i) Fedha zilizotengwa mwaka jana zimetumikaje na kama kuna fedha zozote kati ya hizo zimetumika tofauti na zilivyokusudiwa.

(ii) Miradi yote ya magereza inayohusisha wafungwa imeingiza kiasi gani cha fedha kwa kipindi cha mwaka uliopita na fedha hizi zimetumikaje?

(iii) Wafungwa wanaoshiriki katika miradi hiyo wanafaidikaje?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ingependa kutoa ushauri kuwa magereza yafufue miradi kulingana na mazingira yake ili yazalishe yenyewe yasitegemee Serikali na ikiwezekana yatengwe kulingana na shughuli zake. Yawepo ya kilimo, uhunzi, ufugaji, viwanda vidogo vidogo. Kwa mfano, utengenezaji sabuni Mbeya Kiwira, na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Uhamiaji ni moja ya mihimili nyeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani na yenye manufaa makubwa kwa taifa letu kama kazi zake zitafanywa kwa umakini, na endapo Serikali itafanya maamuzi sahihi yahusuyo Idara hii. Licha ya kuliokoa Taifa na wahamiaji haramu Idara hii inaweza kutumika kuliongezea taifa mapato kwa njia ya uwekezaji ikiwa sera na sheria endelevu zitapitishwa.

Kambi ya Upinzani inatambua juhudi zilizofanywa za kuajiri vijana wenye elimu ya juu na kuboresha vitendea kazi katika Idara hii. Hata hivyo, bado kero za mianya ya rushwa, uzembe na usumbufu usio wa lazima vinadhoofisha utendaji wake. Kambi ya Upinzani inaitaka Idara hii ichukue hatua za makusudi kusafisha maafisa wake wachache wanaopokea rushwa hasa katika vitengo vya utoaji wa fomu za hati za kusafiria mikoani. Maafisa hao wachache wanaichafua sura ya Idara hii muhimu ndani na nje ya nchi yetu. Udhibiti wa Pasipoti zetu nao uimarishwe zaidi, lakini bila kuongeza usumbufu usio wa lazima na kauli ya watendaji iboreshwe zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika mchakato mzima wa uharakishwaji wa shirikisho la Afrika Mashariki, Serikali yetu ni lazima iwe makini sana kwa kuweka mikakati ya kudhibiti udanganyifu na kuwatambua raia wake wote. Kushindwa kufanya hivyo kutalifanya Taifa livamiwe na wahamiaji haramu, na lishindwe kuwatambua watu wake hususan pale mchanganyiko wa raia wa nchi hizi utakapohalalishwa chini ya Serikali ya Shirikisho. Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kwamba Idara ya Uhamiaji iendelee kupatiwa vifaa vya kisasa ambavyo vitaweza kushindana na mabadiliko ya kiteknolojia ambayo huwezesha wahalifu mbalimbali kukwepa mitego inayowekwa na watendaji wetu kunasa wavunja sheria.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo ni kuboresha mawasiliano ambayo yatawezesha vituo vyetu mipakani kuunganishwa na ofisi zingine wilayani, mikoani na makao makuu kiteknolojia ili kuondoa usumbufu na kukosekana kwa habari nyeti za wageni wetu waingiapo na watokapo nchini mwetu.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara hii ishirikiane na Wizara ya Usalama wa Raia ambao wao wana mfumo mzuri wa mawasiliano hasa katika mipaka yetu, mathalani mipaka yetu katika maeneo ya Kagunga, Kigoma, Namanga, Tunduma na maeneo mengine yenye ofisi za mipakani za uhamiaji. Aidha, kuna suala la vibali vya kuingia nchini (*visa*) kwa shughuli za kibiashara ambavyo kila mtu anapoingia lazima

apate viza. Kambi ya Upinzani inashauri kwa mfanyabiashara anayeingia Tanzania na kutoka zaidi ya mara tatu kwa mwezi, ni bora ianzishwe viza ya miaka miwili ili kuondoa uwezekano wa kuijaza pasipoti yake ya kusafiria na hili litaondoa usumbufu kwa mfanyabiashara huyo wa kuomba viza ya Tanzania kila aingiapo. Lakini hatua hii kamwe isiondoe udhibiti wa wageni wanaoingia nchini kwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la uraia ni nyeti sana katika nchi yoyote duniani. Bila kuwepo umakini wa kutosha katika kushughulikia suala hili basi taifa letu linaweza kujikuta katika matatizo mbalimbali. Mfano, kuwepo kwa maadui nchini wanaojidai kuwa nao ni Watanzania, chuki kati ya wananchi na Serikali yao hasa wale waishio mipakani. Tunalisema hili kwani wapo baadhi ya watu ambao wameishi au kuzaliwa Tanzania na hata wengine kutumikia Taifa kwa muda mrefu na mwisho wa siku wakaambiwa kuwa wao si raia wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kimsingi zoezi la kuandikisha Vizazi na Vifo ni muhimu na ni lazima kuzingatiwa. Kushindwa kufanya hivyo kutalifanya Taifa lishindwe kutambua watu wake. Katika kufanikisha hili lazima uwepo utaratibu wa uandikishaji wa mtoto punde anapozaliwa, tena bila ya kuwepo usumbufu wowote. Kufuatiwa kuundwa kwa wakala wa Usajili,Ufilisi na Udhamini (*RITA*) chini ya sheria ya Wakala wa Serikali No. 30 ya mwaka 1997, sheria hii inazipa mamlaka (*semi-automony*) Wakala kujiendesha kibiashara kwa lengo la kutoa huduma bora zaidi kwa Umma.

Kambi ya Upinzani inaona kutokana na umuhimu wa Usajili ambao utalenga kuipunguzia Serikali gharama kubwa katika mifumo mikubwa, mathalani Sensa ya Taifa, Daftari la Wapiga Kura na takwimu mbalimbali za mipango kama upande wa afya, inaitaka Serikali kupitia wakala huyu kupewa kazi ya kutayarisha vitambulisho vya uraia. Tunaamini kuwa kazi hiyo itafanywa kwa ufanisi mkubwa na wakala huyu wa Serikali badala ya kutafuta kampuni za watu binafsi ambapo Serikali huingia gharama kubwa za fedha na rasimali watu katika kukusanya takwimu zinazohusiana na usajili.

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba yangu ya mwaka 2006/2007 nilizungumzia suala la uraia wa nchi mbili (*Dual Citizenship*). Katika nyakati hizi za utandawazi na ushindani wa soko huria, suala la uraia wa zaidi ya nchi moja lina umuhimu wa kipekee. Umuhimu huu unatokana na ukweli kuwa Tanzania kama nchi zingine za Dunia ya Tatu, imekumbwa na tatizo la watu wake wengi kuhamia katika mataifa mengine ikiwa kama jitihada za kujiendeleza kielimu na kiuchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatizo kama hili pia linaeleweka katika Nchi Zinazoendelea zote kwa wasomi wake kukimbilia nchi zilizoendelea (*Brain drain*) kwa maslahi ya kiuchumi. Wasomi hawa ambao ndio nguvu kazi ya Taifa kamwe hawajazichukia nchi zao, wala hawajajuta kuzaliwa katika nchi hizi, bali wamefanya maamuzi haya kukwamua maendeleo yao na familia zao. Inasikitisha kuona kuwa mpaka sasa bado kuna Watanzania wanaoendelea kupoteza uraia wao, kama Waziri alivyosema mwaka huu ni 79 ambao wangeweza kuleta tija nchini kwetu baadaye watakaporejea Tanzania tena.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina watu wake wengi nje ya nchi ambao wangelipenda kuja kusaidia kusukuma gurudumu la maendeleo nchini kwao bila ya kuathiri mafanikio waliyoyapata katika nchi walizopo. Inaeleweka kuwa katika nchi nyingi mathalani Botswana, Namibia, *Swaziland*, na nyingine nyingi ambako Watanzania wengi ambao ni wasomi wakubwa ni wataalamu wa masuala mbalimbali na wawekezaji wazuri. Hii ni hazina kubwa sana ambayo Serikali yetu hadi sasa imeshindwa kuja na mbinu thabiti za kuitumia kwa manufaa ya taifa letu. Hazina hii haihusu wale ambao wana asili ya Tanzania tu, bali hata wengine ambao nao pia wangependa kuja kwetu kushirikiana nasi kupambana na matatizo tuliyonayo.

Mheshimiwa Spika, jitahada hizi zimeweza kuisadia nchi kama vile Ghana, Ethiopia, Afrika Kusini na Rwanda kuongeza mapato yao (*GDP*) kwa asilimia kubwa sana. Kwa mfano, katika Ghana kwa sasa kiasi kikubwa cha uwekezaji kutoka nje (*Foreign Direct Investment- FDI)* kimeongezeka na sehemu kubwa inatoka kwa wawekezaji wa Kimarekani wenye asili ya Afrika, na pia sekta ya Utalii imeweza kufaidika kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, nchi hizi zote zimefanikiwa kwa kiasi kikubwa bila ya kuathiri mfumo wa kisiasa na kijamii katika nchi hizo, na tunaamini kuwa Tanzania ingependa kufaidika na matunda hayo. Vilevile mtindo wa kutowatambua wananchi wetu walio nje ambao wana uraia wa nchi zingine unasababisha chuki isiyo ya lazima baina ya wananchi hao na Serikali yetu kutokana na wao kuhisi kuwa mfumo uliopo unawabagua.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nilipendekeza njia mbalimbali ambazo Serikali yetu ingeweza kulishughulikia suala hili. Njia hizi ni kama ifuatavyo:

(i) Kuanzishwa kwa sheria ya uraia wan chi mbili (*dual citizenship)* ambayo itatoa haki kwa watu wenye asili ya Kitanzania waishio na wenye uraia wa nchi nyingine kupata haki sawa ya kiraia pindi wajapo nchini.

(ii) Kutoa haki maalumu za kiuchumi na kijamii kwa wageni mbalimbali, hasa wale ndugu zetu waafrika waliolowea ughaibuni (*African Diaspora*), wenye nia ya kuanzisha na kuendeleza miradi na mipango mbalimbali ya kimaslahi yenye kulenga ujenzi wa taifa letu.

(iii) Kutoa haki ya kuwa na hati za kusafiria za Kitanzania kwa Watanzania waishio nje bila ya kulazimika kuomba tena uraia hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Mapendekezo hayo, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ilieleze Bunge lako Tukufu, ni lini ahadi ya Rais Mstaafu wa Tatu aliyoitoa Marekani kwa Watanzania waishio huko kuwa kabla ya mwisho wa muda wake (kwa vile Serikali hii ni endelevu) atahakikisha Sheria ya *Dual Citizenship* imepitishwa? Watanzania hao wangependa kujua maandalizi ya Sheria hiyo yamefikia wapi. Mheshimiwa Waziri amesema katika maelezo yake iko katika hatua ya kujadiliwa na Baraza la Mawaziri, ni lini Baraza la Mawaziri litakamilisha mjadala huo wa Muswada ili

uletwe Bungeni na je, hali itakuwaje ikiwa Zanzibar watatoa maoni ya kutokubaliana na suala hilo? Naomba ufafanuzi katika hitimisho la Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, tukifanikiwa kufanya hayo ni wazi hata tatizo la kukosa walimu, madaktari na wataalamu wengine litapungua kwa kiasi kikubwa na kuongeza ajira kwa vijana wetu kutokana na uwekezaji watakaofanya. Tunapoweza kuwahakikishia ndugu zetu hawa kuwa hawatapoteza mafanikio ambayo tayari wameshayapata wakiwa huko nje, ni rahisi kwao kujitolea kuja nchini kufanya miradi ya muda mrefu na muda mfupi, na halafu wakarudi walipotoka kuendelea kujiimarisha na wataitangaza vyema nchi yetu. Napenda kuishukuru Serikali kwa kufuata ushauri za Kambi ya Upinzani kuhusu Idara ya Zimamoto. Tulishauri kuwa Idara hiyo irudishwe mikononi mwa Serikali kuu (Wizara ya Mambo ya Ndani) na kufanya marekebisho ya sheria. Nashukuru kuwa Muswada ulileltwa hapa Bungeni. Kama tulivyosema siku zote nchi hii ni yetu sote, na mawazo bora yasiwekwe tu kando kwa vile yametoka kwa upande wa pili. Kufuata ushauri ni jambo la kiungwana na kwa manufaa ya Taifa letu. Hata hivyo, juhudi zifanyike zaidi kuirekebisha Idara hii ili iweze kufanya kazi kikamilifu hasa katika miji na manispaa yote nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Idara ya Zimamoto inalo jukumu kubwa la kuhakikisha usalama wa maisha ya watu na mali zao, na hivyo basi ni idara inayohitaji umakini wa kiutendaji na kimikakati ili kufanikisha jukumu hilo. Cha kusikitisha ni kwamba watu wamekuwa wakipoteza maisha na mali zao kutokana na mfumo duni wa idara hii ambao unasababishwa na Serikali kutotoa kipaumbele katika kuiboresha idara hii kiutendaji. Kwa mfano, kumekuwepo ukosefu wa vituo vya magari ya zimamoto ya kutosha mikoani, wilayani na katika halmashauri wakati Serikali katika bajeti zake imekuwa ikitenga mabilioni ya pesa kununua magari ya kifahari, kukarabati ikulu, na kupoteza mabilioni mengine kwa kutoa misamaha kedekede ya kodi hasa kwa mashirika ya uwekezaji. Hii ina maana gani? Ni kwamba maisha ya Watanzania na mali zao yamekuwa si ya kuzingatiwa kabisa. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuiangalia kwa makini Idara hii kwani kushindwa kufanya hivyo ni kuhatarisha maisha ya raia wetu ambao ndio msingi wa taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, matatizo yanayodhoofisha Idara hii ni mengi sana yakiwemo ya ukosefu wa vitendea kazi, uchache wa vituo, na uchache wa magari. Mengineyo ni kama yalivyoorodheshwa katika taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Mwaka 2005/2006 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka 2006/2007. Matatizo hayo ni pamoja na ukosefu wa makao makuu ya jeshi la zimamoto na uokoaji, kutokuwepo kwa ofisi za mkoa za zimamoto, uchakavu wa vifaa, uchache wa askari wa jeshi la zimamoto na uokoaji na kutokuwepo kwa mfumo wa komandi moja na hivyo kufanya utendaji wake kuwa mgumu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inayo shauku ya kujua ni namna gani Serikali inachukua hatua za makusudi kuimarisha idara hii muhimu. Si kwamba hatutambui vipaumbele vya Bajeti ya mwaka 2007/2008 kwa upande wa jeshi la Zima Moto, bali hofu yetu ni kuwa vipaumbele hivi vimekuwa vikiwekwa katika maandishi na kukosa utendaji. Baadhi ya malengo yaliyowekwa kufikiwa mwaka 2006/2007

yamerudiwa tena kama malengo yaliyowekwa kufikiwa mwaka 2007/2008. Kwa mfano, mwaka 2006/2007 lengo mojawapo lilikuwa kuanzisha '*command post'* katika kila mkoa lengo ambalo limerudiwa tena mwaka 2007/2008 bila Serikali kutoa taarifa ya kina juu ya utekelezaji wa mpango wa mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, je hii ina maana ya kuwa malengo haya hayakufanyiwa kazi mwaka jana? Na kama ndivyo, basi Kambi ya Upinzani inaona kuwa lipo tatizo la kiutendaji. Kama yamefanyiwa kazi tungependa kujua ni kwa kiasi gani na Wilaya au Mikoa mingapi imeanzishiwa "*Command Post*" na ni muda gani tutakuwa tumefikia Mikoa na Wilaya zote nchini?

Mheshimiwa Spika, kama kila mmoja wetu anavyojua, Tanzania ni taifa linalosifika kwa ukarimu katika kupokea Wakimbizi miongoni mwa mataifa yote ya Afrika na hata Duniani. Kambi ya upinzani inalitambua hili. Watanzania wenzetu wanaoishi mipakani bado tunaendelea kuwapongeza kwa uvumilivu wao waliouonyesha na ambao bado wanaendelea kuuonyesha licha ya kero mbalimbali kama uhalifu ambao umekuwa ukifanywa na wakimbizi na uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, moja ya malengo ya idara ya wakimbizi kwa mwaka 2007/2008, ni kuendelea na zoezi la kuwarejesha wakimbizi makwao. Kambi ya Upinzani inaunga mkono zoezi zima la urejeshwaji wa wakimbizi hasa wa *Congo*, Rwanda na Burundi kwani nchi zao zinawataka kurudi kwenda kujenga mataifa yao. Isitoshe miafaka ya amani imeshafikiwa katika nchi zao na hali ni shwari.

Mheshimiwa Spika, hofu ya Upinzani ni juu ya zoezi zima linavyotekelezwa. Yamekuwepo malalamiko ya watu ambao wanadai kulazimishwa kurudi makwao kama wakimbizi wakati wao wameshakuwa Watanzania. Wanadai maisha yao yote yamekuwa Tanzania kiasi hata cha kupata haki zote ambazo raia yeyote wa Tanzania anaweza kupata, kwa mfano, kuandikishwa na kupewa kadi ya kupiga kura. Wanazo familia zao ambazo wanalazimika kuziacha pamoja na mali zao kama mifugo na mashamba.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inasikitishwa sana na jambo hili na haioni aibu kusema kuwa umekuwepo uzembe mkubwa si tu katika idara ya wakimbizi bali hata idara nyingine kama uhamiaji na ile inayoshughulikia suala zima la uraia. Iweje mtu ambaye alikubaliwa kama raia na hata akapiga kura, leo akaambiwa mkimbizi? Huyu mtu mpaka anaoa, anazaa watoto na anapata mali Wizara ihusikayo na uraia ilikuwa wapi hata inamfukuza leo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inatambua kuwa katika mikoa iliyoko mipakani kama Kigoma, Kagera, na Arusha wapo wakazi ambao kiasili si raia wa Tanzania. Wengine wamezaliwa na kukulia hapo na hata wengine wamezeekea hapo. Sehemu kubwa ya maisha yao imekuwa Tanzania na hata hawajui lolote kuhusu nchi ambazo ndizo asili yao. Ikumbukwe kuwa watu hawa hawakuja kama wakimbizi wa vita bali walikuja katika purukushani za kujitafutia maisha. Kambi ya Upinzani inaona kuwa si jambo jema kuwafukuza watu kama hawa bali ingekuwa ni busara kuweka na

kuwaeleza utaratibu na ustaarabu wa kufuata ili kuishi kihalali nchini hapa. Kila mtu anastahili haki za msingi, na anastahili heshima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la wakimbizi walioko makambini Mheshimiwa Rais katika ziara yake ya Mei, 2007 mkoani Kigoma alitoa agizo kuwa wakimbizi wote wawe wameondoka ifikapo 2008. Je, mkakati huo utatekelezwaje? Namwomba Mheshimiwa Waziri atupe maelezo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani pia inaweka msisitizo kwenye suala zima la uimarishaji wa mazingira yaliyoharibiwa na wakimbizi. Zoezi hili liende pamoja na la urejeshwaji wa wakimbizi makwao ili wakazi wa maeneo hayo waendelee kunufaika na maeneo hayo katika shughuli zao mbalimbali kama ufugaji na kilimo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, baada ya kuyasema hayo, kwa mara nyingine natoa shukurani zangu kwako kwa kunipa fursa hii na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza, nasema ahsanteni sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya. Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kama ilivyokuwa kwa Waheshimiwa Mawaziri waliotangulia, anao wageni, ilikuwa ni vema tuweze kuwatambua: nao ni Kamishna Mkuu wa Magereza, Ndugu Augustine Nanyalo, nakupa pongezi sana kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kushika kazi hiyo nzito.

Tunaye pia Mkurugenzi wa Uhamiaji ambaye yeye kwa wakati huu pia ndiye Kaimu Katibu Mkuu. Kama mnavyojua, jana tu ndio tumetangaziwa jina la Katibu Mkuu Mpya, kwa hiyo, Ndugu Kihomano ambaye ni Mkurugenzi wa Uhamiaji anakaimu nafasi hiyo kwa muda huu ambao tuko kwenye bajeti hapa. Tunaye Mkurugenzi wa Idara ya Wakimbizi ndugu Judith Mtawale, tunaye Kamishna wa Zimamoto na Uokoaji, Ndugu Soteri Mtanturano, tunaye Mratibu wa Huduma za Jamii, Ndugu O. Malisa na Mkurugenzi wa Sera na Mipango katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Ndugu G.R Mbunda, ahsanteni sana! (*Makofi*)

Kama mnavyoona wapo na maafisa wengine: tunao Maafisa Magereza kwenye *gallery* ambao wamekuja kusikiliza hotuba ya Waziri na mijadala ya Waheshimiwa; tunao pia Maafisa Uhamiaji, naona kama sare zile nyingine ni za uhamiaji, basi tunashukuru kwa hayo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge ninayo orodha hapa ya Wabunge 13 walioomba kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Kama kawaida tutaanza na wale ambao hawajachangia, halafu waliochangia mara moja, waliochangia mara mbili, kadri itakavyokuwa. Naomba niwataje angalau wale wanne wa kwanza. Atakayetangulia ni Mheshimiwa Mariam Kasembe ambaye hajachangia, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani ambaye alichangia mara moja,

Mheshimiwa Mauridah Komu, Mheshimiwa Manju Msambya, hao wanne kwa mpangiliao huo ndio watakaoongea. Baadaye tutaendelea tena na watakaotajwa. Kwa sasa hivi namwomba Mwenyekiti, Mheshimiwa Job Ndugai, akalie Kiti, nina shughuli nyingine inayonikabili.

*(Hapa Mwenyekiti (Mheshimiwa Job Y. Ndugai alikalia Kiti)*

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kwanza kabisa asubuhi hii ya leo kuweza kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Mambo ya Ndani. Ninasema ahsante sana, na niko tayari kuchangia kama ifuatavyo:

Kwanza kabisa, napenda nichukue nafasi hii nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kunipa uwezo wa kushiriki vikao hivi vya Bunge vinavyoendelea hapa Dodoma. Lakini vilevile nishukuru kupata nafasi hii naanza kumpongeza ndugu yangu, Shaibu Mnunduma aliyekuwa Afisa Kilimo, Wilaya ya Masasi, kwa kuteuliwa kwake kuwa Mkurugenzi Mtendaji katika Halmashauri ya Bukoba. Namtakia safari njema huko Bukoba akaanze kazi vizuri na akawe mwajibikaji na mchapa kazi kama alivyokuwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Masasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nichukue nafasi hii kuwapongeza ndugu zangu wa Wilaya ya Nanyumbu kwa kuweza kupata Mkurugenzi Mtendaji mpya na kuanzisha Halmashauri mpya. Hivyo nawaomba ndugu zangu wa Nanyumbu washirikiane na mtendaji huyu ili kuweza kujiharakishia kuleta maendeleo katika Wilaya yao kwa kasi mpya, ari mpya na nguvu mpya, kwa ajili ya kuleta maendeleo kwa wananchi ili wawe na maisha bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii sasa kuipongeza Wizara hii ya Mambo ya Ndani kwa kazi nzuri wanazozifanya katika mazingira magumu sana. Ukiangalia bajeti ya kila mwaka jinsi inavyokuwa finyu, lakini kazi zao zinaenda vizuri. Kwa hiyo, nawapongeza sana lakini naiomba Serikali sasa tuiangalie hasa Wizara hii ya Mambo ya Ndani, ni majukumu gani waliyonayo yanayowakwaza na kila mwaka hayawezi kutekelezeka kwa sababu ya bajeti finyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze Wizara hii kwa kushiriki kwao kila mwaka katika maonyesho ya Saba Saba, hasa wenzetu wa magereza na hatimaye mwaka huu kuweza kupata ushindi. Wameweza kuonyesha bidhaa mbalimbali katika maonyesho hayo.

Kazi mbalimbali zinazofanywa na ndugu zetu walioko magereza, zinatuonyesha hali halisi kwamba huko magereza si adhabu tu wanazozipata wafungwa lakini vilevile wanaweza kupata mafunzo yaliyo mengi na hatimaye watakapoweza kutoka watakuwa wajasiriamali wazuri huku nje. Ninawatakiwa kila la heri waendelee kuwa wabunifu; waendelee kutoa elimu mbalimbali kwa hawa wenzetu walioko magereza ili waondokane na ile dhana labda ya uhalifu na mambo mbalimbali ambayo yamewasababisha kuwepo katika magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na salamu zangu nilizoanza kuzitoa, naomba sasa nianze kuchangia moja kwa moja katika Idara hii ya Magereza. Mara kwa mara tunapochangia hotuba mbalimbali hapa Bungeni tumekuwa tukizungumzia sana suala la Jeshi la Ulinzi, Jeshi la Polisi, lakini mara nyingi wenzetu wa Magereza tumekuwa tukitoa mchango mdogo sana. Kwa hiyo, mimi nitachukua nafasi kubwa kuchangia katika Idara hii ya Magereza.

Hawa wenzetu watumishi wa magereza wanafanya kazi nzuri sana ambayo ni ya kuwatunza wenzetu wahalifu walioko ndani ya magereza. Kule kuna mkusanyiko wa watu wa aina mbalimbali, kuna wenzetu wengine wamekuwa majambazi, wengine wameshaua, wengine wana makosa mbalimbali lakini hawa wote wenzetu wa magereza wanawajibika kuwatunza, kuwaelimisha katika kipindi chote wanachokuwa hapo. Hivyo naweza kusema kwamba wenzetu wa magereza wamejitolea mhanga katika maisha yao yote kufanya kazi za magereza. Wanapokuwa katika magereza huwezi kutofautisha sasa askari ni yupi, mfungwa ni yupi, kwa sababu askari hao pengine unaweza kumkuta asubuhi anaamka kupeleka wafungwa porini kwenda kukata kuni. Hawana usafiri, kwa hiyo, askari na yeye anawajibika kutwa nzima, anapigwa na jua na mvua ikinyesha na yeye ananyeshewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mshahara anaoupata ni mdogo na hakuna marupurupu, kwa kweli hawa askari ufike wakati sasa tuwafikirie angalau basi hata kwa kuwaongeza mishahara yao au kuwapa marupurupu maalumu wanapokuwa wanafanya kazi za nje. Kwa kweli ni adhabu kubwa sana wanayoipata kwa sababu huwezi ukajua pengine anapokuwa kazi za nje jambo lolote linaweza likatokea. Anaweza akatorokwa na mfungwa, pengine huko porini kwenye kukata kuni anaweza akatokea mnyama wowote, kwani mnyama hawezi kujua askari ni yupi na mfungwa ni yupi na anaweza hata kumjeruhi hata askari. Wanafanya kazi katika mazingira magumu. Naiomba Serikali iangalie upya kazi za hawa wenzetu ili kuboresha maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ukiwaangalia hawa askari kwa kweli wanafanya kazi katika mazingira magumu sana kwa sababu magereza yaliyo mengi hapa nchini ni yalijengwa toka enzi za ukoloni. Ukiangalia enzi za ukoloni idadi ya wananchi nchini ilikuwa chache katika kipindi hicho lakini sasa hivi ongezeko la wananchi ni kubwa, kwa hiyo, hata matendo ya uhalifu au matendo yanayopelekea wenzetu kupelekwa magereza yamekuwa mengi zaidi hadi kusababisha sasa magereza kutotosha. Wafungwa wanaokuwa magereza ni wengi mno. Kunakuwa na mchanganyiko wa watu wazima na watoto kulala pamoja na hatuwezi kujua mambo yanayofanyika huko magereza ni yapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati umefika sasa naiomba Serikali iangalie ni jinsi gani tunaweza tukaongeza bajeti kwenye Wizara hii ili kuweza kupanua magereza yetu yote ambayo sasa hivi uamekwishachakaa. Kwa hivi sasa kwa kweli idadi ya wafungwa wanaopelekwa magerezani ni wengi, mbanano ni mkubwa mno kulingana na hali halisi ya magereza yetu nchini.

Vilevile katika Jeshi la Magereza, ukienda kutembelea magereza utakuta hata vitendea kazi walivyonavyo kwa kweli kazi vimechakaa. Vitendea kazi ni vichache, na wanafanya kazi katika mazingira magumu mno.

Usafiri hakuna, unakuta magereza wana gari moja pengine ni *kijikenta* tu. Sasa hiki *kikenta* hakieleweki, ni kwa ajili ya matumizi labda kwa askari wa kawaida au kwa wafungwa kwa sababu unakuta hata Afisa Magereza anapotaka kwenda mkoani itabidi atembee kwa gari hili. Hivi jamani tukiangalia kweli tunatenda haki? Wakati ufike sasa tuwaangalie wenzetu wa magereza nao, basi tuwawezeshe kupata hata magari kwa maafisa hawa ili na wao sasa waweze kufanya kazi zao vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine maafisa hulazimika kabisa kwenda mkoani au kwenda Wilaya nyingine kwa kutumia mabasi ya kawaida ya abira. Hii husababisha wakachelewa kufanya kazi zao, pengine tungewawezesha kupata usafiri wangeweza kufanya kazi zao kwa ufanisi mkubwa na kwa haraka zaidi. Nashauri tuwafikirie kupata magari. Magari waliyonayo sasa hivi kwa kweli ni yale tu yanayofaa labda kwa ajili ya kwenda kusomba kuni au maeneo ambayo maji ni ya shida kubebea maji lakini hayafai kabisa kwa kutumia maafisa kama hao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie uchache wa askari katika magereza unasababisha askari hao kufanya kazi katika mazingira magumu. Wanalazimika kabisa kupanga *shift* ambazo pengine hata tungepangiwa sisi tungeshindwa. Unakuta kuwa wengine wanaingia asubuhi, kuna watakaotakiwa kuingia mchana, hata muda wao wa kupumzika ni mdogo, muda wote wanawajibika katika kufanya kazi. Kwa hiyo, tungeangalia vilevile juu ya ongezeko la hawa askari ili waweze kufanya kazi zao kwa nafasi, wapate muda na wao wa kufanya kazi zitakazoweza kuwaingizia kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo Idara hii ya Uhamiaji. Kwenye Uhamiaji mimi sijaelewa kitu kimoja, ningeomba Wizara iweze kunielimisha. Katika nchi yetu kuna uingiaji holela wa wenzetu kutoka nchi za nje, sasa huwa ninajiuliza jeshi letu la uhamiaji, askari mipakani wapo, inakuwaje hawa wenzetu kutoka nje wanaingia kiholela na wakishaingia humu nchini hakuna mtu yeyote anayehangaika kuangalia kama hawa watu wamekuja kwa nia nzuri au kwa nia mbaya?

Matukio mengi ya hivi karibuni ya ujambazi tumegundua kwamba ni wenzetu walio wengi wa kutoka nje. Naomba nielekezwe ni jinsi gani hawa wenzetu wa uhamiaji wanafanya kazi zao na kwa nini sisi nchi yetu imekuwa ikiwaacha watu wanaingia kiholela? Kwa sababu mimi ninachojifunza ni kwamba, mimi natoka Mtwara lakini hawa ndugu zetu wanaokwenda Msumbiji wanashikwa kama wameingia kiholela wanapata mateso makubwa mno.

Hata mali zao wananyang'anywa lakini sasa sisi tumekuwa wakarimu wa kupita mpaka, watu wanaingia kiholela wanakuja kufanya matukio ya ujambazi, wanaiba mali za watu, wanarudi kwao na hakuna mtu anayehangaika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uwajibikaji katika Jeshi hili la Uhamiaji kwa kweli waweze kuangalia suala hili. Tunapata shida, majambazi wanakuwa wengi na sisi wao ndio tunaowategemea kwamba wangekuwa wanawadhibiti wakati wanapoingia katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nimepigiwa kengele, nisingependa nipigiwe kengele ya pili, naomba niseme tu kwamba ninaunga mkono hoja hii kwa asiliamia mia moja na nawatakia kazi njema kwenye Wizara hii ya Mambo ya Ndani, ahsante. (*Makofi*)

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote niipongeze hotuba ya Mheshimiwa Waziri na nimpongeze yeye mwenyewe pamoja na Naibu Waziri, kwa kuweza kusimamia Wizara hii na kufikia mahali kwamba sasa tunapiga hatua nzuri ya kuisimamia na katika kutatua mambo mbalimbali yanayotukabili hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi leo nitazungumzia suala moja tu, na ni suala la vitambulisho. Kitambulisho tukiite ni kitambulisho cha Taifa na ndio mifano mizuri ya nchi zote Duniani kwamba kunakuwa na kitambulisho cha Taifa, kinapewa majina mbalimbali lakini ni kitambulisho ambacho kitamgusa kila mwananchi, kila raia ili aweze kufahamika yeye ni nani, ni mwanamke au ni mwanaume na ana fani gani. Sasa vigezo vya kuwa na vitambulisho mimi nasema ni suala nyeti sana katika nchi yetu, limetuchukua muda mrefu kutoka tumeanza utaratibu wa kuanzisha vitambulisho mpaka ikafika mahali Serikali ikapelekwa Mahakamani katika watu ambao wamejaribu ku – *tende*r na hatimaye kukataliwa *tender* zao. Lakini naipongeza Serikali kwa sababu siyo rahisi kuachia haya mambo kila mmoja ashughulike au mtu yeyote ashughulike kusimamia suala la la vitambulisho. Kuna nchi nyingine pia kuna vitambulisho vya wageni, kwamba wewe ukisimamishwa na kutoa kitambulisho chako unajulikana kwamba hiki ni kitambulisho cha mgeni. Sisi Tanzania tunao wageni asili yake ni wakimbizi wameshaishi hapa nchini miaka mingi tunashindwa kuwarudisha makwao, huko kwao hawana tena au hakuna watu wanaowafahamu wala wakienda kule hawatambuliki.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote niipongeze hotuba ya Mheshimiwa Waziri na nimpongeze yeye mwenyewe pamoja na Naibu Waziri, kwa kuweza kusimamia Wizara hii na kufikia mahali kwamba sasa tunapiga hatua nzuri ya kuisimamia na katika kutatua mambo mbalimbali yanayotukabili hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi leo nitazungumzia suala moja tu, na ni suala la vitambulisho. Kitambulisho tukiite ni kitambulisho cha Taifa na ndio mifano mizuri ya nchi zote Duniani kwamba kunakuwa na kitambulisho cha Taifa, kinapewa majina mbalimbali lakini ni kitambulisho ambacho kitamgusa kila mwananchi, kila raia ili aweze kufahamika yeye ni nani, ni mwanamke au ni mwanaume na ana fani gani. Sasa vigezo vya kuwa na vitambulisho mimi nasema ni suala nyeti sana katika nchi yetu, limetuchukua muda mrefu kutoka tumeanza utaratibu wa kuanzisha vitambulisho mpaka ikafika mahali Serikali ikapelekwa Mahakamani katika watu ambao wamejaribu ku –

*tende*r na hatimaye kukataliwa *tender* zao. Lakini naipongeza Serikali kwa sababu siyo rahisi kuachia haya mambo kila mmoja ashughulike au mtu yeyote ashughulike kusimamia suala la la vitambulisho. Kuna nchi nyingine pia kuna vitambulisho vya wageni, kwamba wewe ukisimamishwa na kutoa kitambulisho chako unajulikana kwamba hiki ni kitambulisho cha mgeni. Sisi Tanzania tunao wageni asili yake ni wakimbizi wameshaishi hapa nchini miaka mingi tunashindwa kuwarudisha makwao, huko kwao hawana tena au hakuna watu wanaowafahamu wala wakienda kule hawatambuliki.

Mimi naishauri Serikali kwamba tuwe na kitambulisho cha watu ambao si raia wa Tanzania kwa wale ambao tunafahamu kwamba kurudi kwao ni mashaka, basi tuwatambue kwa vitambulisho vyao kwa maana kwamba hawawezi kupiga kura, hawawezi kushika uongozi katika nchi yetu na kuwe na kumbukumbu za kumtambua kwamba huyu si Mtanzania ili tutoe nafasi kwa Watanzania ambao wanastahili katika nchi yao kufanya yale ambayo wanatakiwa kufanya kama raia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitambulisho hivi vya wageni kwanza vitadhibiti uhamiaji haramu, ukimsimamisha mtu kama ni mgeni ni lazima awe na kitambulisho kama hana kitambulisho ina maana hatambuliki na ina maana atakuwa ni mhamiaji haramu na hajasajiliwa katika rekodi za nchi. Kwa hiyo, hatua zake zinakuwa ni rahisi kuzichukua. Tanzania ina wahamiaji wengi kuliko nchi yoyote duniani kutokana na hali halisi iliyojitokeza katika nchi zetu za jirani.

Umuhimu wa vitambulisho kwa raia wetu, kwanza vitambulisho vitaimarisha usalama wa nchi, lakini vilevile vitambulisho hivi liwe ni jambo muhimu kwamba viwe vinakidhi vigezo mbalimbali, kwa ushauri wangu. Kuwe na data ambazo mwananchi anapokwenda kupiga kura tusianze kuulizana maswali kwamba wewe umekwishafikisha umri wa miaka 18 na unaruhusiwa kupiga kura, kitambulisho chenyewe kiwe kinasema kwamba huyu hajafikisha umri wa kupiga kura.

Unaingiza kitambulisho chako ndiyo unapata kibali cha kupiga kura, kitambulisho ukiingiza katika mashine kinakataa kinasema wewe hujafikisha umri wa miaka 18 badala ya kuhangaika siku zote na kupata matatizo kwamba waliopiga kura wengi wako chini ya umri wa miaka 18, tutaondoa hili tatizo. Kwa hiyo, data za yule ambaye anapiga kura zitakuwepo kwa maana ya umri.

Lakini vitambulisho hivi viwe na vigezo vilevile vya kupanga mahitaji ya taifa, tunapata mambo mengi, mengine ni ya majanga na mengine ambayo ni muhimu kwa ajili ya shughuli za kitaifa. Kwa hiyo, kitambulisho hiki kiwe kinakidhi haja ya kujua kwamba kama kumetokea ukame katika kanda fulani tunaweza kujua ni idadi ya watu wangapi watakaokuwa wameathirika na hatimaye kujua idadi ya wanawake, wanaume, watoto na hivyo taifa kupanga mipango mizuri kutokana na sensa ambayo tayari imo ndani ya vitambulisho vya wananchi wenyewe.

Kitambulisho pia kiwe na uwezo mkubwa wa kujua idadi ya watu kila mwaka, hakuna haja ya kufanya sensa kila baada ya muda fulani, kikitoka kitambulisho hicho

basi kiwe ni kitambulisho ambacho kitakuwa ni endelevu bila kutumia gharama kubwa ya kuhesabu watu. Kitakuwa ni kitambulisho cha kujua kila mwaka tunajua ni wangapi wamezaliwa, wangapi wamekufa. Kitambulisho hiki kiwe na vigezo kama hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho ni muhimu, kitambulisho hiki kiunganishwe na malipo muhimu ya kodi. Serikali yetu inapoteza mapato mengi sana. kuna Wizara mbalimbali hapa ambazo zinachangia pato la Taifa kwa maana kwamba zinatoza kodi kwa raia ambao wanafanya shughuli zao za maendeleo. Wizara hizi ni Wizara ya Fedha, Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Maliasili na Utalii na hata Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kwa maana ya Halmashauri zetu.

Tunapata matatizo ya bajeti, watu kulipa kodi lakini kitambulisho chetu hiki kiwe kinaonyesha kwamba wewe ukitaka kusafiri ukifika pale *Airport* basi huondoki kwa sababu *database* inasema unadaiwa na Maliasili na Utalii, kalipe kwanza halafu ndiyo usafiri; wewe unataka ku–*renew passport* unaambiwa huwezi ku–*renew passport,* kwanza unadaiwa kalipe kodi; unataka ku–*renew licence* yako unaambiwa huwezi ku–*renew* kutokana na deni ulilokuwa nalo.

Wenzetu ndivyo wanavyofanya kazi, leo tunaangushana na wananchi kupeleka Polisi, Mahakamani na mara nyingine wanakimbia, ya nini kuhangaika! *Traffic* anasimamisha gari, yule mwenye gari anaonekana ana makosa, hana haya ya ku–*negotiate* naye, anamwambia makosa yake, anamwomba kitambulisho chake, anachukua namba ya kitambulisho, anamwandikia faini, anamwambia endelea na safari yako, anampa risiti akalipe na risiti nyingine inakwenda kule kwenye *database.* Siku yoyote akilipa ile ina *clear* kama haku – *clear* basi atakuja siku moja ataingia mahali ambapo atakuwa na shida ya shughuli zake, kitambulisho kile kitamwambia wewe unadaiwa faini ya gari tarehe fulani ulisimamishwa na *Traffic* unadaiwa 40,000/= hukulipa. Sasa tukifanya hivyo tunaipunguzia *TRA* matatizo na tunaipunguzia Serikali kwa ujumla jinsi gani ya kukusanya mapato yake kwa kuweka vizuizi kupitia kitambulisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukione hiki kitambulisho kina manufaa makubwa sana kwa taifa letu, ifike mahali tusema wewe kama unadaiwa mahali basi hata kama Mbunge unataka kugombea kitambulisho chako kiseme kwamba huwezi kugombea ubunge kwa sababu kwanza unadaiwa, kalipe deni halafu uchukue fomu ya kugombea ubunge au udiwani, ifike mahali hapo kuliko kuanza kuulizana huyu vipi.

Sasa kitambulisho hakidanganyi, lakini kikubwa sasa katika vitambulisho tunahitaji *software* na hapa mimi ndiyo sasa tupo mahali nyeti kuiambia Serikali kutoa *tender* kwa makampuni ya kigeni, basi kuwe na mipango miwili tofauti.

Kuna kazi ya kuchapisha kitambulisho, hiyo sawa, kampuni ambayo inaweza ikafanya hiyo kazi. Lakini kuna kazi nyingine nyeti ni *software* yenyewe ambayo itakuwa na *National Data Bank* ambayo *informations* za wananchi wote raia wa Tanzania na wageni zitakuwepo huko.

Sasa ile ni siri ya nchi na ni nyeti kwelikweli hatuwezi tukamkabidhi mtu yeyote wa nje ya nchi au kampuni ya kigeni kujua *informations* za raia wetu katika nchi hii. Mimi nashauri kwamba Serikali ihakikishe kwamba *database* au *software* ambayo itaweka *data bank* za wananchi wetu iwe inasimamiwa na raia waaminifu na vyombo ambavyo vinaamiwa katika ulinzi na usalama wa nchi yetu, ndiyo vipewe kazi hii kwa sababu ndani kuna kuorodhesha ambao ni raia lakini ni watu wanaofanya kazi Usalama wa Taifa, majeshi yetu, Polisi na shughuli nyingine nyeti za Kiserikali.

Utaipaje taarifa hizi kampuni ya kigeni ijue data zetu, data za raia wetu na shughuli zetu? Hizi ni siri za nchi na haziwezi zikatolewa, hata raia wengine wowote ambao watakuwa ni watu muhimu katika nchi hii lakini taarifa zao ni nyeti lazima tuzihifadhi vizuri, tupeleke watu vijana watakaosimamia shughuli hii.

Mimi niseme kwamba *Dar es Salaam University, University Computing Centre* inaweza kutengeneza *software* hiyo. Tuwaamini wananchi wetu, tuwaamini wasomi wetu wa *Dar es Salaam University* kwamba wanaweza kufanya kazi hii. Tunaye Mtanzania ambaye yupo Marekani anafanya kazi katika kampuni ya Kimarekani lakini bado yeye ni Mtanzania, akija Tanzania hapa Marekani wanampa mlinzi (*body guard*) kwa sababu ya taarifa alizokuwa nazo kule ambazo yeye ndiye aliyetengeneza, hawamwachi hivihivi lakini tumtumie basi mtu huyu.

Tumejaribu kuwasiliana naye tukamwambia aje atusaidie katika kuunda *software* kwa ajili ya vitambulisho vyetu Tanzania. Hili ni muhimu kwelikweli na naishauri Serikali na kuiambia suala la *software* kuweka *database* za taarifa zote za raia wetu ni jambo nyeti na la siri, lazima zisimamiwe na watu wetu hapa hapa nchini na vyombo vyetu vya dola vijue kwamba hili ni suala nyeti na siyo kila mtu anakwenda kujaribu *tape* katika zile *database* za mambo kama hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kusisistiza umuhimu wa kitambulisho cha raia na unyeti wake ili Serikali izingatie vizuri pamoja na kwamba hotuba ya Waziri imesema kwamba kutakuwa na *agency*. Sasa hiyo *agency* hakikisheni kwamba ni watu waaminifu na ni watu ambao wamekula kiapo kwa ajili ya maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Anna Maulidah Komu atafuata akifuatiwa na Mheshimiwa Manju Salum Omar Msambya.

**MHE. ANNA MAULIDAH KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia kwenye Wizara hii. Mimi huwa ninazipa *grade* hizi Wizara, nasema Wizara hii ni muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya yote naomba niwape pongezi wote kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mkuu kasema tusipeane pole, niwape pongezi wote kuanzia

Waziri, Makamanda, Wakuu wa Uhamiaji na Maafisa wao, Zimamoto na wote wanaofanya kazi hizi muhimu kwa ajili ya wananchi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naanza na Magereza. Nafurahi sana kwamba hata hotuba ya mwenyewe Waziri inazungumza kwamba raia wa Tanzania au raia wa nchi yoyote duniani anapokamatwa akahukumiwa na akapelekwa jela siyo kwamba haki zake kama binadamu zimefutwa, hapana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hujaenda jela wewe leo nitakwenda mimi, kama sitakwenda mimi jela hata Mheshimiwa Waziri mwenyewe anaweza kwenda. Binadamu hatuelewi saa ngapi kitu kibaya kitakujia na utafanya uhalifu ambao hukuutegemea na utaishia mikononi mwa gereza. Sasa tunapoangalia vitu kama hivi vyenye utu wa mtu na bila ya mtu mwenyewe kujijua, yeye mwenyewe mwisho wake ni wapi, tuwe tunaviangalia kwa upeo mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana wakati nachangia Wizara hii hii niliongea kuhusu manyanyaso na mateso yaliyopo kwenye Magereza yetu. Wakati ule nikiongea jambo ambalo ni baya sana linaloendelea kwenye Magereza yetu nilikuwa na ushahidi lakini siwezi kumfuata ama kumwambia mlete mwanao nikamtoe ushahidi pale Bungeni.

Lakini kwa kweli manyanyaso yapo. Sasa yanapokuja mambo kama haya na sisi tukaja ambao tunazungumza na wananchi, tunawaona wananchi, tunasoma magazeti tunaona mambo ambayo wananchi waliokuwa wanatumikia vifungo na kutoka wanayaandika, na Magereza yenyewe hawakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoleta mambo kama hayo lazima tuyakalie kitako chini na kuyafanyia kazi na kuyachunguza na tukipata ukweli wale wanaohusika wachukuliwe hatua kali. Tusikae tu kimya kusema kwamba Magereza yetu kwa sababu ni mazuri tumetembelea na tumeona watu wanakaa vizuri, wafungwa wako vizuri, yaishie hapo, hapana! Mimi naogopa kwa sababu ninarudia palepale kukwambia kwamba kesho mimi nitakwenda jela yatanikuta yale yaliyopo kule.

Kwa hiyo, naanza kutetea huku nje kabla sijaenda kule ndani. Tuwe makini kwani siyo kwamba kila mmoja ni Malaika, msiniambie kwamba Askari Magereza wote tulionao kwenye Magereza yetu wanafanya vizuri, hapana! Na ndiyo yale mchangiaji wa Kamati ya Kudumu ya Bunge aliyosema kwamba tuhakikishe basi haya mambo ya kusema "sungura mdogo tugawane kidogo kidogo" nchi yetu ni maskini hatutafika, kwani "penye udhia tia rupia". (*Makofi*)

Tuweke kompyuta kwenye Magereza yetu basi, kwenye maeneo ambayo tunawaweka hawa watu. Hawa wamewanyima uhuru wao wa kujitafutia maisha yao nje kutokana na uhalifu au adhabu walizopewa. Tumewakusanya sisi tumewaweka, tuhakikishe asubuhi wanapata chakula, mchana wanapata chakula na wanapolala ni mahali nadhifu hawaambukizani maradhi. Tuweke huo utu na tukumbuke kwamba huo ni utu wa kila mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nakwenda kwenye Uhamiaji, “Yesu na Maria!” Uhamiaji ni chombo nyeti kabisa, uhamiaji ndiyo tunawategemea kule mipakani, uhamiaji ndiyo tutawalaumu asubuhi na jioni kuhusiana na vurugu na wimbi la majambazi waliojaa humu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo asubuhi nilikuwa naangalia *Television* ya *StarTV* kipindi cha Taarifa ya Habari, kilionyesha majambazi wameingia kule Njiro. Nilishangaa na nikacheka maana yake mwisho wa uchungu unacheka. Wasichana waliochukuliwa na hao majambazi kuwekwa kwenye hiyo nyumba ya Mtanzania imejengwa haiishi watu. Majambazi wametoka Kenya, wameingia kule ndani, wamepita wapi? Hata kama ndiyo huwezi ukamjua mtu kama ni jambazi kwa sababu jambazi hana sura unaweza ukaniambia hivyo, lakini kama leo kabla hatujaondoa pasipoti za kwenda *East Africa* tunasema unapotoka Kenya uonyeshe pasipoti na hata unapotoka Uganda uonyeshe pia pasipoti bado hatujasema hakuna ruhusa ya paispoti, wanaingia na kutoka kwa uhuru wake, kesho tutakaposema tunaondoa pasipoti hali itakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar tulikuwa tunalala milango wazi, mimi nazaliwa nimekuta mlango ulikuwa unasindikwa halafu kinasogezwa kiti. Leo Zanzibar tunajenga nyumba za *grill*! Tulikuwa tunatambuana wenyewe kwa wenyewe na tulikuwa tunasema mtu akija Zanzibar anaonyesha pasipoti, hatukujua kwamba tunaondoa pasipoti kwa sababu ya Utanzania lakini kuna vurugu inakuja, leo tunaibiwa mpaka watoto! Uhuru, kwa sababu hatuna tena mambo ya pasipoti. Sasa mfano huo huo tuuchukue na pale ni kisiwa tu jambazi ni mara moja utamkamata, huku Bara je?

Kama Afisa wa Uhamiaji waliopo mipakani hawatatuliza akili zao wakafanya kazi kwa bidii, kweli tutaingia kwenye hatari, na ninarudia tena kusema kwamba hata hatujaondoa pasipoti sijui tutakapoondoa itakuwaje. Mimi hii nitailalamikia kwa sababu ule utaratibu wa kusema tunahamisha Maafisa wanapokaa miaka mitatu au mitano kwenye maeneo tunaulalia. Afisa Uhamiaji au Afisa Magereza anakaa kwenye eneo zaidi ya miaka mitano anaelewa mazingira ya eneo lile, mishahara midogo tunayowapa wanaingia kwenye vishawishi vya ajabu kabisa.

Lazima turudishe ule utaratibu wa kuhamisha Maafisa, Afisa akishafika mahali amekaa zaidi ya miaka mitano jamani aondoke, tusiseme jamani aaah! unajua sungura mwenyewe mdogo kwa hiyo, kumhamisha Afisa ni pesa nyingi, kuhamisha vyombo vyake na kadhalika, hapana! hiki kilio unaposema kwamba hiyo ni pesa nyingi basi unatumia pesa nyingi zaidi unapoingiliwa na majambazi, wanapoingia kwenye mabenki si wanatuathiri zaidi? Mabilioni kwa mabilioni ya pesa wanayachukua.

Sasa hii pesa tunayoiona ni nyingi kumhamisha Afisa kumpeleka eneo lingine kwa muda unaofika, tunapoteza pesa nyingi zaidi kwa makosa yanayotokea, baada ya hapo tuangalie tena. Na mishahara tunaona leo Maafisa wetu hapa kwenye makorido wamevaa vizuri na wamependeza na sare mpya lakini kweli ukienda kwenye maeneo utashtuka.

Ule utaratibu wa Afisa kupewa sare kila kipindi kinachofika apewe sare yake apendeze. Kwenye lile eneo apewe mshahara mzuri, apewe marupurupu ili aone yeye ni Afisa, anapokalia kiti hakuna tena, maana yake sungura mdogo, tutafika wapi kama kila tutakachozungumza hapa ndani tutasema sungura mdogo, hatuwezi kufika!

Tutumie pesa ili tuweze kupata pesa, tutumie pesa ili tuweze kupata ufanisi, ndivyo nchi zinavyokwenda. Mbona tulipotaka kutoa mikopo tuliweza kupata bilioni 26 mara moja? "Penye nia pana njia." Nchi hii ina Madini bwana, Mwenyezi Mungu kaipenda, tusimkufuru kwa utajiri aliotupa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niongelee kuhusu Zimamoto. Ni vichekesho maana yake gari la Zimamoto linapofika mahali watu huzomea badala ya kushangalia. Wanamwaga maji kidogo wakimaliza wanakwenda kutafuta maji wakirudi moto umemaliza nyumba, kuna nini jamani? Mbona kila miaka inavyokwenda mambo yanazidi kuwa mazuri, maana yake sisemi mabaya, sijui ndege gani sasa hivi anapita. Zimamoto, wenzetu wana vitu vinawekwa kwenye majumba, moshi ukizidi tu vinapiga kelele.

Mimi nilikuwa mjinga siku moja Uingereza, nilianza kutafuta hiyo kengele inalia wapi, kumbe nalikuwa nakaanga samaki moshi ukaingia pale! Na sisi tuweke hivi vitu. Tuweke kampeni za kutosha kuwaeleza wananchi wetu madhara ya moto.

Tutengeneze zimamoto zetu na tuweke magari haya mambo yote yaliyoandikwa humu. Hiki kitabu nakwenda kukiweka tena nakwambia kabisa Mheshimiwa Waziri Mungu akijalia na mwakani uwe wewe, nakwenda kuweka. Haya yasije yakaishia kwenye makabrasha mazimamoto.

Ofisi ya Uhamiaji Dar es Salaam inanitia uchungu maana yake bahati mbaya nilikuwa mhusika kuianzisha ile Ofisi pale, leo naambiwa kuna jengo jipya nashukuru, lakini hiki nakwenda kukiweka na haya yote yaliyomo humu hata kama tutashindwa kuyatekeleza yalivyotakiwa lakini nataka nihakikishiwe kwamba yametimia hata kwa 52%.

Zimamoto ni hatari, hapa hapa Dodoma tu kila nyumba unayopita nyumba zimewaka moto, ukingalia umeme wa *TANESCO* yetu ndiyo hivyo tena mara chanzo ni *TANESCO*, mara chanzo ni vitu vya ajabu ajabu lakini ni lazima tuwe na vyombo.

Juzi nimeshukuru nimeona kumepigwa *alert* pale *airport* kwamba ndege ya watu mia mbili inataka kuanguka sekunde mbili au tatu nikaona vyombo vimefika pale unaitafuta zimamoto eti Watanzania, nakuta kuna *Ultimate Security*!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuzungumza kwamba ufinyu wa bajeti kwenye Wizara kama hizi ni hali ya hatari. Tusizinyime bajeti hizi Wizara, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi iliyoshika Magereza,mipaka yetu, nchi yetu kwa moto, uokoaji kwani tulijua *elnino* itakuja?

Tunajua leo kutapasuka saa ngapi huo mlima tunaupigia kelele? Tumejiandaaje? Kweli tutafika mlima umeshapasuka watu wanateketea waokoaji hakuna tutasema maana yake tuna sungura mdogo, tutaeleweka? Tuhakikishe tuchukua tahadhari. Kuna neno moja la Kiarabu, samahani linasema tujitahidi kuweka hadhari kabla haijatokea athari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru muda ni mdogo ningeendelea lakini sasa nakwenda na wakati, naogopa mtu mzima nisije nikapigiwa kengele. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Anna Maulidah Komu na sasa ni zamu ya Mheshimiwa Manju Salum Omar Msambya, atafutiwa na Mheshimiwa Said Amour Arfi kama atakuwepo, simuoni humu ndani kama Mheshimiwa Said Amour Arfi hatakuwepo basi Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes ajiandae.

**MHE. MANJU SALUM OMAR MSAMBYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, lakini kabla sijachangia nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Kaibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara.

Mahususi nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwani mara tu baada ya kuingia kwenye Wizara hii alifanya ziara kwenye Mkoa wangu na siyo ziara tu bali alifanya ziara ya taaluma. Kulikuwa na warsha na hasa ilikuwa inahusu mambo ya uhamiaji, alisimamia vizuri sana na elimu iliyotolewa pale.

Mimi naamini wengi tulioshiriki tulifaidika na mchango wangu hapa kwa leo utakwenda kwenye maeneo mawili yaani Magereza na Uhamiaji. Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe alipokuwa anazungumza amezungumza kwa uchungu sana kuhusu kuhusu Magereza na mimi nitazungumza kuhusu Magereza na nitaanza na hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waswahili wanasema "Lwaa mwanika kunguni." Mtu anayechukua virago vyake au magodoro yake yana kunguni akayaanika nje ni dhahiri na yeye itabidi akae pale anaangalia kila kunguni anayetoka na kumuua. Kunguni wale wanakimbia kutoka kwenye virago yaani wanalikimbia jua, kwa hiyo, na yeye anakaa pale anaunguzwa na jua kama kunguni wanavyoumia na jua.

Kwa hiyo, Askari wa Magereza wanaoshughulikia wafungwa kwa sehemu fulani na kwa namna fulani na wenyewe ni wafungwa. Sasa watu hawa ni vizuri maslahi yao yakatazamwa, tuwatendee haki. Mara nyingi tunasema kwamba maslahi ya watumishi wote yanakwenda pamoja lakini tumekuwa tunaona hapa kwa nyakati tofauti watumishi wa kundi fulani maslahi yao yanatangazwa kana kwamba wenyewe ni muhimu zaidi kuliko wengine

Mimi naiomba Serikali kupitia kwa Mheshimiwa Waziri waangalie kwa undani sana watumishi wa Idara ya Magereza hasa ukitilia maanani adha wanayoipata ambayo wao na wafungwa tofauti ni ndogo sana. Waingereza wanasema "*The difference is just the same*". (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwazungumzia Magereza vizuri, shilingi ina sura mbili. Magereza hao hao kwenye Jimbo langu kijiji cha Ilagala kumekuwa na mgogoro kati ya Magereza na wananchi wakazi wa kijiji kile. Magereza wamevamia ardhi sehemu kubwa, walikaribishwa pale wajenge gereza kwa madhumuni ya kilimo, wakapewa eneo lakini sasa imekuwa ni ile hadithi ya ngamia anaingiza kichwa akataka kuingiza na nundu sasa.

Sasa wamekwenda wanaongeza mipaka na wananchi wanapojaribu kulalamika wanapata vitisho. Naomba Wizara iliangalie hili, najua itakuja hoja upo uongozi wa Wilaya na hata Mkoa, uongozi wa Wilaya huko nyuma walishavuruga utaratibu wa kushughulikia tatizo hili sasa pengine maelekezo yatoke juu. Kwa hiyo, ninaomba Wizara ilitazame hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye eneo la Uhamiaji. Nimesoma kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri hapa na nimemsikiliza alipokuwa anasoma hotuba yake, suala la uraia wa nchi mbili, kwenye hotuba amesema kwamba suala hili sasa liko kwenye ngazi ya Baraza la Mawaziri na litatolewa uamuzi wakati wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mawaziri tunatakiwa tuwashauri sisi na bahati nzuri hapa kuna idadi ya kutosha. Kwa hiyo, watakaokutana kule hata wale ambao hawapo mimi ninaomba wachukue ushauri wangu. Mimi siafiki suala la uraia wa nchi mbili. Waliosoma gazeti la Rai la wiki iliyopita waliona katika ukurasa wa mbele.

Zipo picha za watu ambao wameonekana ni wahalifu, na ile ni sampuli ambayo inatupa sisi hoja ya kukataa uraia wa nchi mbili. Zaidi ya asilimia 90 ya wale watu waliokuwa na sura kwenye lile gazeti siyo Watanzania. Hao wameingia tu katika njia zao wanazozijua wenyewe kinyemela, wameleta vurugu hizo ambazo sasa zipo hapa. Sasa tukishakubali suala la urai wa nchi mbili, tunakubaliana kwamba waje, kunguni wataingia, panya wataingia, paka wataingia, sasa hii nchi itakuwa ni kokoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania haijakuwa na upungufu wa watu kiasi kwamba tuseme waje wengine wajaze nafasi ambazo zimebaki wazi. Lakini wanaotoa hoja ya urai wa nchi mbili wanasema ni njia moja ya kuingiza mitaji. Kwa hiyo, uwekezaji unapata uimara. Mimi ninakataa. Sasa hivi wapo wawekezaji wanaokuja ambao siyo raia wa nchi hii, na wanafuata taratibu zote, wanawekeza, na hizo ajira ambazo tunazijengea hoja, zinapatikana kwa wawekezaji ambao siyo raia wa nchi hii.

Lakini vilevile wapo wawekezaji ambao ni wazawa wapo tayari. Sasa kuweka hoja ya kwamba mtu akishapata uraia wa nchi mbili ndiyo atakuwa mwekezaji mzuri, hapana! Mimi ninaye rafiki yangu mmoja simtaji jina. Mpaka miaka mitatu iliyopita yeye alikuwa ni Mtanzania. Miaka ya nyuma huyo alikwendwa kusoma Ujerumani.

Baada ya kumaliza masomo yake akashawishika akarudi hapa Tanzania, akaoa akarudi tena Ujerumani akashawishika amekuwa Mjerumani tayari. Lakini alinituma mimi Mbunge nije nizungumzie suala la uraia wa nchi mbili upewe msukumo wa haraka.

Mimi nikamwambia wewe kama uliutaka uraia wa Tanzania kwa nini uliukataa kwa mara ya kwanza? Mbona unakuwa na tamaa namna hiyo? Bakia kuwa Mjerumani, utakuja huku tutakukaribisha kwa sababu wewe si mhalifu utaingia kwa Viza kama sisi tunavyoingia Ujerumani kwa Viza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu, nitakalolizungumza ni kwamba ninayo barua hapa na nikishasoma barua hii nitaiweka mezani. Barua hii ni ya tarehe 7 Agosti, 2006 ikiwa imeandikwa na Waziri wa Mambo ya Ndani kamwandikia Mkurugenzi wa Uhamiaji na kwa idhini yako naomba niisome kwa haraka haraka. Imeandikwa na Waziri wa Mambo ya Ndani kwa sababu kulikuwa na hoja hapa Mheshimiwa Joseph Mungai akasimama na akajaribu kusahihisha akasema tusimtaje Waziri kwa jina. Tumtaje tu kwa cheo chake. "Malalamiko ya Bwana Philemon B. R. Heseka Kalenga". Mtajwa hapo juu ametuandikia hapa Wizarani akilalamika kuhusu suala la uraia wake na kwamba hatendewi haki, na ameomba Wizara itazama upya uamuzi wa kumnyima uraia. Msingi wa malalamiko yake ni kwamba: moja, alizaliwa kijiji cha Igulula, Tarafa ya Buhingu, Kigoma mwaka 1942. Amesoma na kukulia hapa nchini. Aidha, anasema wazazi wake wote wawili walizaliwa Tanganyika, baba yake ambaye sasa ni marehemu alizaliwa kijiji cha Igulula na amezikwa papo hapo. Mama yake mzazi bado yu hai na anaishi katika kijiji hicho hicho." Pili, katika harakati za kutangaza dini huko *DRC* aliomba pasipoti ya nchi hiyo na kupata. Aliporejea nchini Zanzibar alielezwa athari za kuwa na pasipoti ya *DRC* kwamba inafuta uraia wa Tanzania.

Hivyo alichukua hatua za kisheria kukana uraia wa *DRC* na kukabidhi pasipoti hiyo kwa Serikali, Idara ya Uhamiaji. Suala la uraia wake liliwahi kupelekwa Mahakamani huko Zanzibar. Mahakama ya Wilaya na baadaye Mahakama ya Mkoa Zanzibar. Mahakama zote mbili zilithibitisha uraia wake. Nakala za hukumu ametuleta. Nimezingatia hoja ya mlalamikaji, lakini kabla ya kumpa majibu ya Rufaa yake nahitaji maelezo ya Idara yako yaani maelezo ya upande wa pili wa suala hili. Napenda kupata maelezo yenu katika muda mfupi ujao ili yanisaidie kulitolea uamuzi tatizo hili ambalo limedumu takriban miaka mitano bila kumalizika. Katika kuandaa maelezo hayo nendeni kijijini alikozaliwa ili ahojiwe mama yake mzazi, ndugu wa karibu, wazee wa Serikali ya Kijiji. Fanyeni haraka ili suala hili sasa liishe. Barua ya malalamiko imeambatanishwa. Nakala ya barua hii Mheshimiwa Waziri alimpa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo." Tarehe 7 Agosti, 2006 mpaka leo suala hili hajapatiwa majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana kwenye Wizara hii nililisema hili, lakini miaka ya nyuma vilevile niliwahi kusema watu wanachanganya ukabila na uraia wanadhani ni kitu moja. Maafisa wa Uhamiaji Kigoma naamini watakuwa walitumwa na Mkurugenzi wa Uhamiaji waende wakafanye uchunguzi wa suala hili.

Lakini mpaka sasa ni mwaka mzima, bajeti moja mpaka bajeti nyingine suala hili halijapatiwa ufumbuzi. Tatizo liko wapi? Huyo mtu amefika mpaka kumwona Waziri kupitia kwangu, nikaenda naye mpaka kwa Waziri. Waziri kwa busara zake nzuri tu aliandika barua hiyo mpaka sasa watendaji hawajatimiza wajibu wao. Huyo mtu anashindwa hata kule Zanzibar alipo sasa hivi kuendesha mambo ya Kanisa lake. Sasa mimi nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri, anipatie majibu ya suala hili sasa.

La mwisho, Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 21 Julai, 2007, Waheshimiwa Wabunge, walipimwa UKIMWI wajue kama wameathirika au la. Kujua afya kunahusika na vitu vingi, kifua kikuu, kansa na shinikizo la damu na kadhalika. Sasa watumishi wa Serikali ni vizuri wakakaa pamoja na waume zao au pamoja na wake zao.

Idara ya Uhamiaji wapo watumishi wanatenganishwa na waume zao na wengine wametenganishwa na wake zao. Masuala haya Wizarani yamefika, hao walitenganishwa wamejaribu kuomba uhamisho ili waungane na familia zao, lakini imeshindikana. Hivi hii siyo njia moja ya kushinikiza watu kuingia kwenye masuala ya UKIMWI? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, binadamu ana hulka mbili. Hulka ya kufurahi na hulka ya kukasirika. Binadamu ana hulka ya kufanya jema na hulka baya. Sasa huyo mtu anaweza akaamua kulinda ndoa yake, lakini siku moja matamanio ya kibinadamu yakamfanya akateleza, akiteleza siku moja anakwenda kuupata UKIMWI.

Mimi naomba Idara ya Uhamiaji itazame uwezekano kwa wale ambao wametenganishwa na wake zao na waume zao kwa sababu ya kazi ijaribu kuweka mazingira ya kuwahamisha ili wakae pamoja waepukane kuingia kwenye janga hili la UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sina tatizo na Mheshimiwa Waziri, lakini kuunga mkono kwangu hoja hii kutategemeana na majibu ya barua hii. Naomba kumalizia hapo. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii na hasa pale ulipotangaza kwamba kama Mheshimiwa Said Arfi hatakuwepo basi atafuatia Mheshimiwa Mbunge mwingine. Basi nikakimbia haraka sana kuja ili nami nitoe mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nijielekeze moja kwa moja katika suala linalohusu msongamano katika magereza. Eneo hili najua na ninafahamu kwamba Kamati imelizungumzia, Kambi ya Upinzani imelizungumzia na Waheshimiwa Wabunge wengi wamelizungumzia ni moja kati ya kero kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitapenda nijikite kabisa katika gereza la Mahabusu la Mpanda Mjini. Gereza la Mahabusu la Mpanda Mjini lilijengwa kama miaka 50 iliyopita, na bahati nzuri katika kutimiza wajibu wangu wa kazi kama Mbunge nimelitembelea gereza hilo hivi karibuni. Ukiingia katika gereza la Mahabusu la Mpanda huwezi kujua rangi ya kuta ni nyeusi ama ni *cream*. Sijui mara ya mwisho gereza hilo lilifanyiwa ukarabati lini?

Mbali ya hali halisi ya uchakavu wa gereza lenyewe, inasikitisha kabisa eneo lile la katikati ambalo ndilo eneo pekee kwa wafungwa kuweza kupata nafasi ya kula chakula chao vizuri, eneo hilo sakafu yote imebomoka. Kuna mashimo yaliyojaa maji hasa wakati wa mvua na kwa bahati mbaya siku niliyolitembelea gereza hilo mvua

ilikuwa inanyesha. Ni eneo ambalo linawakusanya wafungwa pale. Kwa hiyo, walilazimika kutafuta nafasi ya mimi kuweza kuongea na wafungwa katika gereza. Kwa sababu mahali pale palikuwa hapawezekani hata kukaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hiyo inaweza ikasababisha mlipuko wa magonjwa. Napenda kutumia nafasi hii kuiomba Wizara pamoja na mipango yao mingi na tayari wameishapanga, lakini ni vyema wakaangalia eneo hilo ambalo ni muhimu kwa wafungwa ili waweze kupata chakula chao katika mazingira mazuri. Hali ya askari magereza pia katika gereza la Mahabusu la Mpanda si nzuri kwa maana ya makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba hazitoshi, lakini magereza mengi kwa bahati nzuri sana yanayo nguvu kazi tayari. Wanao mafundi uashi wazuri ambao wanaweza wakajenga nyumba za askari na majengo mengine ya magereza kadri yanavyohitaji Magereza. Lakini ni namna gani Wizara inaweza ikayasaidia magereza ambayo yanaweza yakajijengea nyumba.

Napenda kuishauri Wizara iangalie ni namna gani inaweza kuyasaidia yale magereza ambayo yapo tayari kwa kuwatumia wafungwa kwa kujenga makazi ya askari magereza na mahitaji mengine ya magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini gereza la Mpanda ni mfano tu. Nilikuwa nasoma katika gazeti la Mwananchi, wanaeleza hali ya gereza la Babati. Gereza ambalo linaweza kuchukua watu 115, lakini kwa taarifa iliyokuwa inatolewa siku hiyo kwa Mkuu wa Mkoa wa Manyara hilo gereza lilikuwa na zaidi ya wafungwa na mahabusu mara nne ya uwezo wa gereza, na ndiyo hali ambayo niliiona Mpanda siku ambayo nilitembelea gereza la mahabusu la Mpanda. Gereza lenye uwezo wa kuchukua kati ya watu 96 mpaka 100 lilikuwa na watu zaidi ya 300. Hali hii haifurahishi. Hatua za makusudi ni lazima zichukuliwe ili kupunguza msongamano wa wafungwa katika magereza yetu. Lakini mtu hawezi kufika gerezani isipokuwa ni lazima apite katika milango miwili mingine. Ni lazima apite Polisi na apite Mahakamani ndiyo atafika gerezani. Tunaweza tukawa tunaweka lawama katika Idara ya Magereza tutakuwa tunawaonea. Ni namna gani Polisi wanasimamia upelelezi wa kesi kwa haraka kiasi gain; namna gani mahakimu wetu wanavyotoa masharti magumu sana ya dhamana, watu wanashindwa kuwekewa dhamana. Kwa hiyo, mlundikano unaendelea kuwepo katika magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili la dhamana linapaswa liangaliwe na kibaya zaidi ni watendaji wetu wa vijijini. Watendaji ambao wana dhamana ya kutambulisha wadhamini, kuna urasimu mkubwa. Kupata hiyo barua ya kupeleka Mahakamani ili uweze kumwekea dhamana mtu unayetaka kumwekea dhamana ni matatizo katika sehemu nyingi katika nchi yetu. Haki ya dhamana ni haki ya msingi. Lakini inapofikia dhamana ikawekewa masharti, kwamba huwezi kupata barua ya kwenda kumchukulia mtu wako dhamana mpaka ulipe mchango ama wa shule ama michango kadhaa ama kitu fulani ndiyo unapewa barua, tunakuwa hatuwatendei haki na tunavunja haki ya msingi, wakati kwa mujibu wa sheria dhamana ni haki ya mtuhumiwa. Nadhani ni vyema sasa Serikali ikaangalia maeneo ambayo pia ni vikwazo vya kuleta msongamano katika

magereza ikarahisisha taratibu hizo ili kusiwe na msongamano mkubwa katika magereza yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gereza la Sumbawanga Mjini na lenyewe ni tatizo. Nilikuwa nikirejea katika *Hansard* nimekuta Mheshimiwa Paul Kimiti akilalamikia Gereza la Sumbawanga Mjini mara nyingi tu. Lakini hakuna hatua zozote zinazochukuliwa kurekebisha hali iliyopo katika gereza hilo. Pamoja na hotuba ya Mheshimiwa Waziri nimeipitia, lakini sikuona mahali popote ambapo wamejielekeza kuondoa dosari katika baadhi ya magereza niliyoyataja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tutazame pia magereza ya kilimo. Mkoa wa Rukwa ni miongoni mwa mikoa ambayo ina magereza ya kilimo. Tunalo gereza la Molo na gereza la Kalilakulukulu. Magereza haya kwa makusudi kabisa yalianzishwa kwa ajili ya kilimo kuyawezesha magereza yaweze kujitosheleza kwa chakula na yaweze kupata ziada.

Ni maeneo ambayo yanazalisha kwa wingi, lakini yana matatizo mengi. Magereza yana magari machakavu na vifaa vya kilimo ambavyo vimechoka kabisa. Katika mpango nimeona kuna baadhi ya matrekta kule Molo yatafanyiwa ukarabati.

Nilikuwa napenda kumwomba Mheshimiwa Waziri kama alivyoeleza katika malengo yake ya mwaka huu wa fedha 2007/2008 kwamba wanatarajia kununua matrekta manne. Basi katika hayo matrekta manne watakayonunua mapya yapelekwe KalilaKulukulu ili yaweze kufanya kazi iliyokuwa imekusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba kama tutaweza kuyaimarisha hayo magereza ya kilimo kwa kuyapa zana za kutosha, pembejeo na mbegu bora, tutapunguza misongamano ya wafungwa kwenye magereza yaliyopo mjini, tuwapeleke kwenye magereza ya kilimo yaliyopo pembezoni. Nadhani magereza yanaweza yakajitosheleza kwa kuzalisha chakula cha kujilisha yenyewe na cha ziada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nizungumzie pia suala la uhamiaji hasa katika Mipaka yetu upande wa Magharibi. Mpaka wetu upande wa Magharibi ni Ziwa Tanganyika. Kuna Vituo zaidi ya 30 kutoka Kasanga mpaka ufike Kigoma.

Eneo lote hilo lipo wazi. Askari wachache wa Uhamiaji ambao wamewekwa katika maeneo ya mwambao wa Ziwa Tanganyika hawawezi kudhibiti kabisa uingiaji holela wa wageni nchini. Vituo hivyo mbali na kwamba vipo mpakani, na Vituo vingi vya Uhamiaji vipo mipakani, havina mawasiliano na mawasiliano ni duni kabisa.

Hawana *radio calls*, mahali ambapo wamepeleka *radio calls* wamepeleka *radio calls* mbovu hazifanyi kazi. Kwa hiyo, napenda kuishauri Wizara iende ikatazame zile *radio calls* ambazo zimeharibika zitengenezwe haraka ili ufanisi uweze kupatikana katika mipaka yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nizungumzie kwa haraka tu kuhusu wakimbizi. Wakimbizi bado ni tatizo, kasi ya wakimbizi kurudi makwao hasa katika makambi ambayo yamesahaulika ya muda mrefu ya Katumba, Mishamo na Ulyankulu ni tatizo. Idadi ya wakimbizi iliyotajwa katika jedwali mimi bado nina mashaka nayo.

Nadhani idadi ni kubwa zaidi. Kwa sababu watu hao wamekwishakaa nchini kwa zaidi ya miaka 30. Leo katika Mikoa ya Rukwa na Kigoma huwezi kumjua Mtanzania ni nani na mgeni ni nani? Nilikuwa namuuliza siku moja Afisa Uhamiaji kwamba aniambie ni kitu gani ambacho kinaweza kikanitambulisha kwamba mimi ni Mtanzania. Kusema Kiswahili, rangi, nywele, lugha za wenyeji? Ni kipi ambacho unatakiwa Mwenyekiti awe nacho, mimi niwe nacho, Mheshimiwa Waziri awe nacho ili kuthibitisha utanzania wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu tulizembea katika eneo la kuwa na vitambulisho, tatizo ni kubwa kuliko tunavyotazamia. Pamoja na juhudi zinazofanywa nadhani kwamba eneo la wakimbizi bado ni tatizo. Kibaya zaidi ni uharibifu wa mazingira unaofanywa na wakimbizi ambao wamekaa katika maeneo yetu kwa muda mrefu na hakuna *remedies* zozote ambazo kama Wilaya ambayo ilipokea wakimbizi tunapata kutoka Serikalini mbali na hizo huduma chache tunazoletewa tunachangia na wakimbizi.

Vitanda vichache tulivyonavyo katika hospitali yetu ya Wilaya tunachangia na wakimbizi, madawa machache yaliyolengwa kwa ajili ya Watanzania tunachangia na wakimbizi. Hatuwezi kuwanyima hizo huduma kwa sababu ni binadamu na wamekuja kwa sababu ya matatizo katika nchi zao. Naiuliza Serikali Wilaya ambazo zime- *host* wakimbizi kwa kipindi kirefu ni lini zitapata r*emedies*?

Mwisho kabisa, nizungumzie tu zimamoto. Pamoja na ugumu wa upatikanaji wa magari ya zimamoto na jitihada za Wizara zinazofanywa, napenda tu kuomba Wizara ya Mambo ya Ndani katika mipango yao ijayo na katika bajeti zinazokuja kwamba Mpanda sasa ni Halmashauri ya Mji na ni Mji unaokua kwa kasi, tuna uwanja wa ndege ambao unapokea ndege nyingi tu zinazoleta wageni wawindaji na wafanyabiashara wa kawaida. Tunahitaji kuwa na gari la zimamoto. Naomba Wizara itutazame katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia kwenye bajeti hii. Vilevile nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Joseph Mungai, kwa hotuba yake. Nimpongeze Mheshimiwa Lawrence Masha, Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na pongezi hizo kwa mara ya kwanza na pamoja na kuwaheshimu Mheshimiwa Joseph Mungai na Mheshimiwa Lawrence Masha, siungi mkono hoja hii na nitatoa sababu na naamini na wenyewe watanielewa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na kutounga mkono hoja hii kuna sehemu moja ya kwanza lazima nitoe pongezi nayo ni Idara ya Magereza. Wenzetu wa Magereza mengi yamesemwa hapa, kwa kweli nitakuwa mchoyo wa fadhila kutotoa pongezi zangu kwa kazi nzuri sana wanazozifanya watu wa Magereza. Mimi ninapongeza sana. Kule kwangu Karagwe ninayo magereza yangu mawili. Moja la Kayanga na lingine la Kitengure, wale watu huwa wanafanya kazi mpaka mimi mwenyewe kwa kweli ninafurahi. La kwanza, ambalo ninawapongeza watu wa magereza ni nidhamu ambayo ipo kwenye Jeshi la Magereza kwa kweli ni nidhamu ya hali ya juu sana. Wengi tunafahamu kwamba katika matukio mbalimbali yanayotokea ya ujambazi hapa nchini nadhani hatujawahi kusikia Jeshi la Magereza wakifanya vitu vya namna hiyo. Nawapongezeni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niwapongeze watu wa Magereza kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya ya kuwafunza wafungwa wanapokuwa mle ndani. Wafungwa hawaendi kule kufungwa tu, lakini wanaenda kupata mafunzo na wengi wanaotoka kule wanakuja na ujuzi mzuri, wanakuwa wajenzi, wanakuwa ma-*carpenter* na hiyo ni kutokana na kazi wanayoifanya kule askari wa magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niwapongeze kwa shuruba wanazozipata bila wao kupenda, lakini kwa sababu ya *nature* ya kazi zao. Askari wa Magereza ananyeshewa na mvua, anatembea kwenye jua, wakati mwingine anapambana na majambazi ambao wapo ndani, kuna wengine hujeruhiwa na wengine hufa. Lakini bado wanavumilia nawapongeza. Nataka niseme kwamba Wizara iangalie namna ya kujali maslahi yao angalau posho ya mazingira magumu. Askari Magereza anaposhinda kwenye jua au anavyoondoka na wafungwa, basi apewe angalau ile *allowance* ya kuweza kujikimu kwa siku hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije kwenye sababu zangu kwa nini siungi mkono hoja hii, nazo ni mbili. Moja, wengi wanafahamu kwamba Wilaya ya Karagwe ni Wilaya ambayo ipo pembezoni na ipo mpakani mwa nchi ya Tanzania pamoja na nchi ya Rwanda.

Wilaya hiyo kwa miaka mingi sana wananchi wa Karagwe wamekuwa wakipiga kelele kuhusiana na wimbi la wahamiaji haramu. Nadhani kama sitakosea ile Wilaya inaweza ikaongoza kwa nchi hii kuvamiwa na wahamiaji haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda pale utashangaa jinsi wahamiaji haramu walivyozagaa, sio watu wa kutafuta ni watu wapo tu wanapita mitaani, wameigeuza ile Wilaya ya Karagwe kuwa kama mali yao. Mwaka jana nilizungumza hapa Bungeni na Serikali ilichukua *initiative,* ilijitahidi ikaanza kuwaondoa wahamiaji haramu. Lakini walivyoondoka sasa hivi wanaendelea kurudi kwa kasi na ile Ofisi yetu ya Uhamiaji ipo pale na inawafahamu wapo mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kinachonisikitisha ni kwamba hao wahamiaji haramu wanapoingia nchini kwanza anakuja baba na mke wake, anakuja na watoto,

anakuja na wajomba. Vilevile kama haitoshi wanakuja na mifugo yao mingi sana wanaingia nayo katika Wilaya ya Karagwe na Serikali ipo. Njia wanazotumia kuingilia watu wa Uhamiaji wanazijua. Sasa mimi kinachonishangaza kwa nini hawaondolewi pale Karagwe, kuna tatizo gani? Ndiyo maana nikasema kwamba sitaunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wahamiaji haramu wanavyoingia Wilayani Karagwe ukienda sasa hivi, na nitamwomba Mheshimiwa Waziri na Naibu wake wapige kambi pale angalau ya wiki moja. Wanapoingia pale utakuta wanavamia ardhi yote. Sasa hivi wahamiaji haramu ndiyo wamevamia ardhi ya Karagwe, wameifanya ya kwao, wanachunga mifugo yao na kulima. Sasa wananchi wa Karagwe hawana hata nafasi ya kuweza kuzalisha mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine wahamiaji haramu hao wanavyoingia kiholela, kama walivyosema wengi hapa, ndiyo pale mnaposikia ujambazi Karagwe hauishi. Kila siku kukicha kuna ujambazi, sisemi kwamba ni wao peke yao pengine na watanzania wapo. Lakini sehemu kubwa sana ni hao wahamiaji haramu kwa sababu tunashindwa kuwa-*control.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali tafadhali chonde chonde Mheshimiwa Joseph Mungai wewe ni mzee wangu na rafiki yangu nisaidie sana pale Karagwe namna ya kuwaondoa wahamiaji haramu na iwe *once and for all,* siyo iwe zimamoto. Mimi nataka mkakati mzuri ambao utahakikisha kwamba Karagwe wanabakia watu ambao wanastahili kukaa Karagwe, siyo wahamiaji haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ambalo tunalipata ni kwamba hao watu wanapoingia kama Mheshimiwa Said Arfi alivyosema, wanakuja wanafaidi huduma za jamii. Kwa mfano, mtu anaumwa anaenda kutibiwa hospitali na kupewa dawa ambayo alitakiwa apate raia wa Tanzania ambaye ni mtu wa Karagwe. Lakini vilevile wanaingiza watoto shuleni. Sasa hivi ukienda kwenye shule utakuta watoto wale siyo Watanzania, wapo shuleni wanafaidi vitabu vyetu, mishahara ya walimu na kila kitu. Wengine kwa sababu ya uwezo wao ni wafugaji wana uwezo wa fedha wanaingia hata kwenye uongozi, wanachaguliwa wanaanza kushika hata nafasi za uongozi. Kama Serikali haitaweza kuidhibiti hali hii, nasema kwa kweli tutaendelea kupata shida sana. Namwomba Mheshimiwa Waziri katika majumuisho yake anieleze mkakati ambao Serikali imeuweka wa kuwashughulikia wahamiaji haramu kule Karagwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo linanifanya nisiunge mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na hapa kwa kweli niko *serious* ni vitendo vya unyanyasaji wa wananchi raia wa Karagwe kutoka kwenye Idara ya Uhamiaji. Idara ya Uhamiaji wamefika mahali wamekuwa kama ni miungu watu pale Karagwe. Mtu anafika pale anachukua jukumu la kumkamata mtu na kumpiga hadharani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani naamini kabisa anayo barua ya ndugu mmoja anaitwa Thomas Christopher Rwetabaza kutoka

Karagwe. Huyo ni mtu ambaye mimi binafsi ninamfahamu na *I can swear an affidant*, ninaweza hata kula kiapo. Huyu mtu ninafahamu. Ni raia wa Tanzania. Lakini kwa sababu ya maumbile yake amekamatwa na watu wa Uhamiaji pale Karagwe akapigwa hadharani kama mtoto mdogo. Utadhani jambazi anapigwa. Akapigwa, akanyang'anywa pasipoti yake ya Tanzania aliyokuwa anaitumia na mpaka sasa hivi hawajamrudishia. Baada ya kupigwa huyo bwana amelalamika kwenye vyombo vya dola. Aliandika barua mpaka kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Sikumbuki kama Mheshimiwa Joseph Mungai alishakuwa pale, lakini nazungumzia Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama Mbunge wake alinipa nakala ya barua yake. Lakini vilevile akasafiri kutoka Karagwe kwenda Dar es Salaam kwenye Ofisi ya Wizara kulalamika na mimi nilimwongoza. Akaonyesha malalamiko yake lakini mpaka sasa hivi ninavyozungumza huyo bwana na familia yake hawajajua hatma yao.

Mara leo aambiwe siyo raia, muda wowote anaweza kukamatwa, akaondolewa na mama yake mzazi yupo pale wa siku nyingi. Baba yake amezikwa kijiji kimoja kinaitwa Ahakishaka Tarafa ya Nyabiyonza. Lakini sasa huyo mtu kila wakati anakaa kwa mashaka, mke wake, ndugu zake wote hata hawajui hatima yao. Mara wakikaa kidogo anaambiwa kesho wewe tutakukamata na tutakupeleka Rwanda, hana amani. Hiyo ni kwa mtu mmoja ambaye *at least* anajua haki yake. Ningependa kufahamu ni kwa nini Serikali haijamjibu Bwana Thomas Christopher Rwetabaza kwamba je, ni raia au sio raia wa Tanzania? Lakini lingine huyu bwana alilalamikia vitendo vya kinyama alivyofanyiwa na ana ushahidi ni kwa nini Serikali haijaunda hata Tume ya kuwadhibiti wale Maafisa Uhamiaji Karagwe ambao walimpiga.

Mheshimiwa Mwenyekiit, ndiyo maana nikasema siwezi kuunga mkono hoja wakati naona raia wangu wananyanyasika kiasi hiki na Serikali imelifumbia macho na inasikitisha kwamba hata Serikali (dola) Karagwe iliona hili jambo na inalikumbatia. Kwa hiyo, nitapenda kwenye majumuisho Mheshimiwa Waziri anifahamishe ni hatua gani amechukua au hatua zipi anakusudia kuchukua kwa haraka sana ili huyu mtu na ndugu zake waweze kuishi kwa amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kama nilivyosema naendelea kuwapongeza watu wa Magereza kwa kazi nzuri na hata Uhamiaji wanajitahidi ingawa kuna wachache wanaoleta upungufu. Lakini nataka nizungumzie upungufu wa vitendea kazi katika Jeshi la Magereza. Kusema kweli Magereza pamoja na kujitahidi lakini vitendea kazi vyao ni vichache au kama sio vichache havitoshi. Hawana magari, hata nyumba wanazoishi hawa watu wa Magereza, ukienda hapa gereza la Isanga, niliwahi kumtembelea baba yangu mdogo, niliogopa hata kuingia kwenye ile nyumba. Huyu mtu ana mke na watoto halafu nafikiri ana V3, sasa nikasema huyu mtu mwenye V3 kama anakaa katika mazingira kama hayo, je, yule ambaye hana hata V moja? Kwa kweli mazingira ni mabaya hayaridhishi hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Gereza la Kayanga Wilayani Karagwe, nawapongeza wananifanyia kazi nzuri lakini wana gari la siku nyingi sana limechoka, limezeeka na

haliwezi kufanya kazi zao, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mungai awaangalie kwa kuwapatia gari jipya.

La mwisho kuhusu vitambulisho. Wilaya ya Karagwe ni Wilaya ya pembezoni au mpakani, watu wengi wanaingia mle. Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri wakati mnatoa vitambulisho muwe makini sana na ile Wilaya ya Karagwe kwa sababu watu wengi wanaweza kuja kujipatia vitambulisho wakati sio halali kupata vitambulisho hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kama nilivyosema siungi mkono hoja. Haya maneno nimeyasema kwa uchungu sana, sijawahi kusema hapa Bungeni na nitamwomba Mheshimiwa Waziri anisaidie katika majibu yake. Nashukuru sana.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia hoja iliyotolewa leo ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Niseme tu kwa upande wangu naiunga mkono hoja hii kwa masharti tu kwamba mwishoni anipatie maelezo ya kina kuhusiana na matatizo ambayo yamejitokeza katika kitabu hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo nataka kulizungumzia ni kwamba mwaka jana nilipokuwa nazungumzia hotuba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi wakati ule alikuwa Mheshimiwa Chilligati, nilizungumzia suala zima la hali mbaya ya Gereza la Kibiti.

Namshukuru Mheshimiwa Chilligati mara baada ya kutoa mchango wangu Jeshi la Magereza kwa makusudi kabisa lilikwenda Mng'aru wakaona hali halisi ya lile gereza lakini hatua za utekelezaji mpaka leo bado. Sasa hilo ndilo tatizo ambalo linanifanya mimi nisimame leo na kuchangia hotuba hii.

Mwaka jana nilizungumza kwamba gereza hili kuwa ni miongoni mwa Magereza mabaya sana kimajengo katika nchi yetu. Gereza ambalo wafungwa wanaishi, lenyewe ni *full suit,* lina bati juu, lina bati chini na wakati wa mvua inaponyesha lile gereza kule juu bati zote zimetoboka maji yanaingia ndani na pembeni maji vile vile yanaingia ndani. Kipindi chote cha mvua hasa kipindi cha masika wafungwa wanaishi maisha magumu sana kiasi ambacho wakati mwingine hata kulala hawalali.

Vile vilalio vyao vinakusanywa kusanywa na kuhifadhiwa mahali, wanakaushakausha labda wataweza kulala. Lakini kama itanyesha mvua usiku kucha basi hao wafungwa hawalali, wanateseka. Nililizungumza, pia suala la nyumba wanazoishi askari Magereza.

Katika gereza lile la Mng'aru nyumba zote za askari ni za udongo, zimejengwa zaidi ya miaka 20, 30 iliyopita. Nyumba ambayo ni ya matofali ni ya Mkuu wa Gereza tu nayo si nzuri, ni nyumba moja mbaya sana. Sasa nilitaka kujua Mheshimiwa Waziri

katika bajeti yake ya mwaka huu amepanga nini kuhusiana na hilo kwa sababu tayari Maafisa wa Jeshi walishakwenda kule na kuangalia majengo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kinachonipa utata ni jina la gereza. Katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri ukurasa 15 ameandika, msitari wa 6 kutoka chini, gereza lile linaitwa Kibiti lakini kwenye ukurasa mwingine, ukurasa 47 kuna shabaha na malengo kwa mwaka 2007/2008 kwenye Idara ya Magereza kipengele (e).

Kuna aya inayosema, "Aidha, ujenzi wa Magereza utaendelea kufanyika katika Magereza ya mahabusu: Singida, Mbozi, Isopilo, Rombo, Igunga, Kigongoni, Kwamngumi, Wazo, Mng'aro. Sasa sina uhakika *Mng'aro* hii ndiyo ile Mng'aru ya Rufiji au *Mng'aro* hii ni *Mng'aro* gain? Gereza la Kibiti au Mng'aru limejengwa katika Kijiji cha Mng'aru, sasa hili jina la gereza ni lipi ni Kibiti au ni Mng'aru?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni Mng'aru kwa kuwa mwaka huu itapatiwa nafasi ya ujenzi nitaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Lakini kama hili jina sio Mng'aru lile ambalo nalijua mimi ni Mng'aru nyingine kwa kweli masharti yangu kama alivyosema Mheshimiwa Blandes yatakuwa pale pale.

Kwa hiyo, nitaomba katika kujumuisha Mheshimiwa Waziri anieleze jina halisi la gereza la Kibiti au la Mng'aru? Kwa sababu hata wachangiaji wa Kamati ya Kudumu ya Ulinzi na Usalama wameeleza gereza lile ni Kibiti. Msemaji wa Kambi ya Upinzani amesema gereza lile ni Kibiti, lakini hapa kuna jina la Mng'aru ambalo ndilo jina halisi la mahali gani gereza hilo lipo. Kwa hiyo, naomba sana Waziri atakapofanya majumuisho yake basi anieleze kwa uhakika jina halisi la gereza lile ni Kibiti au Mng'aru?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza hali hii nizungumzie kidogo tu katika gereza hilo suala zima la kilimo. Gereza lile ni la kilimo. Katika miaka ya 1980 hadi 1990 gereza hili lilikuwa linatoa chakula kingi sana kwa ajili ya Wilaya ya Rufiji na mara nyingi Wilaya ya Rufiji inapokuwa na matatizo ya chakula basi Serikali ya Wilaya chini ya uongozi wa Mkuu wa Wilaya walikuwa wanachukua chakula kutoka pale gerezani na kupeleka katika maeneo ambayo yana matatizo ya chakula hasa maeneo ya ukame. Lakini kwa miaka zaidi ya mitano au sita hivi gereza lile uzalishaji wake umeshuka sana.

Gereza lile lina wafungwa wengine wana miaka 30, wengine miaka 20, wengine ni wafungwa ambao hawatarajii kutoka ni wa moja kwa moja mpaka kifo chao. Nilipokwenda kuwatembelea walikuwa wanataka sana vifaa vya kilimo, wapewe hawa wafungwa matrekta ya kuweza kufanyia kazi. Nina imani kabisa kama watapewa zana hizi za kilimo kwa mfano trekta moja tu likienda pale litabadilisha hali ya lile gereza na kuwa katika hali nzuri zaidi.

Mheshimiwa Arfi alipokuwa anachangia alisema mwaka huu katika bajeti yametengwa matrekta manne. Matrekta manne ni machache sana kwa Jeshi la Magereza hapa nchini. Lakini mimi nimekuwa nakijiuliza Serikali hii inayokopesha matrekta watu binafsi kwa kupitia Mfuko wa Pembejeo hivi itashindwa kweli kuikopesha gereza ambalo lina nguvu

kazi nyingi kiasi ambacho wanaweza kulima eka 3,000, 4,000 kwa mwaka na wanaweza kurudisha deni lile kwa mwaka mmoja, inashindwa namna gani?

Mtu binafsi mwenye ekari 50 anakopeshwa lakini taasisi ambayo ni ya kudumu haibadiliki inashindwa kukopeshwa trekta moja liweze kufanya kazi ndani ya mwaka mmoja, lina uwezo kabisa wa kurudisha gharama zote za trekta lile, hivi inashindwa nini?

Jeshi la Magereza litaendelea kuombaomba chakula mpaka lini kwa sababu pale gerezani mpaka sasa hivi haliwezi kujitegemea, halina chakula, linapata ruzuku kutoka Serikalini. Lipewe trekta hawa waweze kufanya kazi waweze kuzalisha chakula kingi zaidi. Hivi utaratibu huu kwenye taasisi haupo upo kwenye watu binafsi tu, hili ninaomba nipatiwe ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengine ni kuhusiana na migogoro ya mipaka katika gereza hili la Mng'aru. Gereza la Mng'aru linapakana na vijiji vinne, kuna kijiji cha Ngulakula, Kimbuga, Miwaga na kijiji cha Mng'aru chenyewe. Gereza wakati huo lilipokuwa limeanzishwa walijitengea eneo kubwa sana, wana eneo la ekari zaidi ya 30,000.

Ekari 30,000 ni nyingi sana na wananchi walikubali kwa wakati ule kwa sababu tu kwamba hawa askari wa Magereza pamoja na wafungwa wale walikuwa na uwezo wa kulima eneo kubwa sana. Lakini sasa hivi eneo hili lote halilimwi, linalolimwa hazifiki hata eka 500 kati ya 30,000. Wananchi nao wanataka eneo la kulima watalipata wapi na wakiingia pale askari Magereza wanawazuia! Sasa hao askari wana-*retain* hili eneo ambalo halifanyiwi kazi mpaka lini? Matrekta ya kulimia hawana, wanalikumbatia hilo eneo mpaka lini? Mimi nafikiri kama Magereza imeshindwa kuitumia ile ardhi ni vizuri ardhi hiyo itumike kwa kuwapatia wananchi wanaozunguka eneo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ni kuhusiana na uwezekano wa kuwapatia umeme pale gerezani Mng'aru. Kwa sasa umeme unakaribia kufika Kibiti, tayari nguzo zimetandazwa mpaka Kibiti na nyaya zimeshawekwa. Kutoka Kibiti hadi kufika Mng'aru hazizidi kilomita 7 lakini kuna eneo lingine vilevile unaweza kulichukulia umeme, halizidi hata kilomita 3.

Kwa hiyo basi katika bajeti inayokuja Waziri aweke na hilo au apeleke umeme pale ili wafungwa pamoja na askari wanaowarekebisha tabia zao waweze kufaidika kwa kutumia umeme kwa kuanzisha viwanda vidogo vidogo, kwa kuanzisha kazi mbalimbali. Eneo lile limezunguukwa sana na misitu, wana uwezo wa kutengeneza fenicha, wana uwezo wa kuzalisha sana kiasi ambacho gereza linaweza likajitegemea na kuliingizia pato gereza lenyewe pamoja na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo kama nilivyosema mwanzoni nitafurahi na nitakubaliana na Mheshimiwa Waziri kama atanipatia jina halisi la gereza lakini la pili nitakubaliana kama ile Mng'aru iliyowekwa pale ndiyo hiyo inayotarajiwa kupatiwa ujenzi katika kipindi cha fedha cha mwaka huu wa 2007/2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi.

**MHE. FELIX M. KIJIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu kidogo kuhusu suala la Wakimbizi kwa sababu ni suala ambalo linanigusa sana kule ninakotoka Wilaya ya Kibondo. Wachangiaji hapa wamezungumza, wameeleza athari zinazotokana na suala la Wakimbizi. Kwangu Kibondo nasema tangu mwaka 1993 Wakimbizi walipoingia bado nina Wakimbizi mle ndani ni mwaka wa 15 sasa. Serikali imeweka msisitizo kwamba Wakimbizi wataanza kuondoka kurejea kurudi kwao. Lakini kasi ya urejeaji inakuwa ni ndogo sana na inakuwa ni ndogo kutokana na hawa watu, Mashirika yanayohudumia Wakimbizi kuendelea kukaa hapa nchini kwa kutaka ajira.

Hii imekuwa ni changamoto kubwa sana ambayo imesababisha suala la Wakimbizi lisimalizike hapa nchini. Tumekuwa na Makambi kuanzia mwaka 1972 yako Mpanda kule Mishamo na Katumba, Ulyankulu, Tabora. Hawa watu leo wanaletwa sasa Kibondo tena watu wanakuja kuchujwa na Shirika moja la *IOM*, Shirika la Kimarekani ili wapelekwe kule Marekani kwenda sijui kufanyishwa kazi gani. Sasa hii Kibondo imeonekana ndio uwanja mzuri sana wa kukaribisha Wakimbizi kwa sababu na sisi tumefika mahali ambapo sasa tunaanza kuchoka kukaa na hao watu.

Sasa hivi Kibondo huwezi kulala bila ya kusikia mlio wa bunduki. Huwezi ukatoka Kibondo ukaenda Kigoma ama Kasulu bila kupata *escort* ya Polisi vinginevyo utapata misukosuko mikubwa sana pale njiani. Sasa hali hii tutaendelea nayo namna gani. Kule Burundi hali ni salama, tunaelezwa kila siku hali ni salama na viongozi wanakwenda kutembelea kule kuangalia kama hali ya Burundi ikoje, majibu yanarudi ni salama, kwa nini hawa watu tunawaendekeza? Kuna mawili, ni kuwalea ama kuyalea haya mashirika yanayohudumia Wakimbizi ili tuendelee kuwafaidi kwa sababu kuna watu wanafaidi mashirika hayo na mimi hili nalikemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ni kubwa sana hili la Wakimbizi linalosikitisha, tatizo la ujambazi, mauaji, wizi wa mifugo ni mambo yanayofanyika katika mikoa yenye Wakimbizi kama vile Mkoa wa Kigoma na Kagera nina hakika. Lakini inakuwa ni kama kiini macho, hakuna mtu anawaonea uchungu wananchi wa maeneo hayo kwamba wanaishi maisha ambayo si ya kwao, kigugumizi kinatoka wapi? Kama misaada ya magari imeshapatikana, tuachane na hii misaada ndiyo inatufikisha mahali pabaya, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, napenda nizungumzie pia hii misaada ambayo imekuwa ikitolewa na hawa watu wanaohudumia Wakimbizi kwa sababu ya kupata hiyo misaada ya masharti. Kama anakwambia atajenga majengo kwa ajili ya Wakimbizi lazima mjenzi amtafute yeye, mimi nilikuwa nadhani kwamba kazi kama hii hatuombi kwamba tuendelee kuwa na Wakimbizi, mimi siwataki kabisa hawa kuwaona kule kwangu, sitaki!

Lakini wanachokifanya ni kwamba kazi zote ambazo zinahudumia Wakimbizi kunakuwa na Vishirika vidogo vidogo wanawapatia kwa ajili ya *ten percent*. Wanawapatia hao ndio wanakwenda kuingiza huko kitu kinachoandaliwa kijengwe hakijengeki, hivyo kwa sababu pesa inayotolewa inazunguka mikononi mwa watu wengi. Sasa tunakaa tunazungumza tunatetea suala kama hili lakini tujue kwamba mwisho wake sio mzuri sana ni mwisho mbaya wa kuwatesa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mzungumzaji aliyemaliza sasa hivi amezungumza jinsi anavyopata matatizo na mwingiliano wa Wakimbizi kutoka nchi jirani kule Karagwe. Hii hali pale Kibondo ipo lakini tutaidhibiti namna gani kama tutaendelea kuwa nayo. Tunaelewa kabisa kwamba ile mipaka ama Wilaya ambazo ziko mpakani hakuna mipaka ya kuzuia mtu asitoke nchi jirani kuingia nchi nyingine, lakini tunafanyaje, ni lazima tudhibiti hivyo vipenyo vinavyoingiza hawa watu.

Leo tunapozungumzia kwamba Warundi wanaondoka wakati tayari kuna mkakati wa Jumuiya na Shirikisho kuwafanya hawa watu waingie humu ndani mimi sijui kama hao watu watatoka tena kwa sababu wameshafikia hatua ya kulima mashamba. Leo nikimwuliza Mheshimiwa Waziri kwamba kwa nini Wakimbizi hawajaondoka jibu atakalolitoa ni kwamba wana mashamba ambayo wameyalima. Sasa wanalima mashamba na shamba ndilo linakuzuia Wakimbizi wasiondoke.

Kama dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba Mkimbizi anaondoka, naomba hivi vishawishi vinavyowafanya Wakimbizi kuendelea kuwapo, Serikali ivifutilie mbali, hakuna cha mashamba au kufuga, waondoke waende kule kwao, kwao ni salama salmini. Lakini tuwe makini pia hilo Shirikisho litakapokamilika nina hakika kwamba Wakimbizi wengi ambao tunao hawataondoka, itakuwa kama tunavyoishi na Wakenya hapa, Dar es Salaam ni vurugu tupu, Wakenya, Waganda wanaishi kienyeji. Lakini Mtanzania huwezi ukatoka hapa ukaenda Kenya ukaishi bila ya kuwa na pasipoti, wao wanakuja, wanakaa tu na wala hatuwaelewi.

Nampongeza sana Mkurugenzi wa Uhamiaji amekuwa akipitisha misako mikali kabisa ya kukamata hawa watu lakini wakati mwingine namhurumia akikamata watu mia nne atawasafirisha namna gani wakati hana kasma na bahati mbaya hata kwenye kitabu hiki ambacho tumesomewa na Mheshimiwa Waziri hakuna kasma inayoonyesha kwamba kuna fedha zimetengwa kwa ajili ya kusafirisha hawa wageni haramu wanaovamia nchi yetu na hasa Dar es Salaam ama miji mikuu.

Sasa sijui Mheshimiwa Waziri utanieleza nini kwamba kama unataka Mkurugenzi wako wa Uhamiaji afanye kazi fedha za kusafirisha hawa wavamizi ama wageni haramu wewe utazipata wapi ama yeye atazipata wapi? Kwa sababu nina hakika hiyo misako inaendelea kufanyika na imekuwa ikisaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la vitambulisho ni suala ambalo kusema kweli limekuwa linazungumzwa na limekuwa ni wimbo sawa na wimbo wa Taifa. Hili suala la

vitambulisho ni lazima likamilike sasa hivi, likamilike kila Mtanzania apate kitambulisho.

Nakumbuka kwenye bajeti ya mwaka jana hapa tumeelezwa kwamba fedha zimetengwa kwa ajili ya kutengeneza vitambulisho hivyo lakini tumekwenda tumemaliza mwaka tumeingia kwenye mwaka mwingine wa fedha bado hivyo vitambulisho havijapatikana kuna nini, vinatengenezeka au mtengenezaji yuko wapi?

Hata bajeti ya mwaka kesho bado suala la vitambulisho litazungumziwa na hii ndiyo inasababishwa tuendelee kuwa na watu ambao kusema kweli hawatakiwi kuja kuleta vurugu ndani ya nchi yetu. Vurugu zote zinakwenda Usalama wa Raia, wanapata matatizo ndio Mambo ya Ndani yenyewe matatizo kwa sababu ni Wizara zinazofanya kazi pamoja. Kwa hiyo, nadhani tunapokuja kuzungumza hapa ndani ya Bunge kama Wabunge tuzungumze yale mambo ambayo yanatekelezeka vinginevyo tutakuwa tunadanganya tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia kitabu hiki, nina kitu ambacho mara nyingi nimekuwa nikijiuliza kwa sababu wakati nikipitapita kwenye Magereza unaweza ukakuta mahali fulani chakula hakuna kwa sababu bajeti haiwezi kuzingatia ongezeko la wahalifu. Sasa sijui Wizara imejipanga namna gani kuhakikisha kwamba kwenye bajeti ya chakula kwa wafungwa itaongezwa vipi endapo ongezeko la wafungwa litakuja.

Haya mambo lazima tuyaweke wazi vinginevyo tutakwenda ovyo wakati hatuna uwezo wa kupata fedha zingine, ndiyo tutaanza kukimbilia sijui maafa waongeze, waongeze nini halafu mambo mengine mazito hayakufanyika wakati ni kosa la kuandaa bajeti. Tunapoandaa bajeti ni lazima tuwe tumekaa tujue matatizo ni nini yanayoweza kujitokeza, tutayatatua namna gain. Bajeti itakuja itasomwa kwa Waheshimiwa Wabunge na sisi tutabariki haya maneno.

Kwa mujibu wa Sheria ya Uokoaji, Namba 14 ya Mwaka 2007 kama tulivyosomewa inahusu Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Sasa nadhani tunaweza tukajiridhisha kwamba hilo Jeshi lipo, lakini lipo? Nikitazama pia kwenye maandalizi ya Wizara hakuna mahali ambapo pametengwa kwamba hilo Jeshi litahudumiwa, nadhani itakuwa ni idara sawa sawa na ilivyo Uhamiaji itahudumiwa na fedha kutoka wapi?

Hakuna magari! Tumeelezwa kuna watu 250 sijui wametolewa Vyuo Vikuu, wameajiriwa watakwenda kujifunza, fedha zitatoka wapi? Haikutajwa hapa ndani. Haikutajwa wakati tumeelezwa kwanza inaanza sasa, kama inaanza sasa isingekuwa kwenye utaratibu. Kama iko kwenye utaratibu nashauri kwamba hizi Idara zinazoanzishwa kwenye Wizara zijitegemee kifedha, ziwe na kasma za kwao, hizo kasma zitawarahisishia hata kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Dar es Salaam nimekuwa muda mrefu sana, moto ukitokea mahali uharaka wa kufika kwenye tukio na kuokoa jengo linaloungua ni kitendawili. Kwa sababu magari ni mabovu, mpaka taratibu zifanyike za kuanza kuazima magari kutoka bandarini. Bandarini wana magari ya kisasa, wanasema gari lenye ngazi

ndefu na jengo la Kitega Uchumi linaungua sijui leo kama jengo la *PPF Tower* likiungua tutapata gari wapi la kuzima moto. Lakini magari haya haya ya *Fire* yanatakiwa nadhani yawe kwenye viwanja vya ndege ambavyo kusema kweli baadhi ya Mikoa na Wilaya wamekuwa na viwanja na ndege, vinatoa huduma kama kawaida lakini sasa utakuta kwamba hivyo viwanja havina huduma kama hiyo.

Kule kwangu Kibondo nina kiwanja cha ndege na ndege zinatua za Wakimbizi sasa hivi, hata za Marekani zinakuja hadi juzi nilipowapiga *stop* kwamba wanaharibu uwanja ndio wanataka kutengeneza ule uwanja kwa kiwango cha lami. Sasa Wizara inajipanga namna gani kama uwanja unapanuliwa ina maana uwanja utaendelea kutumika.

Vinginevyo Wakimbizi ambavyo wanasafirishwa hata kuja kuungua pale wakiwa kwenye ndege na hakuna moto, huo moto sijui utazimwa namna gani. Kwa sababu kuna *pickup* ya *UNHCR* inakwenda na pipa la maji, *can you imagine* pipa la maji linazima moto. Ni utaratibu upi ambao tunatakiwa tuufanye wa kwenda kwenye maeneo ya matukio sio ya kuzungumza. Bila kufika kwenye eneo la tukio huwezi ukaamua kitu ambacho kinakidhi mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu kwa walioajiriwa kwa ajili ya Zimamoto, hakuna palipotajwa kwamba hawa watu wametoka shuleni. Lakini kuzima moto sio suala la kuzima mototu, kuna elimu inatakiwa, watu waende wakafundishwe jinsi gani tunazima moto, lakini kitabu hakikueleza. Sasa sijui, nashindwa kujua hawa watu watafundishwa na nani, labda Mkuu wa Kikosi atatoa mafunzo hayo lakini atayatoa namna gani bila ya kuwa *budgeted*? Kwa hiyo, nadhani kwa kweli tunapoamua kufanya kitu tufanye kitu ambacho kinaonekana ili mwaka mwingine wa bajeti tusianze kurudia tuliyoyafanya. Nasikitika kusema kwamba mengi yamejirudia rudia sana, tumerudia mambo tuliyozungumza mwaka jana na haya yanaendelea kwa matatizo madogo madogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu magari hii Wizara ina matatizo ya magari. Magari yaliyopo ni machache. Ukiangalia karandinga kwa mfano, Dar es Salaam, karandinga lipo moja ambalo linazungukia Magereza yote kukusanya mahabusu kuwapeleka Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na hayo, naomba kuunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kijiko kwa kuunga mkono hoja na kwa ushauri mwingi ambao umeutoa kwa Wizara hii. Waheshimiwa Wabunge tutakaporudi saa 11.00 jioni, mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Diana Chilolo, atafuatiliwa na Mheshimiwa Abdallah Sumri, namwona yupo kabisa anajiandaa na wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Raynald Mrope. Baada ya hapo atafuatia Mheshimiwa Naibu Waziri kwa nusu saa na Mheshimiwa Waziri mwenyewe kwa nusu saa, wamegawana saa moja. Basi kwa kuwa shughuli zilizopangwa kwa asubuhi ya leo zimekamilika naomba kusitisha Shughuli za Bunge hadi saa 11.00 leo jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilifungwa mpakas saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mwenyekiti alipokuwa anasitisha shughuli za Bunge mchana, aliwataja wafuatao kwamba watachangia mchana huu; Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa S. Abdallah Sumry na Mheshimiwa Raynald A. Mrope.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuwa mchangiaji wa mwanzo kabisa kwa jioni hii ya leo. Baada ya kukushuru wewe, nitumie nafasi hii pia kuipongeza sana Bajeti hii, nzuri, imeanisha mambo mazuri na ni matumaini yangu kwamba, Bajeti hii ina lengo thabiti la kuimarisha Sekta zote katika Wizara hii ya Mambo Ndani. Namwomba Mwenyezi Mungu, awatie nguvu ili waweze kutekeleza azma yao kama walivyoiandaa. Baada ya pongezi hizi, nitumie nafasi nyingine tena niwapongeze Wakuu wa Megereza, kwa kweli Magereza sasa hivi ni safi sana, wanajitahidi, hali ya usafi inatia moyo. Mimi nina tabia ya kutembelea Magereza, nimetembelea Magereza ya Singida na Dodoma, kwa niaba ya Magereza mengine nina imani kabisa Magereza ya Tanzania sasa hivi ni safi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizi sasa naomba nijikite katika maeneo ambayo ninapenda kutoa mchango kwa jioni hii ya leo. Usishangae kuona mada nyingine zinarudiwa rudiwa na kila mchangiaji anayeinuka, ujue zina umuhimu wake. Tunachangia kwa sababu ya kuweka msisitizo ili Serikali iweze kuona umuhimu wa kuzitekeleza haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza na suala la vitambulisho. Vitambulisho ni muhimu kabisa kwa Watanzania. Tumeshaona matatizo makubwa yanayojitokeza nchini, kwa sababu raia wa Tanzania hatuna vitambulisho. Matukio makubwa makubwa yanayojitokeza sasa hivi, ukikuta majambazi watano wamekamatwa, Watanzania ni wawili, wageni ni watatu. Hivi hawa wageni tutawajuaje? Hatutaweza kuwafahamu hawa wageni endapo Watanzania hatutakuwa na vitambulisho. Ninaomba sana Serikali, madhali suala hili wameshalikubali ni wakati muafaka sasa kutilia maanani, kuweka nguvu zote kuhakikisha sasa wanaandaa vitambulisho ili Watanzania tuweze kuwa na vitambulisho, tupate njia maalum ya kuwatambua wageni ambao wanaingia nchini kwa nia mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani hata Balozi alikuwa ana heshima yake, lakini sasa hivi mimi sioni kama anathaminiwa. Zamani Balozi alikuwa ana majukumu mazito, mgeni yeyote katika eneo lake ilikuwa lazima mwenyeji wake ampeleke kwake akamtambulishe. Lakini sasa hivi tabia hiyo haipo, matokeo yake tunafuga watu wanaoleta athari katika nchi yetu, wanaochelewesha maendeleo ya watu.

Wafanyabiashara wakubwa wakubwa wenye nia njema ya maendeleo na kuleta Pato la Taifa, wanapata tabu ya kuvamiwa na majambazi wanaoingia kwa njia zisizokuwa za halali, kwa sababu tu eti Watanzania hatuna vitambulisho. Naiomba Serikali ilitilie maanani suala la vitambulisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hilo, naomba niongelee suala la mishahara na maslahi ya Askari Magereza. Ni ukweli usiojificha kwamba, askari wanafanya kazi kubwa sana, tena kazi ya ku-*risk* maisha. Askari anaondoka na wafungwa mpaka porini kwenda kusanya kuni. Hivi hawa wafungwa wakimgeuka huko si hatari mojawapo hiyo? Yote hayo wanavumilia kwa sababu ni kazi yao, lakini tunapokuja kwenye maslahi tunawasahau. Ninaomba sana Serikali iangalie suala zima la mishahara, iboreshe mishahara ya Askari Magereza kwa sababu kwa kweli haitoshelezi kabisa kukidhi haja ya mahitaji yao. Nina hakika kabisa hata wanapostaafu hawa maisha yao ni magumu kidogo, unaweza ukakuta hata nyumba hawana, kwa sababu ya mishahara midogo na si mishahara tu hata maslahi mengine. Unampa askari kazi, unamtuma kutoka Dodoma anakwenda Singida kwa nauli yake, anarudi kwa nauli yake, analala kwa fedha yake, anakula kwa fedha yake, hivi anamshahara gani huyu mpaka aweze kumudu mambo yote haya?

Ninaomba sana habari ya kuwakopa Askari Magereza sasa ifikie mwisho. Tunapowapa watu kazi tuwape na ujira wao, kazi na dawa. Unapompa askari ujira wake pale unapompa majukumu, unamtia moyo kufanya majukumu yake vizuri na si hivyo tu, wanapokosa mahitaji muhimu ama wanapokosa maslahi yao, ndiyo hapo rushwa inaingia. Wapo Askari wanaoshawishiwa na wafungwa, bwana shika hii hapa hela ndugu yangu niache mimi nitoroke. Mara nyingi wafungwa wanatoroka kwa njia hizi hizi za ulofa. Askari ananunuliwa kwa vitu vidogo tu, pesa anapokea, anakiuka Sheria, mfungwa anaingia mitini. Ninaomba sana ufike wakati sasa, habari ya kuwakopa askari iishe, tuwape majukumu na ujira wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuongelea hilo, naomba nizungumzie suala la nyumba. Wakati wanachangia Waheshimiwa Wabunge kwenye Bajeti ya Usalama wa Raia, waliongelea sana suala la nyumba. Suala la nyumba linaenda sambamba kabisa na Wizara ya Usalama wa Raia. Askari wetu bado wanaishi kwenye nyumba za mkoloni, ambazo tayari zimeshapitwa na wakati, tena si nyumba, tuseme vijumba maana ni vidogo, vijumba ama vibanda vyenye chumba kimoja na sebule. Alisema siku moja Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar hapa; hivi hii nyumba watalala vipi? Mama na baba pale pale, watoto wa kiume hapo hapo, watoto kike hapo hapo; hivi kweli kama kufundisha maadili hawa askari wanaweza kufundisha maadili hawa? Hata mtoto akikurupuka kupata mimba akiwa mdogo; utakayemlaumu ni nani?

Ninaomba suala la kukarabati vibanda vilivyopitwa na wakati sasa liishe. Tubomoe hivyo vibanda, tujenge nyumba zenye hadhi, angalau zenye kukidhi haja ya mahitaji ya askari wetu, angalau hata vyumba viwili ama vitatu. Watoto wa kike wapate chumba chao na watoto wa kiume wapate chumba chao na wazazi wapate chumba chao. Hii kwa kweli itatia moyo na italeta heshima na maadili ya familia. Ninafahamu wazi

kwamba, majukumu ya Serikali ni mazito, lakini pamoja na hayo suala hili lina umuhimu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee suala la upandaji vyeo kwa maaskari. Askari wengi wanakaa na cheo kimoja kwa muda mrefu mno na wapo wengine hata vyeo hawana. Ni Polisi Konsitebo toka alipoanza kazi mpaka anastaafu; hivi kweli ana hatia gani huyu asipande cheo? Kwa nini askari huyu asipelekwe kusoma, kama ana makosa umempa barua, umemkanya mara ngapi, kama si kuwaonea ni nini? Ninaomba utaratibu wa kuwapeleka askari kusoma utumike vizuri, askari wetu ambao wana mienendo mizuri wanafanya kazi vizuri, wanasifa za kujiendeleza, wapewe nafasi ya kusoma ili waweze kupanda vyeo. Ninajua kwamba, vyeo vya maaskari vinaenda na kusomea.

Baada ya kusema hilo katika suala hilo hilo la kusoma, Serikali imetangaza hapa kwamba, Watumishi wa Serikali wajiendeleze. Watumishi wengi wameitikia wito wa kujiendeleza hata Askari Magereza wameitikia kujiendeleza, lakini wanaambiwa eti wajisomeshe. Hivi mtumishi huyo huyo anayepata kima cha chini leo, unamwambia ajisomeshe, huyu askari ataweze kulisha familia, ataweza kusomesha watoto, ataweza kuweka hata akiba ya kujenga nyumba? Ninaomba sana Serikali iwasomeshe askari, ichukue mzigo huu kwa asilimia mia moja, si suala la askari kujisomesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la chakula. Mimi natembelea sana Magereza lakini najua wanakula vizuri, ingawa si vizuri sana. Hivi kwa nini tusiboreshe mlo? Chakula na adhabu aliyopewa mfungwa hiviendi pamoja. Chukula ni suala lingine na adhabu ni suala lingine. Ninaomba tuboreshe suala la chakula, ninafahamu kabisa Serikali hutenga bajeti ya chakula kwa *ratio* maalum. Kila kichwa cha mfungwa kina chakula chake, kwa hiyo, naomba kile kiwango kilichokisiwa, kitekelezwe hivyo hivyo ili hawa wenzetu waweze kupata mlo mzuri, kwa sababu inawezekana wapo pale kwa bahati mbaya ama wengine wamefika pale kwa sababu ya kutokujua sheria, hata yule mwenye hatia naye chakula ni haki yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemaliza suala la chakula, niingie suala la sare za askari. Askari wetu kwa kweli wana tatizo la *uniform*. Askari unakuta ana kauka nikuvae, anavaa mchana usiku anafua, matokeo yake siku mbili imeshapauka. Tunapoteza hadhi ya askari, ninaomba sana wapewe seti za kutosha. Aidha, *pair* mbili, tatu, angalau moja ikichafuka, anamwachia mama mtoto anafua anavaa nyingine. Nini hakika ukiwa na *pair* nyingi, hata upaukaji na uchakaaji wa haraka haraka hautakuwepo. Ninaomba tuwape heshima ya uaskari, wakivaa vizuri wakiwa nadhifu, heshima yao inakuwepo na kazi yao wataifanya kwa moyo mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la Zahanati ya Gereza la Singida. Zahanati hiyo toka nilipoanza kuiona ni miaka karibu kumi na tano hadi ishirini, mpaka leo ipo hivyo hivyo, yaani ni gofu tu. Ninaomba katika Bajeti hii, Mheshimiwa Waziri aniambie katenga shilingi ngapi kukarabati zahanati hiyo, angalau hata hao madaktari wanaotibu pale, wapate heshima wathaminiwe. Naomba nijue ni shilingi ngapi imetengwa katika zahanati hiyo, angalau iweze kukarabatiwa ilete hadhi na si

kukarabati tu na kupelekewa dawa. Dawa mnazopeleka ni chache. Wafungwa wengi wanapelekwa Hospitali ya Mkoa na Hospitali hii ina msongamano wa wagonjwa, unapompeleka mfungwa ujue atakaa hapo kutwa nzima, kazi ni hospitali tu. Kwa hiyo, ninaomba waongeze idadi ya dawa ili watu hawa waweze kupata huduma zao kwa asilimia mia moja katika zahanati zao hizo hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la *passport* . Ukitaka kupata *passport* kutoka Singida mpaka Dar es Salaam, utamkuta Afisa wa Uhamiaji, utaandikisha na kulipia atakuambia subiri mpaka akusanye watu kumi hadi kumi na tano, ndipo wasafiri kwenda Dar es Salaam kufuatilia hizi *passport*. Mpaka upate ni miezi mitatu. Ninaomba sana, *passport* zina umuhimu wake. Watu siku hizi wanafanya biashara zao, wanasoma na wana safari za kikazi, sasa unapomnyima *passport* na kumcheleweshа, unamnyima haki yake. Watu wana nia njema, wanapenda kujiendeleza lakini utakuta wanakwamishwa na kitu kidogo tu cha *passport*. Ninaomba sana suala la *passport* lihamie Mikoani kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la Askari Magereza kujiandaa kimaisha. Askari hawa kama tutawaacha walivyo, nina hakika watastaafu hata vibanda vya kuishi hawatakuwa navyo. Sasa hivi benki zetu zinakopesha lakini askari magereza hawana nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Asante, unakuwa kama na wewe ulishawahi kufanya hiyo kazi. Sasa nitamwita Mheshimiwa Abadallah S. Sumry.

**MHE. ABDALLAH S. SUMRY:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwako, kwa kunipa nafasi hii ya kuwa mchangiaji wa pili, kwa jioni ya leo juu ya Wizara yetu ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu, Maafisa wote wa ngazi zote, upande wa Uhamiaji, pamoja na Magereza, kwa kazi nzuri wanayoifanya ndani ya Wizara hii katika kila eneo la nchi yetu, tangu mipakani hadi katika Magereza yetu yaliyopo ndani ya Jamhuri yetu ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, napenda kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Mpanda Magharibi, kwa kuniwezesha kufika katika eneo hili na leo hii namshukuru Mwenyezi Mungu, kuweza kuongelea suala la shamba letu la Magereza kule Kalila Nkulukulu ndani ya Jimbo la Mpanda Magharibi. Tangu Septemba, 2004, nilipofanya ziara katika maeneo ya vijiji vyetu vya Gereza la Kalila Nkulukulu kule Ikaka, Ilebula, Sijonga, Kawanzige, Mbogwe, Wazo Jema, Kamakuka, Kakese na Usengule. Vitongoji vyote hivyo vilikuwa na tatizo la shamba letu la Magereza kule Mpanda Magharibi, eneo la Kalila Nkulukulu. Binafsi shauri hili nililifikisha kwa Viongozi wa Magereza, hawa wananchi wameishi eneo hili zaidi ya miaka 25, wakitumia eneo hilo kwa kulilima. Wakati huo ndugu yangu, Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati, alikuwa Waziri na

nilimwandikia barua, lakini mpaka leo hii hakuna jawabu lolote lililoweza kupatikana juu ya ufumbuzi wa tatizo hili la ardhi kwa wananchi wetu huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipoanza kufuatilia shauri hili, ndiyo ilikuwa mwanzo wa Afisa wa Magereza kuandika barua kupeleka kwa Afisa Ardhi wa Wilaya. Tatizo hili nililifuatilia mwezi wa Septemba na mwezi Januari, Afisa Magereza aliweza kuandika barua kwa Afisa Maendeleo ya Ardhi kule Wilaya ya Mpanda, kuomba shamba hili liweze kupimwa na akiomba aweze kupewa hekta 10,000 sawa sawa na eka 25,000. Sasa suala lililopo hapa mbele ya Mheshimiwa Waziri, sijui uhalali wa ardhi hii unaanzia wapi? Unaanzia wakati ameanza sasa kuiomba Idara ya Ardhi, waweze kupima au ni lile Tangazo la Serikali lililotumika kipindi hicho cha nyuma kwamba, eneo hilo ni la kwao. Sasa uhalali unaanzia kwa *Official Gazzette* au uhalali unaanzia pale wanapoomba waweze kupimiwa.

Hili naliomba kwako Mheshimiwa Waziri, niweze kupata ufafanuzi ili wananchi wetu kule waweze kusikia Serikali inasema nini juu ya eneo hili. Wananchi ni wengi sana, eneo ni kubwa na muda wote Gereza letu la Mpanda halijatumia hata hekta 500 kwa kulima tangu lilipoanzishwa mwaka 1974. Sasa ardhi yote hii yenye ukubwa wa eka 25,000, utakuwa na manufaa gani kwa kuizuia tu maeneo hayo na hawa wananchi ambao wanajiajiri, wanapunguza umaskini, wanahitaji kutumia ardhi hiyo na hawawezi kutumia kwa uhuru wa maeneo hayo. Hawa watu wameweza kuwa katika maeneo hayo kama nilivyoeleza miaka 30 iliyopita. Lakini sasa wanaishi kwa mashaka, hawana maeneo mazuri ya kilimo, kwani eneo pekee kwa vitongoji na vijiji kwa kilimo cha biashara na chakula ni eneo hilo tu. Ni eneo la ajira kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Wizara iweze kuona taratibu maalum kwamba eneo hili kwa sasa lipimwe upya, kwa kadri ya mahitaji ya gereza, wakihusishwa viongozi husika wa maeneo yale ili ardhi iweze kutumika kwa manufaa ya wote; kwa manufaa ya gereza letu na kwa manufaa ya wananchi niliowataja wa vitongoji vinavyozunguka eneo hili. Shauri hili lina umuhimu sana kisiasa na sasa imekuwa kero na hoja. Naomba Mheshimiwa Waziri sasa aje aone mwenyewe hali ilivyo na uamuzi utolewe ili furaha, amani na utulivu viboreshwe kati ya wananchi na gereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuwapongeza askari wetu wa fani zote, walio katika Wizara hii. Nawapongeza Askari Magereza kwa kazi nzuri wanayoifanya katika maeneo yetu, hawa ndiyo wanatupa amani na utulivu kwa kuzuia wahalifu waliohukumiwa na sisi tukaishi kwa amani, wakati huo huo kuwajengea tabia bora, tabia njema na mafunzo yaliyo na uadilifu ili baadae wawe raia wema ndani ya jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Wizara iwatazame Askari wetu wa Magereza, naona kila Mbunge amezungumzia hili. Lakini kila sehemu, kuna maumivu hayo na tulipotembelea Magereza yetu, ndugu zetu hawa walikuwa wakilalamikia vitu mbalimbali. Walilalamikia sare, usafiri na kadhalika. Watazamwe kwa jicho la huruma na Serikali sasa ipange mkakati rasmi ili kuweza kuwawezesha usafiri walau wa pikipiki na gari maalum kutoka maeneo yao. Maana hapo walipo, wanaishi mbali zaidi na Hospitali ya Wilaya na inabidi huduma zote wakapate huko, licha ya zahanati ndogo na

dawa cheche walizonazo hapo kwenye Kambi yetu ya Kalila Nkulukulu na wakati huo huo wanahudumia wananchi wa vijiji jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Gereza la Kalila Nkulukulu, lipo kilomita kumi na moja kutoka mjini na sasa umeme umekwishafika kilomita tano kutoka Mjini kuja Misasa. Ninaiomba Wizara kwa makusudi, ipange mikakati kwa sababu gereza hili ni la kilimo ili waweze kufikishiwa umeme katika uneo hili. Muda mrefu sasa wamekuwa tukiomba hili, tangu gereza lilipoanzishwa na ni matumaini yangu sasa Mheshimiwa Waziri kupitia kwako, aweze kutuweka katika chati hiyo na watazame ni jinsi gani tutapata umeme kwa ajili ya askari wetu pale na kijiji jirani cha Kabungu, ambapo pana sekondari.

Vilevile askari wetu wana upungufu wa wafungwa, tuna wafungwa kama hamsini tu katika gereza zima, eneo kubwa la ardhi, watu wanasongamana katika maeneo mengine ya nchi, gereza hili tumeliita gereza la kilimo, lakini hakuna eneo la kilimo linaloonekana linalimwa. Kwa hali hii, haya malilalamiko ya msongamano mkubwa yaliyopo katika magereza mengine, hebu Mheshimiwa Waziri kupitia kwako, tuweze kutazama sura mpya na kulifanya lile gereza lipate uhai mtimilifu kwa kazi zake na lengo lililokusudiwa la kilimo katika gereza hilo. Utaratibu wa zamani wa magereza wa kuhamisha wafungwa toka gereza la wafungwa wengi hadi gereza lenye upungufu.

Mheshimiwa Naibu Spika ninaenda kwa upande wa uhamiaji, nawapongeza sana Maafisa Uhamiaji katika eneo letu, naipongeza Idara ya Uhamiaji katika maeneo yote ya nchi, wanafanya kazi vizuri sana na wanastahili kupewa pongezi. Kuhusu ofisi yetu ya Wilaya kule Mpanda kuna upungufu wa *radio call*, tuna upungufu wa kompyuta kwa ajili ya kumbukumbu mbalimbali, mafuta ya kutosha hatuna, fungu la *OCS* kwa ajili ya Wilaya, tunaomba Wilaya yetu ipewe *OCS*. Ukubwa wa Wilaya ni sawa na ukubwa wa Mkoa wa Kilimanjaro na Tanga. Vilevile fungu kwa ajili ya kulipia gharama mbalimbali, hatma ya wakimbizi wetu waliopo katika maeneo yetu ya Kambi ya Mishamo na Kambi ya Katumba. Sasa hivi wakimbizi wale wameshakuwa wenyeji kwa kiwango cha juu, miaka zaidi ya 35 inasogea 40, ninaomba Serikali itoe tamko rasmi juu ya wale watu, maana mpaka sasa hawajawekwa katika fungu la kuomba uraia na mpaka sasa hawajui haima yao siku zijazo itakuwa nini. Kwa hiyo, Serikali ifanye kila inachoweza ili waweze kuwa katika fungu maalumu ni wapi wataweza kuwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna msemo kwetu unaosema kwamba, chai ikipoa haimwagwi, inachemshwa ndipo inywewe. Kwa hiyo hoja yangu kubwa kutoka Mpanda Magharibi ni kumwomba Mheshimiwa Waziri, juu ya eneo la ardhi kubwa ya Kalila Nkulunkulu, kwa ajili ya maeneo ya wanavijiji wangu niliowataja hapo juu, niweze kupata ufumbuzi wa tatizo hili waweze kuendelea na kilimo. Baada ya kusema hayo, binafsi naiunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. RAYNARD A. MROPE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili kwa upande wa Wabunge, niweze kuhitimisha jioni ya leo kuzumgumzia juu ya Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Kwanza kabisa, naomba

nitoe pongezi zangu za dhati za moyo kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na wafanyakazi katika Wizara hii ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, si kawaida yangu kuzungumza katika Wizara hii, lakini leo nimevutwa kwa sababu maalumu, ambayo ndiyo nataka kuielezea sasa hivi. Wizara ya Mambo ya Ndani, kwa bahati mbaya imetekeleza vibaya, mgogoro uliopo baina ya Gereza la Namajani, pamoja na Wananchi wa Kata yetu ya Namajani. Mgogoro huu ni wa siku nyingi, ulianza kwenye mwaka 1995, lakini uliiva zaidi mwaka 2004 wakati aliyekuwa *DC* wakati huo, alipowaruhusu magereza watanue mipaka yao na katika kutanua, wakaingia sana katika vijiji vya Wananchi wa Ngalole, hasa katika Kitongoji cha Natepo. Huyu *DC* alimwamuru Afisa Ardhi wa Wilaya kwamba, apime maeneo hayo na akapima, kwa hiyo kuanzia wakati huo, huu mgogoro ulikuwa umeiva kati ya wananchi na magereza.

Magereza walifyeka mpaka mpya, ambao walidhani kuwa ndiyo mpaka wao, wananchi ambao ndiyo waliwakaribisha hawa magereza, wakaona hii si halali. Kwa hiyo na wao siku moja wakafyeka mpaka wao, kuwaonesha magereza haki yake wakomee wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Magereza wakatumia mabavu, wakawavamia wananchi wale wakawapiga, wengine waliumia. Lakini na wananchi nao, sisemi ni jambo zuri, lakini waliweza kumpata Afisa Magereza mmoja na yeye wakamuumiza. Kwa hiyo, toka hapo ukosefu wa amani sehemu hii ukaanza. Jambo hili siku ile ile lilipelekwa polisi Masasi, wananchi 85 walikamatwa wakapelekwa Mahakamani Masasi, wakatozwa faini ya shilingi elfu tano tano kila mmoja. Zikalipwa shilingi laki nne na ishirini na tano. Baada ya hapo mpaka leo, mgogoro huu huwa unafukuta, unaendelea kiasi kwamba, hakuna lolote linalofanyika la maana katika kuuzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo mwaka 2006, Mkuu wa Mkoa wa wakati huo, alifanya utaratibu wa kuunda Tume. Baada ya kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani, waliunda Tume ikafanya utafiti wa kina na wa ndani, baadae wakatoa ripoti. Mojawapo ya pendekezo lililokuwemo katika ripoti ni kwamba, Magereza warudi katika mpaka wa zamani waliokuwa wamepewa na Serikali ya Kijiji. Kwa bahati mbaya, wakati huo ripoti hii inatolewa, aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani wa wakati ule, Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati, alikuwa amehamishwa kwenda katika Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Kwa bahati mbaya, toka ripoti hii iletwe katika Wizara ya Mambo ya Ndani mpaka hii leo, hakuna lililofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimejitahidi ndani ya Bunge hili, kulileta tatizo hili kwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi bila mafanikio. Labda Waheshimiwa Wabunge watadhani kwamba, inawezekana nilikuwa naongea naye humu humu ndani na nina vikaratasi vingi tu alivyonijibu. Kwa mfano, mwezi Februari aliniambia nakuomba unipe muda niwe *updated* kuhusu jambo la Gereza la Namajani, nitakupa maelezo ndani ya siku chache, yakaisha. Halafu nikauliza tena, asubuhi hii *RC* wa Mtwara amenipigia simu kuhusu mgogoro uliopo, ameniambia baadaye.

**NAIBU SPIKA:** Mbona hukuniomba ruhusa kwamba, unataka ku-*refer*?

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba samahani, nakuomba ruhusa rasmi.

**NAIBU SPIKA:** Endelea sasa. *(Kicheko)*

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya uchunguzi, taarifa imetumwa kwa Waziri wa Mambo ya Ndani. Ninaahidi nitaitisha, nisome kwanza ndipo tuongee, ikaja nyingine mwezi Aprili, naomba radhi kuwa mpaka sasa sijawahi kuwa na maelezo ya kukupatia. Nitafutatilia tena mchana huu ili nijue *status* ilivyo na ya mwisho hii aliniandikia kwamba, nakuomba radhi Mheshimiwa Mrope, mpaka asubuhi hii sijapata maelezo ya hali ilivyo kuhusu Gereza la Namajani, kwa hiyo, sina maelezo ya ziada, nadhani mmoja wetu afike huko, ikiwezekana ili kuelewa zaidi. Tutajitahidi kufanya hivyo. Sasa hayo ndiyo majibu niliyokuwa nayapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kule inazidi kuwa mbaya, wananchi wameshindwa kulima, karibu kaya 720 hazina mashamba kwa sababu maeneo yao yamechukuliwa na Magereza. Mimi najiuliza, hivi ukifikia hali hiyo kwa Mtendaji Mkuu, sasa niende wapi? Hali kwa kweli ni mbaya, wananchi wamekata tamaa na upande wa Serikali hautoi majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana nimesema kwamba, leo nimeleta jambo hili hapa Bungeni kwa sababu wajibu mmojawapo wa Bunge ni kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali. Je, ndio tunasimamia hivi? Hii ndio ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya? Mimi naona si hivyo, ndio maana naomba sana jambo hili leo lifikie mwisho wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba kupendekeza kwamba, Ripoti ya Tume ya Meja Jenerali Roland Makunda iheshimiwe ili mzozo huu tufikie mwisho wake.

Pili, Wizara ya Mambo ya Ndani kama inahitaji msukumo, sijui nani wa kusukuma, lakini isukumwe ili tuweze kufikia mwisho wa suala hili. Wananchi wanasubiri kwa hamu sana.

Tatu, suala hili liwe limekamilika kabla ya mwezi Oktoba wakati wa msimu wa kilimo kinapoanza, ili wananchi wapate mashamba ya kulima.

Kusema kweli mimi kwa uchungu kabisa, nilikuwa nalileta jambo hili kwa uamuzi wa mwisho. Naomba sana Serikali wanielewe, wala sina nia mbaya, nia yangu ni kwamba, Wizara iamue na hasa iamue kurudi katika mipaka ya zamani, iliyowekwa baina ya magereza na Kijiji cha Namajani. Wakitaka nyongeza basi waombe toka Serikali ya Kijiji sio kutumia nguvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa Magereza walipewa hiyo ardhi na wananchi bure kabisa kwa kukaribishwa kwa ajili ya maendeleo. Huu ndio mfano halisi wa Mwarabu

na Ngamia, baada ya kukaribishwa pale, sasa wamejitanua sana kiasi kwamba, yule Mwarabu (mwananchi) sasa ametupwa nje, hana ardhi.

Sasa hii hatuwezi kukubali na ndio maana katika suala hili nilisema leo nitakuwa *specific* kwa lengo la kupata ufumbuzi na ikibidi Bunge sasa lisimamie jambo hili ili tuweze kufikia mwisho. Haitusaidii kubishana bishana kila siku, tufikie mwisho. Naomba sana Wizara hii ifanye hivyo na kama isipofanya hivyo, basi wananchi tutaendelea kuchukua hatua zaidi. Wananchi pale hawapo tayari kunyang'anywa ardhi yao hivi hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda huu nilikuwa na hayo, nadhani nimeeleweka, kama sijaeleweka basi, nitaeleza zaidi kwenye vifungu, lakini kama nimeeleweka sasa, bila shaka Waziri atanijibu ili nisiweze kwenda kwenye vifungu.

Pamoja na hayo, naunga mkono hoja, bila shaka mmeelewa sauti yangu kwamba siridhiki sana na yale yanayotokea. Kwa hiyo, naomba maelezo mazuri. Asante sana. *(Kicheko)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia tatizo la wahamiaji haramu Wilayani Karagwe. Wilaya ya Karagwe kwa muda mrefu, imevamiwa na wahamiaji haramu kutoka nchi jirani za Rwanda, Burundi na Uganda. Wimbi hili la wahamiaji haramu limekuwa ni kero kwa wakazi wa Wilaya ya Karagwe, kwani wahamiaji hawa huja na makundi makubwa ya mifugo na hivyo kusababisha upungufu wa ardhi Wilayani Karagwe na wengi wao wamekuwa wakijihusisha na vitendo vya ujambazi. Pamoja na juhudi nzuri za Serikali za kuwarudisha, bado wengi wapo na walioondoka baadhi wanarudi kwa kasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Karagwe imeshindwa kumaliza tatizo hili. Wakati mwingine tatizo la rushwa kwa watendaji limekwamisha juhudi nzuri za Serikali. Naiomba Wizara ipange Mkakati wa Kudumu wa kutatua tatizo hili *once and for all*. Pia watendaji waliokaa muda mrefu Karagwe wahamishwe na watendaji waache tabia ya kutumia nafasi zao kuwaonea raia wa Tanzania, kwa kuwatishia kuwaondoa nchini wanapowanyima chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maafisa Uhamiaji wapelekwe maeneo ya vijijini au kwenye kata, kwa kuanzia hasa katika maeneo ya mipakani kama Karagwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali itueleze imejipanga vipi kumaliza wahamiaji haramu wote Wilayani Karagwe?

**MHE. CELINA O. KOMBANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, kwa hotuba yenu nzuri, ambayo iko wazi na isiyoleta maswali mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maelezo ya Wizara 2007/2008, ukurasa 48 kipengele (j), kinasema wazi kwamba, mtanunua matrekta manne kwa mwaka 2007/2008. Mwaka jana nilichangia kwa maandishi, kuomba Wizara iwapatie Gereza la Kiberege ambalo ni la kilimo, trekta moja ili kuongeza ufanisi katika kilimo cha miwa na mpunga, ambacho kina soko kubwa kwa sasa. Naomba kwa kuwa mwaka jana hawakupata, wapatiwe mwaka huu 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, Gereza la Ulanga lilijengwa enzi za kikoloni na linajulikana kama Boma la Mahenge. Boma hilo limeunganisha ofisi zote, yaani Magereza, Polisi, *DC, DED* na Mahakama ya Wilaya. Kwa miaka ya hivi karibuni Ofisi ya *DC* na *DED* zimekarabatiwa. Kwa kuwa boma hilo limeunganisha ofisi zote, Ofisi ya Magereza pamoja na gereza la wafungwa limebaki kama gofu katikati ya ofisi zilizokarabatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba msaada wa Waziri wa kuweka gereza hilo katika mipango ya ukarabati ili lisitofautiane na ofisi za wilaya zilizokarabatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema mambo hayo mawili naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri na ninaiunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hotuba nzuri ya Waziri, naomba ufafanuzi wa mambo yafuatayo: Wizara ina mpango gani wa kuhamisha Gereza la Lushoto kutoka mjini lijengwe zuri na kubwa la Yoghoi?

Wilaya ya Lushoto haina huduma ya Zimamoto; je, Wizara ina mpango gani wa kufikisha huduma hii muhimu Wilayani Lushoto?

Matumizi ya nguvu kazi wafungwa; je, tukitaka kuwatumia wafungwa katika miradi ya ujenzi wa shule, zahanati na barabara vijijini utaratibu ukoje?

Mheshimiwa Naibu Spika, asante. Naunga mkono hoja.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Mheshimiwa Joseph J. Mungai, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Lawrence K. Masha, wakisaidiana na Katibu Mkuu, Ndugu S.Odunga na Wataalamu wao wote, kwa jitihada za kuendelea kuboresha kazi za Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Kabla ya kuchangia hoja hii ya Idara ya Magereza, napenda kumpongeza Ndugu Augustin N. Nanyoro, kwa kueuliwa kuwa Mkuu wa Magereza nchini. Ninamwomba aje atembelee Mkoa wa Rukwa, aone

jinsi tunavyotumia zana chache walizotupatia kwa ajili ya kilimo huko Gereza la Mollo na kuendeleza kuomba msaada wa zana zaidi, kama *tractors* na magari.

Pili, aje aone tatizo la gereza la mahabusu lililopo Mjini Sumbawanga, ambalo lilijengwa miaka ya ukoloni. Mimi nimelitembeleza gereza hilo mara nyingi na kilio chetu ni kujenga gereza lingine. Kwa ufupi, Wizara inasema nini kuhusu maombi haya ya siku nyingi humu Bungeni, bila kusahau makazi ya askari katika mkoa huu kwa ujumla?

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mpango mkubwa wa mamlaka ya bandari nchini *(TPA)*, mwaka huu wa kuendeleza Bandari ya Kasanga iliyoko ziwa Tanganyika, je, kwa msingi huo Wizara inajiandaa vipi ili kuimarisha Ofisi ya Uhamiaji hapo Kasanga, ambapo patakuwa mlango mkuu wa kuingia wageni toka *DRC,* Burundi na Zambia?

Pamoja na hilo; je, mpango wa kudumu wa kudhibiti wageni na wakimbizi Mkoani Rukwa hadi sasa umezaa matunda gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla, kutupatia fedha kwa gari la zimamoto. Lakini tatizo bado ni la mafunzo kwa ajili ya utaalamu wa kuhudumia magari hayo, kuna haja kila mara mafunzo maalumu kwa vikosi hivi kuwa na mipango ya kudumu juu ya taaluma hii na hasa ya namna ya kuokoa watu na jinsi ya kuelimisha pia watu juu ya majanga ya moto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya usindikaji wa mazao ya chakula kama mahindi na alizeti kwa ajili ya mafuta na unga wa kusafirisha kwenye masoko ya nje na ndani. Je, isingekuwa vizuri wazalisahaji katika mashamba ya magereza wakapewa mtaji mzuri wa kutekeleza hayo ili kujipatia faida kubwa na hivyo kuyafanya magereza yetu yaweze kujiendesha bila ruzuku kubwa toka Serikalini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri kuanza ujenzi wa magereza kwa ajili ya *core criminals* peke yao na wawekewe ulinzi mkali ili wasichanganywe na wafungwa wenye makosa makubwa. Kwa wasiwasi wa maingiliano hayo husababisha hata wafungwa wenye tabia nzuri kuambukizwa tabia mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii ya Waziri kwa kila jema walilolitekeleza vizuri. Nawatakia kheri na fanaka katika kazi zote ingawa bado mlundikano wa wafungwa unaendelea licha ya marekebisho tuliyoyafanya ya *Community Service Act No 6 of 2002.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sijui tatizo liko wapi katika sheria hiyo, maana bado mafanikio yake yapo kidogo sana? Naomba Wizara ilifuatilie ili ishauri Serikali na Bunge kwenye maeneo husika ya kufanyia marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii, kwa njia ya maaandishi kuwapongeza Mheshimiwa Joseph J. Mungai, Mheshimiwa Dr. Lawrence K. Masha, Katibu Mkuu na Watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri, yenye mwelekeo wa kutoa huduma bora kwa walengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutamka rasmi kuwa, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia, nikitegemea kuwa, mambo yote nitakayochangia nitapewa ufafanuzi na Waziri auNaibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika,sasa napenda nianze kuchangia hoja zangu kama ifuatavyo: Ni ukweli usiofichika kuwa, mishahara ya askari wa jeshi la magereza ni midogo sana, kulingana na uzito kazi zao, pamoja na hali ngumu ya maisha tuliyonayo. Hali hii inawapa askari wetu kupata vishawishi vya kupokea rushwa kwa lengo la kulegeza sheria za wafungwa au mahabusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile hata maslahi wanayopata ni duni sana, licha ya kuwa duni hata kupata pale wanapotakiwa kupewa ni shida na wanaendelea kukopwa tu, huku wakiendelea kupambana na ukata mkubwa wa maisha. Naomba Serikali itueleze kwa nini bado wanaikopesha Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimechangia mara nyingi sana hapa Bungeni juu ya nyumba za askari, ambazo hata kuita nyumba ni kosa bora niseme vijumba, kwani ni ndogo sana na Wabunge wengi wamesema hoja hii mara nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Serikali inatambua kabisa askari wanazo haki zote za binadamu kuwa wanaruhusiwa kuoa ama kuolewa kisha kupata watoto. Kinachoshangaza ni pale wanapoendelea kuishi kwenye vijumba ambavyo ni vidogo sana, vyenye chumba na sebule. Ili askari hawa waweze kuwalea watoto wao wenye jinsia tofauti ni bora wajengewe nyumba zinazokidhi haja ya familia. Naiomba Serikali itoe ufafanuzi ni lini askari hawa watajengewa nyumba ili tabia ya kulala bila kuzingatia maadili iondoke?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza Serikali kwani mara nyingi husifia utendaji kazi wa askari wa jeshi hili la magereza, tatizo ni kwamba, askari hawa pamoja na juhudi zao, wanakaa bila cheo kwa miaka mingi, hatimaye wengine hustaafu bila cheo. Naiomba sana Serikali iweke utaratibu mzuri wa kuwapandisha askari vyeo ili kuwatia moyo askari wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Serikali kwa kuweka zahanati kila gereza ili kutoa huduma kwa wafungwa, mahabusu na familia za askari kwa ujumla. Naiomba Serikali iongeze mgao wa dawa na vifaa kwenye zahanati hizi ili wafungwa na askari wasihangaike kwenda hospitali zenye raia wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa zaidi ni jengo la zahanati ya Gereza la Singida ni la kizamani na limechoka. Napenda kujua ni lini zahanati hii itajengwa upya

au kukarabatiwa ili liwe na hadhi, uimara na kuwapa matumaini watumiaji. Nategemea Waziri atanipa maelezo ya kuridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sifa ya kwanza ya askari ni mavazi (sare), lakini askari wetu wengine mavazi yao yamechakaa sana. Naiomba Serikali itoe sare za kutosha ili zisichakae upesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kuwa Serikali inawajali wafungwa kutokana na haki za binadamu na imeweka utaratibu kila mfungwa anatakiwa kula shilingi ngapi kwa siku au mlo mmoja. Ni bora utaratibu uliowekwa na Serikali utekelezwe kwa maana ya kutenga fedha inayokidhi haja ya mlo anaotakiwa mfungwa apate, kuna wafungwa wanaofungwa na afya nzuri lakini wakitoka wamedhoofu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana Wakuu wa Magereza nchini kwani wamekuwa wakiwafundisha wafungwa taaluma mbalimbali za uzalishaji mali ili wanapotoka waweze kumudu maisha endapo alikuwa mwizi. Naishauri Serikali kutoa mafungu ya kutosha kuimarisha fani mbalimbali za ufundi kama useremala, ufundi washi, ususi, ushonaji na kadhalika. Hii ni muhimu sana kwani wafungwa warudipo uraiani, watakuwa raia wema, wenye uwezo wa kutafuta pato la familia.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza sana askari wetu kwani wanajituma sana katika utendaji wao wa kazi. Napenda waziri anieleze, tunao askari wangapi, walikuwa wanatakiwa wangapi na wamepungua wangapi? Vilevile nielezwe kwa nini tusizalishe askari wa kutosha na vyuo tunavyo? Askari waliopo wanafanya kazi ngumu sana kwa vile wapo wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali isomeshe askari wa kitengo cha zimamoto wa kutosha, kwani matukio ya moto sasa ni mengi na vilevile vifaa vya zimamoto viwepo hasa kwenye miji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuikumbusha Serikali kuwa, upatikanaji wa *passport* bado ni mgumu sana. Naiomba sana Serikali ipeleke huduma hii mikoani kwa asilimia.

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Gereza la Biharamulo limechakaa, mabati yameoza na linavuja sana. Kuna msongamano mkubwa kwa sababu ya ufinyu wa gereza. Vilevile Gereza la Wilaya ya Biharamulo halina gari kubwa na Mkoa wa Kagera wenye Wilaya nane una lori moja chakavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafungwa wanakata miti ya Mji wa Biharamulo na kuharibu mazingira. Mradi wa gesi haujaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, watumishi wa gereza hawana nyumba, mishahara na maslahi havitoshi.

Wazabuni wanaohudumia Magereza ya Mkoa wa Kagera hawalipwi pesa zao wakati unaofaa na wengine wamefunguliwa mashtaka mahakamani.

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kwa maandishi Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, bajeti ya 2007/2008. Nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wao, kwa kazi yao nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kikosi cha zimamoto na uokoaji kiboreshwe ili kiongezewe utaalamu zaidi wa kiutendaji na kupewa mawasiliano. Pia kiongezewe magari ya zimamoto na kuwekewa vituo maalumu vya kuchukulia maji, badala ya magari kufika maeneo ya matukio yakiwa matupu na mengine yakifika yakimaliza maji hayana sehemu ya kuongeza, hii kusababisha matukio ya moto kuathiri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuiomba Serikali kuangalia tatizo la msongamano wa mahabusu katika Magereza ni kweli vyumba ni vidogo hasa upande wa wafungwa wanaume, hasa Keko Dar es Salaam na Magereza mengine.

Mapendekezo yangu, ni vizuri sasa wananchi ambao wanapata kesi ndogondogo mfano, uzururaji, hawa wasafishe mazingira ya eneo la mji au walipe faini na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa uhamiaji haramu. Hivi karibuni kumekuwa na taarifa za wahamiaji hao, ningependa kupata ufafanuzi hivi sasa hali iko vipi ya udhibiti huo na wale wa Wasomali na Wahabeshi, ambao walikamatwa sehemu mbalimbali za nchi ikiwemo Mkoa wa Mbeya wako wapi; wamechukuliwa hatua gani na kama wamepewa amri ya kurudi kwao; je, Serikali ilihusika katika gharama za kuwarudisha?

**MHE. ZAINAB M. VULLU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, kwa hotuba nzuri na kuwapongeza Watendaji wote wa Wizara hiyo, kwa ushirikiano wao katika kutekeleza majukumu yao.

Baada ya maelezo hayo, naomba nichukue fursa hii kuchangia katika mambo yafuatayo ambayo ningependa nipatiwe ufafanuzi:-

Pamoja na uhaba wa majengo ya magereza nchini, bado kuna tatizo la usafiri wa kubeba mahabusu kutoka magereza kwenda mahakamani na kurudi. Kama hilo halitoshi, bado magari hayo ni mabovu au yamechakaa na kubeba idadi kubwa bila ya kujali au kufuata Sheria za Usalama Barabarani. Je lini tatizo hili litapatiwa ufumbuzi na kuacha kuvunja Sheria za Usalama Barabarani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Magereza lina kazi kubwa sana ya kusaidia kurekebisha na kuwaelimisha wafungwa, hivyo basi, ili waweze kufanya kazi yao kwa ufanisi ni vyema wawe wanalipwa posho ya kutosha na mshahara ambao hautawafanya washawishike kuchukua rushwa. Mfano mzuri ni wakati wa mgomo wa wafungwa; iweje wawe wamepata hata wasaa na vifaa ambavyo walivitumia katika kuandika mabango?

Je, naweza kupewa ufafanuzi, Askari Magereza walikuwa wapi na hatua zipi zilichukuliwa kwao? Naomba nipatiwe ufafanuzi.

Ninapenda kujua lini Gereza la Kigongoni lililopo Bagamoyo litawezeshwa kwa kupewa dhana za kilimo za kisasa ambapo wataweza kulima na kulisha nchi nzima?

**MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na ushirikiano mzuri kati ya Wizara za Kilimo, Chakula na Ushirika na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kupitia Jeshi la Magereza, kwa mfano, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Gereza la Kibondo, kuzalisha vipando hususan vile vya mihogo yenye ukinzani na ugonjwa wa batobato. Naupongeza ushirikiano huu.

Vituo vya kukodisha zana za kilimo. Kwa kuwa magereza ina wataalamu wa kilimo lakini ina upungufu wa zana za kilimo, nashauri magereza yenye mashamba makubwa yapewe matrekta, yaanzishe huduma ya kukodisha kwa wakulima, pamoja na kulima mashamba yao. Utaratibu huu utawasaidia magereza kuongeza uzalishaji wa chakula kwa ajili ya wafungwa hasa ikizingatiwa kwamba, magereza haiwezi kuwa na uhakika wa *population* ya wafungwa kwa sababu wanaingia na kutoka.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara na Maafisa, kwa juhudi zao wanazoendelea kuzifanya katika kuboresha, kuimarisha na kusimamia shughuli za Wizara.

Wananchi wa Wilaya Mpya ya Rorya, wameridhika kwa asilimia kubwa na utendaji kazi wa viongozi wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, naomba kutoa maoni, ushauri na maombi, kwa niaba ya Wananchi wa Wilaya ya Rorya kama ifuatavyo:-

Wilaya Mpya ya Rorya Kaskazini, inapakana na Jamhuri ya Kenya na hakuna kituo cha uhamiaji, kituo kilichopo ni Namagongo, ambacho kipo kilomita 17 kutoka Kijiji cha Kirongwe kilichopo mpakani. Katika hotuba ya bajeti ya Wizara hii ya mwaka 2006/2007, nilitumwa na wananchi kuomba kituo hiki kihamishiwe Kijiji cha Kirongwe maandalizi yamekamilika.

Idara ya Uhamiaji imekwisha pimiwa viwanja kwa ajili ya ujenzi wa ofisi na nyumba za maafisa na familia zao. Bajeti kuhusu ujenzi wa kituo hicho iliandaliwa na Wizara kama ilivyopendekezwa na Mkoa wa Mara. Naomba fedha zilizotengwa 2006/2007 na 2007/2008, zitumike kujenga Kituo cha Uhamiaji cha Kirongwe Wilayani Rorya.

Wilaya Mpya ya Rorya imepatiwa gari na boti kwa ajili ya doria. Kwa kipindi cha wiki tatu, ng’ombe 376 waliibiwa na kupelekwa nchi jirani. Endapo Kituo cha Kirongwe kingejengwa, udhibiti wa wahalifu kutoka nchi jirani ungeimarika.

Wilaya ya Rorya inapakana na Kenya na Uganda katika eneo la Ziwa Victoria. Wafugaji wa Wilaya ya Rorya, wanavamiwa mara kwa mara na wavuvi kutoka nchi jirani. Wananchi wanaomba Ofisi ya Uhamiaji ijengwe katika Bandari ya *SOTA* Shirati ili kudhibiti wahamiaji haramu wanaoingia nchini kupitia Bandari ya *SOTA*. Boti ya doria inunuliwe ili Maafisa wa Uhamiaji waweze kudhibiti wavamizi wanaowatesa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Awali ya yote, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri aliyoiandaa na kuiwasilisha hapa Bungeni. Naomba kuchangia machache kuhusu hoja hii.

Naomba kuipongeza Idara ya Magereza, kwa juhudi wanayoifanya katika kuiwezesha idara kujitegemea. Uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara unaoendelea katika maeneo mengi ni mfano wa kuigwa. Naomba kuishauri Serikali kuelekeza fedha za kutosha ili waweze kuzalisha kwa wingi na ubora zaidi. Hii ni pamoja na Gereza la Tukuyu, wanaolima Zao la Chai na Gereza la Songwe, ambao ni maarufu kwa kilimo cha mahindi.

Naipongeza pia Serikali kwa kuanza kufikiria matumizi ya nishati mbadala. Nashauri Serikali katika Mikoa na Wilaya, washauriwe kutenga maeneo makubwa zaidi kwa Magereza mbalimbali ili waweze kupanda miti katika maeneo ya wazi.

Nashauri pia Magereza kuanza kutumia matofali ya mkaa *(brickets)*, yatokanayo na makaa ya mawe, pumba za mpunga au mbao za kuranda. Juhudi hii itatusaidia sana kuhifadhi mazingira ambayo yanaharibiwa sana na matumizi makubwa ya kuni katika magereza hapa nchini. Vilevile naishauri Serikali kuanza kuangalia tatizo la ufinyu wa ardhi kwa Magereza yaliyojengwa katikati ya maeneo ya miji. Ikumbukwe kwamba, Magereza mengi nchini yalijengwa kabla ya upanuzi wa miji. Ni wakati muafaka sasa Magereza yatafutiwe ardhi sasa nje kabisa ya miji ili kuruhusu upanuzi wa miji yetu hapa nchini. Hatua hii itasaidia Magereza kupata maeneo makubwa kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

Maeneo yaliyokuwa na wakimbizi. Kwa kuwa maeneo hayo yameharibiwa sana kimazingira na kwa kuwa wakimbizi wengi wanarudi makwao, Serikali ianze kuandaa programu kubwa shirikishi ya kupanda miti na kuitunza ili kurudisha maeneo haya katika hali ya asili. Utekelezaji huu ushirikishe pia Wizara ya TAMISEMI na Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naunga mkono hoja hii asilimia mia.

**MHE. MBARUKU K. MWANDORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kumpongeza kwa dhati, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Naibu Waziri, Katibu

Mkuu na Viongozi wengine wote wa Wizara na taasisi zake, kwa hotuba nzuri sana na kwa kazi nzuri za utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, kuhusu Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi maalumu ninazileta kuhusu jitihada kubwa ya kuhamasisha wakimbizi kurudi makwao. Athari za kuendelea kuwepo kwao nchini ni kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada za kupambana na wahamiaji haramu zinahitaji udhibiti na umakini maalumu, kwani wengi wa hawa wahamiaji haramu ndio wanaohusika na uhalifu ukiwemo ujambazi na uporaji wa ardhi na mali nyingine za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa Idara ya Uhamiaji kubadili mahali alipozaliwa mtu wakati wa kutoa pasi mpya za kusafiria, kwa mfano, mimi nilizaliwa katika Jiji la Tanga na pasi zangu zote za zamani zilionesha hivyo, lakini pasi mpya iliandikwa kwamba, mimi nimezaliwa Muheza eti tu kwa sababu Muheza ndiyo yaliyokuwa Makao Makuu ya Wilaya ya Muheza, baada ya Wilaya ya Tanga kugawanywa na sehemu ambayo haikuwa Manispaa kuwa Wilaya ya Muheza. Je, kwa mantiki hii nikiomba pasi mpya hivi sasa, itaonesha kwamba nimezaliwa Mkinga kwa sababu Mkinga ndiyo Makao Makuu ya Wilaya Mpya ya Mkinga?

Utaratibu huu si sahihi na ni kero ambayo inakera wananchi wengi. Utaratibu sahihi ni kuandika mahali halisi alipozaliwa mwenye pasi. Mimi nalazimika kusema uwongo, ninapojaza fomu za uhamiaji kutamka kwamba, nimezaliwa Muheza badala ya Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba, zoezi la kutoa vitambulisho vya utaifa *(National Identity Card)*, liharakishwe hasa kwa maeneo ya mpakani kama kule Wilaya ya Mkinga, ambako kuna utata mkubwa kuhusu uraia wa wakazi wengi huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na haja ya kupunguza mbanano katika Magereza, ninaomba tahadhari kubwa sana ichukuliwe katika kutoa misamaha. Mara nyingi baada ya wahalifu sugu kuachiwa, panakuwa na mlipuko mkubwa wa uhalifu pamoja na ujambazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna umuhimu mkubwa sana wa kuchukua hatua thabiti za kudhibiti ulawiti Magerezani, hasa kwa kuzingatia vita vya Taifa Dhidi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya Mpya ya Mkinga haina gereza. Kwa kuwa kadri maendeleo yanavyozidi kupatikana ndivyo uhalifu unavyokuwa mkubwa na hivyo hoja ya kuwepo gereza, naiomba Wizara ifikirie hilo katika mipango yake ya muda wa kati na mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na kuitakia utekelezaji mwema.

**MHE. PROF. FEETHAM F. BANYIKWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia Hotuba ya Waziri wa Mambo ya Ndani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa maamuzi mazuri ya kuwarudisha makwao wakimbizi kutoka Burundi, hasa wale waliokuwa katika Wilaya ya Ngara. Kambi ya Lukole B imefungwa na waliobaki kambini watakuwa wameondoka ifikapo Desemba, 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujio wa wakimbizi umeleta matatizo makubwa kwa Wilaya ya Ngara. Wakimbizi wengi walijihusisha na matendo ya ujambazi hasa wa kutumia silaha za moto. Watu wengi wameuawa katika Wilaya ya Ngara. Mazingira yameharibiwa kwa kukata miti ili wapate kuni za kupikia na kujengea majumba au kambi. Chakula kilipungua kwa wakazi wa Ngara kwa sababu wakimbizi walikuwa hawataki kula vyakula vya kambini, wanapenda vyakula vinavyolimwa katika Wilaya ya Ngara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha maombi kama nilivyotumwa na wapiga kura wa Wilaya ya Ngara: Wananchi wa Ngara wanaomba kupewa fidia kwa kuwalea wakimbizi ndani ya wilaya yao. Magari yote yaliyokuwa yanatumiwa na Ofisi za *UNHCR* yapewe Serikali ya Wilaya ya Ngara kama fidia kwa wakazi wa Wilaya ya Ngara. Vilevile malori na mabasi yakabidhiwe kwa Mkuu wa Wilaya ya Ngara ili yatumike katika kuleta maendeleo kwa Wilaya. Pia majumba yote yakabidhiwe kwa Mkuu wa Wilaya ili yatumike kwa maendeleo ya Wilaya. Wananchi wanaomba pia kuwepo na fidia kubwa ya vifaa vya hospitali kwa hospitali zote za Wilaya ya Ngara, hasa Murgwanza na Nyamiyaga.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maelezo kuhusu Wizara hii, itashirikiana vipi na Wizara ya Usalama wa Raia kwenye suala la kuwasajili wote wenye simu za mikononi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile Wizara iko kwenye mchakato wa vitambulisho ni bora *data* za watumiaji wa simu za mkononi ziainishwe na kuandikwa kwenye vitambulisho hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kasi ya Kamati ya *Parole* bado ni ndogo sana, bado haina *clarity* kwenye utendaji wake. Jela nyingi zimejaa na kuna wafungwa wengi ambao wangeweza kupewa adhabu za *community service* kwa lengo la kupunguza wafungwa kwenye Magereza. Naomba maelezo.

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wananchi wa Wilaya ya Hai, ninaomba mpokee pongezi za dhati, kwa kazi nzuri mnazofanya na mipango iliyoko mbele yenu, nikianzia kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji wengine wote Wizarani. Baada ya pongezi hizo, ninaomba nitoe maoni/ushauri katika maeneo machache yafuatayo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kuwatumia wafungwa kwa ajili ya shuguli za uzalishaji, kwa maana ya wao kujitosheleza na ziada kuuzwa kwa mashule na vyuo vyetu. Pia kulima mazao ya kibiashara hasa yale mapya, mfano, mbono kwa ajili ya *bio-diesel*. Watumike pia kwenye kazi nyingine za kijamii na kuendelea kupewa stadi za kazi mbalimbali ili kuwaandaa vema kwa maisha mazuri mara wamalizapo vifungo.

Ninaipongeza Wizara kwa kuanzisha miradi ya kuzalisha *gas* kwa ajili ya matumizi Magerezani, ninashauri Mradi huu uenee katika Magereza yote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri kuwa makini zaidi kuhusu wageni haramu, kwani tumeshuhudia matukio mbalimbali na wengine kuwa majambazi sugu. Kuna haja pia ya kuangalia utoaji wa vibali vya kuishi na kufanya kazi hapa nchini, ambapo imekuwa ni biashara kwa *mission town* pale Dar es Salaam. Kuna haja ya kuiangalia na kuimulika Idara ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitajika kuwa waangalifu sana, kwani hii itawaneemesha wageni zaidi na kutoa mwanya kwa wahalifu wa kimataifa. Kwa maoni yangu, ninashauri tusiingie kwenye utaratibu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nina swali; je, ni Wizara ipi yenye dhamana ya kusajili vyama vya kijamii, yaani *NGOs?*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Watendaji wote wa Wizara, pamoja na Taasisi zake, kwa kazi nzuri ya utayarishaji wa bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi, napenda kuchangia hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna utata juu umiliki kitengo hiki, baina ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na *TAMISEMI.* Utata huu unajitokeza katika upungufu wa usimamizi wa karibu wa shughuli na uendelezaji wa shughuli za kitengo. Ni vizuri Wizara ikatoa msimamo juu ya utata huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna manung'uniko miongoni mwa wafanyakazi wa Kitengo cha Zimamoto kuwa vyeo vinatolewa kwa wafanyakazi wanaume zaidi kuliko wanawake. Kuna mwanamke mmoja tu huko Tabora mwenye cheo cha *Assistant Superintendent.* Naishauri Wizara itafakari tatizo hili kwa madhumuni ya kulipatia ufumbuzi mwafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna manung'uniko ndani ya Idara ya Zimamoto kwamba, nafasi nyingi za mafunzo, pamoja na vitendea kazi, vinapelekwa Makao Makuu zaidi kuliko mikoani.

Pamoja na ukweli kwamba, mahitaji ya Makao Makuu ni makubwa zaidi kuliko sehemu nyingine za nchi, hata hivyo, kuna haja ya kusambaza nafasi za mafunzo, pamoja na vitendea kazi hata katika sehemu nyingine za nchi kulingana na mahitaji badala ya kuzisahau kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiunga mkono hoja hii kwa asilimia 100.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia uzima na kuweza kuchangia hutuba ya Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hutuba yake nzuri, inayoonesha ufanisi mkubwa wa kazi zinazofanywa na Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, pamoja na Watendaji, kwa kumsaidia vyema Mheshimiwa Waziri katika kutengeneza kitabu hiki cha hutuba hii iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli Wizara hii ni muhimu sana na inafanya kazi kubwa sana kupitia katika idara zake. Kutokana na utendaji huo ambao umeelezwa katika kitabu hiki, nina mchango mdogo katika Idara ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, idara hii imefanya kazi kubwa sana na zimeelezwa katika kitabu hiki kwenye ukurasa wa 31-35. Pamoja na kazi hii nzuri iliyofanywa na idara hii, lakini kutokana na wimbi kubwa la uingiaji na uhamiaji haramu kutoka nje ya nchi, ambao wanaingia si kwa nia njema bali ni kwa uhalifu, ninaiomba Serikali kupitia Wizara hii, kuna haja ya kujipanga upya na kutangaza vita dhidi ya watu hawa. Kuwaongezea vifaa vya kileo vya uhakika, vinavyoweza kuchunguza na kufahamu hati bandia za kusafiria, mihuri isiyoweza kughushika, pamoja na kuwawezesha wafanyakazi wetu kuweza kumudu mazingira yaliyoko katika sehemu zao za kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa kuna wajanja wengi na wanapita kwenye maeneo yetu husika bila kuwafahamu kutokana na mbinu wanazozitumia na badala yake kuwapa shutuma nzito, watendaji wetu kuwa hawawajibiki ipasavyo na kuchukua rushwa, kumbe hakuna lolote ila ni vifaa duni tunavyovitumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mdogo tu uliotokea kwa majirani zetu Kenya. Hivi karibuni wamefanikiwa kumkamata mhalifu wa siku nyingi, anayetumia mihuri ya nchi mbalimbali wakati wa kusafiri pia huwasaidia wahalifu wenzake kwa kutumia mihuri hiyo. Waswahili wanasema; “mwenzako akinyolewa wewe tia maji,” tuwe macho na watu kama hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Hata hivyo, ningependa kuweka angalizo katika eneo la wakimbizi, ukurasa 55-56, Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi inayofadhiliwa na Serikali ya Denmark, shilingi bilioni 10.9 kwa Mkoa wa Kigoma na Wilaya ya Ngara. Katika kikao cha wadau, Wabunge na Ofisi ya *RAS* Kigoma, kilichofanyika mwezi Mei, 2007, tuliazimia mambo ambayo tulimwagiza *RAS* awasiliane na Wizara (Katibu Mkuu). Mambo hayo ni yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Fedha za Miradi zinazotolewa na Shirika la *UNHCR* zisipitishwe tena katika Ofisi ya *RAS* Kigoma, fedha hizi zipelekwe moja kwa moja kwenye Halmashauri inayosimamia Mradi husika. Urasimu uliopo hauna tija na umejaa usumbufu usiokuwa wa lazima na unachelewesha utekelezaji wa Miradi. *UNHCR* wao wanasubiri kubadilika kwa *protocol* hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zinazotolewa na *DANIDA* zisimamiwe na Halmashauri zetu kikamilifu. Halmashauri za Wilaya ndizo zisimamie mchakato wa kapata *(source),* wakandarasi na isiwe mashirika yanayotekeleza Miradi na *DANIDA* peke yao, kama ilivyo sasa.

Hii inahitaji kubadilika kwa *protocol* iliyosainiwa kati ya Wizara (Katibu Mkuu) na *DANIDA*. Hili lazima lifanyike vinginevyo fedha hizi zinaleta utata katika usimamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri za Wilaya ya Kigoma, Kasulu, Kibondo na Ngara, ndizo zipewe *powers* za kuwasimamia wakandarasi na fedha za miradi ziende kwenye *Accounts* za Benki za Halmashauri za Wilaya husika. *DANIDA* kazi yao iwe ni kufuatilia tu utekelezaji na siyo ilivyo sasa. *Financial loopholes* ni nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yako ishinikize mashirika zaidi ya kimataifa, yajitokeze kusaidia maeneo yetu yaliyoharibiwa na ujio wa wakimbizi, hasa kupata fedha za kujenga barabara ya lami ya Kigoma hadi Nyakanazi. Hili linawezekana kama Wizara yako italipa kipaumbele ni jambo muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabweni ya wafungwa ya zamani ni madogo sana, yanahitaji kuwekewa *vent* zinazoweza kujengwa katika mabweni hayo. Mfano, chumba kimoja kidogo wanalala mahabusu/wafungwa 15 bila dirisha. Hii ni hali ambayo haiwezi kuachiwa tu ikaendelea. *Something has to be done.*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo sugu la mfumo wa maji taka *(Drainage)* katika Gereza la Kasulu ujengwe kwa sababu haupo na mashimo ya maji taka yanatoa harufu kali na kusababisha usumbufu mkubwa kwa wafungwa na Maofisa wa Magereza. Mfano, pale Gereza la Kasulu, mashimo ya maji machafu yapo usoni kwenye nyumba ya Mkuu wa Gereza. *It is dangerous.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukamilishaji wa jengo la *Prisons Community Centre.* Jengo hili limesimama na boma lake ni la muda mrefu. Naomba Wizara itenge fedha kukamilisha jumba hilo, lina manufaa kwa gereza na jamii ya wana-Kasulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba niunge mkono hoja hii iliyotolewa leo 31 Julai, 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokuwa nachangia hoja hii mwaka jana, nilizungumzia hali mbaya ya Gereza la Kibiti/Mng'aru. Katika gereza hili, hali yake kimajengo ni mbaya sana. Mabweni ya wafungwa wote ni *full suit* ya bati. Wakati wa mvua mabweni haya yanavuja sana na kusababisha mabweni hayo kujaa maji hivyo, wafungwa kukosa mahali pa kulala. Wakati wa kiangazi, mabweni hayo huwa na joto kali kiasi cha wafungwa kushindwa kulala.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali mbaya ya majengo si kwa mabweni ya wafungwa pekee, bali pia katika nyumba za askari. Nyumba zote za askari gerezani hapa ni za udongo na za siku nyingi. Ukiingia kwenye kambi hizi huwezi kuamini kama askari anayerekebisha tabia za wahalifu sugu anaweza kuishi humo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara baada ya kuelezea hali mbaya ya gereza hili katika Bunge la Bajeti mwaka jana, Idara ya Magereza ilipeleka maofisa wake pale gerezani na kuchukua matatizo mbalimbali yanayolikabili gereza hili. Matarajio yangu yote ni kuwa katika bajeti ya mwaka huu, baadhi ya matatizo hayo yangeweza kurekebishwa. Lakini cha ajabu katika bajeti yote ya leo, hakuna hata mradi mmoja uliopelekwa katika gereza hili. Hivi najiuliza; ni nani anayepanga bajeti ya Wizara hii? Hivi ni vipaumbele vipi vilivyowekwa na Serikali katika kupanga na kuamua mradi upi uanze na upi umalizie? Kile kitendo cha Maafisa wa Magereza kwenda pale Kibiti ilikuwa ni kiini macho au vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, anieleze ni kwa nini gereza hili halikufikiriwa katika bajeti hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, Gereza la Kibiti/Mng'aru ni la kilimo. La kushangaza ni kuwa gereza hili halina trekta, hali ambayo inafanya gereza lishindwe kutoa ziada *(surplus)* kwa ajili ya pato la nchi. Hivi Serikali inashindwa kukopa trekta kupitia Mfuko wa Pembejeo na kulipeleka katika gereza hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mtu binafsi anakopeshwa; iweje taasisi ya Serikali ishindwe kukopa trekta?

Mheshimiwa Spika, katika Gereza hili la Mng'aru/Kibiti, kuna mgogoro mkubwa wa mipaka baina yake na Vijiji vya Mng'aru, Kimbuga, Ngulakula na Miwaga. Mgogoro huu unatokana hasa na kutotumiwa ipasavyo, ardhi iliyochukuliwa na gereza. Gereza hili

lina ardhi yenye ekari zaidi ya 30,000, lakini inayotumiwa haifiki ekari 200. Hali hii si nzuri hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa ushauri kuwa, kama gereza halina uwezo wa kutumia ardhi hii nzuri, basi mipaka ya gereza ipunguzwe ili wananchi wa vijiji hivyo waweze kuitumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie na suala la umeme kwenye Gereza la Mng'aru. Kwa kuwa Mji wa Kibiti unatarajia kupata umeme hapo Septemba, basi ni vizuri Wizara hii nayo ikachukua umeme toka Kibiti hadi Mng'aru Gerezani (km. 7) ili gereza hilo nalo liweze kufanya kazi nyingi zaidi na kupelekea kuongeza pato la gereza na Pato la Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na wenzangu, kumpongeza Waziri na Naibu Waziri wa Waziri hii ya Mambo ya Ndani, kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikitishwa na Hotuba ya Waziri ukurasa wa 12, kuhusu kifungo cha nje kuwa, baadhi ya Wilaya na kadhalika, wanadai hawana fedha za kuwahudumia. Naona hawa watendaji hatuwahitaji katika ukekelezaji wa maamuzi ya nchi, naomba wawajibishwe au waachie ngazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisisitize ili Watanzania wafahamiane vizuri na Serikali iandae Bajeti ya uhakika kwa Watanzania wote, naomba sasa vitambulisho vya uraia vikamilike. Vitambulishi hivi vitasaidia wakwepaji wa kodi na *TRA* watakusanya mapato bila bughudha yoyote. Wakimbizi watajulikana na mipaka yetu itakuwa na watu wanaofahamiana vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na wenzangu kuunga mkono hoja. Fedha zote wapewe kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. BAKAR SHAMIS FAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa uzima na kuweza kuandika mchango wangu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru Tume ya Haki za Binadamu kuweza kupita katika baadhi ya Magereza nchumi na kujionea hali halisi ilivyo katika Magereza husika. Mengi nimeyaona, sasa ni jukumu ya wahusika ikiwemo Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kurekebisha kasoro zilizojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kati ya malalamiko (shida) ndani ya Magereza hasa Dar es Salaam ni msongamano wa mahabusu unaotokana na sababu kadhaa zikiwemo kucheleweshwa kesi kutokana na kukosekana kwa ushahidi wa kesi husika.

Tunaitaka Serikali ifikirie jinsi ya kupunguza idadi ya siku 60, ambazo kama ushahidi haujapatikana, kesi husika inafutwa. Muda huu unaonekana bado ni mrefu, ipo haja kupunguzwa angalau ifikie siku 45 hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kero ya hapo juu, kero nyingine zinazowakumba wafungwa ni suala zima la chakula kwamba kila siku ni ugali na maharage tu. Ni vyema Serikali iangalie uwezekano wa kufanya marekebisho ya mlo huu, angalau kupata chakula kingine chochote kama wali na samaki japo siku moja au mbili kwa wiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, majengo ya magereza mengi nchini yamechakaa sana ni wakati muafaka sasa kuyakarabati sio tu majengo ya magereza, bali na majumba ya askari na kukamilisha ujenzi wa majengo ambayo tayari yameshaanzishwa ili yapate kukidhi haja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaikumbusha na kuisisitiza Serikali, kuyatilia maanani maoni ya Zanzibar katika mchakato mzima wa Serikali, iharakishe mpango (mradi) wa vitambulisho vya uraia nchini, kwani hili ni jambno muhimu sana katika taifa lolote kujua uhalisia wa raia wake.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa kazi nzuri ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) na maandalizi mazuri ya Bajeti ya mwaka huu wa fedha 2007/2008. Nichukue nafasi hii kutoa mchango utakaofanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2007/2008 nayo ni yafuatayo:-

Wilaya ya Iramba inayo Magereza matatu; lile la Kiomboi, Ushora na Utemini. Gereza la Kiomboi lilijengwa kwa ajili ya mahabusu wa kisiasa, ambalo lilikadiriwa kuwa na idadi ya mahabusu hamsini tu. Kwa kuwa nchi yetu kwa hivi sasa hatuna mahabusu wa kisiasa na kama wapo sio kwa idadi kubwa, gereza hilo liligeuzwa matumizi na kuwa gereza la watu wenye makosa mbalimbali. Kwa maana hiyo, idadi ya mahabusu imekuwa haina kiwango, wamekuwa wakiongezeka bila kujali idadi na uwezo wa gereza kama lilivyojengwa. Sasa gereza linatunza mahabusu takriban 200-250 na idadi ya wafungwa 100-150. Idadi hii ni kubwa na hailingani na *capacity* ya gereza.

Namwomba Mheshimiwa Waziri, waangalie uwezo na waone huruma, kukubali kupokea mahabusu ndani ya gereza hilo wakati wakifahamu vizuri hali halisi ya gereza hilo. Kadhalika Gereza la Utemini na Ushora, bado chokochoko ipo kati ya wananchi na gereza lenyewe kugombea maeneo ya mashamba. Kadhalika utaratibu utumiwe wa kuwaachia wafungwa kufanya kazi huru na hivyo kukutana na raia na kufanya vitendo visivyoathiri.

Kwa kiwango kikubwa utekelezaji na wajibu unaofanywa na Maaskari Magereza ni ya kijasiri, wanafanya kazi kwa hali ngumu na bila kuwa na vifaa vya kutosha. Naomba Gereza la Kiomboi wapewe gari la tani kumi, lenye uwezo wa kukusanya kuni

na shughuli nyingine za uzalishaji. Pia Gereza la Ushora na Utemini, waongezewe trekta kwa shughuli za kilimo na kadhalika.

Shughuli mbalimbali zinazofanywa na Jeshi la Magereza, ziboreshwe na naiomba Wizara iridhie juu ya magereza kufanya shughuli nyingine za kuliletea Jeshi mapato kama vile ujenzi wa barabara, mitaro, nyumba na kadhalika. Zile zabuni zote zinazotolewa na Halmashauri, magereza waziombe, viwango vya utendaji wao wa kazi ni wa kuridhisha.

Naipongeza Wizara kwa jinsi ilivyoendesha zoezi la kufanya mabadiliko ya *passport.* Zoezi naamini linakwenda vizuri, japokuwa vipo vikwazo vidogo vidogo. Kadhalika Mkurugenzi wa Uhamiaji utendaji wake wa majukumu uondoe upendeleo. Niliwahi kufika pale ofisini kwake na kuhitaji kuonana naye kwa tatizo ambalo lilikuwa na uwezo wake kusaidia mbali ya kuniambia nisubiri zaidi ya dakika 45, akiwa anaita watu kwa majina wengi wakiwa na asili ya Ki-Asia.

Kibaya zaidi alitoka bila hata kunitaka radhi na hata nilipomwomba tuongee, aliniambia ana haraka bila kutaka kujua nina jambo gani muhimu, huku akimweleza mtu mmoja aliyekuwa pale mwenye asili ya Ki-Asia twende bwana.

Tabia ya Afisa huyu ni mbaya, mimi kama Mbunge ilinitisha na nilimripoti kwa Katibu Mkuu siku ile. Sina hakika kama anawatendea vipi wananchi wa kawaida. Namwomba Waziri anieleze ni hatua zipi za kumrekebisha zimechukuliwa dhidi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia kuwa wazima na salama. Mimi kwa leo, napenda kujua jambo moja tu katika hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lenyewe ni kuwa nimefuatilia kwa muda mrefu juu ya suala la Mkataba wa Kimataifa kuridhiwa na Serikali yetu ya Tanzania. Mkataba wenyewe unahusu juu ya kutokuwatesa watuhumiwa (Mahabusu) na wafungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, alieleze Bunge lako suala hili limefikia wapi? Je, kuna juhudi zozote zinazofanywa na Serikali za kutaka kuridhia Mkataba huu wa Kimataifa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni hayo tu kwa leo. Asante sana.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote, kwa hotuba nzuri. Nawapongeza kwa kusimamia vizuri urudishaji wa wakimbizi kwao.

Kuna tatizo kubwa hasa kwenye Jimbo la Vunjo, kuhusu nani agharamie mahabusu kupelekwa na kurudishwa mahakamani hasa mahakama za mwanzo.

Mahakama za mwanzo zinawatoza walalamikaji shilingi 7,000, kila mlalamikaji kupeleka mhalifu. Wakati anapoletwa Mahakamani toka mahabusu, mlalamikaji hulipa vilevile. Vitendo hivi ni sugu hasa Kata ya Kirua Kusini, Kituo cha Polisi Uchira.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ya Mambo ya Ndani, itoe ufafanuzi ni nani anapaswa kuhudumia hawa mahabusu kwa usafiri?

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kunipa fursa ya kuchangia hoja hii. Suala la vitambulisho vya uraia, limekuwa likipangiwa mikakati ya kutekelezwa lakini hadi leo bado hatua iliyofikiwa haijakidhi haja ya mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliangalie suala hili kwa kuanzia na Mikoa ya mipakani kama kule Kagera, Kigoma, Mara, Mbeya na kadhalika, baada ya kufanya uhakiki wa kuwatambua raia halali wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uraia wa nchi mbili *(Dual Citizenship)* ni jambo ambalo linafaa lifikiriwe na hatimaye ni vyema lipatiwe ufumbuzi ambao hautaathiri taifa letu kwa namna yoyote ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wahamiaji haramu, ambalo limekuwa likitendeka hasa Mikoa ya mpakani, bado ni kero inayopelekea kuchochea vitendo vya uhalifu. Inakuaje Wasomali na Wahabeshi, wavuke mipaka ya nchi jirani na hatimaye kufika Tanzania; hivi nchi hizo zinawaruhusu kupita bila kikwazo chochote? Serikali inatoa tamko gani juu ya hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna upungufu mkubwa wa Ofisi ya Uhamiaji baina ya mpaka wa Tanzania na Malawi, hasa maeneo yaliyotenganishwa na Mto Songwe hivyo, nikashauri Serikali kufanikisha kero hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, msongamano wa wafungwa bado upo na kuna haja ya kuziwesha Kamati kusukuma kesi ili kuweza kupunguza msongamano wa wafungwa, hasa wale walio na makosa madogo madogo. Ninaishauri Serikali kuwaachia au kuwaruhusu mahabusu walio magerezani zaidi ya miaka mine, ambao upelelezi bado haujakamilika, ambao makosa yao si ya jinai.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri Serikali kuwaachia au kuwaruhusu mahabusu na wafungwa waliobainika kuwa na ugonjwa wa UKIMWI ili waweze kubaki uraiani kuangalia afya zao zaidi.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo langu la Siha, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Joseph Mungai, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa hotuba nzuri ambayo ameitoa asubuhi hii. Ni ukweli usiopingika kwamba, hotuba yake imebeba

mipango mizuri, ambayo ikisimamiwa vizuri mambo yetu katika Wizara hii yatatuweka katika mfumo wa kisiasa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Ombi langu kwa Wizara hii ni kwamba, Siha sasa ni Wilaya na kwa msingi huo, tutahitaji huduma kama zile za Uhamiaji, Magereza na kadhalika.

Sisi wananchi tupo tayari kushirikiana na Serikali ili uanzishwaji wa huduma hizo, uweze kufanyika kwa haraka. Kwa mara nyingine narudia tena kwamba, naunga mkono hotuba hii.

**MHE. MWAJUMA HASSAN KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema nimshukuru mola, kwa kuniwezesha kuishika kalamu na mimi nikaweza kuchangia. Pia kukupongeza wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika, kwa umakini wako wakati unapotuongoza.

Baada ya maelezo yangu hayo, sasa naomba uniruhusu nitoe mchango wangu. Magereza yetu yana upungufu mkubwa sana wa vitendea kazi, pia uhaba wa askari wenyewe. Ukichukulia nyumba za mahabusu hazikidhi haja. Hali hii inawafanya mahabusu kuwekwa katika maeneo ambayo yanasababisha kukosa hewa safi. Jengo linaloweza kuingizwa mahabusu 80 huchukua 150. Je, hii ni haki?

Ukiwaona mahabusu wanaingizwa katika gari, hutegemei kama watafika salama. G gari lenye uwezo wa kubeba mahabusu 30, huingizwa mahabusu 100. Hii ni hali mbaya. Kwa nini Serikali haiyawezeshi magereza yetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuinusuru nchi yetu kuingia watu kiholela ni kuwepo kwa vitambulisho kwa Watanzania wote. Suala hili pia litazuia ujambazi nchini. Mara nyingi sana majambazi huingia nchini mwetu kwa njia ya urahisi na kuweza kuiba na pia kufanya uhalifu nchini. Watu hawa watapita wapi iwapo katika nchi yetu raia wetu wote watakuwa na vitambulisho?

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa zana za kuzimia moto hapa nchini haukidhi haja. Ni juzi tu basi la *Mohamed Trans* liliungua lote ndani ya mji lakini watu walikufa kwa sababu ya ukosefu wa zima moto.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo udhaifu mkubwa katika umalizaji wa kesi mahakamani, jambo ambalo hupelekea kuweka watu mahabusu kwa wingi. Ndiyo sababu inayopelekea magereza yetu kuwa na wafungwa wengi mno.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uhamiaji haramu. Tanzania ni nchi ambayo inapakana na nchi nyingi karibu nchi nane, pamoja na kuwa ukanda mrefu wa bahari kutoka Tanga mpaka Mtwara, ikiwa ni pamoja na Kisiwa cha Zanzibar. Hii inaelekea kuwa na wahamiaji haramu kama Idara ya Uhamiaji haitaimarishwa kuanzia ngazi ya Kata, Mkoa mpaka *National level.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kuongezwe mipaka ajili ya udhibiti, pamoja na vitendea kazi mfano, kuna udhibiti *Namanga Border* lakini kuna watu wanapitia Longido, ambako hakuna Ofisi za Uhamiaji. Vitendea kazi hivi viwezeshwe kuwa na vifaa vya mawasiliano, vyenye kuweza ku-*transmit data* kuelezea mtu kaingia lini na katoka lini. Vilevile Idara ya Uhamiaji iwapatie mafunzo ya ngazi za chini watu wake, kwa sababu wahamiaji haramu wanakuja na mbinu mpya kila siku. Wananchi waelimishwe kutoa *report* wanapomwona mgeni kijijini waripoti kwa Mtendaji wa Kijiji. Tumeona kwenye matukio ya ujambazi kule Mwanga, majambazi walikuwa wamepangisha Njiro, wananchi waliwaona lakini walikuwa hawatoi *report*. Ni vizuri kuwa na utaratibu, mgeni akiingia kwenye mtaa/kijiji Fulani, itasaidia ku-*monitor*. Sababu ya ukanda mrefu wa bahari, kuna haja ya kuimarisha *Marine Immigration* na pia wapewe *training* na vitendea kazi kama *boat*. Swali je, tunao hawa Afisa Uhamiaji wanaofanya *patrol* kwenye ukanda wa bahari?

Kuhusu wageni kupata *visa point of arrival*. Ningependa kujua ni kwa nini wageni wanakuja mpaka Tanzania, ndio wanalipia *visa* ya kuingia nchini? Vilevile zile *form* zetu za *arrival,* maswali yanauliza sababu za kuja Tanzania, kuna kipengele kinasema *seeking employment.* Hivi mgeni anakuja kutoka kote huko kupata *visa* ya kufanyakazi *airport*? Pamoja na kwamba, tunawahitaji hawa wageni kwa sababu za kitalii na kadhalika, *but we have to be proud of our country, although it is expensive to be poor* lakini lazima tuwe maskini jeuri. Tunahitaji na wao pia wanatuhitaji.

Tujiulize kabla hujaomba *visa* kwenda *Europe, America* na kadhalika,. unaambiwa uombe wiki moja kabla, kwingine saa 24 kabla. Bado wanachukua *finger prints* kwa ajili ya uchunguzi. Yote haya ni kuangalia katika nchi zao hawaendi wavamizi, bado lazima uoneshe unazo *funds* za kwenda huko kwa kuonesha *bank statement* ya miezi mitatu iliyopita. Lakini wao wakija Tanzania, hawaoneshi vyote hivyo, wengine hawana hata *credit* ya $ *20* kwenye *account* namba zao. Wanakuja *holidays* kwa mikopo, bado wanakuja mpaka *airport* wanapata *visa.* Jamani!

Mheshimiwa Naibu Spika, je, hatuna Ofisa wa Uhamiaji kwenye balozi zetu kwenye nchi kama USA, UK, Italy, German na kadhalika? Tafadhali tusikubali kunyanyaswa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla Magereza zetu nchini bado zina msongamano. Pamoja na kuwa na Tume ya Haki za Binadamu Tanzania, lazima Magereza haya yaimarishwe na yawe katika hali ya usafi na nafasi za kutosha. Vilevile vitega uchumi vya Magereza viimarishwe, vitasaidia sana kwanza kuongeza kipato kwenye Wizara. Miongoni mwa wafungwa kuna wataalam pia wapewe mafunzo mbalimbali kwa mfano, waweze kutengeneza *furniture* za ofisi zote za Serikali kwa kuanzia. Hii itasaidia Serikali ku-*save* fedha za kigeni kuagiza *furniture* hizi nje. Nina hakika kabisa wakipewa mafunzo na kupatiwa vifaa, hawawezi kushindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *form* za *departure (TIF11).* Kuna sehemu wanayouliza *nnumber of night spent in Tanzania,* idadi ya siku utakazokaa Tanzania. Hizi ni tafsiri tofauti kabisa. Hivi kuna haja gani ya kujaza *departure from;* kwa nini kusiwe na

*connection* kati ya *departure; check in desk* na uhamiaji, ambayo ita-*save stationery* pamoja na kuondoa utata ulioandikwa kwenye *form* hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, vitambulisho vya uraia vikamilishwe haraka iwezekanavyo. *Dual citizenship* ikamilishwe pia.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake, kwa kazi nzuri sana, licha ya matukio machache madogo madogo yasiyoepukika, mengine nje ya uwezo wao yaliyojitokeza katika kipindi cha mwaka uliopita. Aidha, napenda kuwapongeza watumishi wote wa Idara zote, ambao sambamba na Mawaziri na Katibu Mkuu wao, wanafanya kazi nzuri ikiwa ni pamoja na uandaaji wa hotuba hii. Nawapongeza sana na ninaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni muhimu sana kwa uhai wa maisha ya taifa letu ya siku hadi siku. Ndiyo walinzi wa awali wa mipaka ya nchi yetu. Ni kazi nzuri. Wasipowezeshwa kupitia Idara ya Uhamiaji kivifaa na mafunzo, hata kama wanafanya kazi kwa kujituma, huenda asiwepo mtu wa kuitambua kazi yao muhimu hasa kwa kuzingatia ukweli kuwa, mpaka wetu ni mkubwa na mrefu sana kuudhibiti. Mahali pa kuingia ni pengi, halali na njia za panya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi, idara hii iongezewe uwezo wa kifedha kuwawezesha kujipatia vifaa muhimu vya kutumia mipakani na kuwawezesha watumishi wa idara hii kusoma mara kwa mara ili waendane na mabadiliko ya sayansi na teknolojia na nyanja mbalimbali wautumizo waingiaji haramu. Kuwawezesha wananchi na kuwahamasisha waweze kushirikiana kwa karibu sana na idara hii hasa katika kuwang'amua na kuwaripoti waingiaji haramu kwa vyombo vinavyohusika. Serikali iangalie upya sheria zinazohusu usalama wa raia na mali zao hasa vijijini na mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ndiyo inayohifadhi wale ambao wametengwa na jamii au kwa manufaa ya umma au kwa manufaa yao (wafungwa) wenyewe binafsi. Watu hawa wengine wamekata tamaa kwa kuonewa, kwa bahati mbaya au kwa uhalali kabisa. Hawa ndiyo wanaoishi na watu hao. Pamoja na kuwa wametengwa na jamii, bado wana haki zao. Hawa ndio wanaowalindia utu, uhuru na haki zao. Je, tunawalipa kama wanavyostahili? Je, tunawasaidiaje vya kutosha waweze kuishi na watu hao kwa amani?

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira ya magereza yaboreshwe ili wafanyakazi wa magereza waipende kazi yao ili waweze kukaa vyema na watengwa hao ili wakiwa magerezani wasiendeleze chuki kwa Serikali yao na wananchi wenzao walio nje ya magereza. Kitu kitakachotokea, wakitoka nje ya magereza wasiwe wageni sana kwa nchi yao na kutumia muda mrefu kumaliza hasira walizozivuna wakiwa magerezani. Gerezani siyo jehanamu ni kituo cha mafunzo. Waendelee kupewa mafunzo Maafisa wa Magereza ili wautambue umuhimu wa kazi yao muhimu ya kuishi na wenzetu waliopotoka kwa mud,a wakahitajika kupumzishwa mahali, wajifikirie waweze kujirekebisha. Hivyo ni kazi ya askari hawa kukumbushwa mara kwa mara, njia bora zaidi ya kuwahudumia na kuishi vyema na watu hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Magereza huwa ina kikosi kizuri cha ujenzi. Naomba idara hiyo iimarishwe kwa kupewa kandarasi nyingi za ujenzi. Naamini hii ndiyo njia pekee ya kuisaida idara hii iweze kujitegemea na uwezo huo wanao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikosi cha zimamoto naomba kiimarishwe. Ni muhimu sana kuwa na juhudi za kusudi sana kuwezesha angalau kila Halmashauri ipate gari moja. Ni jambo gumu lakini kwa umuhimu wake, naamini hatua kwa hatua itawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kuunga mkono hoja. Baada ya hilo, napenda kutoa ushauri wangu kwenye nyanja chache ifuatavyo:-

Naiomba Wizara ikamilishe upatikanaji wa vitambulisho vya uraia katika mwaka huu wa fedha. Suala hili lifanyike kwa umakini sana na ikiwezekana makampuni ya kizalendo ndiyo yafanye kazi hii. Sababu kubwa ni unyeti wake, kwani Wizara isipokuwa makini itaanika habari nyeti za wananchi walio katika vyombo vya Ulinzi na Usalama wa nchi yetu. Pia naiomba Wizara, ishirikiane sana na Wizara ya Fedha katika ukamilishaji wa mradi huu, kwani vitambulisho vya uraia vitaiwezesha *TRA* kukusanya kodi nyingi sana na kwa urahisi sana.

Naiomba Wizara ilishughulikie suala la uraia wa nchi mbili *(Dual Nationality),* kwa umakini sana. Pamoja na kwamba, wapo Watanzania wengi ambao wapo nchi za kigeni na wangependa kuwa raia wa huko, lakini pia Wizara isipokuwa makini, wageni tu ndiyo watafaidi mradi huu kwa ujanja na nchi isipate mapato yoyote.

Nguvukazi iliyopo Magereza itumike vizuri sana katika kilimo, hasa cha umwagiliaji. Nguvu kazi ni kubwa mno na ikitumika vizuri, nchi inaweza kuwa na chakula cha kutosha na kuuza nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena kuunga mkono hoja.

**MHE. ISSA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza hotuba ya Wizara na naunga mkono hoja hii.

Idara ya Uhamiaji iondolewe Utumishi, iwe kama Jeshi, Polisi, Magereza kwa sababu Idara ya Uhamiaji ni nyeti kwa Taifa letu kwa usalama nchini. Siri yao ibaki mipango yao isiwe Utumishi.

Nataka maelezo yakinifu kuhusu mapato yanayopatikana kwa makusanyo ya *visa* na fedha za *Passport* kwa Zanzibar, kutumika kwa Ofisi ya Makao Makuu ya Uhamiaji Bara. Fedha zinazokusanywa kila baada ya muda makusanyo hayo, Mkurugenzi Mkuu

Uhamiaji hutoa maagizo wapeleke Makao Makuu. Je, Zanzibar hakuna matumizi ya fedha hizo; ushahidi wa mambo hayo upo?

Nataka ufafanuzi juu ya wale wanaopandishwa vyeo; kwa nini hucheleweshwa kupata mafao yao ya kupandishwa vyeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba ufafanuzi. Naunga mkono hoja.

**MHE. GIDEON A. CHEYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri. Aidha, nampongeza yeye, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara, kwa jitihada zao za kuboresha huduma za Wizara hii katika ngazi zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nianze kuchangia Idara ya Magereza. Kwanza, namshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa ziara yake katika Wilaya yetu ya Ileje mwaka wa fedha uliopita. Nina hakika aliona na kuelezwa shughuli za ujenzi wa majengo ya Gereza la Wilaya. Baadhi ya majengo hayo ni jengo la wafungwa na mahabusu wa kike, nyumba za kuishi askari magereza, jengo la kituo cha chekechea na kadhalika.

Pamoja na jitihada za askari magereza wenyewe na mchango wa Halmashauri ya Wilaya, tunaomba Wizara, kwa kupitia Magereza (Mkoa), iendelee kutoa msaada ili kukamilisha miradi hiyo ya ujenzi, kadri itakavyowezekana. Nina hakika maombi rasmi yalikwisha wasilishwa kwa utaratibu wa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara iendelee kuhimiza katika Magereza yote, elimu kwa wafungwa kuhusu haki zao kuhusiana na utaratibu wa *parole.* Baadhi ya wafungwa hawaelewi vigezo na taratibu za kunufaika na mpango wa *parole.* Nilipata maswali kuhusu jambo hili nilipotembelea Gereza la Wilaya tarehe 18 Mei, 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie Idara ya Uhamiaji. Mwaka jana niliomba Wizara iboreshe huduma za Uhamiaji Wilayani Ileje. Nilisema yafuatayo: Wilaya yetu ipo mpakani na Malawi, kumekuwa na tatizo la wahamiaji haramu au wakimbizi wanaopita Wilayani kwenda Malawi au Afrika Kusini. Kutokana na tatizo hilo, haja ipo ya kuimarisha Ofisi na Watendaji wa Uhamiaji Wilayani Ileje.

Tunaomba Wizara ione umuhimu wa kujenga kituo cha kisasa pale mpakani Isongole (Darajani), kama ilivyo Kasumulo kule Kyela. Shughuli za biashara kati ya Tanzania na Malawi kwa Wilaya yetu, zinaongezeka na ni muhimu kuimarisha huduma za kudhibiti masuala ya uhamiaji kwa maslahi ya usalama wa nchi yetu. Natumaini baada ya ziara ya Mheshimiwa Waziri, Wilayani Ileje, atakubaliana na ombi hili na kuendelea kulizingatia katika mipango ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huo mfupi, nawatakieni utekelezaji mwema na naunga mkono hoja.

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, pamoja na wataalam wao wote, kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya. Niwaombee kila la kheri katika kuongeza juhudi zaidi kufanya kazi nzuri zaidi na ninaunga mkono juhudi zao na hoja hii pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi na kuunga mkono hoja hii, napenda nitumie fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa juhudi zake za kuendeleza matumizi ya *biogas* kwa kupikia na mwanga katika Magereza yetu nchini. Bado ipo nafasi nzuri na kubwa kwa Wizara kuendelea kulisimamia suala hili, hata kama Maafisa wetu wa Magereza wa Mikoa na hata wa gereza lenyewe, watakuwa wanalishughulikia. Tatizo lao kubwa hawa ni fedha, uwezo wa ujenzi wa vyungu vya hii *biogas* wanao na hata mafundi wazuri wa ujenzi. Naunga mkono juhudi hizi za Serikali na inapobidi, nitatoa ushirikiano hata wa kiufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia niipongeze Serikali, kwa kazi nzuri inayofanywa na Idara ya Uhamiaji ya Wizara hii ya Mambo ya Ndani. Ninawapongeza Maafisa wetu wa Uhamiaji, wanaojituma katika kazi zao za uhakiki wa uhalali wa wahamiaji walioajiriwa katika migodi, mahoteli, viwandani na hata wafanyabiashara mbalimbali. Juhudi kubwa za aina hiyo, zinahitajika pia katika visiwa vya wavuvi ndani ya Ziwa Victoria.

Nyenzo za usafiri, hususan *boats* zenye nguvu, vinahitajika sana. Kama mafungu ya kununua *boats* hizi zenye nguvu yatakuwa hayatoshi, basi ile busara ya kushirikiana baina ya Polisi, *TRA, Fisheries,* Uhamiaji Mkoa na kadhalika, iendelee kupewa nafasi ili vyombo hivi vitakuwa ni vile vyenye nguvu na ukubwa unaozidi vyombo vya wavunja sheria waliopo katika Maziwa yetu, hususan wale waliopo katika Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naomba kuunga mkono hoja. Asante.

**MHE. FATMA ABDULHABIB FEREJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu ya Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya Magereza yetu hapa nchini si ya kuridhisha na suala hili limekuwa linazungumziwa, haijaonekana kubadilika. Ukiacha hali ya majengo ya Magereza yenyewe kuwa ni ya kutisha kutokana na uchakavu wa majengo hayo ambayo mengi ni ya tokea wakati wa ukoloni, hali ya msongamano wa wafungwa na mahabusu ni tatizo kubwa na lisilovumilika, kwani linawahusu sehemu ya jamii yetu ambayo inapaswa kupatiwa haki zote za Binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hatua zilizochukuliwa ambazo zimeelezwa na Mheshimiwa Waziri, bado msongamano ni tatizo. Naomba Mheshimiwa Waziri, anieleze ni kwa nini Sheria ya *Community Service Act* ya 2002, ambayo ilianza kutumika katika mikoa sita, imefanikiwa kupunguza kwa kiasi kidogo sana msongamano huo ni wafungwa 548 tu wanaohusika katika kutumikia adhabu zao chini ya sheria hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni hatua gani zitakazochukuliwa kuhakikisha Sheria hii ya *Community Service Act* ya 2002, nayo inasaidia katika kupunguza msongamano Magerezani?

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya chakula katika Magereza yetu pia si ya kuridhisha. Chakula wanachopewa mahabusu na wafungwa ni lazima kiwe na virutubisho muhimu vinavyohitakija ndani ya mwili, kwani Serikali ina wajibu wa kuhakikisha, wenzetu hawa wanarudi ndani ya jamii wakiwa wamerekebishwa tabia zao na wakiwa na afya, ili waendelee kuchangia nguvu kazi ya nchi yetu na sio wabaki kuwa mzigo ndani ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali lazima ihakikishe fedha kwa ajili ya chakula cha wafungwa na mahabusu zinapatikana kama zinavyoombwa. Kutokupatikana kwa fedha za kutosha katika Idara ya Magereza kwa ajili ya chakula, kunasababisha Idara hii kuwa na malimbikizo ya madeni na kuonekana kama wanapenda madeni. Chakula ni muhimu kwa maisha, hivyo ni lazima Idara hiyo itaingia kwenye madeni kwa sababu lazima walishe waliopo Magerezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Magereza ina mashamba ya kilimo na mifugo ya kupigiwa mfano kutokana na uzalishaji wake na huzalisha kwa madhumuni ya kusaidia kuwalisha waliopo Magerezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri, anieleze je, kuna ufuatiliaji wa kutosha kuona kwamba mazao hayo ya mifugo na kilimo yanadhibitiwa vizuri na hakuna upotevu? Naomba anieleze ni kiasi gani kilichozalishwa na Magereza kwa mwaka 2006/2007?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali lazima iwachunguze sana na kuweza kuwadhibiti askari na Maofisa wa Magereza, kwani wao ndio wenye dhamana ya kuwarekebisha wafungwa ili warudi kwenye jamii wakiwa na tabia njema. Inasikitisha sana kuona kwamba, baadhi ya wanaotoka Magerezani hasa vijana, hutoka na tabia ambazo hawakuwa nazo walipoingia mfano, sigara. Ni vipi wafungwa hao wanapata tabia hizo mbaya na ikiwa wanaowadhibiti wana tabia nzuri?

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa vitambulisho umekuwa ni wa kusuasua mno, ilihali umuhimu wa Watanzania kuwa na vitambulisho hivyo unaeleweka sana. Ikiwa sehemu moja ya Muungano, yaani Zanzibar, waliweza kwa mafaniko kuweza kutoa vitambulisho vya Wazanzibari na ni vitambulisho ambavyo vimepata sifa za Kimataifa. Je, ni kwa nini Idara ya Uhamiaji isiombe msaada kutoka kwa Kitengo kilichoshughulikia vitambulisho Zanzibar, ili mradi huu uweze kukamilishwa mapema zaidi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, nampongeza Waziri na timu nzima ya Wizara kwa kuzingatia utekelezaji muhimu wa majukumu ya Wizara.

Ningependa kupata majibu katika Bajeti ya mwaka 2006/2007, katika hotuba ya Waziri na katika majibu ya kifungu *(Development Book)* Wizara ilitenga shilingi milioni 20 kujenga *immigration point* eneo la Mulukuru mpakani mwa Tanzania na Msumbiji, eneo hilo limekuwa ni njia ya wahamiaji haramu, mwaka uliopita Wasomali wapatao 150 waliingia nchini kupitia eneo hilo upande wa Msumbiji. Wenzetu wameshajenga *immigration point* (ofisi yao) na hivyo vijana wetu wanapovuka mto hunyanyaswa sana lakini hakuna udhibiti wowote kwa upande wetu.

Vile vile Wizara ya Miundombinu tayari wameanza mpango maalumu wa ujenzi wa daraja la Umoja namba mbili, daraja la chuma kuvukia Msumbiji. Ningependa kufahamu kama katika mwaka huu wa fedha kituo hicho cha uhamiaji kitajengwa hapo mpakani kama utekelezaji wa ahadi ya Serikali katika Bajeti ya mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri na Naibu Waziri, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Pamoja na pongezi hizi naomba nisaidiwe yafuatayo:-

Kwanza ni kuhusu Gereza la kilimo la Butundwe – Geita, ni gereza ambalo lina uwezo wa kuzalisha maharage, mahindi, mpunga na muhogo kwa mkoa mzima wa Mwanza. Tumewapatia mbuga kubwa yenye rutuba ya kutosha. Tatizo kubwa hawana vitendea kazi. Niliwahi kupewa trekta kuu kuu ambalo halifanyi kazi. Naomba wapewe angalau trekta mbili kwa ajili ya uzalishaji litaokoa fedha nyingi za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri aje atutembelee katika gereza hilo ili tuweze kuona jinsi walivyo na maeneo ya uzalishaji nakukaribisha jimbo la Busanda.

Kuhusu Idara ya Uhamiaji, katika Mkoa wa Kagera kumekuwa na matatizo, wananchi wamekuwa watuhumiwa kuwa ni wakimbizi au wahamiaji haramu na hii imekuwa ikitokea kwa watu wenye mali hususani ng’ombe wamesumbuliwa sana, ambao waligoma kutoa pesa walipelekwa wengine Rwanda na wengine Burundi na Serikali za kule zikawarudisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iangalie matatizo haya yanayofanywa na maafisa uhamiaji waroho kulingana na mabadiliko ya utandawazi na kuwa sasa dunia ni kama vijiji nashauri Serikali iruhusu mtu kuwa na uraia wa nchi mbili kama ataona inafaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kifupi naomba trekta mbili kwa Gereza la Butundwe - Geita, Idara ya Uhamiaji isinyanyase wananchi walio mpakani kwa kuwafukuza wakati wanakaa miaka mingi sana tangu enzi za mababu zao.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kupata nafasi ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaompongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri, baada ya utangulizi huo naomba sasa nichangie maeneo machache ya hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya kero kubwa kwa walalamikaji wa kesi mbalimbali ni gharama ya lishe ya watuhumiwa wakiwa mahabusu za kata. Huko nyuma Wizara ilikuwa na utaratibu wa kuteua watu wa kutoa chakula kwa kila mahabusu ya kata. Utaratibu huu ulisitishwa na Wizara miaka ya hivi karibuni, kutokana na hatua hii walalamikaji wanalazimishwa kutoa chakula kwa ajili ya watuhumiwa wao. Pale ambapo mlalamikaji hana uwezo wa kutoa chakula mtuhumiwa wake huachiwa huru na hivi kusababisha mlalamikaji asipewe haki yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ieleze Bunge lako Tukufu sababu za kuondoa huduma ya chakula katika mahabusu za kata kote nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa kupanga kununua vyombo vya usafiri katika Bajeti yake ya mwaka 2007/2008 yakiwemo magari 11 na pikipiki 17 kwa ajili ya idara ya uhamiaji. Kwa kuwa Wilaya ya Kondoa haina gari na kwa kuwa Wilaya hii ni kubwa sana, ninaomba ifikiriwe kupatiwa gari moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huu mfupi, ninaomba kuunga mkono hotuba hii.

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama mdau wa utalii, napata malalamiko mengi mno kila siku kutoka kwa watalii lakini nakosa jibu sahihi la kuwajibu. Tatizo lao kubwa ni ucheleweshaji katika viwanja vya ndege wanapoingia nchini. Wakati mwingine inachukua mpaka saa moja kupita *through immigration*. Anapaswa kuunga mistari mirefu, madirisha karibu matatu tofauti na huu ni usumbufu mkubwa hasa kwa mtu aliyesafiri saa nyingi na amechoka anataka kuwahi hotelini akapumzike.

Mheshimiwa Naibu Spika, sielewi kwa nini pasiwepo na utaratibu wa kuwa na huduma zote kwenye dirisha moja badala ya kumaliza dirisha moja na kuhamia dirisha lingine kwa sasa tunapata ndege chache sana na kama juhudi za Serikai za kukuza utalii, ukifanikiwa, na tukawa tunapata wageni lukuki na ndege zikawa zinaingia kwa wingi, je, kama kila utalii mmoja atachukua *45 minutes, to clear from immigration* tutafika? Ni vizuri Wizara ijipange upya jinsi ya kutoa huduma hii. Kama uwanja wa London unateremsha ndege moja kila dakika tano na huchukui dakika 20 kumaliza *formalities* zote za *immigration,* kwa nini hapa kwetu pawe taabu.

Mheshimiwa Waziri litupie jicho kwani hii ni kero mbaya na inaipaka nchi yetu dosari mbaya. Ni kiasi cha kujipanga vizuri tuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, magereza yetu yamefurika kwa sababu ya mahabusu wengi wanaongojea kesi zao kusikilizwa. Hili limekuwa tatizo na litaendelea kuwa tatizo ingekuwa vyema sehemu ya mahabusu ambao hawajahukumiwa libinafsishwe na kupata makampuni yenye uwezo wa kuwaweka hao mahabusu hadi hapo watakapotakiwa mahakamani. Hii itapunguza kwa kiasi kikubwa msongamano katika magereza yetu. Hoja ya kuwa huenda watuhumiwa watatoroka halipo kwani hayo makampuni yatakuwa *responsible*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kupunguza msongamano, wafungwa wa muda mfupi wawe wanafungwa kifungo cha nje ili kupunguza msongamano magerezani. Najua tumekwishapitisha hapa Bungeni Sheria hii lakini inachukua muda mrefu mno ni vyema madaraka haya yakapewa mahakimu. Pia sheria zetu zingeangaliwa upya ili makosa ambayo siyo ya hatari wakosaji wawe wakitozwa faini badala ya kifungo. Kwa njia hii tutapunguza msongamano na pia kuingizia taifa pesa kwa ajili ya maendeleo.

**MHE. HEMED MOHAMED HEMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha kuamka salama mimi na wenzangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nikupongeze wewe binafsi kwa jitihada zako za kutuongoza pale tunapokosea na kutupongeza pale tunapopatia. Pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha hotuba yake ambayo ni imani ya Watanzania kuona magereza yatakuwa mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hayo sasa naomba uniruhusu niende katika mchango wangu. Kuhusu upungufu wa magari ya kusafirisha mahabusu, mwanadamu aliye na akili timamu anapokea ajue maisha yake yanaweza kugeuka mara moja ama tajiri kuwa maskini ama mzima kuwa mgonjwa ama kuwa huru na kukosa uhuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli magari wanayochukuliwa mahabusu inaonekana wazi kuna ukosefu wa magari na kama hivyo sio basi ni udhaifu wa wakuu wa magereza mahabusu kuingizwa kwa wingi sana katika gari, jambo ambalo hulazimika kusimama na kuvua shati zao kwa kuashiria joto. Hali hii inaonekana wazi na kila mtu kitendo hiki, sio vizuri gari lenye uwezo wa kuchukua watu 50 huingizwa mahabusu 80, watakaa vipi?

Kuhusu hali ya magereza nchini, magereza mengi nchini yana hali mbaya ama hali mbaya kwa magereza yenyewe ama yana ufinyu kwa mahabusu. Hii leo Naibu Waziri wa Katiba na Sheria alijibu suala la Mheshimiwa Omar Kwaangw' swali Namba 326. Alithibitisha gereza la Babati liko hoi. Pia gereza la Mpanda huko Rukwa lina hali mbaya sana, kubwa zaidi ni kuwaweka mahabusu katika magereza kwa wingi sana, jambo ambalo hupelekea mahabusu kukosa hewa ya kutosheleza pia kupumzika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vitambulisho vya uraia iko haja Mtanzania wa leo kutambulika kueleweka kwa Mtanzania, njia pekee ya kutambulika ni kuwa na vitambulisho, kukosekana kitambulisho kinaiwezesha nchi yetu kuwa na wageni ambao hawaeleweki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukuwa kwa matendo ya ujambazi hapa nchini kunasababishwa na wageni wanaoingia nchini kiholela. Hivyo basi wakati umefika Watanzania wapatiwe vitambulisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu zimamoto, hali ya sekta hii sio nzuri, haina vitendea kazi vya kutosha, ni miezi miwili iliyopita Watanzania wenzetu walikufa kwa ajali ya gari lililoungua huko Singida, gari hili la *Mohamed Trans* iliungua hivi hivi mbele ya umma lakini kukosekana kwa gari la zimamoto wenzetu waliungua wote. Ni vyema sasa Serikali ifanye mipango ya kuhakikisha kila wilaya iwepo gari la zimamoto. Naitakia Wizara husika ifanikishe azma yake.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua nafasi hii kuipongeza Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri. Baada ya pongezi hizo sasa napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mazingira ya kazi, mazingira ya kazi ya askari magereza hasa kwa askari magereza wa mikoani na wilayani ni mabaya sana, moja, wengi wanaishi kwenye nyumba mbovu sana. Lakini pia wengi wanaishi kwenye nyumba za kupanga, pili, askari wengi hawana vifaa vya kutosha vya kufanyia kazi kwa mfano, gari, pikipiki na hata *uniform* na viatu.

Nashauri Serikali kupitia Wizara hii, ikarabati nyumba za asakri na ijenge nyumba zaidi za askari, inunue viatu, *uniform* na vifaa vingine vya muhimu kwa askari magereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu msongamano katika gereza la Mbozi ni dogo sana na kutokana na msongamano wa mahabusu kunasababisha waishi kwa shida sana. Naomba kujua Serikali kupitia Wizara hii ina mpango gani wa kupanua gereza hilo? Lakini pia ningependa kujua uchimbaji wa kisima kirefu cha maji safi na salama pale gereza la Mbozi utakwisha lini? Maana taarifa za jumla kwamba kazi inaendelea bila kuonyesha *time frame* hairidhishi hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana naunga mkono hoja.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri.

Kuhusu msongamano wa mahabusu/wafungwa, Gereza la Babati lina msongamano mkubwa sana hasa kutokana na Wizara ya Simanjiro na Hanang kuendelea kupeleka wafungwa Babati. Uwezo wa gereza la Babati hauzidi watu 115, lakini sasa linapokea watu zaidi ya 1,000. Huku ni kukiuka kwa kiwango kikubwa haki za binadamu.

Pili gereza la Babati ni chakavu sana, tatu yapo malalamiko ya askari wa magereza kuwa stahili zao zinacheleweshwa. Nashauri kuwa Wizara ichukue hatua za makusudi za kukarabati gereza la Babati lakini hasa kupunguza na kuondoa kabisa msongomano. Nitashukuru pia kama Mheshimiwa Waziri atatembelea Babati kwa kuzingatia kuwa Babati ni Makao Makuu ya Mkoa mpya wa Manyara.

Kuhusu Idara ya Zimamoto, naishukuru Serikali kwa kutenga fedha katika mwaka 2006/2007 kununua gari la zimamoto kwa Halmashauri ya Mji wa Babati. Kwa kuwa sijapata taarifa kama sasa gari hilo limenunuliwa na kama limefika Babati, naomba kufahamu kama Halmshairi ya Mji wa Babati limepokea gari hilo.

Pili, naomba kufahamu kama uundaji wa kikosi cha zimamoto na uokoaji kwa ajili ya Halmashauri ya Mji wa Babati limekamilika au upo kwenye hatua gain? Namtakia Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kazi njema nikiwa na imani kuwa matatizo niliyoyaeleza yatapatiwa ufumbuzi. Ahsante sana na naunga mkono hoja.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilipata fursa ya kutoa mchango wa hoja hii, napenda kusisitiza maeneo kadhaa ambayo nadhani sikuyaeleza vizuri. Nimezungumzia gereza la mahabusu Mpanda pamoja na kuwepo kwa magodoro lakini vyumba ni vinne vyenye uwezo wa kulaza wafungwa 18 tu lakini msongamano ni mkubwa, gereza la mahabusi la Mpanda wana gari chakavu la muda mrefu bovu hata kupeleka wagonjwa na kuchukua chakula wanaomba msaada wa gari toka Idara nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilieleza kwa uchache sana kuhusu maslahi ya askari kwa maana ya makazi, posho, mishahara na malipo mengine ni lazima yatazamwe kuzingatia ugumu wa kazi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikua nadhani ni vyema gereza la mahabusu Mpanda likabakia kuwa gereza la mahabusu na wafungwa wote wapelekwe Kalila ili kupunguza msongamano. Nilizungumzia pia juu ya wakimbizi na athari tunazopata uharibifu wa mazingira na maliasili zetu tena kwa kutumia silaha za kivita ni hatari sana, jambo hili lisifumbiwe macho.

Kazi ya kuhakiki wakimbizi Katumba na Mishamo irudiwe pia kwa kuangalia vijiji vya wenyeji vinavyozunguka makambi hayo, wakimbizi wamezagaa sana kwa sababu usimamizi wa sheria ya wakimbizi haikusimamiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu magereza ya kilimo na kuhodhi maeneo makubwa na kuleta migogoro na wananchi wanaoishi karibu na magereza hayo, gereza la Kalila kama eneo linalopakana na kijiji cha Sijonga hawalitumii warekebishe mipaka ya gereza ili wananchi waendelee na kuendeleza ardhi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliona niongezee hayo kama niliyotangulia kueleza katika mchango wangu. Ahsante sana.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na viongozi watendaji wa Wizara hii kwa hotuba nzuri ya Bajeti ya mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, naomba kutoa masikitiko makubwa juu ya hali ya magereza na nyumba za Maofisa wa Magereza Wilaya ya Muheza. Kutokana na hali mbaya ya gereza la muda la Wilaya ya Muheza na ubovu wa nyumba za Maofisa wa Magereza Muheza, mwaka 2004/2005 nilimwomba Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi wakati huu Mheshimiwa Capt. John Chiligati, afike na kuona hali hiyo. Mheshimiwa Capt. John Chiligati alifika na alishuhudia yafuatayo:-

Kwanza ni kuhusu gereza dogo la muda la Wilaya ya Muheza. Gereza hilo ni dogo na ni la muda kwa maana kwamba Wilaya ya Muheza haina gereza la Wilaya hadi leo (2007).

Gereza hilo limejengwa kwa miti/fito na tope licha ya kupigwa plasta na rangi. Kutokana na udogo wa gereza, mahabusu wengi hulazimika kupelekwa gereza la Maweni, Tanga na hivyo kuongeza na kudumisha msongamano.

Pili ni kuhusu nyumba za maofisa wa magereza Muheza, zipo nyumba tatu za maofisa zilizojengwa kwa miti, fito na tope. Nyumba zimeezekwa kwa makuti na zinavuja! Hii ndio heshima wanayopewa wafanyakazi wa Serikali na ndio *standard* ya nyumba za Serikali katika karne hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu pendekezo la kufungwa kwa gereza hilo dogo la Wilaya ya Muheza. Kutokana na hali mbaya ya gereza na nyumba za maofisa wa gereza la Muheza ni vema Serikali ikafunga kituo hicho hadi hapo itakapopata uwezo wa kujenga gereza la Wilaya ya Muheza na nyumba za maofisa wa magereza.

Kuhusu haki za binadamu kuvunjwa, kuwaweka maofisa wa magereza kama wafanyakazi wa Serikali katika nyumba za miti, fito, tope na makuti yanayovuja huku wakilipa kodi za nyumba kama sheria inavyowabana ni sawa kabisa na kuvunja haki za binadamu za wafanyakazi halali wa Serikali!

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mpango wa ujenzi na ukarabati magereza, mabweni na nyumba za maofisa kwa mwaka 2007/2008, kwa kuwa hata katika Bajeti ya mwaka 2007/2008, kama pia ilivyokuwa mwaka 2005/2006, mwaka 2006/2007 hata baada ya Mheshimiwa Waziri katika Wizara husika kushuhudia niliyosema mwaka 2004/2005 na leo mwaka 2007/2008 na kwamba Muheza haipo kabisa katika mpango wowote ni dhahiri kwamba Wizara itatoa sasa idhini ya kufunga gereza lile dogo na nyumba mbovu za maofisa gereza la Muheza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maelezo yote naunga mkono hoja ili wafungwa na watendaji wa Wizara hii, Magereza na Idara ya Uhamiaji waweza kupata huduma muhimu kwa mwaka 2007/2008.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuwa na afya njema na kuniwezesha kuchangia Wizara hii.

Nachukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Mambo ya Ndani na Naibu Waziri pamoja na timu yake ya wataalamu kwa Bajeti yao yenye mwelekeo mzuri kwa utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Magereza ni mojawapo ya Idara muhimu katika Serikali yetu ina majukumu muhimu kwa jamii yetu, kwanza ina jukumu ya kumrekebisha raia anapofanya maovu anapopewa adhabu ya kufungwa gerezani na kuwa raia mwema anapotoka na kuwa mfano bora kwa wenzake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu msongamano wa mahabusu pamoja na wafungwa, hii inasababishwa na upungufu wa majengo na mahabusu wengi kuwekwa kwa muda mrefu bila kuhukumiwa na kusababisha kurundikana. Kwa hivyo, tunaiomba Serikali majengo yaliyokuwa hayajamalizika yamalizwe kujengwa na majengo yaongezewe mabweni na yaliyopo yafanyiwe ukarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uhamiaji, Serikali iwapatie vitendea kazi vya kisasa pamoja magari, pikipiki, vyombo vya mawasiliano na kadhalika ili wapate maendeleo kwa watumishi hao na vile vile waongezwe mshahara na posho kwani wanakabiliwa na kazi kubwa na nzito pamoja na kuongeza juhudi katika udhibiti wa uhamiaji haramu nchini, kama vile Warundi, Wanyarwanda, Wasomali na Wahindi, wengine nao ni wahalifu pia wanapambana nao, hawa waangaliwe pamoja na kujengewa nyumba zilizo bora za kuishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu magereza, hawa askari wa magereza wanafanya kazi katika mazingira magumu kwa hiyo, tunaiomba Serikali hawa wapatiwe vitendea kazi ukiwemo usafiri, boti, gari, pikipiki na vile vile maslahi yao yaongezwe kwani wafungwa waliomo gerezani, watu tofauti wakiwemo majambazi, wahalifu, wavuta bangi, wala unga na watu wenye tabia mbalimbali kwa hiyo, Serikali iwape kipaumbele askari hao kwa kuwajengea nyumba, askari hawa na nyumba zao zikarabatiwe wanazoishi hivi sasa. Nawatakia kheri na naunga mkono hoja.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kuleta hotuba yao ya Bajeti Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni mara yangu ya kwanza kuchangia Wizara hii katika msimu huu na naomba nijikite zaidi katika masuala ya utekelezaji kazi wa Wizara hasa katika mgogoro baina ya gereza la Namajani la Wizara hii na wananchi wa Kata ya Namajani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro huu ni wa siku nyingi kuanzia mwaka 1995 na mpaka leo haujapatikana muafaka kati ya taasisi hii na wananchi waliowakaribisha

magereza kuanzisha gereza la kilimo hapa. Mnamo mwaka 2004 aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Masasi aliamuru taasisi ya magereza ijipimie ardhi wanayotaka na kumlazimisha Afisa Ardhi atoe mawe ya Wizara ya Ardhi ili yasimikwe kwenye eneo walilojipimia. Eneo hili limekuwa kubwa zaidi ya lile walilokuwa wamepewa mwanzo na Serikali ya Kijiji cha Namajani. Ikumbukwe kuwa eneo la awali, magereza walipewa bure na kijiji na mipaka yake walionyeshwa bayana na halikuhusisha kitongoji cha Natepo, Kijiji cha Ngalole.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kujipimia eneo jipya kwa kumtumia *DC* wa Wilaya, bwana Ali Rufunga, magereza walijiongezea eneo kwa kutumia dola bila kibali cha wenye ardhi ambao ni wananchi na hivyo kuzua mgogoro huu ambao haujasuluhishwa mpaka leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro huu tayari umekwishapelekea uvunjaji wa amani kwani mwaka 2004, ulizuka ugomvi baina ya askari magereza na wananchi wa Ngalole, Namajani kuhusu mpaka waliojiwekea magereza na matokeo yake yalikuwa baadhi ya askari na wananchi kujeruhiwa. Wanakijiji 85 walipelekwa Mahakamani Masasi ambako walitozwa faini ya shilingi 425,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, toka hapo uhusiano baina ya magereza na wananchi wa Namajani ni mbaya sana *(delicate)* mpaka leo. Mkuu wa Mkoa wa Mtwara kwa barua yake yenye Kumb. Na. J.10/11/299 ya tarehe 20 Mei, 2006 kuhusu mgogoro huu alisema: "Napenda kukufahamisha kwamba uongozi wa Mkoa pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi tunachukua hatua mbalimbali kutafuta ufumbuzi wa mgogoro wa gereza la Namajani na wananchi wa Kitongoji cha Natepo, Kijiji cha Ngalole. Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi amekwisha agiza iundwe Tume ndogo ya kuchunguza undani na ukweli wa tatizo hilo. Wilaya imeagizwa na Mkoa kusitisha zoezi la kuwatoa wananchi wa kijiji cha Natope kwa nguvu mpaka hapo maamuzi ya mwisho yatakapotolewa." Ni wazi kwamba patakuwepo na mashauriano kati yaWizara, Mkoa na ngazi zote zinazohusika ili kufikia uamuzi wa haki na kwa kuzingatia maslahi ya pande zote husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume iliundwa chini ya Uenyekiti wa Meja Jenerali (Mstaafu) Rowland Makunda, ambaye alikwenda kiundani zaidi ili kufikia uamuzi wa haki kwa kuzingatia maslahi ya pande zote. Tume ilikamilisha kazi yake na kupeleka taarifa kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati na Mkuu wa Mkoa wa wakati huo Mheshimiwa Henry Shekiffu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kukabidhiwa ripoti ya Tume, Mheshimiwa Waziri aliomba muda aipembue kumbe katika kipindi hicho hicho akateuliwa kuwa Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Huo ulikuwa mwezi Oktoba, 2006. Bahati nzuri nami pia, kama mwakilishi wa wananchi wa Namajani, nililetewa nakala yangu ya ripoti ya Tume. Katika baadhi ya mapendekezo muhimu ya Tume, iliagizwa kuwa magereza warudi na kuheshimu mipaka ya awali kama walivyopewa na kijiji cha Namajani na sio kujitanua kuhusisha Kitongoji cha Natepo, Kijiji cha Ngalole.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliamini kwa uamuzi huu wa Tume ya Serikali, suala hili sasa lingekuwa limekwisha. Kwa bahati mbaya toka uongozi wa Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati kuondoka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, hakuna chochote kilichoendelea katika kuumaliza mgogoro huu. Nimejitahidi sana kuwasiliana na Mheshimiwa Waziri Mheshimiwa Joseph Mungai, bila mafanikio na uthibitisho upo wa hatua nilizochukua kuwasiliana naye bila mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Namajani nao wamechoshwa na dana dana hii na wameandika barua kwa Waziri Mkuu tarehe 2 Julai, 2007 kuhusu kunyang’anywa ardhi pamoja na mashamba yetu. Wamemwomba Waziri Mkuu aingilie kati mgogoro huu. Ili kutatua mgogoro huu natoa mapendekezo yafuatayo:-

Kwanza, mapendekezo yaliyotolewa na Tume ya Serikali ya Meja Jenerali (Mstaafu) Rowland Makunda yatekelezwe mara moja ili kuwezesha wananchi wa Ngalole kupata ardhi ya kulima katika msimu huu wa kulima unaoanza mwezi Oktoba, 2007.

Pili, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ipewe muda usiozidi msimu wa kilimo wa Oktoba, 2007 ili iwe imekamilisha uamuzi wa haki kwa kuzingatia maslahi ya pande husika. Endapo suala hili halitakamilika Oktoba, 2007, rufaa waliyokata wananchi kwa Waziri Mkuu kumuomba aingilie kati mgogoro huu nitaomba itekelezwe.

Tatu, Bunge kama msimamizi wa utekelezaji wa shughuli za Serikali nayo ichukue hatua mwezi Oktoba, 2007 kuingilia utendaji wa Wizara hii kuhusiana na suala hili. Hatua hii ichukuliwe kutekeleza jukumu lililopewa Bunge kusimamia utendaji Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaunga mkono hoja ya Wizara endapo Waziri atafafanua na kutoa ufumbuzi kwa mgogoro huu wa gereza Namajani na wananchi.

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nitoe pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa Wizara hii kwa hotuba nzuri yenye mpangalio safi na ufafanuzi mzuri wa malengo na mikakati ya Wizara katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, jimbo la Mbozi Magharibi liko kwenye mipaka ambayo hivi sasa ina maingiliano makubwa ya watu wa Mataifa mbalimbali hususan waendao na kutoka nchi zilizoko Kusini na Magharibi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli za watu hawa pia ni za aina mbalimbali. Halali na zisizo halali kama inavyodhihirishwa na matukio mbalimbali ya ujambazi, uvushaji wa bidhaa kinyume cha taratibu kama dawa ya kulevya na uhamiaji haramu. Mpaka huu wa nchi yetu na Zambia wenye urefu usiopungua kilometa 120 kwa sasa

unavuja (uko *porous)* kwa uvushaji wa bidhaa za wahamiaji haramu kama ilivyo kwa maeneo ya mipaka mingine kama Horohoro, Holili, Namanga, Sirari na Kisumulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu kubwa ni uchache wa watumishi wa Idara ya Uhamiaji, vitendea kazi vichache na duni au kutokuwepo kabisa vitendea kazi, elimu ndogo na mbinu hafifu za kukabiliana na wahalifu kwa mfano ukosefu wa vifaa vya kudungua wavushaji wa dawa za kulevya mpakani pia watumishi wa Idara ya Uhamiaji kukaa mahali pamoja muda mrefu suala linalosababisha baadhi ya watumishi hao kuanza kushirikiana na wahalifu katika kuvunja sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya wananchi wa Jimbo langu hasa pale Tunduma ni kuongezewa uwezo wa kukabiliana na wimbi la uhalifu wa mpakani kwa kupatiwa usafiri – gari na pikipiki za kufanyia doria kwenye mpaka huu wenye urefu wa zaidi ya kilometa 120. Hii itawezesha watumishi wa uhamiaji kwa kushirikiana na askari polisi kuzungukia mpaka ule na kuhakikisha hakuna uvunja wa sheria. Pia kwa sasa wananchi wenyewe wameanza kuchangia ununuzi wa pikipiki kwa kushirikiana na Mbunge wao hivyo basi Serikali iwape nguvu kwa kusaidia zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuimarisha rasilimali watu kwa kuongeza idadi ya watumishi kwa kuwapeleka mafunzoni watumishi hao ili wapate elimu na mbinu za kupambana na wahalifu, kuwanunulia watumishi vifaa vya utambuzi wa bidhaa haramu kwa mfano dawa za kulevya na kuwahamisha watumishi wa uhamiaji kila baada ya miaka mitatu au minne ili wasizoeana na wahalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Waziri Mheshimiwa Joseph Mungai, Naibu Waziri Mheshimiwa Lawrence Masha, kwa hotuba yake nzuri na bunifu ambayo ninaunga mkono hoja asilimia mia moja. Pia ninawapongeza wataalamu husika kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mpango mzuri na bunifu ulioainishwa katika Bajeti hii lakini sikuona chochte kilichozungumzwa kwa gereza la Kilimo, Liwale ambalo lina miaka zaidi ya 25 tangu lianze na lina matatizo kibao. Gereza hili halina umeme, linahitaji kiasi cha shilingi 74,822,618 kufikisha umeme kwenye gereza hilo ili lijikwamue kutoka kwenye giza.

Mheshimiwa Naibu Spika, gereza la kilimo la Liesale linahitaji kuboreshwa hata kama kwa mpangilio wa awamu kwa awamu. Hivi sasa gereza halina maji salama, hasa wakati wa kiangazi mto na visima hukauka. Hawana usafiri wa uhakika, *KIA* mbovu kabisa haitumiki wameazimwa *Isuzu* ambalo ni bovu, linahitaji matengenezo makubwa. Gereza halina ofisi iliyopo imejengwa kwa miti na kukandwika kwa matope. Wafungwa na mahabusu hawana *mess* wala vyoo vya nje ya maselo. Mapungufu haya yote yanaathiri sana ufanisi wa shughuli za magereza hata kama mkuu wa magereza akiwa mbunifu.

Napendekeza Serikali ifuatilie kwa karibu mapungufu hayo ili kuboresha gereza hilo hasa kwa kutilia maanani sehemu kubwa ya Wilaya ya Liwale ni Selous yenye wanyamapori wakali ambao ni tishio kwa usalama wa askari magereza, wafungwa na hata mazao yanayolimwa na gereza hilo. Ni muhimu kwa gereza hilo kupatiwa usafiri *Land Rover 110* au *Land Cruiser* kwani barabara ni mbaya na Liwale ni eneo la mchanga mwingi hivyo gari linalofaa ni lenye *four wheel drive.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Gereza la Liwale limezungukwa na mashamba ya korosho ya wananchi ambao hadi leo wanaendelea na kudai fidia. Ninaomba Serikali kuwaeleza wananchi lini fidia ya mashamba hayo italipwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nikitembelea gereza la Liwale kila ninapokuwa Jimboni kwangu na nitaendelea kufanya hivyo, naomba Serikali iniunge mkono kwa kurekebisha mapungufu niliyoyaona ili kuboresha gereza hilo na maisha ya askari magereza ambao pia hawana nyumba bora za kuishi.

**MHE. KHADIJA SALUM AL-QASSMY:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia leo hii nikawa mzima na nikaweza kuchangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili napenda kukupongeza wewe kwa jinsi unavyoliongoza Bunge letu hili Tukufu kwa ujasiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia katika Idara hii ya Magereza kuhusu kurundikana kwa mahabusu ndani ya magereza kiasi kwamba hali inatisha, naiomba Serikali pamoja na kuboresha zaidi kwani hali ya magereza mengi yanalalamikiwa kuwa ni mabovu, hakuna hali ya kufurahisha, chakula hakiridhishi na hata mazingira ya ndani yanahatarisha maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nijielekeze kwenye Idara ya Zimamoto, sekta hii ni muhimu sana hasa ukizingatia inawahusu sana wananchi na mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ijitahidi kununua magari ya zimamoto kwani ni hivi karibuni tu kulitokea maafa makubwa katika mkoa wa Singida na watu walipoteza maisha yao kwa kukosa magari na vifaa vya zimamoto. Kwa hiyo, watu wengi waliungua katika basi la *Mohamed Trans* bila ya kuokolewa maanini kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu na kama kungekuwa na vifaa vya kutosha basi watu japo kidogo wangeokoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumaliza naomba kuchangia kuhusu vitambulisho. Kwa kweli katika nchi yetu kuna wimbi kubwa la ujambazi kutokana na watu kutotambuliwa uraia wao na kuingia katika nchi kiholela.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali suala hili ilishughulikie kwa nguvu zake zote ili lifikiwe muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwa Waziri na Naibu Waziri wake na watendaji wake wote. Ahsante.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Joseph Mungai, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Lawrence K. Masha. Nawapongeza sana watendaji wote wa Wizara na Katibu Mkuu wa Wizara. Pia nampongeza sana Ndugu Kilomano, Mkurugenzi wa Uhamiaji kwa kazi nzuri anayofanya katika uhamiaji.

Mchango wangu uko sehemu tatu, kwanza ni kuhusu ucheleweshaji wa kesi mahabusu, pili ni utoaji holela wa *passport* kwa wauza unga (dawa za kulevya) na tatu ni magereza yatumike kuboresha uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu spika, mimi ninashangaa sana kuhusu ucheleweshaji wa kesi kwa mahabusu kwani unapocheleweshа kesi ni kama umeshahukumu. Kibaya zaidi mahabusu anakaa miaka nane bila hukumu kisha anaonekana hana hatia. Hivyo, kwa vile tatizo ilikuwa hana kosa basi inabidi walipwe fidia na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kama zile hukumu za kifo kuna idadi kubwa ya wafungwa wamehukumiwa kunyongwa na Majaji lakini Mheshimiwa Rais amekuwa siyo mwepesi wa kusaini hukumu hizo, je, msimamo wa Serikali ukoje juu ya hukumu ya kifo? Kama Mkuu wa nchi huwa siyo rahisi kusaini adhabu za kifo, ningashauri Serikali ikiwekekana kufuta adhabu hiyo ya kifo badala yake kuwa na kifungo cha maisha ili wazalishe ili kuongeza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wimbi la dawa za kulevya linatokana na kutokudhibiti nyaraka *(documents)* za kusafiria ikiwa ni pamoja na utoaji holela wa *passport.* Nashauri kuwa na umakini sana katika utoaji wa *passport* kwani kuna raia wasio waaminifu wana *passport* za nchi moja na majina tofauti. Hivyo watumishi wasio waaminifu basi wakitoa *passport* kinyume cha taratibu basi wafukuzwe kazi au wapewe adhabu kali.

Nashauri magereza yetu yawe kiuchumi zaidi kuliko ilivyo sasa kuwa ni sehemu ya mateso na kubadilisha tabia.

Mheshimiwa Naibu spika, mwisho naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. MKIWA ADAM KIMWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, siku za hivi karibuni kumekuwepo na matokeo mengi sana ya moto. Sababu kadhaa zimekuwa zinatolewa zinazosababisha majanga ya moto katika makazi ya watu. Ikiwa ni pamoja na hitilafu za umeme, uzembe na hujuma za makusudi. Kwa muda mrefu saa Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wanalalamika kuhusu utendaji wa vikosi vya zimamoto. Utendaji wa Idara ya Zimamoto umekuwa ni wa kusuasua kutokana na uchache wa magari ya kuzima moto hasa katika Makao Makuu ya Wilaya za nchi. Aidha, uchache wa mafunzo wanayopatiwa vikosi vya zimamoto na uokoaji inaathiri kwa kiasi kikubwa utendaji na ufanisi katika vikosi hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapana budi Serikali ichukue hatua za makusudi kuviimarisha vikosi vya zimamaoto na uokoaji kwa kuvipatia zana na vifaa mbalimbali yakiwemo magari ya zimamoto pamoja na mafunzo ya kisasa yatakayoweza kukabiliana na majanga ya moto nchini, Serikali ihakikishe kwamba Miji Mikuu, Makao Makuu ya Wilaya pamoja na sehemu muhimu na nyeti wapatiwe magari ya kuzimia moto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uhamiaji, ulimwengu unabadilika na teknolojia duniani inakuwa. Kutokana na hali hiyo uharamia wa kuchapisha *passport* bandia umekuwa unaongezeka. Hali hii ilisababisha hatua za kudhibiti waingiaji haramu nchini iwe ngumu. Serikali katika miaka ya hivi karibuni imechukua hatua ya kubadilisha *passport* na kutoa *passport* mpya. Taarifa tuliyonayo ni kwamba *passport* hizi mpya utaalamu mkubwa umetumika kuzitengeneza kiasi ambacho inakuwa vigumu kuzikopi ( kutengeneza za bandia).

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi napata mashaka iwapo ni kweli *passport* zetu haziwezi kurudufiwa kwa sababu tumekuwa tunasikia mara kadhaa zimekamatwa noti za bandia za Marekeni (dola) za bandia, ilhali tukijua wazi kwamba teknolojia inayotumika kutengeneza fedha za Marekani ni kubwa mno lakini bado wapo watu wenye uwezo wa kuzirudufu.

Naomba Mheshimiwa Waziri anithibitishie hivi ni kweli *passport* zetu siyo rahisi kurudufiwa? Na ni hatua gani ambazo Serikali inachukua kudhibiti pasi zetu zisitumike ovyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo yanayosonga mbele ya dunia pamoja na kukua kwa utandawazi suala la mtu kuwa raia wa nchi mbili ni la kawaida, nchi kadhaa zimekuwa zinaruhusu mfumo huu, mfumo ambao umeonekana unawapa fursa wananchi wao na kadhalika kuongeza Pato la Taifa. Labda kusuasua kwa nchi yetu kubadilika na kutumia mfumo huu wa *dual citizenship* ni kutokana na hofu kwamba utaathiri mifumo ya kisiasa na kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sioni sababu ya kuwa na hofu hivyo nchi kadhaa za Afrika zimefaidika na mfumo huu na hatuoni athari zozote katika mifumo ya kisiasa na kijamii. Ni vema basi Mheshimiwa Waziri aeleze Bunge lako Tukufu ni lini Serikali itaruhusu mfumo huu wa *dual citizenship,* na kama Serikali haijawa tayari itueleze ni sababu zipi zinazokwaza kuchukua hatua hizo?

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri na watendaji wake wote kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu msongamano magerezani, wanaougua kansa. Wizara inawagharamia kwa matibabu kwa kuwapeleka *Ocean Road Hospital* na kwa chakula. Wafungwa hawa si *productive* na hivyo hakuna mantiki ya kuwaweka magerezani kuongeza msongamano. Aidha, wale wanaugua UKIMWI *(HIV/AIDS)* wangekuwa miongoni mwa wale wanaopaswa kuwa nje ya magereza kupunguza msongamano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vitambulisho vya Utanzania, jambo hili limeachwa kwa muda mrefu kiasi kwamba sasa huwezi kumtambua nani Mtanzania halisi lakini baya zaidi katika mikoa ya mipakani wageni wamekuwa wengi zaidi na kuanza kushika nafasi za uongozi. Si ajabu hata Bunge hili Tukufu likapata Wabunge wasio Watanzania hapo baadaye. Naiomba Wizara iwe na uangalifu mkubwa wakati wa kutoa vitambulisho ili kuwabaini wale wasio Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu zimamoto, kazi za zimamoto bado ni duni kwa upande wa vifaa. Ni aibu kuwa hadi leo baadhi ya Wilaya haina gari la zimamoto. Suala la zimamoto lipewe uzito mkubwa ili yatokeapo majanga Serikali isiingie katika aibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu elimu kwa wafungwa, wafungwa ni binadamu na wana haki ya msingi ya kujua maendeleo ya matokeo mbalimbali nchi kwa kuwapatia magazeti na *TV*. Ni kitendo cha aibu leo kusikia wafungwa hapa Dodoma kumuandikia barua marehemu Amina Chifupa, awatetee Bungeni, ni dhahiri hawajui kinachoendelea nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kupunguza magereza, kinga ni bora kuliko tiba, kuongeza idadi ya magereza maana yake ni kukubali ongezeko la wafungwa, hili halitufikishi mwisho. Ili kupunguza idadi ya magereza nchini hatuna budi kuimarisha taaluma kwa jamii na kuboresha hali ya maisha.

**MHE. JANET B. KAHAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri Joseph Mungai kwa jukumu la kuiongoza Wizara hii. Napenda pia kumpongeza Naibu Waziri Lawrence Masha akisaidiana na Katibu Mkuu, wataalamu wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupongeza magereza kwa bidii zao katika kilimo, kilimo ni uti wa mgongo. Kwa miaka mingi magereza wamekuwa katika kilimo cha mahindi, mboga na kadhalika ushauri wangu kwa magereza wangeweza kupanua zaidi eneo la kilimo wakizingatia pia kilimo cha mazao ya biashara kama korosho, kahawa na kadhalika na mazao mengineyo yakiwemo ndizi, matunda, mahindi na kadhalika kwa ajili ya biashara ya hapa ndani ya nchi na nje ya nchi *(export).* Kilimo ndani ya magereza kitapata nguvu kazi zaidi toka kwa wafungwa wenyewe. Aidha, wataalamu wa kilimo watumike zaidi katika kuzalisha kilimo cha maua pia kingefaa kifikiriwe na magereza ili kuwawezesha kuwapatia kipato ili waweze kujitegemea na kuleta maisha bora kwa wafungwa na wananchi kwa ujumla. Kilimo kiwe cha kisasa kuzingatia vifaa *(machinery)* na vitendea kazi vya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, magereza wamefanikiwa sana katika kutengeneza samani *(furniture)* nzuri sana, kwa bahati mbaya soko ni dogo. Iwapo Wizara hii ingetilia mkazo kwa kutenga fungu la kutosha katika kuendeleza mradi huu ukakua zaidi katika mikoa yote. Samani zinazotengenezwa hapa nchini zinahitaji ufanisi mzuri na *good finishing* kwa kiwango cha juu kabisa ili kulishinda soko la samani na kutoka nje ya nchi pamoja na uamuzi wa Wizara ya Maliasili na Utalii kutoendelea kutotuma magogo nje ya nchi, ni wakati muafaka sasa kuhakikisha magereza wanatumia nafasi hii kutengeneza

samani nzuri kushindana na soko la samani zinazoletwa nchini kwetu toka nchi za nje. Aidha, Wizara itafute wawekezaji na kuwa na ubia nao ili wafanikishe hatua hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uhamiaji, uraia wa nchi mbili *(Dual Citizenship)* ni muhimu katika nchi yetu kwani kuna nchi nyingi pia duniani ambazo zina uraia wa nchi mbili. Tukizingatia kuwa nchi yetu ina Watanzania wengi nje ya nchi ambao wamefuata kazi na maisha bora ili waweze kurudi nyumbani Tanzania na kuwekeza au kusaidia familizo zao, ni vema tukafikiria basi kukubaliana na wazo la kuruhusu *dual citizenship* kuanza haraka. Wananchi wengi wanakwama na wana woga wa kurudi hapa nchini kutokana na kuona huenda wakashindwa kuhamisha mali zao au kutokana na kutorudi katika makazi yao ya muda ya nje. Ni bora basi tukafikiria jambo hili ili kuwawezesha wenzetu walete maendeleo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu zimamoto, Jeshi la Zimamoto na uokoaji wa maisha ya binadamu na pia vifaa mbalimbali. Eneo hili lingetiliwa mkazo katika kila mikoa na Wilaya, inabidi kufikiria kuunda vizuri kikosi hiki na kuweka *budget* ya kutosha ijayo ili kuwezesha kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, uokoaji wa majini, moto na kadhalika ni kitu cha kutiliwa mkazo sana hasa katika kipindi hiki matukio kama haya yanatosha mara kwa mara. Aidha, vituo vya magereza vilivyopo karibu na barabara kuu za kwenda mikoani, ni muhimu kuwe na vituo vya magereza vilivyo karibu na magereza ili vituo hivyo viweze kuhakikisha kuwa wanatoa huduma, kwa watu wanapopata ajali. Vifaa vya uokaoji katika maji kama maziwa, mitoni, baharini ni lazima na viwe vya kisasa ili kuokoa maisha ya watu wengi kwa mfano *MV Bukoba*, maisha ya watu yangeweza kuokolewa na bila kupoteza maisha ya watu wengi. Kwa hiyo, miji iliyo kandokando na maziwa na kadhalika iwe na magereza yenye vitengo maalumu vya uokoaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuiru Mwenyezi Mungu kwa kujalia uzima wa afya njema na kuhudhuria kikao cha leo. Napenda kukupongeza wewe Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge pamoja na uongozi wa Kambi ya Upinzani kwa kutuongoza vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kuna wageni mbalimbali wanaoingia nchini bila kufuata taratibu zinazotakiwa na kwa kuwa baadhi ya wageni hao hushiriki katika vitendo vya uharifu, naiomba Serikali iharakishe upatikanaji wa vitambulisho vya Kitaifa ili wageni wote wanaoingia nchini kinyume cha sheria waweze kukamatwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ulinzi unahitajika kuimarishwa zaidi katika maeneo ya mipakani na sehemu nyingine muhimu kama vile mabenki na kadhalika. Hii ni pamoja na kuwapatia walinzi wetu vitendea kazi vya kisasa ikiwa ni pamoja na nguo zinazozuia risasi kupenye *(bullet proof)* ili waweze kukabiliana na vitendo vya ujambazi na uhalifu mwingine kwa uhakika na umakini zaidi kuliko ilivyo hivi sasa ambapo walinzi wetu wamekuwa wakipoteza maisha katika matukio mbalimbali yaliyotokea hivi karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wananchi wanaokamatwa na kuwekwa rumande bila ya kuambiwa makosa yao, hubambikizwa kesi na kuwekwa rumande kwa muda mrefu wakiwa katika msongamano mkubwa. Kwa hivyo, mahabusu hawa huanza kuadhibiwa kabla ya kuhukumiwa, ni vema Serikali ikaliangalia hili kwa makini ili wasiokuwa na hatia wasiadhibiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, zimamoto ni idara ambayo ina jukumu la kuokoa maisha ya watu na mali zao endepo janga lolote la moto litatokea, hivyo ni vema idara hii ikapatiwa vitendea kazi vya kutosha ikiwa ni pamoja na magari. Hii itasaidia watendaji kufika katika eneo la janga kwa haraka zaidi kuliko ilivyo hivi sasa ambapo maisha ya watu na mali zao hupotea kwa sababu idara hii haina vitendea kazi vya kutosha. Kuna mrundikano mkubwa wa wafungwa katika magereza mbalimbali hapa nchini jambo ambalo ni hatari kwa usalama na afya za wafungwa pamoja na askari wanaolinda wafungwa hao. Kwa hivyo, ni vyema idara ya magereza kupatiwa majengo ya kutosha pamoja na vitendea kazi muhimu, pia maslahi yao yanapaswa kuangaliwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ukiukwaji wa haki za binadamu katika baadhi za magereza hapa nchini, suala hili linapaswa kuangaliwa kwa makini. Ahsante.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuchangia kwa kuzungumza kwa sababu Wizara hii. Katika mkoa wangu una matatizo naomba nijibiwe, naomba sana nielewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza na magereza, hivi Wizara pamoja na Serikali Magereza ya Mkoa wa Kagera wanakumbukwa? Kweli maisha yao pamoja na kazi ngumu ya kulinda wafungwa wenye kila mmoja au akili yake na matatizo yake. Kwanza majengo, pili usafiri, pa kulala, kweli tunaridhika nao hasa yale maghorofa ya Bukoba Mjini wanavyolala.

Pamoja na familia zao kimetengwa chumba na sebule kila askari anachukua chumba kimoja kimoja. Je, kweli hiyo ni haki? Watoto wao hawatakuwa na malezi mazuri. Hata Serikali imeshindwa kukarabati maeneo ya Kitengure, Ngurutunga, Rwanlumba, Kayanga, Biharamulo hizi zote nilizozitaja zinatia aibu kwa Wizara pamoja na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majibu na mimi pamoja na wananchi kutoka Wizarani na naomba magari angalau moja moja kupeleka wafungwa hospitali pamoja na mashambani kuliko askari kutembea nao kwa mguu mwisho wamdhuru au kutoroka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakwenda kwenye mipaka, sasa hii ndio basi matatizo yanayojulikana Ngara, Kigoma na Karagwe. Hii mipaka mibaya sana, naomba niambiwe imewekwa mikakati gani? Kulikuwa na huruma kupokea wakimbizi, sasa imeshakuwa msalaba na ni mMatatizo makubwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine naomba nieleweshwe kuhusu gari la zimamoto ni la mtu au ofisi ya mtu binafsi au ni la manispaa. Naomba majibu je, ni lini idara ya zimamoto Bukoba itakuwa na ofisi yao kuliko kudandia ofisi na hili nipatiwe majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakwenda kwenye uraia. Kulingana na muingiliano wa mipaka yetu, je, Wizara pamoja na Serikali ina mikakati gani pamoja na suala la vitambulisho limeishia wapi, naomba majibu, lazima tuwe makini na nchi yetu. Naomba yote niyachangie kwa maandishi, naomba sana kwani yananiumiza sana ukilinganishia na kuchangia kwa maandishi hatujibiwi vizuri sana, naomba angalau kidogo ufafanuzi wa kuridhisha. Ahsanteni na naomba kuwasilisha.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Joseph Mungai kwa kuwasilisha vizuri Bajeti ya Wizara yake. Pia napenda kumpongeza Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Lawrence Masha, kwa kuwajibika vizuri na shughuli za kila siku za Wizara yake. Aidha, nawapongeza watendaji wakuu wa Wizara na wafanyakazi wote kwa kutimiza majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mchango ufuatao:-

Mosi, Wilaya ya Tandahimba hivi karibuni imepata *OCD* wa kwanza tangu kuanzishwa kwa Wilaya hiyo, napongeza sana hatua hiyo. Hata hivyo naiomba Wizara sasa kuhakikisha inaipatia fedha idara hiyo ili iweze kuwa na jengo lake lenyewe kwani kiwanja kilichopatikana na kutengwa kwa ajili ya ofisi ya polisi Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, siku za nyuma katika kijiji cha Mbuyuni Chiumo, Jeshi la Magereza lilichukua eneo kwa ajili ya kilimo. Shughuli hizo kwa sasa zimesimama, hakuna kinachoendelea. Ningependa kupata maelezo kuhusu mpango wa Jeshi la Magereza kuendeleza eneo hilo. Kama jeshi hilo halina mpango, basi eneo lile warudishe kwa wananchi ili waendeleze kilimo badala ya kuachwa kama lilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili lilipitisha Azimio la Kufuta Viza kati ya Tanzania na Msumbiji, lakini baadhi ya wananchi wa jimboni kwangu wamekuwa wakilalamikia kuwepo kwa mwendelezo wa viza hadi sasa kule mpakani. Ombi langu ni kuwa Wizara ya Mambo ya Ndani ichukue hatua ili kudhibiti vitendo hivyo kule mipakani.

Mheshimia Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuipongeza Wizara kwa hatua iliyochukua kwa kuwapandisha vyeo watumishi wa Idara ya Uhamiaji kwa mserereko baada ya kukwama katika vyeo walivyokuwa navyo hapo awali kwa muda mrefu.

Aidha, naiomba Wizara hii kupitia kwako Mheshimiwa Naibu Spika, na Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani kuwaangalia pia wale watumishi ambao nao wanastahili

kupatiwa vyeo/kupandishwa vyeo baada ya kumaliza mitihani ya kupandishwa vyeo. Kwa kuwa wamekaa muda mrefu uliopita kwa njia ya msererekо kwa kadri wanavyostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara pia iwe na utamaduni wa kusamehe watumishi ambao hapo nyuma walikuwa wakifanya vibaya kazini kwani kuwadhamiria kufanya vibaya. Hii ina maana ya kutoshikilia tabia ya mtumishi mbaya isiyofutika ingawa matumishi huyo ameonyesha kujisafisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tabia hii imejengeka sana kwa Idara ya Uhamiaji hasa kwa watumishi wa kike. Tujali kazi pasipo kujali madhara binafsi kupeleka tabia ya kutojali ubinadamu na ushauri wa wakuu wa kazi na wanaolalamika binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Tume ya viongozi, naipongeza Wizara kwa kukamilisha mapendekezo ya kuruhusu uraia wa nchi mbili *(dual citizenship)* pamoja na maendeleo ya mradi wa vitambulisho kwa haraka sana ikiwa ni pamoja na ujenzi wa nyumba za kuishi, hoteli za utalii, ongezeko la watu pamoja na ujenzi wa viwanja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ukweli huo naiomba Wizara kuweka mkakati wa kujenga kituo kimoja kikubwa cha zimamoto kwa mwaka ujao wa fedha ili kwenda sambamba na ukuaji wa Mji na kuhakikishia wananchi usalama kwa janga la moto likitokea; na kwa kuwa hivi sasa kuna viwanja vya kutosha chini ya mpango wa viwanja 20,000 Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahi kupokea malalamiko ya wananchi wa Kinabiji kukatwa miembe yao na Jeshi la Magereza. Nashauri uongozi wa Jeshi hilo kufuatilia malalamiko hayo. Aidha, suala la fidia nalo lilijitokeza na kama magereza watalipwa fidia kwa wenye maeneo yao, naomba hilo lizingatiwe na walipwe kwa umuhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. RITA L. MLAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nawapongeza sana Waziri Mheshimiwa Joseph Mungai na Naibu Waziri Mheshimiwa Lawrence Masha, kwa Bajeti yao nzuri na kazi nzuri wanayoifanya. Ninapenda kuwaambia kuwa huduma ya utoaji wa *passport* imeboreshwa vizuri sana. Pongezi pia ziwafikie watendaji wa Wizara yenu wote kwa kazi nzuri.

Napenda kuchangia kuhusu *dual citizenship*. Nashauri juhudi za kuhakikisha nchi yetu inakubali kuwepo na *dual citizenship* ziongozwe. Tukiwaruhusu watu wawe na *dual citizenship* tutawapata Watanzania wengi waliozaliwa nje au wanaoishi nje kuweza kurudi nyumbani kufanya kazi na kuwekeza katika biashara na hatimaye kukuza uchumi.

Pia tutawavutia wageni wanaopenda kuwekeza waje nchini kwetu. Tatizo linalowakabili wawekezaji wengi ni kutoruhusiwa kumiliki ardhi wakiwa wageni. Taratibu za utoaji wa uraia huo (*dual citizenship)* ziwe makini ili tusipate watu

wabaya watakaoharibu nchi. Nina hakika mnao wataalamu wazuri watakaofuata mwongozo mzuri wa hilo suala nzima kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache, napenda kuunga mkono hoja hii.

**MHE. TEDDY L. KASELLA -BANTU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Bila kuchelewa nampongeza sana Mheshimiwa Joseph Mungai, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa hotuba yake nzuri, na naiunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hasa mradi wa vitambulisho vya raia wa Tanzania. Tunakwenda au tuko kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki, nchi zingine kama Kenya wana vitambulisho, sisi bado ambapo Mheshimiwa Waziri amesema katika hotuba yake, njia nzuri ya kutoa vitambulisho ni ya kuwa *smart card* ambayo wakala atachaguliwa na kazi hii itakamilika Desemba, 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina shida na wakala ila nina tatizo la muda. Naona hadi mwaka 2009 ni mbali mno. Hasa ikizingatia kwamba sasa Burundi na Rwanda wanajiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hivyo wao wana vitambulisho, sisi hatuna, na jinsi tulivyo wapole, hatutajulikana kama sisi ni Watanzania. Tutachanganyika na pia tunaweza kupoteza haki zetu kama raia wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitambulisho ni muhimu na ninaomba na kushauri vipatikane mapema iwezekanavyo kama mwaka 2008 viwe tayari.

Mheshimiwa Naibu Spika, askari au Maafisa wa Uhamiaji kupewa vitendea kazi ili waweze kufanya kazi ipasavyo mikapani hasa kama usafiri ili kukabili wahamiaji haramu; ambao wengi wanaingia na silaha na kutumia silaha hizo vibaya. Kwa misingi hiyo tutapunguza sana uhalifu wa kutumia silaha hasa wanaotoka Pakistani/Ethiopia ambako ndiko kunaaminika kwamba kuna magaidi (wanafanya ugaidi).

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna adhabu kubwa sana inayotolewa kwa askari magereza wakati mfungwa anapotoroka chini ya ulinzi wa askari magereza. Ikitokea mfungwa ametoroka, askari magereza anakatwa robo ya mshahara wake, na pengine uhamisho na uhamisho huo, hapewi posho *(Transfer Allowance).* Naomba adhabu hii ipunguzwe na huwa zinapelekwa wapi? Naomba adhabu iwepo lakini isiguse mshahara wa askari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Askari wengine hawapati *promotion* kwa zaidi ya miaka mitatu kama ilivyo utaratibu. *Promotion* ni muhimu na ni motisha kwa askari magereza na kwa kila mfanyakazi. Kwa misingi hiyo, naomba wapewe *promotion* ili kuongeza tija na motisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahi kwamba zimamoto zitafika hadi Wilayani. Hongera sana, zinapopangwa basi naomba nami kwenye Jimbo langu ni kubwa na lina haki kama Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi zimwendee Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanazozifanya pamoja na ufinyu wa bajeti.

Aidha, pongezi za pakee ziende kwa Jeshi la Magereza *Brigade* ya Ujenzi kwa kazi nzuri za miradi ya ujenzi wa nyumba wanazozifanya. Nashauri wazidishe juhudi katika kuzingatia ubora (*quality*) ya kazi zao ili kujiwekea katika nafasi nzuri zaidi ya kuwa wakandarasi wenye daraja la juu nchini ambapo Serikali haitalazimika kutafuta wakandarasi wa nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu ni kama ifuatavyo:-

Moja, kuna wahamiaji haramu wengi zaidi nchini ikiwemo Zanzibar, Serikali kupitia Idara yake ya Uhamiaji iongeze juhudi za kuwadhibiti wahamiaji hao kwa kuwashirikisha wananchi ambao ndio wanaoishi nao.

Pili, kuna baadhi ya Watanzania walioukana uraia wao na kuwa raia wa nchi zingine, lakini bado wanaendelea kuishi nchini. Serikali ina mpango gani wa kuwachukuliwa hatua watu hao.

Tatu, ili kuboresha ufanisi wa Idara ya Uhamiaji, Idara hiyo ibadilishwe kuwa Mamlaka ya Uhamiaji .

Nne, elimu itolewe kwa jamii namna ya kuwatambua wakimbizi na wahamiaji haramu na namna ya kutoa taarifa zao kwa mamlaka husika ili kuirahisishia kazi Idara ya Uhamiaji kufuatilia.

Tano, ili kuboresha ukulima wa kisasa kwenye magereza, Wizara itenge fedha kwa ajili ya kununua matrekta na vifaa vyote kwa ajili ya kilimo baada ya kuendelea na kilimo cha mkono kinachofanywa na wafungwa (wanafunzi wa magereza)

Sita, nyumba za Askari Magereza ni ndogo, kongwe na chakavu, Wizara ichukue hatua za kuzipanua na kuzifanyia matengenezo ya mara kwa mara.

Saba, Ofisi za Idara ya Uhamiaji zilizopo mipakani mwa nchi ziimarishwe na ziboreshwe zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kutoa rambirambi zangu za dhati kwa familia za marehemu wote waliopoteza maisha yao kwa kipindi chote cha kuanzia mwezi Januari tulipompoteza Mbunge mwenzetu aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

Aidha, nitoe rambirambi zangu za dhati kabisa kwa aliyekuwa Mbunge Viti Maalum Vijana Taifa. Mungu aziweke roho za marehemu hao mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwapongeze Mawaziri wote wawili kwa hotuba yao nzuri waliyowasilisha hapa Bungeni leo. Pamoja na wataalamu wote katika Wizara hii kwa kufanikisha majukumu yote katika Wizara hii kwa ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi zangu naomba nianze na suala la uhaba wa magereza Mkoa wa Manyara unaoongoza kwa kuwa na Gereza moja ambalo linahudumia Mkoa mzima. Kwa kweli imekuwa vigumu sana kwa wananchi wa Wilaya ya Simanjiro, Kiteto, Hanang na Mbulu za Mkoa wa Manyara; kutoka Simanjiro kwenda Babati ni kilomita 400. Kwa nini lisijengwe gereza katika kila Wilaya? Ukianzia na Wilaya ya Simanjiro ambapo wananchi wanateseka? Watu wengi wanaopata kesi wanashindwa kufuatilia kwa umbali hata kwa gharama. Gereza kwa Wilaya ya Simanjiro ni muhimu. Tunapoteza mapato mengi. Mara nyingi wafungwa wanatoroka kwa kuwa wanaweza kucheleweshwa kituoni huku wakingojea usafiri wa kwenda Manyara.

Je, Serikali inasema nini kuhusu gereza la Wilaya ya Simanjiro? Watampa ushirikiano kwa kuwa bado watanzania tuko nyuma sana na tunadanganywa na vitu vidogo vidogo tunaiuza nchi bila kujua. Naomba sana wekeni ulinzi wa kutosha kabisa katika viwanja vya ndege. Msifikiri watu haramu ni Wasomali tu na watu weusi ni majambazi hata wazungu siyo wema kwetu imarisheni ulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa Simanjiro katika machimbo ya madini. Wapo wahamiaji haramu wengi wanaojiita Wajaluo wa Tarime. Naomba Wizara hii ifuatilie kuhusu watu hawa kwa sababu wapo Wakenya wengi wanaojihusisha na biashara ya madini wanajiita Wajaluo wa Taime. Naomba sehemu zote zinazochimbwa madini Tanzania ulinzi na ukaguzi wa mara kwa mara uimarishwe hata kwenye migodi ya dhahabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja hii.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuishukuru na kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri ya utekelezaji wa kazi zote za kila siku. Mchango wangu utahusu:-

Moja, magereza ya kilimo Wilaya ya Kilombero. Mkoa wa Morogoro Kitaifa umepewa jukumu la kuzalisha chakula cha ziada kwa niaba ya Taifa nzima yaani

*National Granary*. Katika Wilaya yangu kuna magereza mawili ya kilimo yaani Gereza la Kiberege na Gereza la Idete.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Rais alipotoa wito wa Mkoa huu kuingia katika kuzalisha chakula kwa wingi, magereza hayo pia yanahusika na wito huo wa Mheshimiwa Rais na ni budi wajipange katika kutekeleza azma hii. Mimi kama Mbunge wa Wilaya hiyo, nafahamu kuwa magereza hayo yanahodhi ardhi kubwa kuliko wanavyoweza kuitumia. Ili kuiweka ardhi yote katika matumizi ya kilimo napendekeza mambo yafuatayo ambayo naomba Waziri katika majumuisho yake ayatolee maelezo.

Moja, kuingia ubia na wananchi wanaozunguka mashamba hayo ili ardhi yote iweze kulima kwa mtindo wa *lease* ama ya kurudia kila mwaka *(annually renewable)* na *lease* ya muda wa kati wa miaka mitatu au mitano. *Lease* hiyo ni kwa kilimo cha mazao yasiyo ya kudumu. Pili, Magereza itafute wabia wa ndani na nje kwa maana ya wawekezaji kwa dhumuni ya kutumia fursa mbalimbali za masoko ya mazao nchi za nje za mazao yasiyo asilia katika soko la *AGOA*, *Canadian Pact Korea* Kusini, China na kadhalika Tatu, magereza itathmini matumizi halisi ya ardhi ambayo wanaweza kuitumia na iweze kuirudisha ile ya ziada Serikalini kufuatana na Sheria ya Ardhi. Na.4 na Na.5 ya mwaka 1999.

Ni jukumu langu kama Mbunge wa Wilaya ambayo magereza hayo yapo kuomba Taasisi hii ya Magereza kujenga mahusiano mazuri na wananchi wanaozunguka maeneo yao.Katika Gereza la Kiberege kwa mfano kumekuwa na malalamiko ya wananchi wa kijiji cha Sululu kwamba mashamba yao huwa yanashambuliwa na wanyamapori ambao huwa wanatokea kwenye mapori ya mashamba ya magereza ambayo hayalimwi. Siyo vizuri kuhodhi ardhi wakati kuna watanzania wengi ambao wanahitaji ardhi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo lazima kulima mazao tuliyoyazoea tu, lakini juhudi zifanywe ili mazao kama jatropha, michikichi yaweze kulimwa kwa wingi ili kuitumia ardhi kikamilifu. Mazao hayo yamekuwa na soko miaka ya hivi karibuni kwa ajili ya utengenezaji wa mafuta ya *diesel (bio-fuel).*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza wale wazungumzaji wetu, sasa nitamwita Mheshimiwa Naibu Waziri, aanze kujibu hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge, mmezizungumza. Mheshimiwa Naibu Waziri, atatumia dakika 30 na Mheshimiwa Waziri dakika 30. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii, kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi pia nichangie hoja iliyoko mbele yetu, aliyoiwasilisha leo asubuhi Mheshimiwa Joseph J. Mungai, Mbunge wa Mufindi Kaskazini na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yotena mimi pia ningependa kuungana na Wabunge wenzangu na Watanzania kwa ujumla, kutoa salamu za rambirambi kwa

familia ya kijana mwenzangu, Marehemu Amina Chifupa Mpakanjia. Ningependa pia kutoa salamu za rambirambi kwa familia zilizopata misiba kutokana na ajali za magari, zilizotokea hivi karibuni katika Mikoa ya Arusha na Singida, zikiwemo na familia za waliokuwa Wakurugenzi wa *Nyanza Cooperative Union*, Mzee Hezron Ndonho, Mzee William Kasubi na mzee wangu, Marehemu Stephen Masaba Kazi, jirani yangu niliyemrithi kiti hiki ninachokikalia sasa hivi. Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuchukua fursa hii, kumshukuru Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kunipatia nafasi ya kulitumikia Taifa letu chini ya uongozi mahiri wa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward N. Lowassa na kwa kunipatia nafasi ya kufundishwa kazi na mwanasiasa mzoefu, Mheshimiwa Joseph J. Mungai, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wananchi na Viongozi wa Wilaya ya Nyamagana, ambao wananipa ushirikiano mkubwa sana katika utendaji wangu wa kazi katika Wilaya ya Nyamagana. Nawashukuru sana, nawapenda sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, sitawataja kwa majina…

**NAIBU SPIKA:** Umemsahau mke wako, baba! *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe shukrani za pekee kwa familia yangu kwa ujumla, kwa kunivumilia kwa kutokuwepo nao katika vipindi virefu nikiwa nafanya kazi za Serikali. Ninaomba Mungu, watoto wangu wakikua, hizi kazi zote ambazo tunafanya ili kuboresha maisha ya Watanzania, wataelewa kwamba ni kwa sababu ya kutenda wema katika kuboresha maisha ya kila Mtanzania, ndio maana nilikuwa siwezi kuwa nao katika kipindi hiki wakiwa wanakua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, sitawataja kwa majina, heshima hiyo kama ilivyo kawaida, nitamwachia mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri. Kazi yangu hapa leo itakuwa kugusia maeneo mbalimbali ambayo yanahitaji maelezo au ufafanuzi kutokana na michango ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, mimi nitaangalia maeneo mawili makuu; eneo la Zimamoto na Uokoaji, pamoja na eneo la Magereza. Muda ukiruhusu, nitaangalia eneo la Uhamiaji. Lakini, kabla sijaanza kujibu hoja za Wabunge kwa ujumla, ningependa kuchukua nafasi hii, kujibu yale ambayo yalikuwa yameelezwa na ndugu yangu, rafiki yangu, Waziri Kivuli wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya katika hotuba yake aliyoiwasilisha leo asubuhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ningependa kwa ruhusa yako, kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge hasa wale wa Upinzani, katika hotuba yake Mheshimiwa

Mhonga ameelezea suala la msongamano ndani ya Magereza kama ni suala ambalo limetambuliwa kwa mara ya kwanza na upande wa Upinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako, ningependa kunukuu Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Katika sura ya 8, ukurasa wa 131 katika kuelezea Utawala Bora chini ya aya ya 107, Chama cha Mapinduzi kimeeleza wazi kabisa kwamba: "Tutajitahidi kuendelea kupunguza msongamano Magerezani." Pia katika aya 107(c) tumesema: "Tutazingatia kwa ukamilifu haki za binadamu katika utendaji wa vyombo vya dola." Hatuna haja ya kukumbushwa kuhusu haki za binadamu, tunafahamu kabisa kwamba, Watanzania wote wana haki zao, Watanzania wote wana haki ya maisha bora wakiwemo wafungwa na mahabusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Msemaji Mkuu wa Upinzani, kuna baadhi ya maswali ambayo ameuliza na ningependa kuyapa majibu. Nikinukuu, ameeleza kwamba: "Katika Idara ya Magereza kuna kipindi ambapo askari wanapotenda kosa, wanakatwa fedha kiasi kadhaa katika mishahara yao." Anauliza; kwa nini na hizi pesa zinapelekwa wapi? Ningependa kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, hili ni Jeshi la Magereza, kuna *code* zake za *discipline* ambazo ni tofauti na maeneo ya uraiani. Wana *discipline code* ambayo iko wazi, ambayo inaeleza pale ambapo Askari Magereza anapofanya kosa, jinsi anavyopigwa *fine* na hizo pesa zinakokwenda. Hizo pesa zinaingizwa katika *Prison's Award and Fines Fund* na hizo pesa huwa zinatumika katika kuboreshea Mabwalo, kutoa rambirambi kwa Maafisa wa Magereza waliofariki na kadhalika. Ningependa kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, *ERV* huwa zinatolewa kila pale ambapo Askari Magereza anakatwa kwenye mshahara wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuongelea suala la Mkakati wa Serikali wa Kupanua Magereza, hususan pale ambapo tunaongelea Magereza ya Watoto na Magereza ya Wakubwa. Ni kweli kabisa kwamba, tungependa kujenga Magereza mengi zaidi ya watoto, lakini kutokana na bajeti tuliyonayo, tunashindwa kufanya hivyo kwa wakati huu. Lakini, katika Magereza yote na niko tayari kwenda na Mheshimiwa Mbunge kuyatembelea, ningependa kumfahamisha kwamba, watoto hutenganishwa na wakubwa siku zote, hakuna gereza ambalo watoto wanalazwa pamoja na wakubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maelezo yake Mheshimiwa Waziri Kivuli, ameeleza kwamba, tarehe 11 Julai, 2007, mimi hapa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, nilisema katika majibu yangu kwamba, nilikana kuwepo kwa Maambukizi ya UKIMWI Magerezani na amesema ni jambo ambalo si kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako ningeomba kusoma *Hansard* ya tarehe 11 Julai, 2007 ili kuweka suala hili sawa. Nilichosema siku ya tarehe 11 Julai, 2007 nikijibu swali Na.192 ambalo alikuwa ameuliza Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, nilisema kwamba: "Madai ya Mheshimiwa Mbunge kuwa wafungwa wanaandamwa na maradhi ya kuambukiza kama vile ya UKIMWI, hayana ukweli wowote.

Viwango vya maradhi Magerezani haviko tofauti na vilivyo katika Jamii." Naomba kurudia: "Viwango vya maradhi Magerezani haviko tofauti na vilivyo katika jamii." Tunatambua kabisa kwamba, kuna wagonjwa ndani ya Magereza na ndio maana tuna kila aina ya tiba ndani ya Magereza na hao wafungwa wanapata tiba wanayoihitaji katika muda ambao unatakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Idara ya Zimamoto, naona Mheshimiwa Mbunge ametushukuru kufuata ushauri wa Wapinzani kuhusu kuboresha Idara ya Zimamoto. Kwa mara nyingine tena kwa ruhusa yako, naomba niinukuu Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, ukurasa wa 140 aya ya 114 inasema ifuatavyo: "Katika miaka mitano ya Ilani hii Chama cha Mapinduzi itaielekeza Serikali kufanya mambo yafuatayo:-

(a) Kwa kushirikiana na Halmashauri za Jiji, Manispaa, Miji na Wilaya kujenga uwezo wa kukabiliana na majanga ya moto.

(b) Kujenga uwezo wa nchi kukabiliana na dharura za ajali na halaiki katika maeneo nyeti na ya watu wengi.

(c) Kutazama upya Idara za Maafa ya Serikali kwa lengo la kupata njia za kuimarisha."

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi hapo kwamba suala la kuimarisha Idara ya Zimamoto ni suala ambalo lilikuwa ndani ya roho na moyo wa Watanzania wote, ambao wako ndani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue muda huu, kuongelea Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa ujumla. Kuna Wabunge tisa ambao wamechangia suala la Zimamoto na Uokoaji. Katika hoja zao, wameongelea utata wa umiliki wa Askari wa Zimamoto na Uokoaji kati ya TAMISEMI na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, wameongelea suala la ununuzi wa magari ya Zimamoto, uanzishwaji wa Ofisi za Mikoa na kadhalika. Kabla sijaanza kujibu hoja moja moja, ningependa kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge, katika Bunge lililopita, tulipitisha Sheria ya Zimamoto na Uokoaji. Hivi sasa tunavyoongea, pamoja na kwamba, imesharidhiwa na Mheshimiwa Rais, bado haijawekewa sahihi na Mheshimiwa Waziri ili ianze kufanya kazi. Tukumbuke kwamba, Serikali iliileta Sheria ya Zimamoto upya kwa kutambua kwamba, kulikuwa na upungufu katika Idara ya Zimamoto na kwamba, baadhi ya matatizo ambayo yangeweza kusababisha Taifa letu kupata matatizo katika kukabiliana na majanga ya moto ni kutokuwa na sheria hiyo *in place*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kwamba, hivi sasa mchakato wa kuandaa *Regulations* za Sheria ya Zimamoto na Uokoaji, unakaribia kukamilika na lengo la Serikali lilivyoelezwa katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri leo asubuhi ni kuhakikisha kwamba, kabla ya mwisho wa mwaka huu, Sheria ya Zimamoto itakuwa imeshakuwa *effected* na *Regulations* zitakuwa *in place* kuhakikisha

kwamba yote haya ambayo yalikuwa yameongelewa na Waheshimiwa Wabunge yanawekwa sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na suala la kwa nini Jeshi la Zimamoto na Uokoaji halina kasma yake na liko chini ya kasma 51? Isingeweza kwa kipindi hiki kuwa na kasma yake yenyewe, kwa sababu hiyo sheria yenyewe ilikuwa bado haijawa *put into force*. Serikali imeishatambua na imeshakubali kwamba, pale ambapo hii sheria itakuwa *effected*, bajeti itakayofuata, Jeshi la Zimamoto litakuwa na kasma yake lenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na wasi wasi uliooneshwa kwamba, ikitokea moto katika jengo kama la *PPF Tower* au majengo mengine marefu Dar es Salaam na sehemu nyingine hapa nchini kwamba, magari na vifaa vya Zimamoto tulivyonavyo visingeweza kukabiliana na moto ambao ungetokea. Ningependa kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge ambao walikuwa na wasi wasi huo kwamba, kwa mfano, katika Jiji la Dar es Salaam, tunazo *Fire Trucks* ambazo ni za Jiji, ambazo zitakuwa Chini ya Jeshi la Zimamoto, ambazo zina uwezo wa kupandisha *ladder* kwa urefu wa mita 54, ambao kwa Bara letu la Afrika tuko nchi tatu tu ambao tuna magari yenye uwezo wa kufanya hivyo. Hizo nchi zikiwa ni Ethiopia, South Africa na Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ningependa kuwakumbusheni kwamba, urefu wa hiyo *ladder* kwenye gari siyo kitu pekee ambacho kinasaidia kuzima moto na ndio maana katika *Regulations* ambazo tutaziunda chini ya Sheria hii, tutahakikisha kwamba, kutakuwa kuna *Regulations* ambazo zitahakikisha kwamba, ndani ya nyumba yoyote ambayo inazidi ghorofa nne, lazima kuwe na mitambo maalum ya kuzima moto *(Sprinklers)* na masuala mengine kama hayo. Kwa sababu lazima tukae tuelelewe kwamba, ukiangalia nchi nyingine; Singapore, New York na kwingineko, kuna majengo ambayo yana ghorofa 100, 110 na hakuna *Fire Truck* ya aina yoyote ile ambayo inaweza ikafika huko. Kwa hiyo, ina maana kwamba, lazima tuzingatie usalama ndani ya majengo yenyewe na ndio sababu mojawapo tulileta Sheria ya Zimamoto na Uokoaji haraka mbele yenu ili kuhakisha kwamba, majengo yetu yako salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja nyingi ambazo zimetolewa kuhusu Magereza yetu. Jumla ya Wabunge 49 wamechangia hoja za Magereza na hoja hizo zimezungukia maeneo kuu saba. Suala la msongamano wa magereza, ukarabati wa magereza, uchakavu wa nyumba za askari, maslahi duni, vitendea kazi duni, ukosefu wa vyombo vya usafiri na migogoro ya ardhi kati ya magereza na vijiji vinavyopakana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuanza na suala la migogoro ya ardhi katika maeneo ya magereza na vijiji vinavyopakana. Hili suala limeongelewa na Mheshimiwa Abdallah S. Sumry, Mheshimiwa Raynald A. Mrope, Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba na naamini kuna Mbunge mmoja mwingine ambaye alikuwa ameliongelea suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ningependa kumfahamisha Mheshimiwa Raynald A. Mrope kwamba, suala lake ni kweli kabisa limefika Wizarani kwetu, tulikuwa tukilifanyia kazi na naamini kabisa kwamba, kuna ahadi iliyokuwa imetolewa kwake kwamba, mimi kama Naibu Waziri, ningekwenda huko kukagua tatizo lenyewe ili

tuweze tukalimaliza hilo tatizo kwa mara moja. Naomba kueleza kwamba, pamoja na Tume ambayo ilikuwa imeundwa kuchunguza tatizo la Gereza la Namajani, tatizo ambalo lilikuja kujitokeza katika kufutilia tatizo la pale ni kwamba, kulikuwa kuna Tume nyingine kabla ya hapo, ambayo ilitoa mapendekezo tofauti. Sasa kutokana na kwamba kulikuwa kuna Tume mbili ambazo ziliundwa kuchunguza suala hilo hilo moja na zimetoa mapendekezo tofauti, tuliona kwamba ni busara tufuatane naye Mheshimiwa Mbunge ili kwenda na kuhakikisha kwamba tunalimaliza jambo hili kwa uhakika na lisije likarudia tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamuahidi Mheshimiwa Raynald A. Mrope kwamba, tutakapomaliza Bunge hili, akiwa tayari, mimi niko tayari kutokurudi Dar es Salaam, nifuatane naye twende tukatatue suala hili mara moja. Ningependa kuwahakikishia wale Wabunge wote wengine ambao wana matatizo ya ardhi na Magereza katika maeneo yao, hili ni suala ambalo tungependa kulimaliza haraka iwezekanavyo na niko tayari kufuatana nao ili kuhakikisha kwamba, suala hili tunalitatua mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la msongamano wa Magereza ni kweli kabisa kwamba kuna msongamano ndani ya Magereza yetu, kama nilivyoeleza hata Ilani yetu ya Uchaguzi inatambua kabisa kwamba, kati ya kazi kubwa tulizonazo ni kuhakikisha kwamba tunapunguza msongamano ndani ya Magereza. Ningependa kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kwamba, mpaka hivi sasa tumejitahidi sana. Mwaka 2006 kipindi kama hiki, tulikuwa na jumla ya wafungwa na mahabusu 44,562 ndani ya Magereza yetu. Leo hii tunavyoongea, tuna jumla ya mahabusu na wafungwa 39,782. Bado msongamano upo, tutajitahidi kadri ya uwezo wetu, kufanya yale yote ambayo yalikuwa yameelezwa na Mheshimiwa Waziri, ndani ya hotuba yake ya bajeti ili kuhakikisha kwamba, msongamano tunaendelea kuupunguza.

Naomba kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge, msongamano magerezani siyo Tanzania tu. Kwa kweli msongamano wa magereza ni kitu ambacho kinaonekana katika nchi karibu zote ulimwenguni. Suala ni kiasi kile cha msongamano. Sisi *of course,* kwa kutambua kwamba, msongamano ni tatizo, tutaendelea kufanya yale yote ambayo tunaweza tukafanya ili kuhakikisha kwamba, tatizo la msongamano tunalipunguza.

Kuhusu suala la magari ndani ya magereza yetu, ningependa kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kwamba, kwanza nafikiri mtakumbuka kwamba tulikuwa tuna ile *pilot project* ya Dar es Salaam ya kuwa na mabasi ya kuweza kuwasafirisha mahabusu. Kwa hivi sasa tunatarajia kwamba, ifikapo tarehe 31 August, 2007, mabasi matatu makubwa, *minibus* nne, pamoja na *pickups* sita na hizi *pickups* ni *escort pickups* zitakuwa zimeshapatikana na zitakuwa zimeshaanza kazi. Ningependa kuwafahamisha, zimeshalipiwa sasa hivi zinafanyiwa ukarabati ili kuhakikisha kwamba, zinakidhi *specifications* za kuweza kubeba wafungwa. Kwa kutambua pia kwamba kuna magereza mengi hapa nchini, ambayo yanahitaji usafiri, Wizara yangu imetenga fedha za kununua *pickups* nyingine 46, ambazo zitasambazwa katika magereza mbalimbali hapa nchini. *(Makofi)*

Kuhusu makazi ya askari, kama ilivyoelezwa ndani ya Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, tutajitahidi kufanya kama vile ambavyo wenzetu katika JWTZ, pamoja na Polisi walivyofanya; kutumia vyombo vyetu kama *NSSF* na *PPF* ili kupata mkopo ili kuweza kujenga hizo nyumba, tutajitahidi kufanya hivyo.

Kuhusu maslahi duni ya Askari Magereza, kama ilivyokwishawahi kusemwa hapa ndani ya Bunge Tukufu, ile *exercise* ya kupitia mishahara ya wafanyakazi wote kwa ujumla ikishakamilika, tuna uhakika kabisa kwamba, Askari Magereza hawatasahaulika.

Labda ningesema mara nyingi tukiongelea hali mbaya ya magereza yetu, watu wengi hapa ndani ya Bunge wamekuwa waki-*refer* katika Ripoti ya Mheshimiwa Kisanga. Ningependa kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwamba, Ripoti ya Mheshimiwa Kisanga ni ya mwaka 1998. Miaka mingi imeshapita, kuna vitu vingi sana ambavyo Waheshimiwa Wabunge, wataviona wakienda kutembelea magereza yetu kwamba, hali imekuwa tofauti. Pamoja na kwamba, bado tuna kazi ya kufanya, lakini kazi imekuwa tofauti ndani ya magereza yetu na kutokana na Ripoti ya Kisanga, tumefanya vitu vingi kwa mfano, kuboresha mavazi ya wafungwa, kuwatoa wafungwa kwenye vilago na kuwaweka kwenye magodoro, kuongeza fungu la chakula, tumeendelea kukarabati mabweni kutokana na bajeti tulizonazo na huduma za tiba zimeboreshwa ndani ya magereza yetu na tumejitahidi sana kupanua na kuongeza mabweni.

Pia tumekuwa tuki-*implement extra mural labour* kwa kiwango kikubwa zaidi ili kuweza kuondoa wafungwa ndani ya magereza na tumekuwa tukitumia *system* ya *parole* ili kuhakikisha kwamba, wafungwa wanatoka gerezani pale ambapo inathibitika kwamba wamerekebishika.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niingie kidogo kwenye suala la uhamiaji kwa muda huu mdogo uliobaki. Wabunge wengi wameongelea suala la wahamiaji haramu, kwamba mipaka yetu iko wazi sana na tungeongeza kasi ya kuweza kulinda mipaka ili kuhakikisha kwamba, wahamiaji haramu hawaingii hapa nchini. Ningependa kuwakumbusha ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, nchi hii ni kubwa sana. Tunapakana na nchi nane, tuna maziwa matatu ambayo yanakaa kama mpaka wa nchi yetu na tuna Bahari ya Hindi. Ni vigumu sana kuhakikisha kwamba, maeneo yote haya yanafungwa ili wahamiaji wasiingie hapa nchini. Ni nchi chache kama Marekani au Israel, ambao wana uwezo wa kujenga ukuta kuzuia watu kupenya kwenye mipaka. Ningependa kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwamba, ulinzi wa kwanza tulionao ni wananchi wenyewe (Watanzania). Tungependa sana kwa kupitia Bunge lako Tukufu, kuwasisitizia Watanzania kwamba, pale mnapoona wahamiaji haramu ndani ya nchi yetu, ninyi ndiyo mnawatambua, tunaomba mtusaidie katika Idara ya Uhamiaji na idara zote za ulinzi hapa nchini ili kuwaripoti hawa watu ili tuwafanyie kazi kuhakikisha kwamba nchi inaendelea kuwa yenye usalama na utulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niseme kwamba, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. Nisingependa kengele inigongee. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuja kukamilisha hoja yangu. Kabla sijaingia kwenye kumalizia kutoa maelezo ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri, ameanza kuyatoa vizuri sana, ningependa nianze kwa kutambua na kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote, waliochangia hoja hii. Tumepata michango mizuri sana, jumla tumekuwa na wachangiaji 74, wachangiaji 12 kwa kuzungumza humu ndani ya Bunge na 63 wamechangia kwa maandishi. Wote hao nawashukuru sana.

Waliochangia humu Bungeni ni Mheshimiwa Benson M. Mpesya, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati, akafuatiwa na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara hii, Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, Mheshimiwa Mariam R. Kasembe, Mheshimiwa Mohamed R. Abdallah, Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, Mheshimiwa Manju S. O. Msambya, Mheshimiwa Said A. Arfi, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa Abdul J. Marombwa, Mheshimiwa Felix N. Kijiko, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Abdallah S. Sumry na Mheshimiwa Raynald A. Mrope.

Nawashukuru wote kwa michango yenu ambayo Waheshimiwa Wabunge wote, wamesikia na wananchi wamesikia humu Bungeni, pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Lawrence K. Masha. Kwa hiyo, jumla kwa kuzungumza humu Bungeni wamechangia Waheshimiwa Wabunge 13 akiwemo Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi)*

Waliochangia kwa maandishi ni wafuatao; kwa vile orodha ni ndefu nitakwenda kwa *speed*, Mheshimiwa Eng. Christopher K. Chiza, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa Raynald A. Mrope, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Mbaruk K. Mwandoro, Mheshimiwa Dr. James A. Msekela, Mheshimiwa Phares K. Kabuye, Mheshimiwa Mussa A. Zungu, Mheshimiwa Gideon A. Cheyo, Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Profesa Philemon M. Sarungi, Mheshimiwa Zaynab M. Vulu, Mheshimiwa Savelina S. Mwijage, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mheshimiwa Rita L. Mlaki, Mheshimiwa Balozi Abdi H. Mshangama, Mheshimiwa Juma A. Njwayo na Mheshimiwa Gosbert B. Blandes.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Masolwa C. Masolwa, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Bakar Shamis Faki, Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri, Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, Mheshimiwa Teddy L. Kasella-Bantu, Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mheshimiwa Celina O. Kombani, Mheshimiwa Profesa Feetham F. Banyikwa, Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa Paschal C. Degera, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Yono S. Kevela, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye, Mheshimiwa Daniel N. Nsanzugwanko, Mheshimiwa Abdul J. Marombwa, Mheshimiwa Mgeni J. Kadika, Mheshimiwa Dr. Lucas J. Siyame na Mheshimiwa Janet B. Kahama.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Ania S. Chaurembo, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Khadija Salum Ally Al-Qassmy, Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Issa Kassim Issa, Mheshimiwa Hassan C. Kigwalilo, Mheshimiwa Dorah H. Mushi, Mheshimiwa Said A. Arfi, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis na mwisho Mheshimiwa Wilson M. Masilingi. Narudia kusema nyote asanteni sana kwa michango yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, michango hii ni mingi na nikisema tunapitia moja moja wala muda hautaniruhusu, mingine imekuja jioni hii. Kwa hiyo, hatukuipata nafasi ya kuifanyia uchambuzi kama ile iliyotolewa katika kipindi cha asubuhi mpaka saa saba, kabla ya Bunge kuahirishwa, hiyo angalau tumeweza kuifanyia kazi. Lakini tumepata picha ya kiujumla na tumeiona kwa uwazi kabisa, *concern* ya Waheshimiwa Wabunge, mambo ambayo wangetaka kuyaona, tunayarekebisha pale ambapo kuna kasoro. Kwa wale ambao wametupa pongezi, kwa niaba ya wenzangu wote, napenda kuwashukuru sana kwa pongezi mlizotupa na napenda kuwahakikishia kwamba, hotuba zenu tutazifanyia kazi kwa kina na pale panapohitajika majibu, tutajitahidi kutoa majibu kwa wale ambao sitapata nafasi ya kutoa majibu humu Bungeni.

Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa kujibu hoja nyingi sana kwa ufasaha mkubwa sana. Naiona faida nzuri sana ya kuwa na msaidizi kijana na tena aliye msomi mzuri, nimeona amejibu vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nitoe maelezo ya ziada kwa maeneo machache, ambayo nadhani yanahitaji maelezo yaliyogusiwa na Kambi ya Upinzani, kwa sababu ama wametoa maelezo ambayo kidogo hayana usahihi au wamehoji kutaka maelezo fulani. Nafikiri ni vizuri tuyatoe. Lakini nianze kwa kumshukuru sana Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, kwa kusema wazi kwamba, wanaunga mkono hoja hii. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Katika moja ya jambo alilouliza ni malalamiko ya kutumia vibaya wafungwa katika baadhi ya magereza na ametaja Gereza la Kiberege, Wami Mkuu, Kibiti na Kigong'oni na akasema kwamba, wakati mwingine hata baada ya mfungwa kufunguliwa, anaendelea kufanya kazi kwa wale wanaosimamia gereza. Napenda kuliweka wazi kwamba, taratibu haziruhusu askari kutumia mfungwa kwa kazi binafsi. Kama kuna mahali pamefanyika hivyo, tukipewa ushahidi tutachunguza na kuchukua hatua. Kinachotakiwa mfungwa baada ya kufunguliwa, anatakiwa aende zake kwao, siyo abaki pale katika eneo la gereza. Kwa hiyo, huo ndiyo utaratibu uliopo.

Pia ameuliza kuhusu fedha za UKIMWI kwamba, zinatolewa na Benki ya Dunia lakini hatukusema zinatumika vipi, inawezekana katika kutoa maelezo tumepitiwa hatukutoa maelezo Mheshimiwa Mbunge akayaona. Lakini katika mwaka 2006/2007, zilitolewa jumla ya shilingi milioni 500 kwa ajili ya kudhibiti UKIMWI katika magereza na zimetumika katika kufanya mambo manne; kwanza, kutoa elimu kwa wafungwa, askari na familia zao. Kutoa elimu ili waweze kujikinga. Pili, zimetumika kununua

mashine nne za kupima *CD4* katika magereza yetu. Kwa hiyo, sasa tunazo hizi mashine katika magereza. Nyingine zimetumika kununua vitanda vinavyotoa unafuu zaidi, kwa wale ambao wameathirika. Lakini sehemu kubwa ya fedha zinatumika kununua madawa ya kupunguza makali ya UKIMWI kwa wale walioathirika. Kwa hiyo, hayo ndiyo matumizi ya hizo fedha ambazo Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani aliuliza.

Alihoji pia chakula cha wafungwa akasema, Serikali inasema zitumike shilingi 2,500 kwa siku. Ningependa kusema, kiwango kilichoruhusiwa kwa sheria iliyotungwa na Bunge hili ni shilingi 1,400 kwa siku. Kutokana na idadi ya wafungwa tulionao, ingetakiwa katika bajeti tupewe shilingi bilioni 22. Lakini ukiangalia katika bajeti hii kwa chakula cha wafungwa, tumepangiwa shilingi bilioni 11.6, hii ni kutokana na ufinyu wa bajeti.

Sasa ukiangalia hizo takwimu ni nusu ya matumizi halisi yanayohitajika kufikia kile kiwango ambacho kiko kwenye Sheria ya Bunge. Sasa tunafanyaje, tunatumia maarifa mbalimbali, pamoja na juhudi za kujitegemea kwa chakula kile ambacho Magereza yetu yanazalisha katika mashamba yao.

Pia ameuliza kwamba, mwaka wa fedha 2006 shilingi milioni 500 zilitolewa kwa ajili ya kuboresha viwanda na mashamba zimetukaje? Nimeeleza katika hotuba yangu ya bajeti, inawezekana hotuba ya wenzetu wa Upinzani, iliandaliwa kabla ya kuiona hotuba yangu ya bajeti, tumenunua mashine mpya ya kiwanda cha viatu kule Karanga Moshi na mashine mpya katika Gereza la Ukonga, kwenye viwanda vya mle ndani na kwenye karakana. Pia tumenunua matrekta na zana zake. Kwa hiyo, fedha hizo zimetumika vizuri na Kamati ya Bunge husika, inapewa maelezo yanayohitajika.

Amehoji pia kwamba, hakuna mfungwa aliyeachiwa huru katika Wilaya ya Maswa toka mwaka 1996, Sheria ya Parole ilipoanza. Hapana hiyo siyo sahihi, napenda kumwarifu kwamba, tarehe 28 Mei, 2007 na tarehe 27 Juni, 2007, wameachiwa kwa *parole* wafungwa sita katika Wilaya ya Maswa na wengine watano wamependekezwa kutoka kwa utaratibu huu hivi karibuni. Kwa hiyo, Wilaya ya Maswa haijaachwa. *(Makofi)*

Lakini napenda pia ifahamike, hali maalum ya Wilaya ya Maswa. Wilaya ya Maswa ina gereza dogo tu, inaweza kuchukua jumla ya wafungwa wastani wa 100. Kwa hiyo, wafungwa wengi katika Wilaya ya Maswa, hupelekwa katika Magereza mengine. Wanapoachiwa kwa *Parole* kutoka magereza hayo ambayo hayako katika Wilaya ya Maswa, ukichungulia Maswa unaweza ukafikiri wamesahauliwa, hakuna wanaoachiwa kwa njia ya *Parole*.

Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, ametaka maelezo kuhusu ukosefu wa vituo na magari ya zimamoto na uokoaji. Ningependa nieleze kwamba, suala hili la huduma za uzimamoto na uokoaji, sasa ndiyo tunalivalia njuga kama nilivyoeleza, kwa makosa ilikuwa imefutwa sheria. Ukiwa huna sheria na utendaji wako hauendi vizuri. Lakini Waheshimiwa Wabunge, mapema mwaka huu, tumetunga upya ile Sheria ya Zimamoto

na mwaka huu ndiyo tuko katika mchakato wa kuliunda upya, liweze kutekeleza majukumu kama inavyotakiwa.

Halafu amehoji uchache wa askari wa zimamoto, lakini ningependa aangalie vizuri ukurasa wa 28 wa Hotuba yangu ya Bajeti, atakuta tumetoa mafunzo kwa wakufunzi 354 na pia napenda kutaarifa kwamba, kati yao 250 wameajiriwa mwaka 2005/2006 ili kuongeza nguvu ya jeshi hili. Utaratibu huu wa mafunzo kwa askari wa zimamoto utaendelea.

Mheshimiwa Mbunge, pia aliuliza suala la kurudisha wakimbizi wanaporudishwa kwao wahamiaji haramu wanapelekwa na raia. Napenda nihakikishe kabisa kama kuna raia yeyote amechanganywa na wahamiaji haramu, mara ninapopata taarifa hufanya marekebisho na nimeshafanya mara mbili, tatu, marekebisho kuhusu jambo hilo. Pamoja na wakimbizi, tutofautishe kati ya wahamiaji haramu na wakimbizi. Hawa wanaondolewa kwa utaratibu wa msako ni wahamiaji haramu. Hii hufanywa na kila nchi na Mheshimiwa Naibu Waziri, amefafanua kila nchi ikiwakuta wahamiaji haramu inatoa katika nchi yake. Kila nchi hujitahidi kuzuia wahamiaji haramu wasiingie. Hata nchi za wakubwa, iko nchi moja ya wakubwa kabisa inajenga hata ukuta, leo hii wanajenga ukuta kati ya nchi yao na nchi ya jirani kuzuia wahamiaji haramu.

Kwa hiyo, tatizo hili la wahamiaji haramu liko mahali pote duniani. Lakini kama raia, kwa kweli raia hatakiwi achanganywe huko na wakimbizi, huwezi ukamwondoa mkimbizi ukamchanganya na uhamiaji haramu, kwa sababu sheria yetu ya wakimbizi hairuhusu na mikataba yetu tuliyoisaini ya kimataifa hairuhusu, kumrudisha mkimbizi kwa lazima. Mkimbizi anarudi kwao kwa hiari yake. Hivi sasa tumeingia kipindi ambapo badala ya kusema warudi tu kwa hiari, tupo katika *stage* sasa ya kuwahimiza wakimbizi kurudi kwao, yaani kipindi cha *promotion of voluntary repatriation*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilidhani hayo niyatolee maelezo ya ziada kuhusu sera kwamba, tunatekeleza Sera ya CCM. Nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa sababu alikuja na silaha zenyewe kabisa zinazohitajika, nazo ni Ilani ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sasa niyagusie masuala kama matatu, pamoja na kwamba sitaweza kuyaunganisha na kila Mheshimiwa Mbunge aliyoyasema. Napenda kwa haraka niyagusie masuala matatu kwa kifupi. Suala la ardhi, pamoja na kwamba limetolewa maelezo, napenda niseme kwamba, Jeshi la Magereza halijichukulii ardhi, ardhi hiyo iliyo mikononi mwao huwa wanaomba na wanapewa. Sehemu nyingine wanakaribishwa na wanapewa. Wanapewa na Vikao vya Wilaya na Mikoa. Mheshimiwa Abdallah S. Sumry, ameeleza vizuri hapa kwamba, wana eneo kubwa katika Mkoa wa Rukwa, Wilaya ya Mpanda ni kweli kabisa na ni kweli hawalitumii lote.

Lakini mimi na mwenzangu Naibu Waziri, tunashirikiana nao katika mikakati ambayo tunataka kuianzisha ya kuweza kutumia hayo maeneo. Ninachoomba kwa nia nzuri ile ile ambayo maeneo hayo yalitolewa, tupeni muda tuyafanyie kazi. Lakini kama mahali pataonekana pana *land pressure*, pana tatizo la ardhi, kwa kupitia vikao vilevile,

sisi kama Mawaziri tunaoongoza Wizara hii, tutakuwa tayari kushirikiana na wenzetu wa ngazi ya Mkoa na ngazi ya Wilaya, tuone namna ya kufumbua tatizo hili.

Lakini kwa ujumla hata Mheshimiwa Abdallah S. Sumry mwenyewe amesema kwamba, Wilaya ya Mpanda nadhani nilimsikia, kama nilimsikia vizuri, amesema ni kubwa kuliko Mkoa wa Tanga na Mkoa wa Kilimanjaro. Mimi nilipokwenda kule kwa kweli nimeona maeneo mengi ambayo yako wazi. Lakini kama inaonekana wanayohitaji ni hayo ya Magereza na sisi tutapata nafasi ya kueleza tunataka kufanya nini, kwa sababu kile tunachotaka kufanya kina faida pia kwa maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Raynald A. Mrope, kwa ruksa yako alisoma barua ambazo huwa tunaandikiana humu Bungeni. Kwanza, inathibitisha kwamba kila aliponiandikia nilimjibu, sikudharau. Nilionesha *seriousness* ya kuchukua hatua. Mheshimiwa Raynald A. Mrope atakumbuka baadaye tulikaa, nikamwambia bwana pamoja na nia yangu nilitaka nije mimi mwenyewe, naona haiingii vizuri katika ratiba. Nimem-*assign* Mheshimiwa Naibu Waziri, atakuja na mwenzangu naye hajapata nafasi, lakini sasa hivi ametoa *commitment* kwamba, hata safari hiyo ikibidi kuianzia hapa mtaianzia hapa. Kwa hiyo, bwana nakushukuru kwamba aliunga mkono kwa unyonge lakini nategemea sasa atatuunga mkono kwa moyo kabisa wa ki-CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la vitambulisho, Mheshimiwa Mohamed R. Abdallah alilifafanua vizuri sana. Napenda niseme vile alivyolifafanua mwenzetu kwa kweli ndivyo inavyotarajiwa. Teknolojia iliyochaguliwa kutumika kwa vitambulisho vya taifa kwa uamuzi wa *cabinet,* teknolojia ya *smart card,* inawezesha mfumo huu tutakaoutumia wa vitambulisho kuweza kuchanganya na mambo mengine, ambayo watalaam wanaita ku-*interface* na orodha ya usajili wa vizazi na vifo. Kwa hiyo, watu watakuwa wamesajiliwa, wana vitambulisho, lakini pia kutakuwa na utaratibu kwamba kila anayezaliwa naye anakuwa *captured*. Pia itaweza ku-*interface* na sensa ya watu. Kwa hiyo, kuhesabu Watanzania tuko wangapi, itakuwa kama *automatic*. Itaweza pia ku-*interface* na Daftari la Wapiga Kura. Kama alivyosema Mheshimiwa Mohamed R. Abdallah, hata masuala ya kodi, *TRA* inaweza kushirikisha humo. Lakini tutakwenda hatua kwa hatua, kutokana na fedha zinavyopatikana. Namshukuru sana kwa namna alivyokuwa anaeleza, nilimgundua moja kwa moja kwamba, mwenzetu anaonekana ni *IT literate,* nampa hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo ningependa kulifafanua ni la uraia wa nchi mbili. Jambo hili naona nilifafanue kwa sababu lina uelewa tofauti. Nilimsikia Mheshimiwa Manju S. O. Msambya anasema haliungi mkono kabisa. Lakini mimi nikijua matatizo yaliyopo katika eneo analotoka, namtegemea aliunge mkono kwa sababu hili litaleta *solution* katika maeneo ya mipakani hasa ukilichanganya na lile la vitambulisho.

Uraia wa nchi mbili, naomba tulielewe kwamba, lina pande mbili. Tuzielewe pande mbili za uraia wa nchi mbili, tuelewe kuna upande wa Watanzania wanaohusika na uraia wa nchi nyingine na kuna upande wa wageni wanaosema wanaomba uraia wa Tanzania. Kwa hiyo, tulitazame kwa sura zote mbili, tusilitazame kwa sura moja.

Wapo Watanzania wengi, tunaposafiri huko nchi za nje tunakutana nao. Mwingine anasema mimi ni raia wa hapa *Sweden,* kwa sababu ya kuolewa au kwa sababu ya kuoa. Mwingine anasema nchi hii niliko ukizaliwa tu hapa inakutambua kuwa ni raia. Sasa Sheria ya Tanzania kwa sasa inasema ukiwa na uraia mwingine, unaupoteza ule wa nyumbani. Sasa vijana wetu na wenzetu Watanzania wanasema, hawataki kuupoteza huo uraia. Wengine wanasema tukiruhusiwa kuwa na uraia wa huku tuliko lakini tukawa nao pia wa nyumbani, tunaweza kuwekeza nyumbani kwa urahisi zaidi. Kwa hiyo, napenda niseme lina pande mbili. *(Makofi)*

Kuhusu wageni kuwa raia wa Tanzania, kwa mujibu wa sheria yetu mtu hakurupuki tu akawa raia wa Tanzania, kuna utaratibu wa kuomba. Utaratibu wa kuomba uraia wa Tanzania unaanzia ngazi ya chini; ngazi ya kijiji, ngazi ya kata, ngazi ya mkoa, ndipo uje ngazi ya taifa na hapa ngazi ya Taifa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Kamati inayomshauri, kutokana na ushauri ule ulioanzia chini. Kuhusu Zanzibar nako mchakato unaanza chini, unapita kwenye ngazi inayoitwa shehia unapita pale unazungumzwa na ngazi ya juu kabisa ni kikao ambacho Mwenyekiti ni Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Kiongozi, ndiyo ina-*process* na kusema kwamba, sasa huyu tumekubali. Tunapokaa kwenye Kamati ya Kitaifa yule *assistant director* wa *immigration* na msaidizi wake kutoka Zanzibar, tunakuwa nao, wanatuthibitishia huyu amekubaliwa, huyu hakupendekezwa ndipo tunapotoa uraia. Sasa tukisema tutaleta uraia wa nchi mbili kuruhusiwa, utaratibu wa kuomba lazima utakuwepo, haitakuwa *automatic* kwamba mtu ajiombee tu.

Kwa wanasiasa liko pia tatizo la kusema mtu akiwa na uraia wa nchi mbili, atakuja kupiga kura, kwa sababu ni raia hata kama anakaa nje, wakati wa kupiga kura anaweza akaja. Hili katika utungaji wa sheria, linaweza likaangaliwa na nadhani katika sheria ama katika Katiba inasema kwamba, Bunge laweza kutunga sheria kwamba, mtu mwenye uraia wa aina mbili asiruhusiwe kupiga kura. Haya ni mambo yanayoweza kutungwa katika sheria.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa napenda jambo hili lisitazamwe mno kwa wasiwasi. Nimesema katika hotuba yangu kwamba, jambo hili tumelifikisha katika ngazi na liko katika ngazi ya *Cabinet* tukisema jambo liko katika ngazi ya *Cabinet* maana yake Waraka umeshafikishwa kwenye *Cabinet.* Lakini *Cabinet* ikanituma kwamba, sasa tumeyaona mapendekezo haya lakini Waziri chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, mzungumze na Serikali ya Zanzibar kwamba na wenzetu walielewe linalosemwa humu nao wawe hawana wasiwasi nalo, ndipo tulipofikia. Tutakapomaliza *stage* hiyo litarudi tena Baraza la Mawaziri tutalifanyia uamuzi.

Tukilifanyia kwenye Baraza la Mawaziri litakuwa halijaisha, lazima lije kwenu tena, itungwe sheria iweke utaratibu utakavyokuwa. Kwa hiyo, mimi nilipenda kuchukua nafasi hii kueleza ili kupunguza wasiwasi unaoendana na jambo hili, pamoja na lile la vitambulisho nalo kwamba, tumefika nalo pahali pazuri. Napenda niwashukuru tena wote waliochangia, nafahamu kabisa kwamba, sikujibu hoja ya kila mtu sasa tusije tena kusema kwamba, tunataka maelezo kwa sababu mengine nimesema tutayatolea maelezo.

Labda Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, mwenzangu ananikumbusha hapa kwamba, yule mwananchi, Ndugu Thomas Christopher Rwetabaza, ulieleza hapa na ukasema huungi mkono hoja. Sisi tumechunguza habari zake. Jambo lake lile lilipofika tumelichunguza na tukaona hakuna sababu ya kumnyang'anya *passport.* Kwa hiyo, tumetoa maagizo kwamba, *passport* yake arudishiwe. Hapa nilikuwa naletewa *note* kwamba, *message* imekwisha pokelewa kwamba, amerudishiwa. Kwa hiyo, hii ni *dot.com generation* unaweza pia hata wewe ukatafuta katika mtandao wakakuambia ni kweli *passport* imerudishwa. *(Makofi)*

Kuhusu Mheshimiwa Manju S. O. Msambya, yule Ndugu Philemon B. R. Esaka, tulichunguza, jambo lake lilitaka kufanana na hili, kuna utata wa uraia wake. Lakini tumekuta kwamba, jambo lake liko Mahakamani. Ni *criminal* katika Mahakama ya Kwanza, ambako alipelekwa kushtakiwa na hili liko Zanzibar, kwa kuwa Zanzibar yeye alishinda na Idara yetu ya *Immigration* ikafanya *appeal* kwenda ngazi ya pili akashinda. Lakini sasa iko *appeal* kwenye *High Court* ya Zanzibar, *Criminal Appeal No. 5* ya mwaka 2004.

Sasa napenda nimwombe Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa vile wewe ni Mbunge mzoefu, tumekuwa nawe hapa Bungeni ingawa kuna kipindi ulikwenda kuwa Mkuu wa Wilaya, lakini na Ukuu wa Wilaya ni mambo ya Serikali. Tuelewane kabisa kwamba, jambo hili haitakuwa busara tukalizungumzia hapa, wakati liko Mahakamani. Lakini napenda kukuhakikishia kwamba kiutawala, sisi Mawaziri tumeamua tutalitazama, tulione limekaakaeje, lakini kwa hatua ya kulizungumza hapa Bungeni naomba tuishie hapa tu kwa kutambua kwamba jambo hili liko Mahakamani.

Narudia kusema kwamba, nawashukuru sana Wabunge wa Upinzani na Wabunge wote, kwa kuunga mkono hoja yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Lakini lazima tuingie katika hatua ya kufanya maamuzi ya kina zaidi. Katibu.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 29 – Magereza**

Kif. 1001 – *Prisons Headquaters* ... .... ...... ... Sh.4,907,261,200.00
Kif. 2001 – *Parole Department* ... .... ...... ..... Sh. 355,450,700.00
Kif. 2002 – *Prisons Welfare and Rehabiliation* .... Sh.57,326,550,600.00
Kif. 2003 – *Resettlement of Offenders* .... ...... ...... Sh. 638,026,000.00
Kif. 3001 – *Prisons Staff College* ... .. ...... ........Sh. 143,175,000.00

Kif. 3003 – *Prisons Trade School* .... .... ... ..........Sh. 346,210,300.00
Kif. 3004 – *Prisons College Kiwira* .... ...... ........Sh. 810,324,000.00
Kif. 4001 – *Prison Building Brigade* .... ..... .........Sh. 996,056,500.00

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 4002 – *Prisons Industries* .... ...... ..... ..... Sh. 409,551,200.00

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Asante Mheshimiwa Mwenyekiti. *Vote* ya 29, kifungu cha 4003, kifungu kidogo cha 270300 - *Vehicles and Mobile Equipments.* Wakati nachangia nilichangia kwa maandishi.

**MWENYEKITI:** Tafadhali umesema kifungu gani? Tumia kipaaza sauti.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Nilisema kifungu kidogo 270300.

**MWENYEKITI:** *Sub-Vote* gani?

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** *Sorry 4003.*

**MWENYEKITI:** Ngoja kidogo hatujafika huko. Kifungu kinachofuata ndiyo hicho, sasa subiri kidogo sisi tuko 4002.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 4003 – *Prisons Farms* ..... .... .... ..... ..... Sh. 488,372,800.00

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba wala hukukaa, haya endelea. *(Kicheko)*

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Maana yake naona unasema haraka halafu unachelewa kuingia humu. Nashukuru sana. Nilichangia kwa maandishi na limekuwa ni ombi langu la muda mrefu tangu mwaka juzi. Mwaka jana nilipeleka maombi kwa Mheshimiwa Waziri aliyepita na nilipewa trekta kuukuu kwa Gereza la Londwe. Gereza la Butundwe ni la kilimo, liliomba mbuga kubwa kwenye eneo Isima na tukawapa eneo kubwa sana. Lakini kwa sababu ya kukosa vifaa, wanashindwa kulifanyia kazi na wananchi wengine waliachia eneo hili kuona kwamba, eneo litafanyiwa kazi. Kwa hiyo, nilikuwa naomba trekta ikiwezekana hata matrekta mawili na gereza hili linaweza kulisha magereza yote ya Mkoa wa Mwanza na Kagera, kwa kutoa mpunga mzuri. Nilikuwa naomba hilo.

**MWENYEKITI:** Mimi sitamruhusu ajibu, kwa sababu ni d*evelopment*. Nenda utafika kwenye *development* kuna *Prisons Farm,* siyo hapo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 51 – Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

Kif. 1001 – *Administration and General* .... .... Sh. 936,123,725.00

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, Mheshimiwa Phares K. Kabuye, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa George M. Lubeleje na Mheshimiwa Yono S. Kevela. Tunaanza na Mheshimiwa Kevela.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui nizungumze na programu au niende moja kwa moja?

**MWENYEKITI:** Sema kwanza tukusikie.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Katika mchango wangu wa maandishi nilikuwa nimechangia kuhusu suala la adhabu ya kifo. Lakini bahati mbaya, Mheshimiwa Waziri, hakutoa ufafanuzi wa aina yoyote na adhabu hiyo inaonesha kwamba, haitekelezeki na nikatoa ushauri kwamba, ifutwe badala yake kuwe na kifungo cha maisha. Sasa nilitaka niombe ufafanuzi tu msimamo wa Serikali unasemaje, kwa sababu kuna wafungwa wengi wana adhabu hiyo ya kifo na bado wanateseka?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hili swali halihusiki kabisa na magereza, linahusika na Wizara iliyomaliza kazi juzi, ya Sheria na Mambo ya Katiba. *(Makofi)*

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Nashukuru Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kupata nafasi. *Vote 51,* programu ya *10, sub-vote* 1001, kifungu kidogo 250100 – Mshahara wa Waziri. Swali langu ni la kisera tu. Katika mchango wangu wa maandishi katika Idara ya Uhamiaji, niliulizia kuhusu wageni kupata *visa at the point of arrival.* Pamoja na wageni kupata *visa* wakati wanaingia nchini katika ile fomu ya kuomba *visa* kuna sababu zinazowauliza kwa nini wanaingia ndani ya nchi. Kuna kipengele ambacho huwa kinasema, *seekig for employment*. Sasa ningependa kujua; je, huu ni utaratibu kwamba mtu anaweza kutoka nje ya nchi na kuja hapa kupata *permit* akifika *airport* au kule anakotokea? Ningeomba ufafanuzi kwa hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ningependa kujibu hoja ambayo imetolewa na Mheshimiwa Lucy F. Owenya kama ifuatavyo:-

Serikali imeshaona tatizo na hicho kipengele cha *seeking for employment* na tuko katika harakati za kuweza kukiondoa katika zile fomu za kuingilia hapa nchini. Tatizo

letu ni kwamba, hivi sasa hizi fomu zetu ni za Afrika Mashariki kwa ujumla na tunashirikiana na wenzetu katika nchi za Afrika Mashiriki ili tuhakikishe kwamba, nchi zote tunaondoa kipengele hicho kwa pamoja. *(Makofi)*

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Asante Mheshimiwa Mwenyekiti. Kwanza kabisa, naomba niweke rekodi sawa kwenye *Hansard.* Wakati namaliza kuchangia nilisema naomba kuwasilisha, sikusema naunga mkono hoja. Kwa sababu ni mengi sana nilikuwa nauliza na nilikuwa nahitaji ufafanuzi. Kwa hiyo, nisingeunga mkono hoja wakati sijapata ufafanuzi na hata hivyo, sitaunga mkono hoja kwa sababu yatahitaji utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende moja kwa moja kwenye maombi yangu ya ufafanuzi. Wakati Mheshimiwa Waziri akinijibu, alitumia mara nyingi Ilani. Nakubali lakini kuandika ni jambo lingine na utekelezaji ni jambo lingine. Ndiyo maana kila mtu hapa aliyesimama, ameongelea au amelalamika kwamba, hayajafanyiwa kazi. Kwa mfano, msongamano wa wafungwa, karibu Wabunge wengi wameelezea hata matatizo ya magereza. Kwa hiyo, nilitaka hilo niliweke sawa.

Halafu nilikuwa nasema kwamba, katika majibu yake Mheshimiwa Waziri alielezea matatizo ya sheria akisema kwamba, unaweza ukaiba ng'ombe watano, lakini utafungwa ile ile miaka mitano. Kwa hiyo, tatizo pale linaonekana ni sheria na msongamano, ndiyo maana unazidi. Sasa katika mchango wangu, niliomba Waziri atuelezee kwa nini sheria ya *Parole* na *Community Act,* hazitumiki ili kupunguza huu msongamano. Tatizo ni nini; je, yanahitaji kuletwa hapa Bungeni labda tufanye marekebisho kwa ajili ya kuondoa msongamano ule katika magereza yetu? Kwa hiyo, nilikuwa naomba ufafanuzi wake.

Halafu suala la pili, Mheshimiwa Rais, mwezi Mei, 2007 alikuwa Mkoani Kigoma, alitoa tamko kwamba, mwaka 2008 wakimbizi wote wawe wameondoka. Rais akiongea, mara nyingi ndio inakuwa ni kama *final say* au ni amri. Sasa Wizara ina mkakati gani katika kutekeleza hilo ili 2008 kweli wakimbizi wote wawe wameondoka? Naomba ufafanuzi juu ya hayo.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nifafanue kwa kurejea kwenye hotuba yangu, juu ya hatua ambazo zinachukuliwa na ataziona wazi kabisa. Akiangalia Kiambatisho F, ataona kabisa zile *graph* namna ambavyo wakimbizi wanapungua. Utaona zile *bars* zimelala zinakwenda chini. Inakuonesha kabisa kwamba, kuna hatua zinachukuliwa za kuondoa wakimbizi.

Kwa hiyo, hili la mwisho alilolisema la wakimbizi na tamko la Mheshimiwa Rais, nimetamka pia katika hotuba hii si mara moja, mara mbili au mara tatu kwamba, mwaka huu nimesema tumeanza kuona mwanga mwishoni mwa handaki na kwamba tunachukua kila hatua, kuhakikisha ifikapo mwisho wa mwaka huu wa fedha, tunafunga makambi na makazi ya wakimbizi. Kwa hiyo, aliloagiza Rais ndilo ambalo tumetamka tunalitekeleza humu.

Kuhusu *parole* na kifungo cha nje; kifungo cha nje aangalie Kiambatisho (d), tumeonesha wale 931 wote waliotoka mkoa kwa mkoa, ambao wamekwishatoka kwa *parole.* Lakini pia nimesema kwamba, kwenye Sheria ya *Parole* wigo ni finyu, natarajia kuleta mapendekezo ya kuongeza wigo ili wafungwa wengi zaidi, waweze kuingia katika utaratibu huu wa *parole.* Kwa hiyo na utekelezaji wa Bodi ya *Parole* tumeonesha katika Kiambatanisho (c).

Ukiangalia Kiambatisho (c) na (d), kwa kweli ni maelezo ya kutosha kwa wasi wasi alionao Mheshimiwa na kama kutakuwa na maeneo ambako tunahitaji kuchukua zaidi, tuko tayari kushirikiana na Mbunge yeyote, ambaye anaweza kutupa ushauri, tuchukue hatua gani zaidi. Lakini maelezo yaliyomo katika kitabu hiki, mimi naona yanatosheleza kabisa. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Ninaomba maelezo kwamba, katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 47 kifungu (f) - kuendeleza ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa nyumba za maafisa na askari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, askari wetu wanafanya kazi nzuri sana ya kujenga nyumba za kuishi na mfano mzuri ni Gereza la Mpwapwa, wamejenga nyumba. Nashukuru sana Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati wakati akiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, alifika pale. Lakini zile nyumba kumi hazijakamilika hadi sasa. Sasa nilikuwa naomba tu maelezo, kwa sababu wanaishi katika nyumba, nyumba ni chache nilikuwa naomba zile nyumba zikamilishwe. Naomba maelezo.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyonukuu; kuendeleza ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa nyumba za maafisa. Yale maneno kuendeleza ujenzi, maana yake katika mwaka huu wa fedha katika bajeti hii, tunazo fedha za kukamilisha zile nyumba za pale Mpwapwa, pamoja na maeneo mengine ambako ujenzi wa majengo unaendelea. Kwa hiyo, namhakikishia kwamba, hilo ndilo ambalo litafanyika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa George M. Lubeleje, ulitakiwa uende kwenye maendeleo. Tunaendelea.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa mipango ya Serikali ni kuhakikisha kwamba, mipaka yetu yote na nchi za jirani inalindwa na kufanyiwa utaratibu maalum na hasa kwa kuangalia uwezekano wa kuwa na Ofisi za Uhamiaji ili kudhibiti wahamiaji haramu; na kwa kuwa katika Bajeti ya mwaka jana, Wizara iliazimia kutekeleza mpango wa namna hiyo hiyo wa kisera katika mpaka wa Tanzania na Msumbiji, kupitia Muhukulu, kwa kutenga shilingi milioni 20 ambazo hazijatolewa na hazikufanya kazi mpaka mwaka huu; sasa nilikuwa napenda Mheshimiwa Waziri aniambie; je, katika mpango wake wa kisera wa mwaka huu, hizo shiling milioni 20 zipo na zitafanya kazi ile ambayo ilikwishatengewa katika kipindi kile cha mwaka jana? Nilikuwa naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Jenista J. hagama, alilifuatilia sana jambo hili mwaka jana. Napenda kumhakikishia kabisa kwamba, katika bajeti ya mwaka huu zimetengwa fedha kwa ajili ya kujenga jengo katika kituo anachokizungumzia. *(Makofi)*

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Asante Mheshimiwa Mwenyekiti. Katika Hotuba yake Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 14, 15 na 20 amezungumzia kuhusu kilimo na uimarishaji wa mashamba ya magereza. Ni kweli magereza yanamiliki mashamba mengi makubwa na mazuri. Wanalima katika mashamba yao na pia wanalima katika mashamba ya watu binafsi. Lakini wakati huo huo, Serikali imepanga bajeti ya Wizara hii ya shilingi bilioni 11. Kwa maneno ya Waziri ni kwamba, hela hiyo wanayoipata katika kulima mashamba yao, wanaongezea kufidia pengo lile la bajeti. Kwa kuwa Serikali sasa ina mpango huu wa kuleta Mapinduzi ya Kilimo, yaani *SDP;* kwa nini basi Serikali haitumii nafasi hii ya magereza kuwapatia pembejeo na zana za kutosha ili waweze kulima mashamba mengi kwa kutoa mazao mengi ambayo yatatosheleza katika nchi hii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, hilo linafanana na la Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, kuna *prisons farm.* Hii ni Wizara haiendi kulima wala haitoi pembejeo. Kwa hiyo, usubiri kwenye *prions farm development.* Tunaendelea.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti. Wakati nachangia asubuhi hapa, nilizungumzia matatizo yaliyompata Ndugu Thomas Christopher Rwentabaza, jinsi alivyopigwa na Maafisa Uhamiaji wa Karagwe na pia alivyonyanyaswa na kunyang'anywa *passport.* Katika majumuisho Mheshimiwa Waziri, ameeleza kwamba, ametoa maelekezo kwamba, Bwana Thomas Rwentabaza aweze kupatiwa *passport* yake. Nilijitahidi kutoka nje kuzungumza naye, nione kama ni kweli amepewa *passport,* amenihakikishia kwamba aliitwa pale *Immigration* Wilayani Karagwe na akaambiwa kwamba ameambiwa apewe *passport* yake.

Kwa bahati mhusika nadhani hakuweza kupatikana, alikuwa nje ya kituo. Naamini kabisa kwamba, maelekezo ya Mheshimiwa Waziri ni sahihi na hayawezi kupingwa na *juniors.* Vilevile nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri na hasa kwa kasi ambayo ameonesha kushughulikia tatizo hili. Mimi asubuhi kwa sababu ya uchungu ule, sikuweza kuunga mkono hoja hii, sasa hivi kwa moyo mkunjufu naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti. Kwa kweli sina tatizo kwa sababu mimi na Mheshimiwa Waziri ni marafiki.

**MWENYEKITI:** Kaa mbali kidogo na kipaza sauti.

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Kuna mambo ambayo ameshanijibu, isipokuwa naomba ufafanuzi juu ya kilio changu cha kila siku kwamba, Gereza la Biharamulo linavuja, wafungwa na mahabusu wanateseka, sikupata majibu wakati wa mchango wangu kwenye maandishi.

Pili, Mji wa Biharamulo miti yote imekwisha, wafungwa wanafyeka ili kupikia na Mkoa nzima wenye Wilaya nane, wana lori moja chakavu. Nilikuwa naomba ufafanuzi. Asante.

**MWENYEKITI:** Suala la kwanza litajibiwa kwenye *development rehabilitation,* la pili unaweza kujibu kuhusu magari ya magereza.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba hii ya bajeti, nimeeleza juu ya mradi unaohusu Mkoa wa Kagera, ambao umepangiwa shilingi bilioni 10.9, mradi huo unaofadhiliwa na nchi ya Denmark na ndiyo maana katika shukrani pale mwisho, nimeishukuru nchi ya Denmark. Maeneo yote kulikokuwa na matatizo kutakuwa na *financing* kwa ajili ya magari. Nimetamka mle kwenye *paragraph* inayohusika kwamba, ununuaji wa magari na vifaa vya ofisi, pamoja na miradi ya *biogas* kwenye magereza. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Wale niliowaambia wakati ukifika wa *development* nitawaita.

Kif. 1002 - *Finance and Accounts* .... .... ..... ... Sh. 348,677,550.00
Kif. 1003 - *Policy and Planning* ..... .... .... ... Sh. 269,097,537.00
Kif. 1004 - *Community Service Secretariat* .... .... ..Sh. 455,050,609.00
Kif. 1005 - *Information, Education and Communication* .. .... ...... ...... ..... ..... ..... ...... Sh. 43,000,000.00
Kif. 1006 - *Management of Information Systems* .... Sh. 37,000,000.00
Kif. 3001 - *Fire and Rescue Services* .... ..... ...... Sh. 1,037,555,594.00
Kif.3002 - *Fire and Resare Services Training Inst.* .... Sh. 329,143,321.00
Kif. 4001- *Refugees Unit* .... .... .... ..... ..... . ... Sh. 539,288,662.00

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 93 – Uhamiaji**

Kif. 2001 – *Immigration Zanzibar* .... ..... .... ... Sh. 592,970,100.00
Kif. 2002 - *Immigration Mainland* ... ..... ..... Sh.12,786,173,900.00

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 29 – Magereza**

Kif. 1001 – *Prisons Headquarters*... ... ...... ... ... ... .... ..Sh. 200,000,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 – *Prisons Welfare and Rehabilitation* ... … … Sh. 2,033,000,000

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante. Nilikuwa naomba ufafanuzi juu ya gereza la Wilaya ya Biharamulo, kila mara tangu mwaka jana, nilikuwa nalia kwamba nimelitembelea na taarifa ya matembezi yangu nimempatia Waziri pale. Kuna matatizo makubwa gereza, lilijengwa enzi za wakoloni limetoboka mabati yote, mvua inaponyesha wafungwa wananyeshewa. Nikaomba ufafanuzi hilo gereza kama alivyokuwa ameniahidi kwamba, litakarabatiwa sasa katika fungu hili pesa imo ya kulikarabati mwaka huu?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Phares K. Kabuye, pamoja na kumshukuru kwa namna anavyofuatilia matatizo ya wafungwa katika gereza lililo katika jimbo lake. Napenda pia nimpongeze sana kwamba, yeye ni miongoni mwa Wabunge wanaotembelea gereza. Napenda nimhakikishie kwamba, jibu ni ndiyo katika mpango wa mwaka huu. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 4001 – *Prison Building Brigade*… … … … ..... ...Sh.1,971,680,000

**MHE. ABDUL J. MWAROMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Ninataka Mheshimiwa Waziri, anipatie ufafanuzi kidogo. Nilipokuwa nachangia.

**MWENYEKITI:** Hapa inabidi utaje kifungu gani.

**MHE. ABDUL J. MWAROMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu ni 29, *sub vote* 4001, kifungu kidogo 6306 - *Completion of Prison Wards* na 6307 *Completion of Staff Houses*. Nilipokuwa nachangia nilielezea kwanza, jina halisi la gereza ambalo lilikuwepo Kibiti, ambalo hatulijui mpaka sasa hivi linaitwa ni Kibiti au Ng'aru, kwa sababu kitabu cha Mheshimiwa Waziri katika kurasa mbili tofauti, kinaeleza majibu mawili tofauti, sasa hilo nilitaka nilipatie ufafanuzi, gereza ni lipi? Lakini nilimweleza hali mbaya ya Gereza la Kibiti au hilo la Ng'aru. Katika gereza lile nyumba zote zimejengwa hasa lile gereza lenyewe kwa bati, juu bati, chini bati linavuja sana. Wakati

wa mvua linavuja, wakati jua kali ni joto mle ndani, kiasi ambacho hata kuishi ni sana kwa wale wafungwa.

Sasa nilitaka kujua katika kipengele (e), ukurasa ule wa 47, yameainishwa majina ya magereza ambayo yatafanyiwa ukarabati mwaka huu na kuyakamilisha. Kuna jina pale chini kabisa katika kipengele (e), linaitwa Ng'aru, nilitaka kujua; je, gereza hili ndiyo hilo au sio hilo?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumfafanulia Mheshimiwa Abdul J. Marombwa kwamba, gereza la kwenye wilaya yao linaitwa Kibiti na Gereza la Ng'aru liko Mkoa wa Tanga, hilo ndilo tunalolizungumzia. Lakini napenda kukiri kusikia matatizo anayoyazungumzia ya Gereza la Kibiti, pamoja na kwamba, haliko katika orodha ya yale ambayo yalipangwa mwaka huu. Napenda kumhakikishia kwamba, nitafutalia hilo tatizo na tunatafuta namna, kama kuna *emergency* tutatafuta namna ya kulishughulikia Gereza la Kibiti. Mimi mwenyewe nitalitembelea gereza hilo hivi punde, kujionea mwenyewe hali halisi ilivyo.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fungu namba 29, kifungu kidogo 4001, kifungu kidogo zaidi 3401 na 6307. Kifungu 3401 kinahusiana na masuala ya maji, ambapo katika Gereza la Namtekela lililopo Nkasi kule Namanyele, halijawahi kuchimbiwa kisima cha maji na wafungwa wamekuwa wakinywa maji wanayochimba kwenye visima vya kawaida, ambayo hayana usalama kabisa. Nilikuwa naomba waweze kutusaidia, angalau kisima kimoja cha kuchimbwa kitaalamu.

Kwa upande wa nyumba, kifungu kidogo 6307, pia katika eneo la Namtekela, sijaona nyumba iliyojengwa na Serikali, bali wamekuwa wakijenga nyumba zao za kawaida na kuweka majani juu badala ya bati. Ukienda pale kuna nyumba chache tu za bati, nyingi askari wanazokaa ni za majani. Nilikuwa nadhani kiusalama si vizuri na pia wao kujijengea nyumba zao, wanazijenga kama nyumba binafsi, kwa hiyo, anapohama kama askari mwingine anakuja anahamia kwenye nyumba hiyo ya binafsi. Naomba tafadhali sana, gereza litusaidie maana linazalisha sana kilimo cha mahindi na maharage, kwa hiyo nilikuwa naomba idara hii itusaidie.

**MWENYEKITIl:** Maliza, wewe unauliza je, hizi fedha na kule kwangu wanaweza kujenga hizo, ndiyo swali lenyewe sio?

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Nashukuru umenisaidia kuuliza hivyo hivyo. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumfahamisha kwamba, kwenye hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri, ukiangalia ukurasa wa 48 (g), tumetenga fedha kwa ajili ya kuimarisha mifumo ya maji safi na maji taka katika magereza ya hapa nchini. Ningependa kumhakikishia kwamba, mimi mwenyewe nitakuja hapo Nkasi kuangalia tatizo na tutajitahidi kutumia kifungu hiki ambacho kimewekwa ili kuhakikisha kwamba,

Gereza la Namtekela linapata maji na katika kipindi hicho hicho tutaangalia suala la hizo nyumba za askari.

*((Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 4002 – *Prison Industries*… … … … … … Sh. 104,320,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 4003 – *Prison Farms*… … … … … … .... ..... ..... Sh. 360,000,000

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante. *Vote* 29, *sub-vote* 4003, kifungu kidogo 4428. Kama nilivyosema awali nilipokuwa nachangia, niliomba trekta kwa Gereza la Butundwe, ambalo linazalisha maharage na mahidi. Limeomba mbuga kwa wananchi wa Nyamagomo, wamejitolea kutoa mbuga ya Isima eneo kubwa kwa ajili ya kuzalisha mpunga na ni sehemu yenye rutuba sana. Kwa bahati mbaya magereza ya rufani, imeshindwa kulima vyema kwa sababu ya kukosa vifaa. Niliwahi kuomba kuanzia 2002 wakapewa trekta moja ambalo lilikuwa kuukuu na bovu, nikaahidiwa tutajitahidi tukipata trekta zima tutawaletea. Sasa trekta hilo halijapatikana, naomba Mheshimiwa Waziri katika bajeti ya safari hii, nadhani sitaahidiwa tena kwa ajili ya mwakani, nadhani watatuletea. Naomba chonde chonde waweze kuzalisha, kwa sababu gereza hilo linaweza kuzalisha mpunga ambao unaweza kulisha magereza yote ya Mkoa wa Mwanza na Kagera.

**MWENYEKITI:** Umeeleweka.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 48 wa hotuba, kuendeleza uzalishaji katika mashamba ya kilimo na mifugo kwa kuyapatia zana na pembejeo zinazotakiwa ikiwemo ununuzi wa matrekta manne. Sasa tukishapata fedha hizi, Kamishna Mkuu wa Magereza na timu yake ya wataalamu, huamua kwa kuangalia eneo lipi watapata matokeo mazuri zaidi kwa kuzielekeza hizo zana. Kwa hiyo, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kama hilo eneo lake lina sifa za sura hiyo, basi anaweza akawa na matumaini lakini kwa taratibu za kibajeti, siwezi kumpa uhakika wa moja kwa moja, kwa sababu lazima menejimenti nayo ifanye kazi yake.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuzidi kutuelekeza juu ya vifungu. *Vote* 29, *sub-vote* 4003 na *item* 4428, nilitaka kusema nikuwa Jeshi la Magereza linamiliki mashamba mengi makubwa na mazuri sana, lakini bado halijitoshelezi kwa chakula chake chenyewe, achia mbali kwa ajili ya kuuza. Wakati huo huo inafanya kazi katika mashamba ya kibinafsi kwa kujiongezea kipato ili kuziba hili pengo. Nilitaka kusema kuwa Serikali ina mpango huu wa kuleta mapinduzi ya kilimo kwa kutumia Programu ya *SDP*, sasa kwa nini basi haiwapatii Jeshi la Magereza vifaa vya kutosha na mbolea ili kuanza kuzalisha kwa wingi, kujitosheleza wao

na kwa taifa letu? Vilevile ingekuwa ni mfano kwa mashamba darasa, wananchi wangeweza kuiga pale maelekezo ya kilimo na uzalishaji ungekuwa mkubwa sana katika nchi hii. Kwa hiyo, suala ilikuwa ni kufafanuliwa kwamba, kwa nini sasa Serikali katika Wizara hii haileti matokeo mazuri kwa muda mfupi, nchi yetu ikaneemeka kwa chakula na isiendelee kuagiza chakula kutoka nchi nyingine. Asante.

**MWENYEKITI:** Anasema magereza ingeweza kuwa mfano na yakazalisha vya kutosha kabisa kwa ajili yao wenyewe.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yetu kwa kupitia Shirika la Magereza, yaani *Prisons Corporation Soul,* inaangalia mikakati ya kuweza kutumia mashamba ya magereza kwa ukamilifu ili kuhakikisha kwamba, yanalisha wafungwa wote na mahabusu wote katika magereza ya hapa nchini. Uzuri wa kutumia Shirika la Magereza ni kwamba linao uwezo wa kukopa katika Mfuko wa Pembejeo na lina uwezo wa kukopa katika mabenki binafsi. Kwa kipindi hiki tunaangalia mkakati wa kuweza kuimarisha *Prisons Corporation Soul* ili kuhakikisha kwamba, yale ambayo ameyatoa kama mfano, yanatekelezeka.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante. *Vote* 29, *sub-vote* 4003, *item* 4428 - *Enhancement of Prison Farm.* Katika wilaya yangu nina magereza mawili; Libelege na Itende. Katika mchango wangu wa maandishi, nilikuwa nimependekeza kwa Waziri, kwa vile yale maeneo ni makubwa na magereza hailimi yote na wapo wananchi wanaowazunguka wao, basi wawakodishe angalau kwa kulipa chakula, labda magunia mawili, matatu, ili mashamba yawe safi na isiwe chanzo cha wanyama kwenda kwenye mashamba ya wanakijiji. Kwenye haya maeneo kuna wakijiji wamewazunguka lakini unakuta wao mashamba safi pale pa magereza pamekuwa pachafu na ni *source* ya wanyama kula mazao yao. Sasa sikupata ufafanuzi wote, naomba Waziri anijibu.

**MWENYEKITI:** Nyie magereza mnafuga misitu? *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu maeneo anayoyazungumzia na ni katika maeneo ambayo ule mkakati ambao aliueleza Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kutumia *Prisons Corporation Soul* ili tuyafanyie *development,* tunaufanyia ukazi. Tunaomba atupe muda, tunataka kufanya kitu kikubwa ambacho pia kitahusisha na wananchi. Tumekwishaanza kuandaa hili jambo na tutakapokuwa tayari, tutalitolea taarifa.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante. *Vote* 29, *sub-vote* 4003, *item* 4428 - *Enhancement of Prison Farms.* Katika mchago wangu nilitoa maelezo kwamba, kule jimboni kwangu yako maeneo ya Mbuyuni Chiumo ambapo wakati tukiwa wilaya moja Newala, kabla hatujagawanywa. Wananchi walitoa maeneo yao kuwapa Magereza Newala ili yatumike kwa kilimo. Magereza ya Newala, wamekuwa wakiendeleza kilimo kwa muda mrefu, lakini baadaye wakayaacha maeneo yale kwa miaka kumi hivi sasa na kwamba, hakuna jambo lolote la kimaendeleo kwenye mashamba yale linaloendelea. Juzi nilipopita kwenye maeneo yale, wapiga kura walinilalamikia kwamba, kuna tatizo gani magereza hawaendelezi haya maeneo na kama

hawana mpango wowote, basi waturudishie wananchi tuliokuwa tumewapa ili tufanye shughuli zetu za kilimo? Sasa nilitaka kupata maelezo, maana kwenye mchango wangu wa maandishi Waziri haku-*respond* vyovyote. Nilitaka kupata maelezo, mpango alionao, ama vinginevyo, warudishe kwa wananchi ili wafanye shughuli zao za kilimo.

**MWENYEKITI:** Jibu kama ni lile alilojibiwa Mheshimiwa Castor R. Ligallama, lakini naomba mjibu kusudi watu wasikie huko Nachingwea.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sahihi kabisa, kwa maeneo haya yote ambayo yako chini ya Magereza, tunayafanyia kazi. Napenda nirudie kama mahali kuna *land pressure,* tuko tayari kuzungumza uwezekano wa kurudisha sehemu. Lakini sisi tuna mpango wa kuyaendeleza maeneo hayo kwa kutumia *Prisons Corporation Soul,* wao wenyewe, pamoja na *joint ventures* ambazo ziko katika hatua ya mazungumzo. Kwa vile hayajakamilika, hatuwezi kuyatolea maelezo, naomba Mheshimiwa Mbunge atuvumilie, ndani ya miezi hii kumi na miwili, tutakuwa tumekamilisha maandalizi.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fungu hilo hilo la 29, kifungu kidogo 4003, inahusu Gereza la Namajani.

**MWENYEKITI:** Hebu sema kwanza linahusu nini?

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Gereza la Namajani. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwamba, nimesikia kauli zao na kusema kweli mimi naamini Wananchi wa Namajani nao wamefurahi kwamba, sasa hili suala litashughulikiwa vizuri, hakutakuwa na matatizo.

La pili ni kwamba, katika Gereza hili la Namajani la Kilimo, naomba Mheshimiwa Waziria au Naibu Waziri, awaeleze na hata kuwalazimisha magereza katika sehemu ile, wasipeleke ng'ombe wao katika mashamba wakati wa masika, ambao kwa kweli walikuwa wanafanya kama kwa kukomoana tu na pia kupitisha ng'ombe wale katika visima ambavyo watu ndiyo wanavitegemea. Ng'ombe wanaenda kucheza cheza pale halafu hali inakuwa mbaya, wananchi wanategemea maji hayo. Naamini katika *spirit* hii tuliyotoka nayo leo ni mwanzo mzuri wa kuhakikisha kwamba, yale matatizo au mgogoro uliokuwepo Namajani, hivi sasa utakwisha ili tuweze kufanya kazi za kimaendeleo. Hilo nilikuwa nalisisitizia tu kwa kumalizia kwamba, nimeona nia yao ni nzuri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, tutakusomea kifungu cha kupoteza muda wa Spika, kwa sababu wanasema mkitoka mwende, sasa ukitueleza hapa yote kule mtakwenda kueleza nini maana mtakuwa mmeshamaliza?

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu la 51 – Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

Kif. 1003 – *Policy and Planning… … … … …* .... ..... Sh. 884,000,000
Kif. 1004 – *Community Service Secretariat… … … …* Sh. 884,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu la 91 – Uhamiaji**

Kif. 2002 – *Immigration Mainland… … … … …* Sh. 4,459,000,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Bunge lako Tukufu lilipokaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia kifungu kwa kifungu, Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2007/2008 ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na limeyapitisha bila ya mabadiliko yoyote.

Kwa hiyo, naomba kutoa hoja kwamba Makadirio hayo sasa yakubaliwe na Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2007/2008 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mimi sina matangazo ya ziada. Kwa hiyo, napenda kuahirisha kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.30 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano, Tarehe 1 Agosti, 2007 Saa Tatu Asubuhi)*